

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Kwanza – Tarehe 6 Novemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Tukae. Karibuni sana.

Waheshimiwa tusikilizane. *Brass Band* tunawashukuru sana, mnafanya kazi nzuri sana, karibuni sana Bungeni.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE: Kiapo cha uaminifu.

KIAPO CHA UAMINIFU

Wabunge wafuatao waliapa Kiapo cha Uaminifu:-

1. Mhe. Julius Kalanga Laizer;
2. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara;
3. Mhe. Timotheo Paul Mnzava; na
4. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka.

SPIKA: Katibu

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada mitano ya Sheria ya Serikali ifuatayo:-

Kwanza, Muswada wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Mkuu ya Nchi ya Mwaka 2018 (*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill, 2018*).

Pili, Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018 (*The Tanzania Teachers' Professional Board Bill, 2018*).

Tatu, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 02 wa Mwaka 2018 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2018*).

Nne, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2018 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2018*).

Tano; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 (*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018*).

Kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari miswada hiyo mitano imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi zinazoitwa:-

Kwanza, Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma Kuwa Makao Makuu ya Nchi Na. 5 ya Mwaka 2018 (*The Dodoma Capital City (Declaration) Act No. 5 of 2018*);

Pili, Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania Na. 6 ya Mwaka 2018 (*The Tanzania Teachers' Professional Board Act No. 6 of 2018*);

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Tatu, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya Mwaka 2018 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act of 2018*);

Nne, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) Na. 8 ya Mwaka 2018 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act No. 8 of 2018*); na;

Tano, Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Na. 9 ya Mwaka 2018 (*The Public Private Partnership (Amendment) Act No. 9 of 2018*).

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawaita wawasilisha hati, nitambue uwepo Bungeni wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii. (*Makof/ Vigelegele*)

Karibu sana Mheshimiwa Waziri; pole sana kwa yote. Tulikuombea na Mwenyezi Mungu amekubali maombi yetu sasa uko pamoja nasi, karibu tena, karibu sana. (*Makof/*)

Hati za kuwasilisha Mezani, sasa nimuite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Ashatu Kijaji tafadhali.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Mapendekazo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. MARIA N. KANGOYE (K.n.y. MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu!

NDG.STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza linaelekezwa kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na litaulizwa na Mheshimiwa Esther Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 1

Kulinda Ajira za Vijana Nchini

MHE. ESTHER M. MMASI aliuliza:-

Ukosefu wa ajira bado ni changamoto kubwa hasa tunapoangalia takwimu za kidunia na hata katika nchi yetu:-

(a) Je, Serikali imejipangaje katika kulinda ajira za Vijana kupitia Sera ya Ajira?

(b) Kwenye kada ya TEHAMA nchi yetu imekuwa ikipokea nafasi nyingi za ajira kwa Vijana kwenye Taasisi za kifedha kwa kazi nyingi kupelekwa nje ya nchi ikiwemo nchi jirani. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Esther Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Sera ya Taifa ya Ajira imeweka mikakati ifuatayo katika kulinda ajira za vijana:-.

(i) Kuhamasisha mazingira bora ya uwekezaji katika sekta zenyewe uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira hususani kilimo, ujenzi, viwanda na biashara;

(ii) Kuwajengea vijana ujuzi wa fani mbalimbali kupitia programu za ukuzaji ujuzi ili vijana wengi zaidi wapate ujuzi stahiki utakaowawezesha kuwa na sifa za kuajirika, kujajiri na kuwaajiri wengine;

(iii) Kusimamia sheria na kanuni za kuwawezesha vijana wazawa wengi zaidi kushiriki katika miradi mikubwa ya maendeleo kama sehemu ya nguvu kazi na watoa huduma; na

(iv) Utekelezaji wa Sheria ya Uratibu wa Ajira kwa Wageni Na.1 ya Mwaka 2015 ili kulinda nafasi za kazi kwa Watanzania, kwa kuhakikisha Watanzania wanafanya kazi ambazo vinginevyo zingefanywa na wageni.

Mheshimiwa Spika, kada ya TEHAMA ni moja ya Kada ambazo zimewawezesha ajira nyingi hapa nchini hivyo Serikali

imefanya juhudhi kubwa kuhakikisha kunakuwepo naa Wataalam wa kutosha wa sekta hii na kulinda ajira zao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ni kutoa Wataalam wengi wa fani ya TEHAMA kuititia Vyuo Vikuu na Vyuo yya elimu ya Juu kwa kuhamasisha wanafunzi wengi zaidi kusomea fani za sayansi ikiwemo suala la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, pili ni kuendesha programu za ukuzaji ujuzi ili kuwajengea uwezo Watanzania katika fani ya TEHAMA kuititia mpango wa kitaifa wa kukuza ujuzi na tatu ni kutoa mikopo ya asilimia 100 kwa wanafunzi wa Elimu ya juu kwa Kada ya TEHAMA.

SPIKA: Mheshimiwa muuliza swali, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER M. MMASI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali langu kwa Serikali; Vijana wanaohitimu nchini Tanzania ni takribani laki sita mpaka laki nane kwa mwaka lakini vijana wanaoingia kwenye ajira rasmi na zisizo rasmi ni takribani ni asilimia kumi mpaka 25.

Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali kutohana na masuala mazima ya *retrenchment* yanayoendelea nchini Tanzania. Kwa sasa tunayo taarifa ya kwamba kampuni ya *TTCL* ina mpango wa *down size* wafanyakazi zaidi ya 500; lakini pia ukienda kwa taasisi zisizo za Kiserikali mfano *TBL* tumeshuhudia hapa miezi michache iliyopita kwamba wali-*retrench* zaidi asilimia 80 na wakati huo huo wakihamishia sehemu kubwa ya *operations* mfano *payroll function*, lakini pia siyo hivyo tu *finance Department* ilipelekwa Mauritius; swali langu la kwanza; nini kauli ya Serikali haswa ukiangalia hali halisi ya ombwe kubwa la vijana wanaohitimu pasipo kuwa na ajira?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kumekuwa na utamaduni mbaya sana unaoendelea kwenye taasisi za kifedha ambapo taasisi hizi zinakuwa zinajisajili Tanzania lakini sehemu kubwa sana ya majukumu ya *IT* yanakuwa

yanafanyika nje ya nchi. Mathalani benki ya *Stanchart* (*Standard Chartered*), *Baclays*, lakini *Citi Bank* pamoja na *Stanbic bank*, wamekuwa na utamaduni wa sehemu kubwa ya *ITzinakuwa zinafanyika nje ya nchi*. Ukiangalia *NBC, supply of payment* inafanyika South Afrika; ukiangalia *Stanchart account opening* na pia *transaction process* zote zinafanyika nchini Kenya. Ukiangalia *Baclays function management* zinafanyika nchini India, swali langu kwa Serikali. Nini kauli ya Serikali hasa ukiangalia uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi hawa wanaohitimu shule ya TEHAMA? Naomba kupatiwa majibu stahiki na Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa swali zuri lenye mifano halisi, majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Mavunde tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la kwanza la kuhusiana na *retrenchment*. Ni dhahiri kwamba sisi kama nchi katika Sera ya Ajira tunaendelea kulinda ajira za vijana katika nchi yetu kwa kuhakikisha kwamba vijana wengi zaidi wanapata fursa ya kuweza kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, alichokisema Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Mwaka 2004 imeweka vigezo ni katika hatua gani mwajiri anaweza akafanya *retrenchment*. Sheria ile pia imetoa nafasi kwa vyama vya wafanyakazi kushiriki moja kwa moja katika majadiliano kabla jambo hili halijafanya.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa waajiri wote ni kwamba waendelee kufuata sheria inavyozungumza ya namna ya kuweza kuwaondoa wafanyakaza kazini kwa kuwa jambo hili lipo kisheria. Kazi yetu kama Wizara ni kuhakikisha kwamba taratibu za kisheria zimefuatwa ili Watanzania wengi haki zao za kimsingi zisiondolewe katika utaratibu huu wa uachishwaji wa kazi ambao wa sheria imeuzungumza vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, kuhusu kazi nydingi kufanyika nje ya nchi. Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu anachokisema Mheshimiwa Mbunge na sisi tulikiona tumefanya ziara ya ukaguzi tumekwenda makampuni mbalimbali; na hivi sasa tumeleshatoa maelekezo ya kazi hizi namna gani zifanywe.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa kwenye eneo la TEHAMA pia ni kwamba ukiruhusu mambo hayo yote yafanyike nje ya nchi ni hatari pia kwa usalama wa nchi. Kama Serikali tumechukua hatua na tumetoa maelekezo kuwataka waajiri wote kurekebisha eneo hili. Sasa hivi tunafanya *follow up* na vile vile tunafanya kaguzi ili kukagua waajiri wote ambao wamekiuka agizo letu tuweze kuwachukulia hatua.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri nimeduona.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa niongeze kipengele kidogo kuhusu masuala ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Serikali imeanzisha Tume ya TEHAMA ambayo pamoja na majukumu mengi kabisa iliyonayo inakwenda kuanzisha Bodi ya kutambua wana TEHAMA wote ili wana TEHAMA hao watambulike kutokana na elimu yao na ujuzi wao wanalionao kama wanavyotambulika Mainjinia, Madaktari na Wahasibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tunaamini kwamba tutapata taaluma stahiki za kufanya kazi kwenye maeneo ya TEHAMA. Ahsante.

SPIKA: Kwa umuhimu wa swali hili nitaweka nyongeza angalau mmoja; Mheshimiwa Zungu, nimeduona.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa swalii. Kwanza niipongeze Serikali kwa jitihada zake za mikakati ya ajira kwa vijana na Sera ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo liko eneo ambalo Serikali kama wakitilia mkazo na kulifuatilia; sehemu ya *hand-looming*. Huu ni mtambo mdogo sana ambao unatumika hasa na nchi ya India ku-create ajira kwa vijana na wananchi wa kawaida kwa kufanya biashara ndani ya vyumba vyao. Haihitaji umeme wala teknolojia yoyote zaidi ya kuwa na chumba na mtu mmoja unapata nyuzi wanatengeneza *gray cloths* na vile vitambaa wanauzia viwanda vya kutengeneza nguo; na matokeo yake wanapata kati ya laki moja na nusu mpaka laki mbili kwa siku. Je Serikali ina mkakati gani wa kutazama eneo hili la ku-create ajira badala ya kuacha vijana wengi ambao sasa hivi hiyo nguvu kazi zinapotea? (*Makofî*)

SPIKA: Majibu ya ushauri huo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri mzuri wa Mheshimiwa Mbunge wa lengo la kuongeza ajira hasa kwa vijana. Kwa kuongezea tu na sisi kama Serikali tuliona pia tuna jukumu la kutengeneza mazingira wezeshi kwa vijana wengi. Ndiyo maana kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu hivi sasa tunaendesa programu ya kukuza ujuzi nchini ambayo imeanza mwaka 2016 mpaka 2021 lenye lengo la kuwafikia takribani vijana milioni 4.4 nchi nzima ili vijana kupitia ujuzi mbalimbali waweze kujiajiri na kuajiri vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo fursa aliyosema Mheshimiwa Mbunge tunaichukua na tutaiboresha ili vijana wengi zaidi waweze kupata ajira.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, tunaendelea na swalii linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea.

Na. 2

Utaratibu wa Kukimbiza Mwenge Nchi Nzima

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA aliuliza:-

Tarehe 9 Desemba, 1961, Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere alisema tutauwasha Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro ili umulike nchi nzima na kuleta upendo, amani na kadhalika:-

Je, utaratibu huu wa kukimbiza Mwenge nchi nzima kila mwaka umetoka wapi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tarehe 9 Desemba mwaka 1961, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alisema nanukuu;

"Sisi tumekwisha uwasha Mwenge wa Uhuru na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike ndani na nje ya mipaka yetu, ulete matumaini pale ambapo hakuna matumaini, ulete upendo mahali penye chuki na heshima palipojaa dharau." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kukimbiza Mwenge wa Uhuru nchi nzima kila mwaka ulianzishwa mwaka 1964 baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na Muungano wa nchi mbili zilizokuwa zinaitwa Tanganyika na Zanzibar. Utaratibu huu ulianzishwa kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 1992 mbio za Mwenge wa Uhuru zilitumika zaidi kueneza na kuwakumbusha Watanzania falsafa inayotoa

misingi ya sera ya ndani ya nchi yetu baada ya kupata Uhuru. Misingi hiyoni kujenga Taifa lenye amani, linalojitegemea na lenye kuheshimu misingi ya utu na usawa wa binadamu; na mbio hizi zilihasisiwa na Baba wa Taifa mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, pili, katika karne ya 20, kwa kutumia falsafa yake, mbio za Mwenge wa Uhuru zilitumika kumulika hata nje ya mipaka ya nchi yetu ili kuhamasisha vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe, dhuluma, ubaguzi na hasa katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, tatu, wakati tunaingia katika karne ya 21, mbio za Mwenge wa Uhuru baada ya kutimiza azma yake ya awali ya uhamasishaji wa msingi wa utaifa wetu na ukombozi wa Bara la Afrika, mbio hizi ziliendelea kukimbizwa nchi nzima kwa lengo la kuendeleza mapambano dhidi ya maadui ujinga, maradhi na umaskini katika nchi yetu. Kupitia utaratibu huu Mwenge wa Uhuru umekuwa ni chombo muhimu cha kuchochaea maendeleo ya wananchi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la amani, haki, utu, muungano wetu na maendeleo kwa wananchi halina mipaka ya kijigrafia wala muda maalum wa kulishughulikia. Hivyo, Serikali inaona ni muhimu kuendelea na utaratibu wa kuukimbiza Mwenge wa Uhuru nchi nzima kila mwaka ili uendelee kufanya kazi ya kuimarisha misingi ya Taifa letu na kuhamasisha maendeleo ya wananchi.

SPIKA: Sasa maswali ya nyongeza haya hamuujuji Mwenge? Mheshimiwa Mtalea swali fupi.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu ya Serikali, Serikali inakiri kwamba zoezi la kuukimbiza Mwenge nchi nzima ilikuwa na tija tu kati ya mwaka 64 mpaka mwaka 92 na ndio maana hata kwa wananchi mvuto wa kuupokea

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mwenge umepungua; sasa hivi Mwenge unapokelewa na Watumishi wa Serikali, wanafunzi na Madiwani pekee. Pia katika mikesha ya Mwenge Watumishi wanalazimishwa kukesha kwenye Mwenge jambo ambalo limekuwa kichocheo kikubwa cha kuharibu ndoa za watu lakini pia maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi... (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mt Olea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Serikali ina mpango gani sasa...

SPIKA: Mheshimiwa Mt Olea inaelekea huna swali tunaendelea na swali linalofuata, linakwenda Ofisi la Rais, TAMISEMI, swali la Mheshimiwa *Engineer Christopher Kajoro Chiza Mbunge* wa Buyungu. (*Makofii*)

Na. 3

Hitaji la Hospitali ya Wilaya na Vituo vya Afya Kakonko

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA aliuliza:-

Sera ya Serikali ni kuwa na Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya katika kila Kata:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kakonko?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya katika Kata za Kiziguzigu, Kasanda, Gwarama, Rugenge, Nyamutukiza na Kata nyingine ambazo hazina Vituo vya Afya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua za awali za kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kakonko zimeanza ambapo limetengwa eneo lenye ukubwa wa ekari 32 katika Mtaa wa Kanyamfisi karibu na yanapojengwa Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajenga Hospitali za Wilaya kwa awamu ambapo katika awamu ya kwanza zimetengwa shilingi bilioni 100.5 kuanza ujenzi wa Hospitali 67 za Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko itapewa kipaumbele cha kujenga Hospitali ya Wilaya katika awamu inayofuata.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa shillingi bilioni 4.2 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo tisa vya afya katika Mkoa wa Kigoma. Kati ya fedha hizo, halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imetengewa Sh.500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Gwanumpu. Maeneo yaliyobaki zikiwemo Kata za Kizuguzugu, Kasanda, Rugenge, Gwarama na Nyamtukuza yatapewa kipaumbele kulingana na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Injinia Chiza, tafadhali swali la nyongeza.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naishukuru pia Serikali kwa kututengea Sh.500,000,000 za kujenga kituo cha Afya cha Gwanumpu na nimetoka Jimboni kazi sasa imeanza, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo sasa nina swali moja tu. Pamoja shukrani hizo, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa anajua kabisa Ubunge wangu bado mbichi; sasa ananiahidi nini kwa awamu hii inayofuata; kwamba itaanza lini ili Kata za Kiziguzigu, Kasanda, Rugenge, Gwarama na Nyamtukuza nazo zipate fedha za kujenga vituo vya afya? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kama ambavo tumeainisha kwenye ilani yetu ya CCM kwamba kila kata tutajenga kituo cha afya na kila Wilaya ambako hakuna Hospitali ya Wilaya tutaenda kujenga, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, miongoni mwa maeneo ambayo tutahakikisha yanajengwa vituo vya afya ni yale ambayo yana upungufu mkubwa ikiwa ni pamoja na Wilaya yake ya Kakonko.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie, hakika pale ambapo bajeti itaweza kupatikana ikaongezeka hatutawasahau Kakonko na hasa tukiwa tunajibu fadhira ambazo wananchi wa Kakonko na hasa Buyungu walitoa kwa Chama cha Mapinduzi.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza fupi.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia ujenzi wa Hospitali za Wilaya katika Mkoa wangu wa Arusha, Wilaya mbalimbali kama Longido, Monduli na nynginezo na upanuzi mkubwa wa vituo vya afya ukiendelea, nataka kufahamu; Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha wanaleta wataalam wa kutosha hasa wa dawa za usingizi ili wananchi wa Arusha wapate huduma, hasa ya mama na mtoto? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika.....

SPIKA: Yes, sawa endelea.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, Serikali

imewekeza katika uboreshaji wa vituo vya afya takribani zaidi ya 300 nchi nzima. Hata hivyo tunatambua kwamba uboreshaji huu unaendana sambamba na kuongeza huduma za upasuaji. Sisi kama Serikali sasa hivi tumeshapeleka watumishi zaidi ya 200 kwenda kusomea masuala ya usingizi. Tunatumaini ndani ya muda mfupi huu watumishi wale watakuwa wamekamilisha mafunzo hayo na tutawasambaza katika vituo vya kutolea huduma.

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na swalilinalofuata, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda.

Na. 4

Hitaji la Gari la Wagonjwa – Kituo cha Afya Bukoli

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA aliuliza:-

Je ni lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Bukoli?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalilisa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina gari saba zinazotoa huduma kwa wagonjwa (*ambulance*). Gari tano zinatoa huduma katika Vituo vya Afya vya Katoro, Nzera na Chikobe ambavyo vimeanza kutoa huduma za upasuaji. Gari mbili zinatoa huduma katika vituo vya afya vinavyobaki kikiwemo Bukoli ambacho kipo katika ukarabati ili kukiwezesha kutoa huduma za upasuaji. Halmashauri inashauriwa kuweka kipaumbele na kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa gari za wagonjwa kulingana na mahitaji.

SPIKA: Mheshimiwa Lolesia, nyongeza.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, takwimu zinaonesha kwamba katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Geita kuna changamoto kubwa sana ya vifo nya akinamama wakati wa kujifungua; na kwa sababu hiyo wengi inatokana na kwamba wakati wa kujifungua, pale wanaposhindwa kuwapeleka hospitali ya rufaa ya Mkoa inakuwa ni vigumu kwa sababu hakuna usafiri. Kwa hiyo, ni muhimu sana kituo cha afya cha Bukoli kipatiwe kwa kweli gari la wagonjwa. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuona umuhimu huo wa kupatiwa gari la wagonjwa katika kituo cha afya cha Bukoli? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile sambamba na gari la wagonjwa kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi, hasa katika vituo hivi nya afya ikiwemo cha Bukoli pamoja na kituo cha Katoro, Chikobe, vyote hivyo. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha kwamba inapunguza tatizo hili?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri yale ya awali. Nafahamu changamoto kubwa inayolikabili Jimbo la Busanda hali kadhalika Mkoa mzima wa Geita.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ombi lake tunalichukua, pale inapopatikana fursa tutaangalia nini cha kufanya kwa ajili ya kuweza kulishughulikia eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa ajili ya kupunguza hili tatizo la vifo nya akinamama na watoto; na hasa tuna kesi kubwa sasa hivi ya akinamama wengi kupata *fistula* kwa sababu ya kuwapeleka maeneo mbalimbali kwa kuwa

referral system inapatikana mbali; ndiyo maana tumejielekeza katika kuimarisha vituo hivi nya afya.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali yetu imejipanga; na mpango mkakati wa hivi sasa ni kwamba tunatarajia kukamilisha vituo nya afya 350 kwa lengo kubwa la kupunguza tatizo hili. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba Serikali itafanya kila liwezekanaloo; hata kule sehemu ya Songambele na sehemu ya Mkoka jambo hili lipo katika kipaumbele chetu kuhakikisha wananchi wanapata huduma vizuri.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Afya anataka kuongezea, labda ataeleza na ule ugomvi wenu na upande wa Geita Vijijiini wa hospitali ya Wilaya inajengwa wapi. Mheshimiwa Waziri wa Afya. (*Kicheko*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Jafo; lakini nimesimama kwa sababu ya hoja ya Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, kwamba Geita ni moja ya mikoa yenye idadi kubwa ya vifo vitokanavyo na uzazi. Kwa hiyo nakubaliana, nataka tu kuongeza majibu ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi au ukarabati wa vituo nya afya tunajikita pia katika kuboresha huduma ambazo akinamama wajawazito wanapatiwa. Kwa mfano tumeifanya tathmini, wanawake ambaa wanakwenda katika vituo nya kutoa huduma za afya hawapimi, hawafanyiwi vipimo muhimu; kwa mfano wingi wa damu, labda mkojo na shinikizo la damu. Hivi leo Mheshimiwa Makamu wa Rais anazindua kampeni ya Kitaifa ya kuhimiza uwajibikaji katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi; na kipaumbele tumeweka Geita, Kigoma, Kagera na mikoa yote ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la kupunguza vifo halitamalizika kwa kujenga majengo tu, pia tunataka

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kusimamia ubora wa huduma anazopewa mama mjamzito pamoja na vitoto vichanga. Tunasema jiongeze tuwavushe salama.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana kwa majibu mazuri Mheshimiwa Waziri. Ila kwa kweli huko Geita, Busanda huko kunahitaji jicho la kipekee, maana shule ya msingi Katoro kwa mwaka huu ina wanafunzi 7,000. Naambibi Januari mwakani watakapoingia darasa la kwanza itakuwa na wanafunzi 10,000. Sasa hiyo inakupa picha ya jinsi kituo cha afya kilivyo busyyaani. (*Makofii/Kicheko*)

Tunakwenda swalii kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, swalii la Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini. Mheshimiwa Mwalongo tafadhalii.

Na. 5

Kuifanyia Ukarabati Hospitali ya Kibena

MHE. EDWARD F. MWALONGO aliuliza:-

Hospitali ya Kibena ni kongwe sana na imechakaa sana:-

Je, ni lini Serikali itaifanyia ukarabati?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuifanyia maboresho Hospitali ya Kibena katika maeneo mbalimbali

katika kipindi cha mwaka 2018/2019. Kwa sasa Serikali inafanya upanuzi wa jengo la radiolojia ili kusimika mashine mpya ya *X-Ray*. Ujenzi huu utagharimu jumla ya Sh.39,750,000. Vile vile upanuzi wa jengo la upasuaji unaendelea chini ya ufadhili wa Shirika la *UNICEF*.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe katika eneo la Wikichi ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Serikali ilipeleka kiasi cha Sh.3,234,787,370 ambazo zimeweza kutumika katika ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (*OPD*) ambao umekamilika kwa asilimia 95.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni saba kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali hiyo kwa kujenga majengo ya *X-Ray*, upasuaji, uchunguzi wa maabara na kichomea taka hatarishi. Sanjari na hilo, kupitia fedha za *Global Fund*, hospitali itajengewa jengo la huduma ya mama na mtoto na hivyo kuifanya hospitali hii kuwa na uwezo wa kutoa huduma muhimu za afya katika Mkoa wa Njombe.

SPIKA: Mheshimiwa Mwalongo swali la nyongeza kama lipo.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. imeuliza kuhusu Hospitali ya Kibena; nimepewa majibu kidogo sana juu ya Hospitali ya Kibena lakini zaidi majibu yamejikita kwenye hospitali mpya ya mkoa inayojengwa. Hospitali ile ya Kibena ni hospitali chakavu, ina wodi moja tu ya akinababa. Wanaopata ajali na wanaougua maradhi mbalimbali wote wanalazwa katika wodi moja. Hospitali hii haina *fence* tangu wakati imerithiwa kutoka Kampuni ya *TANWART*. Naomba sasa *commitment* ya Serikali, ni lini Serikali itatusaidia kuboresha hospitali ya Kibena kwa maana ya wodi ya wagonjwa na *fence*?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; Serikali imetusaidia tumepewa fedha kujenga Kituo cha Afya Ihalula, lakini hata sisi katika halmashauri yetu kwa kushirikiana na wananchi katika Kata ya Makoa wamejenga kituo cha afya, Kata ya Kifanya wanaendelea na ujenzi wa kituo cha afya, ndiyo wanakamilisha. Naomba pia *commitment* ya Serikali, je, ni lini itatusaidia sasa vifaa kwa ajili ya vituo hivi vya afya ambapo viwili vimekaribia kukamilika na kimoja kinakaribia kukamilika?.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dokta Ndugulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA

WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimeeleza kwamba na bahati nzuri nimepata fursa ya kutembelea hospitali zote mbili, hii ambayo ni Hospitali ya Kibena pamoja na hospitali mpya ya rufaa ambayo tunaendelea kujenga. Sisi kama Wizara, msukumo wetu sasa hivi ni kuweka nguvu kwa kuhakikisha kwamba ile Hospitali mpya ya Rufaa ya Njombe inakamilika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na changamoto na mimi binafsi nimeona katika Hospitali ile ya Kibena na ndiyo maana sasa hivi maboresho makubwa ambayo tunayafanya ni kupanua ule wigo wa utoaji huduma. Kwa hiyo nataka nimhakikishie tu kwamba sisi kama Serikali tunataka tukamilishe ile hospitali kubwa na ya kisasa ili huduma za msingi kwa wananchi wa Njombe Mjini ziweze kupatikana pamoja na Mkoa mzima wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vifaa kwa vituo vipyaa vya afya ambavyo tunaendelea kuviboresha, Serikali kuititia Bohari ya Dawa (*MSD*) inaendelea kununua vifaa hivyo na kadri inavyofika kutoka kwa Washitiri tutakuwa tunavisambaza, ikiwa ni pamoja na vituo hivi ambavyo viko Njombe Mjini.

SPIKA: Kwa sababu ya muda Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Kilimo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, tafadhalii.

Na. 6

Kukifanya Ukarabati Chuo cha Kilimo Mlingano

MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU aliuliza:-

Chuo cha Kilimo cha Utafiti cha Mlingano Wilaya ya Muheza kipo katika hali mbaya:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye Kituo cha Kilimo Mlingano ili kiweze kufanyiwa ukarabati?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swalii Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya uchakavu ya miundombinu katika baadhi ya vyuo vya kilimo ikiwemo Chuo cha Kilimo cha Mlingano. Changamoto hizo ni pamoja na uchakavu wa ofisi, madarasa, mabweni ya wanachuo, maabara, nyumba za watumishi, maktaba pamoja na Karakana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuvikarabati vyuo vya kilimo kupitia *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*SDP II*) ili viweze kutoa mafunzo ya kilimo kwa ufanisi. Uboreshaji huo unatarajiwa kuviwezesha vyuo kuzalisha wataalam wenye umahiri unaokidhi mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika sekta ya kilimo. Aidha, uboreshaji huo pia utavutia wanafunzi kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kati kuijunga na vyuo kama ilivyo kuwa zamani na hivyo kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2018/2019, Serikali imepanga kuvifanya ukarabati vyuo vya kilimo vyote nchini ikiwemo Chuo cha Kilimo cha Mlingano ambapo jumla ya shilingi bilioni nne zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Balozi, swali la nyongeza tafadhalii.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri na yenye kutia moyo ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, tunashukuru sana kwa kutengewa fedha hizo kwa sababu majengo ya chuo hicho yako kwenye hali mbaya sana. Hata hivyo, suala la kutengewa fedha na suala la kupelekewa fedha ni vitu viwili tofauti. Ningependa kujua, fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya Chuo cha Mlingano zitapelekwa lini ili kazi hiyo iweze kuanza?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili linahusiana na suala la mbegu ambazo zinafanyiwa tafiti katika Chuo hicho cha Mlingano na mbegu ya zao la chai. Atakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri, mwanzoni mwa mwaka huu tulikwenda na wadau, Makampuni ya Chai ya Amani kwenye ofisi yake pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Chai.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa ambalo lilitujia huko lilikuwa ni waruhusiwe kuweza ku-*blend* chai hiyo hapa hapa nchini, ku-*pack* chai hiyo hapa nchini; na badala ya kwenda kuuza kwenye mnada chai hiyo kule Mombasa. Sasa alielekeza mambo fulani fulani yafanyike na yameshafanyika na naambiwa mambo hayo yako kwenye Wizara na bado hawajayatolea uamuzi. Ni vizuri sasa hivi akaliambia Bunge hili na wananchi wa Muheza kwamba uamuzi huo ni vipi, kwa sababu tunataka kuweka kiwanda...

SPIKA: Swali sasa Mheshimiwa.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU: ...kwa hiyo, nataka kujua uamuzi wa Serikali ni nini?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa kifupi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA): Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimpongeze sana; ni kweli alifika ofisini kwangu kuulizia swali lake la pili, juu ya kiwanda kile cha *East Usangara* ambapo wao wanafanya usindikaji na walikuwa wanataka kufanya *blending*.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake hili la (b) ni kwamba, sisi kama Serikali tulikuwa na policy mwaka 2006 kwamba wale wasindikaji wote wa chai wawe wanaomba *separate registration* wanapotaka kufanya *blending*. Katika kuepuka ukiritimba ni kwamba Bodi ya Wakurugenzi imeshakaa kuhakikisha kwamba tunawatendea haki wafanyabiashara wote na kuboresha zao la chai ili sasa yule ambaye anasindika aweze pia kupata na kufanya *blending* ama *packaging* kama anataka. Jambo hili tumeshaanza kulfanya kazi ndani ya wiki mbili litakuwa limeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini nikija katika swali lake lile la kwanza, ni kwamba sasa hivi vyuo hivi vya kilimo ambavyo nimezungumzia, Chuo cha Mlingano chenyewe kimetengewa Sh.570,000,000 kwa sababu ile bilioni nne ni katika vyuo vyote nchini; na hizi Sh.570,000,000 mwezi ujao wa Desemba zitakuwa tayari zimeshafika ndani ya chuo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Bado tuko Wizara hiyo ya Kilimo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Dokta Christine Gabriel Ishengoma. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, tafadhali.

Na. 7

Utafiti wa Mbegu ya Alizeti Inayotoa Mafuta Mengi

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA aliuliza:-

Wakulima wengi wamehamasika katika kilimo cha alizeti lakini alizeti inayolimwa haitoi mafuta kwa wingi:-

Je, Serikali ina mkakati gani katika kuimarisha utafiti wa mbegu ya alizeti inayotoa mafuta mengi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ikiwemo alizeti Serikali inatekeleza mkakati wa miaka mitano, yaani 2016/2020 wa kuendeleza zao la alizeti ambao unalenga kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima, kuhamasisha matumizi ya kanuni bora za kilimo, kujenga uwezo wa vyama vya wakulima kuzalisha mbegu bora za daraja la kuazimiwa yaani QDS na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya usindikaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Vituo vya Utafiti vya Ilonga (Morogoro), Makutupora (Dodoma), Tumbi (Tabora), Uyole (Mbeya), Ukiriguru (Mwanza) na Naliendele (Mtwara) inaendelea kufanya utafiti wa mbegu bora za alizeti ambapo mbegu tano aina ya *record, hysun 33, agura 4, NSFH 145* na *NSFH 36* zimesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kati ya mbegu hizo, mbegu aina ya *record* inayozalishwa nchini tangu mwaka 1985

imefanyiwa maboresho na kuiwezesha kuwa na tija ya uzalishaji wa tani 1.5 mpaka tani mbili kwa hekta; ukinzani dhidi ya magonjwa, kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kutoa mafuta mengi kwa asilimia 48 mpaka 50. Aidha, mbegu ya *record ni open pollinated variety (OPV)* inayoweza kutumiwa na wakulima kwa misimu miwili hadi mitatu ukilinganisha na mbegu aina ya chotara ambazo zinaingizwa kutoka nje ya nchi na kutumika kwa msimu mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha mbegu nydingi zaidi zinazalishwa na kuwfikia wakulima, Kituo cha Utafiti Naliendele kinakamilisha utafiti wa aina tatu mpya za mbegu ya alizeti katika msimu wa 2018/2019. Aidha, Serikali imeingia ubia na sekta binafsi kufanya utafiti na kuongeza uzalishaji wa mbegu nchini badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi ambapo Kampuni ya *Silver Land* na *Quality Food Product* zipo katika hatua ya majoribio ya aina mpya ya mbegu za chotara za alizeti ambazo zitazalishwa nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, nilikuona.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Licha ya majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili mafupi ya kuuliza. Swali la kwanza; kwa kuwa tafiti bado zinaendelea kwenye Taasisi zetu hapa nchini na mara kwa mara tafiti hizi huchukua muda mrefu ili mbegu ziweze kutolewa na kuthibitishwa na kuanza kutumika kwa wakulima. Je, kwa msimu huu kuna mkakati gani wa Serikali wa kuwawezesha wakulima kupata mbegu hizi ambazo hazipatikani mara kwa mara?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa viwanda vyetu vinakabiliwa sana na tatizo hili la malighafi ya alizeti ili viweze kuzalisha mafuta ya kutosha ya alizeti ambayo ni mazuri sana kwa upande wa lishe. Je, kuna mkakati gani wa kuhamasisha wakulima katika mikoa mbalimbali hapa nchini ili waweze kulima zao hili la alizeti ili tuweze kupata mafuta ya kutosha hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu kutoka kwa Mheshimiwa Mgumba, Naibu Waziri wa Kilimo. Tatizo la mbegu ya alizeti ni kubwa sana, mbegu bora inayotoa mafuta kwa wingi. Majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kama nilivytangulia kujibu kwenye swalii la msingi, kuna mbegu zaidi ya aina tano mpya zimeshasajiliwa na vituo vyetu ambavyo nimevitaja. Kwa hiyo lile tatizo la zamani, kwamba mbegu ya *record* ilikuwa haizalishwi vizuri na haitoi mafuta vizuri lilihishamalizika kwa sababu vituo vyetu hivi vya utafiti vimefanya utafiti na vimeshaiboresha. Kwa hiyo sasa hivi inazalisha zaidi ya asilimia 48 mpaka 50.

Mheshimiwa Spika, kuanzia sasa ni kwamba mbegu hizi zinapatikana, tuna mawakala tumewaongeza kwa hiyo sasa upungufu huo hautakuwepo. Pia tumeweza kuendeleza shamba letu la Msimba. Tumeshapata wafadhili, wadau wa maendeleo na Serikali, tumeongeza bajeti kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwenye shamba la Msimba kule Kilosa ili kuongeza uzalishaji wa mbegu na kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kuhusu mikakati ya kuhamasisha wananchi. Mikakati hiyo kama Serikali tumeshaianza.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kwanza ni kuingiza mazao yote yanayotakana na mbegu za mafuta kwenye zao la kimkakati, mbegu za mafuta kwa maana ya alizeti, michikichi, nazi, karanga, ufuta, soya na mengineyo, yote sasa tutayaundia bodi kwa ajili ya usimamizi wa kuzalisha mbegu hizi na kumaliza tatizo la upatikanaji wa mazao ya mbegu ya mafuta nchini na kuongeza uzalishaji wa mafuta wa hapa hapa nchini badala ya kuagiza nje ya nchi .

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika hamasa hiyo tumeanza kama miezi miwili iliyopita Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa pamoja na Wizara ya Kilimo

tulikwenda Mkoani Kigoma kwa ajili ya kufua na kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya mbegu mafuta nchi nzima kwa kuanzia na zao la michikichi. Kwa hiyo mikakati hiyo ndani ya Serikali tumeshaianza na hivyo nimwondoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge; Serikali tunalitambua hilo. Lengo letu kubwa ni kuanza kujitosheleza kuzalisha mafuta ndani ya nchi ili tuweze kuokoa fedha za kigeni .

SPIKA: Tunaendelea na Maliasili na Utalii swalii la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

Na. 8

Kuufanya Mji wa Mikindani Kuwa Kivutio cha Utalii

MHE. TUNZA I. MALAPO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mji Mkongwe wa Mikindani uliopo katika Manispaa ya Mtwara Mikindani unakuwa kivutio cha utalii?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka mkakati mahsusii wa kuendeleza Mji Mkongwe wa Mikindani na kuutangaza ndani na nje ya nchi kama kivutio cha utalii. Mwaka 2016 Wizara kupitia Idara ya Mambo ya Kale ilianzisha kituo kipya cha mambo ya kale ndani ya Mji wa Mikindani. Kwa kuanzia Wizara imepieleka watumishi wawili na itaendelea kuongeza idadi ya watumishi kadri upatikanaji utakavyokuwa. Kituo hicho kimelenga kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya malikale zinazopatikana katika Mji Mkongwe wa Mikindani. Aidha, mwaka 2017 kupitia Tangazo la Serikali

namba 308 Wizara ilitangaza mji huu kuwa urithi wa utamaduni wa Taifa. Mji Mkongwe wa Mikindani ni kati ya maeneo...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hasa kule nyuma kule tuwe katika hali ya mkutano kidogo ili tuweze kusikiliza Serikali inajibuje maswali ya Wabunge wenzetu na wananchi pia wanafautilia, kwa hiyo tupunguze hizi sauti.

Mheshimiwa Naibu Waziri Japhet endelea.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Mji Mkongwe wa Mikindani ni kati ya maeneo ya kitalii ambayo yapo katika mpango wa kuboreshwa mandhari yake ya fukwe na maeneo ya wazi ili yatumike kwa shughuli za utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatumia maonesho ya ndani na nje ya nchi katika kutangaza vivutio vya malikale vinavyopatikana katika Mji wa Mikindani. Aidha, Wizara inatumia vyombo vya habari kutangaza kivutio hiki; kwa mfano mwaka 2017, Wizara kwa kushirikiana na kituo cha runinga cha *Channel Ten* ilandaa kipindi cha ushiriki wa sekta binafsi katika uendelezaji wa Mji wa Kihistoria wa Mikindani. Kipindi hiki pia kilitumika kutangaza vivutio vya malikale vilivyo ndani ya Mji Mkongwe wa Mikindani. Sambamba na hatua hizo Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mtwara ilizindua Siku ya Mikindani (*Mikindani Day*) tarehe 06 Oktoba, 2018 kwa lengo la kuutangaza zaidi Mji huo ndani na nje ya nchi.

SPIKA: Mheshimiwa Tunza, nilikuona.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika Mji ule wa Mikindani kuna vivutio ambavyo vimechakaa, vipo lakini vimechaa. Sasa nataka kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha vivutio vile vinakarabatiwa vinakuwa vinavutia lakini bila kupoteza ile hali yake ya asili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalı langu la pili ya nyongeza; Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha ina-*brand*, sisi tukipita pale tunajua ni Mikindani kwa sababu ni kwetu lakini mtu mwininge akipita hawezi kujua kama ile Mikindani inayovuma kwenye historia ndiyo hii. Sasa Serikali ituambie ina-*brand* vipi, inautangaza vipi ili kuwa kivutio kinachovutia na hivyo kuongeza Pato la Taifa? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, majibu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwamba tumeandaa mkakati mahususi wa kuutangaza Mji wa Mikindani, ikiwa ni hatua mojawapo ya kutangaza vivutio vyote viliwyopo Kusini hilli tunalifanya vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu namna ya kukarabati yale majengo ambayo yana historia kubwa ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu Mheshimiwa Mbunge pamoja Waheshimiwa Wabunge wote naomba kuwaambia kwamba gharama za ukarabati ni kubwa sana kurudishia katika ile hali. Kwa hivyo basi, ambacho tunakifanya sasa hivi ni kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kuhakikisha baadhi ya maeneo yanakarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuanzia, mwaka ujao wa fedha tunatarajia kukarabati karibu majengo mawili katika eneo lile ili kuyarudishia katika ile hali iliyokuwepo awali kusudi yawe ni kuvutio kizuri kwa upande wa watalii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalı la pili ambalo linahusu kuutangaza Mji wa Mikindani; kama tulivyosema tutaendelea kuutangaza. Kuhusu *branding* yake mimi nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maendeleo ni hatua, hatua ya kwanza ilikuwa kwanza kuutangaza Kitaifa tumeshafanya, kuandaa vipindi mbalimbali tumeshafanya, sasa tunaandaa namna ya kuutangaza peke yake ule Mji ile *branding* tutashirikiana na ninyi wadau wote ili tuone namna gani

tutautangaza, kila mtu akifika pale aone kwamba nimefika kwa kweli maeneo ambayo ni Mji mkongwe wa historia kubwa. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, uliza swalî lako.

Na.9

Wananchi Kuruhusiwa Kulima Maeneo ya Hifadhi ya Makere Kusini

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Mwaka 2017 wakati Mheshimiwa Rais akiwa katika ziara Mkoa wa Kigoma, katika Wilaya ya Kasulu aliwaruhusu wananchi waliokuwa wakillima katika maeneo ya Hifadhi ya Makere (Kagera Nkanda) kwa sharti kwamba wasiongeze maeneo mengine zaidi ya yale waliyokuwa wakilima:-

Je, kwa nini *TFSwanapingana* na agizo la Mheshimiwa Rais na wanawatesa wananchi kwa kuwapiga na kuwanyan'ganya baiskeli na pikipiki?

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swalî la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Rais kuagiza kumegwa kwa sehemu ya msitu wa Makene Kusini ili kutoa maeneo kwa wananchi kulima Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kasulu ilitekeleza agizo kikamilifu kwa kupima eneo la msitu huo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia upimaji huo jumla ya hekta 10,012.61 zilitengwa kwa ajili ya kilimo kwa wananchi

wa maeneo hayo. Hivyo Kijiji cha Uvinza kilipewa hekta 2,174 na Kagera Nkanda kikapewa hekta 2,496; na eneo lingine la hekta 5,342.61 zilitengwa kwa ajili ya wananchi wengine wa vijiji vya Nachenda, Mgombe na Nyakitonto.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kijiji cha Uvinza kililalamika kuwa eneo walilopata halitoshi hivyo wakaomba waongezewe eneo ambalo ni ardhi chepechepe yaani ardhi *oevu* karibu na Mto Makene na Mto Malagarasi ambalo kitaalam hairuhuswi kulima kwa sababu itasababisha uharibifu mkubwa na kupotea kwa sifa ya uhifadhi. Mto Malagarasi ni muhimu kwa ikolojia na kwa ajili ya ujenzi wa mitambo ya umeme wa maji katika maporomoko ya Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa wananchi wanaendelea na shughuli za kilimo katika maeneo hayo yaliyotengwa na kuridhiwa na vikao vyote vya Mabaraza ya Mkoa na Wilaya. Wizara kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa imekamilisha mchakato wa ramani mpya ya msitu huo.

Mheshimiwa Spika, tatizo liliojitokeza sasa ni kwa wananchi wachache kwa maslahi yao kukataa kufuata taratibu na kutaka kulima ndani ya msitu nje ya maeneo yaliyotengwa huku wengine wakiendelea na uwindaji haramu wa wanyamapori. Wananchi hao wasiofuata sheria ndio waliozuiwa na mamlaka husika kwa Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002, Sura 323 katika kifungu cha 26 ambacho kinakataza kufanya shughuli zozote za kibinadamu ikiwa ni pamoja na kilimo na ufugaji ndani ya msitu wa hifadhi. Mtu yoyote akibainika kufanya hivyo hatua za kisheria hufuatwa.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wananchi kuendelea na kilimo katika maeneo yaliyotengwa na kuachana na kilimo cha kuhamahama ambacho ndicho kinachowafanya kuvamia maeneo ya hifadhi za misitu. Aidha, natoa ushauri kwa wananchi kufuata kanuni bora za kilimo kwa kutumia mbolea ili mashamba yao yaendelee kuzalisha mazao wakati wowote.

SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke ameridhika, aaa! bado ana swalii, tafadhali!

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza; nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuridhia kutoa eneo ambalo wananchi wamekuwa wakilima ili wananchi hao waendelee kulima kwa sababu kutokana na kilimo wananchi wanapata chakula, wanapata mavazi, wanapata ada za watoto na vile vile wanapata pesa kwa ajili ya kujiunga kwenye vikundi mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii langu la kwanza; jibu linaonesha kwamba maeneo yametengwa kwa ajili ya kilimo kwa maana ya Mvinza, Kagerankanda, Nyachenda, Nyakitonto, Mgombe na Nyamihusi. Maeneo hayo wananchi pamoja na viongozi wao wa vijiji hawakuweza kushirikishwa ndiyo maana wananchi wameendelea kulima maeneo yale ambayo wamekuwa wakilima kwa sababu...

SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke nenda moja kwa moja kwenye swalii...

MHE. JOSEPHINE J . GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ndiyo nakuja kwenye swalii...

SPIKA: Unachangia hoja, nenda kwenye swalii.

MHE. JOSEPHINE J . GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua sasa watu wa *TFS* wanapingana na agizo la Mheshimiwa Rais kwa sababu wameendelea kuwapiga wananchi, wanawauwa, wanawatoboa nyazo za miguu na kuwakata mikono, je, hiyo ni halali ?

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili, je,...

SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke hayo madai unayoyatoa ni makubwa sana sidhani kama yana ukweli kwa kiasi hicho...

MHE. JOSEPHINE J . GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, yana ukweli...

SPIKA: Kwa hiyo kwa kuwa na wewe huna swalii tunaendelea na Wizara ya Nishati...

MHE. JOSEPHINE J . GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nina swalii la mwisho.

SPIKA: Mheshimiwa Augustino Vuma Holle Mbunge wa Kasulu Vijijini.

Na.10

Kigoma Kuunganishwa Kwenye Grid ya Taifa ya Umeme

MHE. AUGUSTINO V. HOLLE aliuliza:-

Kwa muda mrefu Mkoa wa Kigoma umesubiri kuunganishwa kwenye *Grid* ya Taifa ya Umeme:-

Je, ni lini Serikali itaunganisha Mkoa huo kwenye *Grid* ya Taifa ya Umeme?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Augustino Vuma Holle, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* mwezi Desemba, 2017 ilikamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga njia ya kusafirisha umeme ili kuunganisha Mkoa wa Kigoma na *Grid* ya Taifa kutokea Tabora. Mradi unahuishaa ujenzi wa njia ya umeme ya msongo kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Kidahwe Mkoani Kigoma kupitia Urambo na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Nguruka umbali wa kilomita 370. Kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa vituo vya kupozea umeme vya 132/33 KV katika Miji ya Urambo na Nguruka. Gharama ya kazi hizo inakadiriwa kufikia Dola za Marekani 81,000,000 na ujenzi wa mradi unatarajia kuanza mwezi Machi, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande mwengine inatekeleza ujenzi wa mradi wa kusafisha umeme...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa mara nyingine; sasa kelele imehamia huku. Tusikilizane ndugu zangu; endelea Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande mwengine inatekeleza ujenzi wa mradi wa kusafisha umeme wa *North West Grid KV 400 Mbeya – Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi* wenyewe urefu wa kilometra 1372. Mradi huu utawezesha kuyaunganisha maeneo ya Magharibi na Kaskazini Magharibi mwa Tanzania katika *Grid* ya Taifa na kuondoa matumizi ya mitambo ya mafuta katika maeneo hayo. Kwa sasa mikataba ya makubaliano ya fedha imesainiwa kati ya Tanzania na Benki ya Dunia pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika na mradi utagharimu Dola za Kimarekani 455,000,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanza utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa *MW 45* kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi. Ujenzi wa mradi huo utaenda sambamba ujenzi wa wa njia ya kusafirisha umeme wa mgongo wa KV 132 yenye urefu wa kilometra 53 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe Kigoma unatarajiwu kujengwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 na kukamilika 2020/2021.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu Vijijini, swali nyongeza.

MHE. AUGUSTINO V. HOLLE: Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa kama Mkao bado hatujaunganishwa kwenye *Grid* ya Taifa na kumekuwa na tatizo kubwa sana la kukosa nishati hii muhimu na kupelekea mkoa wetu kuwa mionganoni mwa mikoa maskini; sasa je, Wizara ya Nishati imejipangaje vipi kuhakikisha kwamba inakamilisha kwa haraka na kwa ufanisi mradi wa REA awamu ya tatu katika Mkao wa Kigoma ambaao kimsingi umezinduliwa muda umeenda sana katika Kijiji au Kata ya Lusese? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati Mheshimiwa Subira Mgalu tafaddhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya kufuatilia changamoto ya nishati. Ni kweli Mkao wa Kigoma pamoja na Mkao wa Katavi kazi za upelekaji umeme kuititia mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa kwanza zilichelewa kutohana na matatizo ambayo yalikuwa nje ya uwezo wa Wizara yetu ya Nishati pamoja na Wakala wetu Vijijini. Hata hivyo mradi huo umeshazindua rasmi na mkandarasi anaendelea na kazi ya survey na watakamilisha hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, aomba niwatoe hofu wakazi wa Mkao wa Kigoma pamoja na Katavi kwamba kwa kweli kwa maelekezo ya Serikali na mkandarasi aliyeeteuliwa ana uwezo na hivyo atafanya kazi kwa haraka iwezenenavyo nakushukuru. (*Makof*)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Hussein Bashe, swalii la nyongeza.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuuliza swalii dogo la nyongeza. Pamoja na shukurani za dhati kwa niaba ya wananchi wa Nzega kwa kutatua tatizo la umeme katika chanzo cha maji katika Mji wa Nzega, Wizara ya Nishati nilitaka tu nipate kauli ya Waziri

ama Naibu Waziri. Mradi wa *REA Phase III* katika Jimbo la Nzega unasuasua; mkandarasi ameonekana *site* mara moja alipokuwepo Waziri na kuweka nguzo. Hata hivyo mpaka sasa nguzo zile zimesimama vile vile na maeneo ambayo aliahidi kuwashaa umeme mpaka leo hayajawashwa. Ni lini mradi huu utapata *speed* ambayo wananchi wa Jimbo la Nzega wanaitaraja? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Bashe anavyotupa ushirikiano kati ka kupeleka umeme kwenye Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, nitangulie tu kusema, kwa sasa Wakandarasi katika Jimbo la Nzega wanafanya kazi katika vijiji 11 na katika Jimbo la Mheshimiwa Bashe wanakamilisha kazi katika maeneo ya Migua karibu kabisa na Ziba katika Jimbo la Igunga. Kwa hiyo nimwambie tu Mheshimiwa Bashe kwamba vile vifaa vyote ambavyo vilikuwa vinasubiriwa kuja ikiwepo nyaya na transfoma vimeshafika tangu juzi; na sasa hivi katika Jimbo la Mheshimiwa Bashe kuna transfoma 12 zimebekwa juzi. kwa hiyo nimpe uhakika Mheshimiwa Bashe na wananchi wa Nzega kwamba kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji 32 katika Jimbo lake litakamilika kabla ya mwezi Julai mwaka ujao. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilimwona Mbunge wa Kasulu Mjini amesimama. Tafadhalii Mheshimiwa, swali fupi la nyongeza.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina swali fupi sana la nyongeza kuhusu huu mradi wa *Northwest Grid* kutoka Mbeya – Tunduma mpaka Nyakanazi. Bunge hili tulishauri kwamba kwa sababu njia ni ndefu, takribani kilometra 2500, tulishauri kwamba angalau mkandarasi awe zaidi ya mmoja ili mmoja aweze kuanzia Kigoma kwenda Nyakanazi wakati mwingine anatoka Tunduma kuja Mpanda mpaka Kigoma. Maadam fedha zimepatikana sasa, je, ushauri huo umezingatiwa? Vinginevyo

kitakachotokea ni kwamba itakuwa ni kazi ya muda mrefu kwa sababu njia ni ndefu sana. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt. Kalemani majibu tafadhali.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa swali hili muhimu sana katika ukanda wa Kusini na hasa Magharibi mwa upande wa Kigoma, Katavi pamoja na Iringa.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika mradi huu ni kweli kwamba tumepata fedha kutoka Benki ya Dunia jumla dola milioni 455 ambayo itatekeleza mradi wa kusafirisha umeme mkubwa wa *kilovott* 400 kutoka Iringa kupita Mbeya hadi Sumbawanga. Taratibu za kuanza mradi katika *portion* hii zimeshaanza, ujenzi rasmi utaanza mwezi Machi mwakani.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wanashauri Waheshimiwa Wabunge, na ye ye akiwemo, mradi huu ni mrefu sana, una umbali wa kilometra 2872 ambapo tumeugawa katika *portion* tatu. Kutoka Iringa, Sumbawanga hadi Tunduma ni *portion* moja ambayo tutaanza mwezi Machi na kuanzia Mei utaanza kuanzia Sumbawanga hadi Mpanda na kutoka Mpanda hadi Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, lakini mbali na mradi huo, tumeona wananchi wa Katavi na Kigoma watachelewa sana kupata umeme wa gridi tumeanza kujenga mradi mwingine wa kutoka Ipole, Sikonge kupeleka *kilovott* 132 Katavi ili kurahisisha wananchi wa maeneo ya katikati kupata umeme wa *grid* mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile mradi mwingine wa nne unaopeleka umeme wa *grid* katika Mkoa wa Kigoma ni pamoja na ule wa kutoka Tabora kupita Urambo hadi Kaliua umbali wa kilometra 370 nao uaanza kujengwa mwezi Februari mwaka ujao. Kwa hiyo ni matumaini yetu wananchi wa Katavi na Kigoma wataanza kupata umeme wa *grid* kuanzia mwezi Oktoba mwakani.

SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri, tunaendelea na Mbunge wa Igalula Mheshimiwa Musa Ntimizi.

Na. 11

Hitaji la Umeme Vijiji vya Jimbo la Igalula

MHE. MUSA E. NTIMIZI aliuliza:-

Katika mradi wa kupeleka umeme vijiji, Jimbo la Igalula limepitwa na umeme katika baadhi ya maeneo ya Kata za Kigwa, Igalula, Goweko na Nsolola tu kati ya Kata kumi na moja za Jimbo hilo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katka Kata na Vijiji vya Jimbo la Igalula vilivyobaki?

(b) Katika Kata ya Igalula, Kijiji cha Igalula ambapo kuna bwawa la maji kuna hitaji la nguzo kumi tu kwa ajili ya kusaidia kusukuma mitambo ya maji. Je, Serikali itasaidiaje kupeleka nguzo hizo ili kutatua tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Jimbo la Igalula, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme vijiji kupitia mradi wa REA /// mzunguko wa kwanza. Katika Jimbo la Igalula lililopo Wilayani yui jumla ya vijiji 98 vitanufaika na Mradi wa REA ///. Kupitia mradi huu jumla ya vijiji 25 vitaunganishiwa umeme. Aidha, vijiji 73 vilivyobaki vitapatiwa umeme kupitia REA ///Mzunguko wa Pili utakaoanza kutekelezwa Mwezi Julai, 2019 na kukamilika Mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mkandarasi kampuni ya *Intercity Builders Limited* anaendelea na kazi za ujenzi wa

miundombinu ya kusambaza umeme katika vijiji vya Kata za Ibelamilundi, Ibiri, Kigwa, Goweko, Nsololo na Igalula. Aidha, vijiji vya Kigwa B, Goweko *Market*, Goweko Tambukareli, Goweko Juu, Imalakaseko, Igalula I na Igalula II vilipatiwa umeme kuititia Mradi wa *REA* Awamu ya Pili uliokamilika mwezi Desemba, 2016.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Mradi wa *REA* III unaondelea sasa katika Jimbo la Igalula zinajumuisha ujenzi wa njia ya msongo wa *kilovott* 33 yenye urefu wa kilometa 66.79; njia ya umeme wa msongo wa *kilovot* 0.4 yenye urefu wa kilometa 102.242; ufungaji wa transforma 34; pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 2,235. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 6.62.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Igalula ambako kuna bwawa la maji, *TANESCO* imeshakamilisha kazi na umeme umeshawashwa katika kituo cha pampu ya maji. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Igalula, Mheshimiwa Ntimizi, tafadhalii, uliza swali la nyongeza.

MHE. MUSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru, pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwanza nitoe shukrani za dhati kwa ziara ya Mheshimiwa Waziri, alipokuja Jimboni kwangu nilimweleza shida ya umeme katika bwawa la maji na sasa tayari transforma imefungwa na umeme unawaka. Nashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko kidogo, *REA* awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu katika Jimbo la Igalula lenye vijiji takriban 98 ni vijiji sita tu ndivyo vimepata umeme katika Jimbo la Igalula; na katika vijiji hivyo sita ni baadhi tu ya maeneo ya vijiji ambavyo vimepata umeme maeneo mengine hayajapata umeme. Kwa mfano, katika Kata ya Igalula, lenye vijiji sita ni kijiji kimoja tu ndiyo kimepata umeme. Je, Serikali haioni usambazaji wa umeme katika Jimbo la Igalula unasuasua na hauridhishi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; Mheshimiwa Waziri alikuja kwenye ziara katika Jimbo la Igalula, alitembelea Kata ya Miswaki, Loya na Lutende. Alijionea hali ya uzalishaji mpunga mkubwa katika eneo lile na halmashauri ilivyowekeza mashine za kisasa za kukoboa mpunga katika eneo lile; akaahidi kupeleka umeme katika kata hizo tatu za Lutende, Loya na Miswaki. Je, ni lini zoezi hili litakamilika na wananchi wa kule waweze kupata umeme? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swalii hilo kwa kifupi.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, kama ambavyo ameeleza kwenye kusoma majibu ya Mheshimiwa Mbunge. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Ntimizi anavyofuatilia maendeleo ya nishati katika Jimbo lake. Sambamba na hilo nipokee shukrani alizotupatia kwa kupeleka maji katika Kata yake ya Igalula na wananchi zaidi ya 1,000 wanapata maji kupitia mradi huo.

Mheshimiwa Spika, na sasa njielekeze katika maswali yake mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza ni kuhusiana na vijiji vitano vya Igalula. Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge, hivi mkandarasi sasa hivi yuko katika kijiji cha pili katika Kata ya Igalula na vijiji vyote vitano katika Kata ya Igalula vitapelekewa umeme kupitia mradi huu unaoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili; Mheshimiwa Mbunge ni kweli nilitembelea kata ya Lutende, Miswaki pamoja na Loya. Ni maeneo ambayo yana makazi mengi na yana uchumi mzuri. Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge, Mradi huu wa kupeleka umeme katika kata hizo tatu tutautoa katika Jimbo la Manonga, Kata ya Simbo na mkandarasi ameshaanza kazi; ingawa kutoka Simbo kuelekea Lutende ni kilometra 20 lakini wakandarasi wameshaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kutoka Lutende kwenda Miswaki ni kilometra 27, kutoka Miswaki kwenda Rarya ni kilometra 13

na kuna jumla ya vijiji 14. Nimpe taarifa kwamba transfoma 17 zimeshapelekwa katika kata hizo tatu na wananchi wa kata hizo watapatiwa umeme ndani ya miezi sita ijayo. (*Makofi*)

SPIKA: Hongera sana Mheshimiwa Waziri, unalijua Jimbo la Igulula kama Chato vile. (*Kicheko/ Makofi*)

Ahsante sana. Sasa tusikilizane Waheshimiwa, kaeni chini kwa sababu sasa ni zamu ya Mbunge mpya kabisa wa CCM kuuliza swali. Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara. (*Makofi/Kigelele*)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa ya kuuliza swali katika Bunge hilli Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wana-CCM wote popote walipo kwa kunikaribisha Chama cha Mapinduzi. Nawashukuru wananchi wa Ukonga kuendelea kuniamini, pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kuchukua baadhi ya maeneo ya Jimbo la Ukonga kuingiza kwenye umeme wa *peri-urban*; eneo la Mbondole, Kitonga, Chanika, Kibanguro, Viwege, Zingiziwa na Buyuni, Mgeule na Mgeule Juu vimeingizwa kwenye *peri-urban*. Sasa ningependa nijue, ni lini sasa maeneo hayo muhimu katika Jimbo la Ukonga kwa kuwaheshimu watu waliouna mkono juhudu za CCM watapata umeme haraka iwezekanavyo? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Subira Mgusu, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwita, Mbunge wa Jimbo la Ukonga kupitia Chama Cha Mapinduzi na nimpongeze sana kwa kushinda kwa kishindo katika uchaguzi huo. Kwanza ameishukuru Wizara yetu kwa namna ambavyo tumeingiza maeneo ya Jimbo lake la Ukonga kwenye mradi wa *peri-urban*.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Mwita Waitara atakubaliana na mimi tulifanya ziara katika maeneo hayo katika maeneo mbalimbali ambayo ndiyo imekuwa kivutio cha kuipigia kura Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi uliopita. Sasa kazi imeanza ya kupeleka umeme katika maeneo hayo kupitia *TANESCO* na kwa kupitia mradi wa peri-urban tuko katika hatua za kumpata mkandarasi na hivi karibuni kazi ambazo zimesalia katika maeneo mbalimbali zitakamilika. Hata baada ya Bunge hili pamoja na Mheshimiwa Mbunge tutawasha umeme katika maeneo ya Zingiziwa, Buyuni na Mbondole kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Shirika la Umeme la *TANESCO*. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa, nyumbani kumenoga. (*Makofi*)

Twendeni Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano swali la Mheshimiwa Lijualikali, Mbunge wa Kilombero.

Na. 12

Ujenzi wa Barabara ya Kidatu – Ifakara

MHE. PETER A. LIJUALIKALI aliuliza:-

(a) Je, ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara umefikia hatua gani?

(b) Je, barabara hii inatarajiwa kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA),** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali, Mbunge wa Kilombero lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kidatu-Ifakara yenye urefu wa kilometra 66.9 ni sehemu ya barabara ya Mikumi –

Ifakara – Mahenge/Lupiro – Kilosa kwa Mpepo – Londo Lumecha yenyeye urefu wa Kilometra 534.4 inayounganisha Mkao wa Morogoro na Ruvuma katika Mto Londo.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa ujenzi wa barabara hii seuemu ya Kidatu – Ifakara (kilomita 66.9) na daraja la Ruaha Mkuu (mita 130) ulisainiwa tarehe 24 Julai, 2017 kati ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na mkandarasi aitwaye *Reynolds Construction Company* kutoka nchini Nigeria kwa gharama ya Euro 40,441,890.81 bila VAT na inasimamiwa na Mhandisi Mshauri aitwaye Nicholas O,Dwyer Company Limited kutoka Ireland kwa gharama ya Euro 1,648,310.00 ambapo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika tarehe 2 Aprili, 2020.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa mkandarasi ameleta mitambo eneo la kazi kwa asilimia 90 na amekamilisha ujenzi wa kambi na maabara ya vifaa vya ujenzi kwa asilimia 100. Aidha, mkandarasi anaendelea na upimaji wa barabara, uhamishaji wa nguzo za umeme, simu na mabomba ya maji na kusafisha eneo la barabara pamoja na kujenga njia za mchepuo. Maandalizi ya eneo la kusaga kokoto na kufanya matengenezo ya kawaida ya barabara ya kutoka Kidatu hadi Ifakara ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

SPIKA: Mheshimiwa Lijualikali.

MHE. PETER A. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hii barabara inasuasua sana na ilisimama kwa takriban miezi minne mpaka mitano. Ikumbukwe kwamba Serikai illingia mkataba wa ujenzi na wahisani wa *EUna USAID* kwa masharti kwamba Serikali italipia gharama za fidia pamoja na kuruhusu mashine na vifaa vingine viingie nchini bila VATwala ushuru mwingine.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi ninavyokwambia tayari mashine zimeingia lakini zimeshikiliwa na *TRA*. *TRA* wanadai kwamba hawatambui mkataba kati ya Serikali na Hazina, wao wanataka fedha zao tu na hii imesababisha hii barabara iende kwa kususasua sana. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri

aniambie ni kwa nini *TRA* wanazishikilia mashine hizi wakati mkataba unaruhusu mashine ziingie bure? Hali hii inasababisha barabara iende kwa kususasua. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nijue kama itawezekana kwa yale madaraja ambayo yapo sasa hivi kama tunaweza tukayachukua tukayapeleka sehemu zingine zenye uhitaji hasa Mlimba na Kilombero kwa sababu sasa hivi huku kwetu barabara zile za mitaa ni mbovu sana. Kwa hiyo tunaomba baadhi ya haya madaraja yafanye kazi kwenye mitaa mingine. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Elias Kwandikwa majibu ya maswali hayo mawili tafadhali. Mheshimiwa Waziri, nimekuona, tafadhali majibu Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na barabara ya Ifakara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mgogoro uliokuwepo wa *interpretation* ya mikataba ukiwepo mkataba wa *European Union*, lakini pia Bunge hili lilipitisha msamaha wa *VAT mwaka jana*, kwa hiyo zile taratibu za Kanuni zilikuwa hazijakamilika. Kwa sasa tumeshamaliza kuchambua ule mkataba wa *European Union* pia na taratibu za *VAT* nazo zimekamilika. Kwa hiyo mgogoro huo Mheshimiwa Mbunge haupo tena ndiyo maana vile vifaa sasa vimetoka na mkandarasi anaanza kazi. Hilo tumelimaliza, hiyo sasa ni historia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwa yale madaraja ambayo yalikuwa yanatumika, baada ya kukamilisha sasa lile daraja kubwa la zege kiutaratibu yale madaraja huwa tunayapangia kwenda kujenga maeneo mengine kulingana na uhitaji. Kwa hiyo kama uhitaji utakuwepo na kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, nayo yatakuwa

considered kwa ajili ya kupeleka hayo madaraja ili pia yakatumike eneo hilo.

SPIKA: Nashukuru sana, tuendelee bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliiano. Swali la Mheshimiwa Hassan Selemani Kaunje Mbunge wa Lindi Mjini.

Na. 13

Upanuzi wa *Road Reserve*

MHE. HASSAN S. KAUNJE aliuliza:-

TANROADS ilifanya upanuzi wa *Road Reserve* tangu mwaka 2011 ambayo ilihuisha tathmini ya mali zilizopo kwenye maeneo husika:-

Je, ni lini wananchi wa Lindi watalipwa stahili zao?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliiano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za Mwaka 2009 iliongeza eneo la hifadhi ya barabara kutoka mita 22.5 mpaka mita 30 kwa barabara kuu na barabara za mikoa kutoka katikati ya barabara kila upande wa barabara. Kwa kuzingatia sheria ya zamani ya barabara (*highway Ordinance Cap. 167*) wananchi waliojenga ndani ya mita 22.5 kutoka katikati ya barabara wamevunja sheria hivyo Wizara kupitia *TANROADS* imekuwa ikichukua hatua ya kuweka alama za Xnyekundu na wananchi hao wanatakiwa waondoke eneo hilo na hawatalipiwa fidia yoyote kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika Wizara kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imechukua hatua ya kuweka kumbukumbu ya mali zote zilizopo ndani ya mita 7.5 zillizoongezeka kutoka eneo la hifadhi ya barabara la mita 22.5 hadi mita 30 kila upande wa barabara kwa kuziwekeea alama ya *X* ya kijani kwa ajili ya uthamini na malipo ya fidia endapo eneo hilo litahitajika hapo baadaye kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa barabara.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kaunje, swali la nyongeza.

MHE. HASSAN S. KAUNJE: Mheshimiwa Spika, ikikupendeza nina swali dogo la nyongeza. Kwanza nitoe pole kwa wananchi wa Ukerewe kutokana na ajali ya kivuko, lakini vile vile pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kunikubalia na kuniletea kivuko katika Jimbo langu baada ya kumwomba ndani ya siku 90. Swali langu dogo ni kwamba; kivuko kile kimekuwa na hitilafu za hapa na pale, je, Mheshimiwa Waziri yuko kwenye nafasi ya kuelezea usalama na uhakika wa kivuko kile? Ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa; Mheshimiwa Kaunje, swali lako hili na lile la msingi havina uhusiano kabisa, kwa hiyo hatutalipa nafasi ya majibu.

Waheshimiwa Wabunge nina mawili ya kuanzia kabla ya matangazo; la kwanza ni hili, kwamba tulikuwa tuko... Naomba tusikilizane Waheshimiwa, kule, nawaona wote kwenye kioo changu hapa.

Tulikuwa tuko likizo kidogo tumerudi, sasa kurudi kwenye kanuni zetu watu wanasa hau kidogo, kwa hiyo, ndiyo maana tunakumbushana kumbushana; swali lolote la nyongeza lazima liwe linaendana na swali la msingi kwa namna moja au nyingine.

La pili, Waheshimiwa Wabunge kuna maswali ambayo yana madai mazito sana; nikichukua swali kwa mfano la Mheshimiwa Genzabuke, ambalo haiwezekani

kama hayo mambo yapo Mbunge ukategemea kuja kuuliza swalii la nyongeza kwa Naibu Waziri Bungeni. Kama hayo mambo yapo ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa na sisi kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni lazima uwasiliane naye, lakini vile vile mimi kama Spika sina taarifa, hujaniambia kama kuna mambo mazito kiasi hicho yakawa yanatokea.

Hata hivyo, tatu, endapo jambo hilo ni kweli Kasulu ina Wabunge kadhaa wote wamekaa chini hawasemi, Mbunge wa Jimbo yuko kule hasemi hilo jambo, jirani yake yupo hajasema hilo jambo, kama kuna ukatili wa aina hiyo kweli. Kwa hiyo, kidogo inaweza kutuletea shida badaye na hasa mtu akisema kwamba, hebu kauli hii ifuatiliwe kwenye Kamati ya Maadili, utajikuta Mheshimiwa Mbunge unachukuliwa hatua bila sababu. Kwa hiyo, maswali yale menginemengine kwa kweli, hatutayaruhusu, tunataka vitu ambavyo vinaendana na kanuni zetu, unazungumza kitu ambacho ni cha uhakika, chenye kujenga nchi na kadhalika.

Lingine, ni lile ambalo tulinong'ona kidogo jana kule, mmeona kila jina la Mbunge, baada ya jina la anayeuliza swalii kuna bracket mbele ya jina. Kwa mfano, leo tumeanza na swalii la Mheshimiwa Esther Michael Mmasi, bracket yake imeandikwa Viti Maalum, hakuna neno lingine limeongezeka hivyo, ndivyo Bunge linavyomjua; hayo mengine ya kwake na chama chake. Mheshimiwa Abdallah Ali Mtalea, Temeke kwenye bracket, hivyo ndivyo ilivyo rasmi na kadhalika wote. Kwa hiyo, kwa maana ya meza hii ndio hivyo, kila jina lako linapoandikwa inaanndikwa na nafasi yako ambayo ndio inatambulika rasmi hapa Bungeni.

Sasa niende kwenye matangazo:-

Matangazo nianze na Wabunge ambaao walikuwa wanaumwa, sasa wamerudi humu Bungeni ni pamoja na Waheshimiwa wawili wote wa Makunduchi, Zanzibar.

Mheshimiwa Haji Ameir Haji, karibu sana na Mheshimiwa Ameir Timbe; Mheshimiwa Timbe yuko wapi?

Kule, ahsante sana. Tunashukuru sana kurudi kwako kwa sababu, alipata ajali ya gari na akalazwa Muhimbili kwa muda mrefu, tunashukuru kwamba, sasa hivi tuko naye. (*Makofi*)

Sasa wageni tuanze na Waheshimiwa, Mheshimiwa Mbunge wa Monduli kupitia Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Kalanga. Yeye wageni wake wanaongozwa na mke wake Sara, naomba usimame mama; wengine subirini kwanza tunamtaka Mama Sara peke yake, wengine kaeni, eeh, huyo hapo shemeji yetu huyo! Karibu sana! Karibu Bungeni. Ameavaa *traditional*, anapendeza kweli kweli, ahsante sana. Pia, ameambatana na Mwenyekiti wa Malaiguanaan, Mzee Lekisongo, eeh! Sasa huyu akishasema tena, nani anabisha kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Selasini mbona unaangalia nyuma? Angalia mbele, kanuni zinakataa kumpa mgongo Spika. Pia, yuko Katibu wa CCM Monduli. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, waliomsindikiza Mheshimiwa Kalanga zaidi ya 100 kutoka Monduli... (*Makofi*)

Mheshimiwa Selasini hebu tazama. (*Kicheko*)

Jamani karibuni sana kutoka Monduli, karibuni sana, Mbunge tumempokea. Huu ni ushahidi kwamba, kwa kweli, Mheshimiwa Kalanga anakubalika na CCM inakubalika, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Pia, tuna wageni wa Mheshimiwa Waitara ambao ni viongozi, Wanachama wa CCM na wananchi kutoka Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar-es-Salaam wakiongozwa na *M-NEC* kutoka Mkoa wa Dar-es-Salaam Ndugu Nassor Majid na Mwenyekiti wa CCM Ilala, Ndugu Ubaya Chuma.

Pia, tuna wageni 40 wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava. Wageni wa Mheshimiwa Mnzava? Karibuni sana, hawa wote wanatoka Korogwe, karibuni sana,

wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara Ndugu Alex Mnyeti. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, aah hebu simama tena Mheshimiwa Mnyeti, ahsante sana, yuko *Galleryya Spika*. Eeh, kuna watu wakisikia jina la Mnyeti hapa utawasikia tu, pamoja na baba mzazi wa Mheshimiwa Mzava Ndugu Paul Mzava, karibu sana. (*Kicheko/Makofi*)

Ninao wageni wangu 163 ambaao ni wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambaao ni wanafunzi 159 wa kidato cha sita na Walimu wanne wa kutoka Shule ya Sekondari ya Irumwe, Mkoani Mbeya, wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Shule Ndugu Maranatha Baraka. Wageni kutoka Mbeya! Karibuni sana na Makamu Mkuu wa Shule. Aaa! Mnapendeza kweli, hii shule ni lazima itakuwa ni moja ya shule bora kabisa. Ahsanteni sana na karibuni sana hapa Bungeni muweze kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi na Naibu Spika yupo anachapa kazi vizuri. (*Makofi*)

Wageni wanane wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambaao ni Makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Ilala, Mkoa wa Dar-es-Salaam, wakiongozwa na Ndugu Issa Bendera. Karibuni sana, wako pale juu. (*Makofi*)

Wageni 24 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira ambaao ni Viongozi wa Umoja wa Vijana kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Billy Chidambwa. Karibuni sana vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka hapa hapa Mkoa wa Dodoma. Huyu Ndugu Billy Chidambwa ndiye Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Mkoa wa Dodoma na timu nzima ambayo imetutembelea, karibu sana mjengoni. (*Makofi*)

Wageni 39 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaao ni Wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Fanuel Nzuzu. Wanamaombi? Natumaini watakuwa mahali.

Wageni 28 wa Mheshimiwa Zubeir Kuchauka ambaao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Liwale Mkoani

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Lindi wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya Ndugu Mohamed Kitura. Karibuni sana wageni wetu kutoka kule Liwale. (*Makof*)

Wako watu wanadai mke wa Mheshimiwa Waitara, Mama Waitara pale ulipo naomba usimame, yuko na mwanetu pale. Mama Waitara bado hujaonekana, hebu simama tena! Eeeh! Anapendeeza! (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni jamaa zake kutoka Kasulu. Wageni wa Mheshimiwa Genzabuke kutoka Kasulu karibuni sana, ahsante sana. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa. Karibuni sana. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambaye ni mdogo wake kutoka Ngara Mkoani Kagera, Ndugu Mwenge Godlaid. Karibu sana.

Nina tangazo, yale maswali mawili yaliyobaki tutayapangia wakati mwингine katika muda huu.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Kampuni ya *Vision Investment in a Yoratibu* mbio za *Dodoma Marathon* 10 hapa Bungeni kwa ajili ya kuandikisha Wabunge watakaoshiriki mbio za hisani, *Dodoma Marathon* ili kulitangaza Jiji la Dodoma pamoja na fursa zake.

Mbio hizo za hisani zitafanyika tarehe 10 Novemba, 2018 katika Uwanja wa Jamhuri kuelekea Barabara ya Arusha kuanzia Saa 12:30 asubuhi. Hizi ni mbio za hisani kwa hiyo si *marathon* ilee, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge ambao mtapenda kushiriki mbio hizi tunaombwa kujiorodhesha majina yetu pale mapokezi.

Naomba tena wale wanafunzi wangu kutoka Mbeya hebu simameni tena. Kuna sifa zenu nilikuwa sijalitajia Bunge hapa. Hawa wanafunzi hawa ni wa Shule ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi na ni wa kidato cha sita na wamefaulu wote, hongereni sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Naomba pia, niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa, katika Mkutano huu wa 13 wa Bunge la Kumi na Moja Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kushirikiana na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* watatao chanjo na elimu kuhusu homa ya ini (*Hepatitis B*) kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kipindi chote cha mkutano huu. Zoezi hili litaenda sambamba na upimaji wa maambukizi ya homa ya ini, sio maambukizi yale mengine, homa ya ini.

Chanjo ya homa ya ini hutolewa katika awamu tatu, awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu, ambapo kila awamu utapata dozi fulani ambapo baada ya dozi ya kwanza dozi ya pili hurudiwa baada ya mwezi mmoja na dozi ya tatu baada ya miezi sita.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa, dozi ya pili itakuwa mwezi Disemba, 2018 na kwa kuwa, katika kipindi hicho hatutakuwa na shughuli za Bunge hapa Dodoma hivyo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) utaandaa vituo viwili ambavyo kwa Dodoma huduma hii itatolewa katika Kituo cha Afya cha Bunge na Dar-es-Salaam itakuwa katika Taasisi ya Saratani (*Ocean Road*), tafadhalii Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria zoezi hili muhimu bila kukosa. Jambo hili ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Anna Lupembe anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria ibada katika eneo la *Chapel* yetu ya Pius Msekwa, ghorofa ya pili, saa saba mchana leo. Tutashirikiana na Wanamaombi ambaao wapo hapa Bungeni leo.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria Kwa Ajili ya Kutunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Kwa Ajili ya Kuweka Utaratibu wa Utoaji Leseni, Kudhibiti, Kufuatilia na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo za Fedha Pamoja na Mambo yanayohusiana na Hayo (*A Bill for An Act to Make Provisions for Licensing, Regulation and Supervision of Microfinance Business and to Provide for Other Related Matters*)

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

SPIKA: Baada ya Muswada huu kusomwa mara ya kwanza, tutaupeleka kwenye Kamati ya Bajeti ya Bunge ili waweze kuushughulikia kwa haraka iwezekanavyo, wakishirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ili katika Mkutano huu tuweze kujadili sheria hii inayopendekezwa; Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha.

SPIKA: Wheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nimesikia kelele nyingi sana huku wakisema Mheshimiwa Kuchauka vipi?

Naomba Mama Kuchauka nimirambulishie hapa, naomba asimame anyoshe mikono. Mama Kuchauka, eeh. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, mimi niombe Mwongozo. Kabisa hii.

SPIKA: Yuko pale. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Ahsante, endelea.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, hili Bunge lina utaratibu na tunapokuwa tumealika pengine familia na wageni mbalimbali wanakuja kujifunza Bungeni. Sasa kuna maneno yanazungumzwa na Wabunge kwa kweli, ni ya faragha ambayo yanadhalilisha watu wengine. Kwa mfano, umemsimamisha mke wa Waitara, Wabunge wa Upinzani wanasema ana mke wa Dodoma, tutavunjiana ndoa kwa *design* hii. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: We acha uoga huo.

MHE. MUSUKUMA J. KASHEKU: Mheshimiwa Spika, humu ndani kuna watu wameoana hatuzungumzi. Sasa ni vizuri tukawekeana mipaka, ili kuheshimu hawa watu wageni kwa sababu, humu kuna watu wameolewa wengine na mwanaume mmoja wako wanane hatujawahi kuwataja humu ndani. Sasa ni vizuri tukawa na heshima tunapowaalika wageni wetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Muongozo wako.

MBUNGE FULANI: Umekoleza.

MHE. PASCHAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) Kuhusu jambo lililotokea leo mapema hapa Bungeni wakati swalii namba tisa linaulizwa, kuna Mbunge alijaribu kutoa tuhuma nzito sana kuhusu mambo yanayofanywa na *TFS*, watu kutobolewa miguu, kupokonywa pikipiki na kufanyiwa matendo mengine mabaya...

SPIKA: Swalii hilo nimelitoa sasa unalirudishaje tena kwenye *floor?* Tunaendelea na shughuli Mheshimiwa, nililitoa hilo swalii sasa huwezi kuliingiza tena kiaina dirishani.

MHE. PASCHAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusikia.

SPIKA: Nimelitoa kwa taarifa yako. Katibu.

NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa
Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali Pamoja na
Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya
Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, karibu sana Mheshimiwa Dkt. Mpango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, ijadili na kutoa maoni na ushauri kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na kuboresha mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kinachowasilishwa sasa mbele ya Bunge lako Tukufu ni kwa mujibu wa kifungu cha 94 cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016 kinachoelekeza Serikali kuwasilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kinajumuisha mapitio ya hali ya uchumi, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/2018 na robo ya kwanza ya 2018/2019, maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2019/2020, ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka ujao, mfumo wa ufuutiliaji tathmini na utoaji taarifa na vihatarishi vyatuekelezaji wa mpango. Aidha, tumeambatisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka

mitatu ya kwanza ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano yaani mwaka 2016/2017 mpaka mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali 2019/2020 mpaka 2021/2022 kimeainisha masuala muhimu ambayo yanatakiwa kuzingatiwa na Wizara, idara zinazojitegemea, wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wakati wa kuandaa bajeti zao za mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya ninayoyawasilisha yamezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 mpaka 2020/2021), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile maandalizi ya mapendekezo ya mpango na mwongozo yamezingatia sera, mikakati na programu mbalimbali za maendeleo ya kisekta zikiwemo Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo awamu ya pili, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Programu ya Sekta ya Afya, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2016, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021, Mkakati Jumuishi wa Kuendeleza Viwanda wa Mwaka 2025 na Mpango Kabambe wa Sekta ya Utalii wa Mwaka 2006. Hivyo, ni vyema Waheshimiwa Wabunge watakaposoma vitabu vya mwongozo na mapendekezo ya mpango warejee pia mikakati na programu za kisekta.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa ushauri na maoni yatakayotolewa katika Kikao hiki cha Bunge yatazingatiwa kikamilifu katika kuandaa Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa 2019/2020 ambao utawasilishwa Bungeni tarehe 11 Machi 2019 kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, ushauri wa Waheshimiwa Wabunge utatumika kuboresha mwongozo wa kuandaa mpango na bajeti ya Serikali ya

mwaka 2019/2020. Hivyo, nawasihi Waheshimiwa Wabunge katika nafasi yenu ya uwakilishi wa wananchi mtumie weledi na uzoefu wenu katika kutoa maoni na ushauri kuhusu maeneo muhimu ya miradi inayopaswa kuzingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Viashairia vya Uchumi. Aya ya saba hadi ya 15 ya kitabu cha hotuba yangu zinaelezea mwenendo wa viashiria vya uchumi kidunia, kikanda na kwa Tanzania. Naomba nипитие aya hizo kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, mwenendo unaonesha kuwa Tanzania ni mionganini mwa nchi zinaofanya vizuri. Katika mwaka 2017 pato la Taifa limeendelea kukua kwa kiwango cha asilimia 7.1 ikillinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2016 na kuongoza ukuaji katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2018, Pato halisi la Taifa lilikuwa kwa asilimia 8.4 ikillinganishwa na asilimia 5.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Shughuli za kiuchumi ambazo ziliikuwa kwa kiwango kikubwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2018 ni pamoja na ujenzi ambayo ilikuwa kwa asilimia 20, habari na mawasiliano asilimia 18.3, usafirishaji na uhifadhi wa mizigo 9.2% na kilimo 7.1%.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei uliendelea kushuka na kuwa chini ya asilimia tano (5) kwa takribani ya kipindi chote cha mwaka 2017/2018. Kwa upande wa sekta ya nje; mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalikuwa dola za Marekani milioni 8,949.4 ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.8 kutoka mwaka 2016/2017. Hii ilitokana na ongezeko la thamani ya mauzo ya mazao ya korosho, karafuu, tumbaku, chai na mkonge pamoja na kuimarika kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,483.9 mwishoni mwezi Juni, 2018 sawa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 5.6. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kuwa tulivu ikibadilishwa kwa wastani wa kati ya Sh.2,231.17 na Sh.2,264.97 kwa dola moja ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa lilifikia dola za Marekani milioni 27,774.86 Juni, 2018. Uchambuzi wa deni la Taifa unaonesha kuwa deni hilo ni himilivu ambapo viashiria vyote veya athari za madeni vimeendelea kuwa chini ya ukomo wa hatari unaokubalika kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hali ya ustawi wa jamii imeendelea kuimarika kutokana na ukuaji wa uchumi ambao kwa kiasi kikubwa umechangia kupungua kwa umaskini na hali hii inadhihirishwa na utafiti ambao ulifanywa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia mwaka 2015/2016 ambao ulionesha kuwa idadi ya Watanzania wanaoishi chini ya mstari wa umaskini ilipungua kufikia asilimia 26.3 ikilinganishwa na asilimia 28.2 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa utafiti mpya wa matumizi ya kaya binafsi unaendelea hivi sasa na utafiti huo unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2019 na kutupatia hali halisi ya viwango veya umaskini nchini. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa Tanzania umeongekeza kufikia wastani wa miaka 64.3 mwaka 2017 na unatarajiwa kuongezeka hadi wastani wa miaka 64.9 mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, vile vile, hali ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula nchini kwetu imeendelea kuimarika ambapo kwa Mwaka 2017/2018 uzalishaji ulifikia tani milioni 15.9 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.3. Hivyo, nchi ilijitosheleza kwa chakula kwa asilimia 120.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa baadhi ya viashiria veya sekta ya kibenki umeendelea kuimarika baada ya Serikali kuchukua hatua za kuongeza ukwasi. Kufuatia hatua hizo, mikopo kwa sekta binafsi imeanza kuonesha mwenendo unaoridhisha ambapo hadi Juni, 2018 mikopo hiyo ilikua kwa asilimia 4.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.3 Juni, 2017. Maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria veya uchumi yanapatikana katika sura ya pili, sehemu ya kwanza ya kitabu cha mwongozo na sura ya pili ya kitabu cha mapendekezo ya mpango.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018. Mapato ya ndani katika mwaka 2017/2018, yalifkia shilingi triliioni 17.9 sawa na asilimia 90 ya lengo la shilingi triliioni 19.9. Kati ya fedha hizo, shilingi triliioni 15.1 zilitokana na mapato ya kodi, sawa na asilimia 89 ya lengo; shilingi triliioni 2.2 zilitokana na mapato yasiyo ya kodi, sawa na asilimia 101 ya lengo na shilingi bilioni 541.5 zilitokana na mapato ya ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, sawa na asilimia 79 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo nafuu iliyotolewa ilikuwa shilingi triliioni 2.46 sawa na asilimia 62 ya makadirio ya shilingi triliioni 3.97. Mikopo iliyopatikana kutoka ndani na nje ni shilingi triliioni 7.0 sawa na asilimia 90.9 ya lengo la shilingi bilioni 7.76. Kati ya mikopo hiyo, shilingi triliioni 1.35 ni kutoka vyanzo vya nje na shilingi triliioni 5.70 ni kutoka vyanzo vya masoko ya ndani. Kati ya mikopo ya ndani, shilingi triliioni 4.83 zimetumika kulipa mtaji wa deni la ndani (*Rollover*) na Shilingi bilioni 869.2 ni mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, matumizi halisi ya Serikali yalifkia shilingi triliioni 25.32 sawa na asilimia 80 ya bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi triliioni 31.71. Kati ya kiasi hicho, shilingi triliioni 18.77 zilikuwa ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia 93 ya lengo la shilingi triliioni 20.27 na shilingi triliioni 6.54 zilikuwa ni matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 57 ya bajeti ya shilingi triliioni 11.43. Matumizi ya fedha za maendeleo hayajumuishi baadhi ya fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja (*D-funds*) kwenye utekelezaji wa miradi ambazo hazikupita kwenye Mfumo wa Malipo wa Serikali. Fedha hizo zitajumuishwa pindi taratibu za kiuhasibu zitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi ya Maendeleo Mwaka 2017/2018 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2018/2019. Aya ya 19 ya kitabu cha hotuba imeelezea kwa kifupi baadhi ya miradi iliyotekelzwa katika kipindi cha mwaka 2017/2018 na robo ya kwanza ya mwaka 2018/2019

ambapo Serikali ilitekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo yafuatayo:-

Viwanda, nishati, uchukuzi, barabara, mawasiliano, elimu, afya, maji, madini, kilimo, utalii na utawala bora. Aidha, taarifa za kina za utekelezaji wa miradi hiyo zimeainishwa katika sehemu ya kwanzza ya Kitabu cha Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali (sura ya kwanzza) na Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 (sura ya tatu).

Mheshimiwa Spika, Mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha 2016/2017 – 2018/2019. Yapo mafanikio mengi yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya kwanzza ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano (2016/2017 – 2018/2019). Mafanikio hayo yanajumuisha yafuatayo:-

(i) Ukuaji wa uchumi. Hapa ni kuendelea kuimariika kwa uchumi wa Taifa, ambapo uchumi ulikuwa kwa wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2017 kutoka ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2016 na mfumuko wa bei kuendelea kupungua na kuwa katika wastani wa kiwango cha tarakimu moja, chini ya asilimia 5.0.

(ii) Mapato ya kodi yaliongezeka kutoka shilingi triliioni 12.43 mwaka 2015/2016 hadi shilingi triliioni 15.19 mwaka 2017/2018 na mapato yasiyo ya kodi yaliongezeka pia kutoka shilingi triliioni 1.18 mwaka 2015/2016 hadi shilingi triliioni 2.21 mwaka 2017/2018. Aidha, ongezeko la mapato yasiyo ya kodi lilitokana na kuimariika kwa ufuutilaji na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato hususan Wizara ya Madini ambayo mapato yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 207.9 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 301.2 mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina mapato yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 243.4 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 803.5 mwaka 2017/2018. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mapato yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 73.3 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni

92.2 mwaka 2017/2018; Idara ya Uhamiaji kutoka shilingi bilioni 115.3 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 159.3 mwaka 2017/2018.

(iii) Upande wa Ulipaji wa Madai. Serikali ililipa jumla ya shilingi triliomni 2.28 za madai yaliyohakikiwa ya Wakandarasi, watoa huduma, Wazabuni, watumishi wa umma na madai mengineyo. Kati ya kiasi hicho, shilingi triliomni 1.61 zililipwa kwa wakandarasi, shilingi bilioni 144.6 kwa watoa huduma, shilingi bilioni 818.3 kwa wazabuni, shilingi bilioni 285.9 kwa watumishi wa umma na shilingi bilioni 29.1 kwa madai mengineyo.

(iv) Barabara. Mtandao wa barabara kuu za lami uliongezekwa kutoka kilomita 7,646 Juni 2016 hadi kilomita 8,298.12 Juni 2018 na mtandao wa barabara za mikoa nao uliongezekwa kutoka kilomita 1,398 hadi kilomita 1,687 kwa kipindi hicho. Aidha, ujenzi wa Barabara ya Juu ya *Mfugale Flyover* pale *TAZARA* ulikamilika na kuanza kutumika na ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo unaendelea.

(v) Reli; ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* umeanza, ambapo kwa awamu ya kwanza ya Dar es Salaam – Morogoro (kilomita 300) ujenzi umefikia asilimia 24. Maandalizi ya ujenzi kwa sehemu ya Morogoro – Makutupora (kilomita 422) nayo yameanza. Faida zitakazotokana na kukamilika kwa reli hii ni pamoja na kupungua kwa muda wa kusafirisha abiria na mizigo, kuongezeka kwa kiwango cha usafirishaji wa abiria na mizigo, kuongezeka kwa mapato ya Serikali, kuongezeka kwa fursa za ajira na kupanuka kwa biashara katika vijiji na miji inayopitiwa na reli hiyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali imeendelea kuboresha reli ya kati inayotumika sasa ambapo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuwezesha usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari ya Mwanza kwenda Bandari ya *Port Bell* – Uganda ambapo katika mwaka 2017/2018 wastani wa shehena ya mizigo ilikuwa tani 200,000 ambayo ilisafirishwa kwenda huko Uganda. (*Makofii*)

(vi) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania. Ndege mpya tatu aina ya *Bombadier Q400* na moja aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* zilinunuliwa na kuanza kufanya kazi. Vilevile sehemu ya malipo ya ndege mbili aina ya *A220-300* zinazotarajiwa kuwasili Novemba, 2018 na moja aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* inayotarajiwa kuwasili mwaka 2020 yamefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutohana na kuboreshwa kwa *ATCL*, idadi ya mikoa inayohudumiwa na ndege za *ATCL* imeongezeka na kufikia kumi. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Kagera, Mbeya, Kigoma, Ruvuma, Mtwara, Dodoma, Tabora, Kilimanjaro na Mwanza. Aidha, Shirika pia linatoa huduma Zanzibar. Vilevile shirika limeanzisha ofisi katika Miji ya Mumbai, Bujumbura, Guangzhou na Entebbe. (*Makofii*)

(vii) Viwanja vya ndege. Kwanza ni ujenzi wa jengo la tatu la abiria na miundombini yake katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ambaao umefikia asilimia 78. Aidha, upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza umefikia asilimia 70 na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro umekamilika. Upanuzi huu umewezesha kuongezeka kwa abiria na mizigo, mapato ya Serikali, ajira, biashara za hoteli na maduka na idadi ya watalii.

(viii) Bandari. Mafanikio yaliyopatikana ni ujenzi wa gati la kupakua na kupakia magari na upanuzi wa gati Na.1 katika Bandari ya Dar es Salaam ambaao umefikia asilimia 35; upanuzi wa Bandari za Tanga na Mtwara asilimia 76 na asilimia 30 kwa mtiririko huo. Pia kukamilika kwa ujenzi kutawezesha kuongezeka kwa uwezo wa bandari kuhudumia magari kati ya 300,000 na 500,000 kwa mwaka; kupungua kwa muda wa kupakua magari na hivyo kuongeza ufanisi wa bandari; kuongezeka kwa mapato ya Serikali na kuhimili ushindani kutoka bandari za nchi jirani.

(ix) Mafanikio mengine yalikuwa upande wa kilimo. Kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo kiliongezeka kufikia asilimia 7.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2016. Ukuaji huu umewezesha kuongezeka kwa usalama wa

chakula; kupungua kwa mfumuko wa bei ya chakula kufikia asilimia 3.8 Juni 2018 ikilinganishwa na asilimia 9.8 Juni 2017; na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi kutoka dola za Marekani milioni 866.4 mwaka 2016/2017 kufikia dola za Marekani milioni 1,152.4 mwaka 2017/2018, sawa na ongezeko la asilimia 33. (*Makofi*)

Vilevile, upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka na kufikia tani 51,700.5 mwaka 2017/2018 kutoka tani 36,482 mwaka 2015/2016 na tani 435,178 za mbolea zilinunuliwa na kusambazwa katika mwaka 2017/2018 ikilinganishwa na tani 302,450 zilizonunuliwa katika mwaka 2015/2016. Aidha, katika kuimarisha ushirika na masoko ya mazao, vyama vya ushirika viliongezeka kutoka 7,888 mwaka 2015 hadi 10,990 mwaka 2017. (*Makofi*)

(x) Huduma za afya. Mafanikio yaliyopatikana ni kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa hospitali 10 za wilaya, vituo vya afya 295 na nyumba za watumishi wa afya 306. Aidha, bajeti ya ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi iliongezeka kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 269 mwaka 2017/2018. Pia kuanza kutoa huduma ya kupandikiza figo kwa wagonjwa 28 na hivyo kupunguza gharama kwa wastani kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 20 kwa mgonjwa mmoja endapo angepelekwa nje ya nchi.

Vilevile, Serikali imeanzisha huduma ya kupandikiza vifaa vya kusikia kwa watoto ambapo jumla ya watoto 11 wamepatiwa huduma hiyo na hivyo kuokoa shilingi milioni 64 kwa mtoto mmoja endapo angepata huduma hii nje ya nchi.

(xi) Nishati. Mafanikio yaliyopatikana ni uzalishaji wa umeme kuongezeka kutoka MWh 6,950,280 mwaka 2016/2017 hadi MWh 7,010,590 mwaka 2017/2018 ambao umewezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuongezeka kwa idadi ya wananchi walionunganishiwa umeme ambapo hadi kufikia Oktoba 2018 jumla ya vijiji 5,181

tayari vimeunganishiwa umeme. Aidha, shughuli za kiuchumi pia zimeongezeka. Pia ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji Mto Rufiji MW 2,100 umeanza. Pia, maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kusafirishia Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga yamekamilika.

(xii) Huduma za maji. Miradi 1,595 ya maji vijijiini imekamilika, ikiwa na jumla ya vituo vyatukio vya kuchotea maji 126,110 na uwezo wa kuhudumia wananchi 31,652,500.

(xiii) Viwanda. Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa azma yake ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo viwanda vipyta zaidi ya 3,306 vilijengwa katika mikoa mbalimbali ikijumuisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za ujenzi hasa saruji, marumaru na nondo lakini pia upande wa kilimo; kusindika matunda, mafuta na ngozi. Ujenzi wa viwanda vipyta umechangia kupatikana kwa ajira mpya 482,601 mwaka 2017/2018.

(xiv) Kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma. Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka katika Jiji la Dar es Salaam kuja hapa katika Jiji la Dodoma ambapo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na watumishi wa umma 6,531 kutoka Wizara zote wamehamia Dodoma. Aidha, inatarajiwa kuwa Mheshimiwa Rais atahamia rasmi Dodoma kabla ya tarehe 31 Desemba, 2018. (*Makofii*)

(xv) Kwa upande wa madini, Sheria za Madini zilifanyiwa mapitio ili kuiwezesha nchi yetu kunufaika zaidi na rasilimali za madini. Aidha, Serikali ilikamilisha ujenzi wa ukuta wenye mzingo wa kilometra 24.5 kuzunguka Mgodi ya Tanzanite Mererani ambaa umeweza kipunguza utoroshwaji wa madini.

Mheshimiwa S[rika, juhudhi hizi na nyinginezo zimewezesha kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli yanayotokana na madini kufikia shilingi bilioni 301.2 mwaka 2017/2018 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 194.4.

(xvi) Upande wa elimu, Serikali ya Awamu ya Tano ilianzisha na imeendelea kutekeleza utaratibu wa kutoa elimu msingi nchini bila ada ambapo Serikali imekuwa ikitoa shilingi bilioni 20.9 kila mwezi. Juhudi hizi zimechangia ongezeko la wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza kutoka 1,568,378 mwaka 2015 hadi 2,078,379 mwaka 2018 na kidato cha kwanza kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 562,695 mwaka 2017.

(xvii) Usafiri wa majini. Serikali iliendelea kujenga na kukarabati meli na vivuko katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kazi hizi zitarahisisha na kuongeza uwezo wa usafirishaji wa abiria na mizigo. Aidha, uwezo wa meli hizo ni kama ifuatavyo: Meli mpya katika Ziwa Victoria itabeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo; meli katika Ziwa Nyasa itabeba abiria 200 na mizigo tani 200; na ile ya Ziwa Tanganyika abiria 600 na tani 400 za mizigo.

Mheshimiwa Spika, changamoto za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na bajeti na hatua za kukabiliana nazo. Changamoto kubwa zilizojitokeza katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2017/2018, ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Ugumu wa kusanya kodi kutoka kwa wafanyakishara waliopo katika sekta isyo rasmi kwa kuwa hawana sehemu rasmi na za kudumu za kufanya biashara na hawatunzi kumbukumbu.

(ii) Kutofikiwa kwa lengo la kodi zinazotokana na ajira (*Pay As You Earn*) kulikosababishwa na kutofikiwa kwa malengo ya ajira mpya na kutoongezeka kwa mishahara kwa wafanyakazi kama ilivyokuwa imetarajiwaa. Vilevile, kodi hizi zimeathirika kutokana na kupunguzwa kazi kwa wafanyakazi kwenye migodi ya madini kufuatia kupungua kwa shughuli za uchimbaji wa madini kwa baadhi ya migodi.

(iii) Kushuka kwa biashara za kimataifa kulikopelekea kutofikia malengo ya uingizwaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kama ilivyokuwa imetarajiwaa.

(iv) Upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, hivyo kupunguza ufanisi kwa utendaji kazi wa Mamlaka.

(v) Kupungua kwa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo wakati wa utekelezaji wa bajeti.

(vi) Changamoto ya masoko na bei ndogo za mazao kwa wakulima; na

(vii) Kuendelea kuwepo kwa madai mbalimbali yakiwemo ya wakandarasi, watoa huduma, wazabuni na watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza mapato, Serikali imechukua hatua mbalimbali, ikiwa pamoja na:-

(i) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi na utoaji wa elimu kwa walipakodi ili kuongeza mwamko wa kulipa kodi;

(ii) Kuimarisha mifumo na taasisi zinazokusanya mapato ili kudhibiti ukwepajji kodi na uvujaji wa mapato ya Serikali;

(iii) Kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara na uwekezaji wa sekta binafsi; na

(iv) Kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kuititia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (*Development Corporation Framework*).

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020. Misingi iliyozingatiwa katika kuweka malengo ya uchumi jumla ni pamoja na:-

- (i) Uwepo wa amani, usalama, utulivu na umoja hapa nchini na katika nchi jirani;
- (ii) Kuimarika kwa viashiria vyatya uchumi jumla na maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
- (iii) Kutengamaa kwa uchumi wa dunia; na
- (iv) Utulivu wa bei za mafuta katika soko la dunia na hali nzuri ya hewa.

Mheshimiwa Spika, shabaha na malengo ya uchumi jumla. Shabaha na malengo ya uchumi jumla ambayo yanatokana na takwimu mpya za mwaka wa kizio wa 2015 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa kufikia asilimia 7.3 mwaka 2019 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 7.2 mwaka 2018 na kuongezeka kwa wastani wa asilimia 7.6 katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/2020 – 2021/2022).
- (ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 5 katika Kipindi hicho cha Muda wa Kati.
- (iii) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.7 ya Pato la Taifa mwaka 2019/2020 kutoka matarajio ya asilimia 12.5 mwaka 2018/2019 na wastani wa asilimia 12.9 katika Kipindi cha Muda wa Kati.
- (iv) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 21.1 ya Pato la Taifa mwaka 2019/2020 na kufikia wastani wa asilimia 20.2 katika Kipindi cha Muda wa Kati.
- (v) Kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kutoka matarajio ya asilimia 2.9 mwaka 2018/2019 hadi wastani wa asilimia 1.1 katika Kipindi cha Muda wa Kati;

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.5 katika Kipindi cha Muda wa Kati.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Awali wa Mapato na Matumizi ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/2020 – 2021/22). Mapato ya ndani (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi trillioni 23.20 mwaka 2019/2020 kutoka shilingi trillioni 20.89 mwaka 2018/2019 na kukadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 10.1 katika kipindi cha muda wa kati hadi shilingi trillioni 28.11 mwaka 2021/2022. Mapato ya ndani katika Pato la Taifa yanakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 14.6 mwaka 2019/2020 hadi asilimia 14.9 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 11.8 hadi shilingi trillioni 21.12 mwaka 2019/2020 kutoka shilingi trillioni 18.00 mwaka 2018/2019 na kukua kwa wastani wa asilimia 10.1 katika kipindi cha muda wa kati hadi shilingi trillioni 24.38 mwaka 2021/2022. Uwiano wa mapato ya kodi na Pato la Taifa unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 12.7 mwaka 2019/2020 hadi asilimia 12.9 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, mapato yasiyo ya kodi (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadariwa kuongezeka hadi shilingi trillioni 3.08 mwaka 2019/2020 kutoka shilingi trillioni 2.89 mwaka 2018/2019. Aidha, mapato yasiyo ya kodi (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 10 na kufikia shilingi trillioni 3.72 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo nafuu inatarajiwa kupungua kutoka shilingi trillioni 3.38 mwaka 2019/2020 hadi shilingi trillioni 3.28 mwaka 2021/2022. Mikopo kutoka nje na ndani (*ikijumuisha rollover*) inatarajiwa kuwa shilingi trillioni 6.91 mwaka 2019/2020 na shilingi trillioni 6.76 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kukua hadi shilingi trillioni 33.5 (asilimia 21.1 ya Pato la Taifa) mwaka 2019/2020 kutoka shilingi trillioni 32.47 ambayo ni asilimia 22.5 ya Pato la Taifa mwaka 2018/2019 na kukadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.7 hadi shilingi trillioni 38.17 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, mishahara (ikijumuisha mishahara ya taasisi) inakadiriwa kuwa shilingi trillioni 7.55 na kukadiriwa kuongezeka hadi shilingi trillioni 8.42 mwaka 2021/2022. Malipo ya riba na mtaji kwa deni la ndani na nje yanakadiriwa kuwa shilingi trillioni 8.62 mwaka 2019/2020 na kuongezeka hadi shilingi trillioni 11.02 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha kulipia bidhaa, huduma na ruzuku kinakadiriwa kuwa shilingi trillioni 4.93 mwaka 2019/2020 na kuongezeka hadi shilingi trillioni 5.16 mwaka 2021/2022. Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa shilingi trillioni 12.38 ambayo ni asilimia 7.8 ya Pato la Taifa mwaka 2019/2020 na kuongezeka hadi shilingi trillioni 13.55 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, maelekezo mahsusii ya mwongozo. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye mwongozo na kusimamia Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake. Aidha, Kamati za Mipango na Bajeti za kila Fungu zinatakiwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 17(3) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Mwongozo umebainisha masuala muhimu ambayo hayana budi kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji wa mipango, bajeti na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahitaji ya Rasilimali Fedha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:-

(i) Wahakikishe kuwa makusanyo yote yanawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

(ii) Kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa kukusanya mapato;

(iii) Kubuni vyanzo vinya mapato ikiwa ni pamoja na vile vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021;

(iv) Kutoingia mikataba yenyeye vifungu vinavyotoa misamaha ya kodi bila kupata ridhaa ya Waziri wa Fedha na Mipango; na

(v) Kuhakikisha kuwa kampuni zote ambazo Serikali ina hisa zinaendeshwa kwa ufanisi na hivyo kutoa gawio stahiki kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa udhibiti katika Matumizi ya Fedha za Umma, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:-

(i) Kuhakikisha thamani halisi ya fedha inazingatiwa katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi kwa kuzingatia misingi ya Kanuni za Ununuzi wa Umma kama *Force Account*, ununuzi wa pamoja na ushindanishwaji wa zabuni;

(ii) Kutumia TEHAMA katika mawasiliano Serikalini, kama vile majalada ya kielektroniki kwa lengo la kupunguza gharama za kuongeza ufanisi;

(iii) Kuhakikisha hati za madai na mikataba ya watoa huduma wa ndani inakuwa katika Shilingi ya Tanzania ili kupunguza athari za mabadiliko ya viwango vya ubadilishanaji fedha;

(iv) Kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi hasa kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani;

(v) Kutenga fedha za kulipa madeni yaliyohakikiwa kwa kutumia Ukomo wa Bajeti uliotolewa;

(vi) Taasisi na Mashirika ya Umma yenyе uhitaji wa mikopo kuhakikisha zinapata kibali kutoka kwa Waziri wa Fedha na Mipango kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134 pamoja na Kifungu cha 60(4) na 62(b) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufuatilia kwa ukaribu mikataba yenyе dhamana ili kuepuka madeni sanjari.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:-

(i) Kuhakikisha kuwa Taasisi na Mashirika ya Umma yanachangia asilimia 15 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura 370, ikijumuisha ziada na itolewe kwa wakati;

(ii) Kuimarisha ufuatilaji wa Hisa za Serikali katika kampuni ambazo Serikali ina hisa chache;

(iii) Kuhakikisha Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibashara yanaandaa Mwongozo wa Gawio utakaotoa utaratibu wa malipo ya gawio kwa Serikali;

(iv) Kuchambua taarifa za fedha na mwenendo wa Taasisi na Mashirika ya Umma na kupendekeza hatua stahiki za kuboresha, kuunganisha au kuyafuta kwenye daftari la Msajili wa Hazina; na

(v) Kufuatilia viwanda na mashamba yaliyobinafsishwa ili kubaini kama yanaendeshwa kuendana na mikataba ya mauzo na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kurejesha Serikalini mashamba na viwanda ambavyo wamiliki watabainika kukiuka mikataba ya mauzo.

Mheshimiwa Spika, maelekezo mahsusini ya Mwongozo yameainishwa kwa kina katika Sura ya Kwanza, Sehemu ya Pili ya Kitabu cha Mwongozo.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020. Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka ujao wa fedha yameainisha maeneo ya kipaumbele yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2019/2020. Maeneo hayo yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango huu. Maeneo hayo ni yafuatayo:-

(i) Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda. Ujenzi wa viwanda ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi Ruvuma, Mtwara, Kigoma na Bagamoyo; Kukuza kilimo cha mazao, Mifugo na Uvuvi; Maliasili za madini, misitu na wanyamaporii; Utalii, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa kipekee wa sekta ya kilimo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na kwa ustawi wa wananchi wetu, Serikali itaweka msukumo zaidi katika uendelezaji wa sekta hii kwa kutekeleza mikakati ya programu mbalimbali hususan ASDP II, uboreshaji wa masoko ya bidhaa za kilimo na uimarishaji wa bei za mazao ya kilimo.

(ii) Ujenzi wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji. Kipaumbele kitatolewa kwa miradi ifuatayo: Nishati, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mtambo wa kufua umeme katika Mto Rufiji; Maendeleo ya reli ikijumuisha ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* na usafiri wa anga ikiwemo kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania. Aidha, maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na barabara, madaraja, bandari, usafiri wa majini, teknolojia ya habari na mawasiliano, ardhi na maeneo ya uwekezaji na biashara, huduma za fedha na ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Vilevile, Serikali

itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo yaliyotolewa katika Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara nchini wa Mwaka 2010 ikiwa ni pamoja na kusimamia mapendekezo yaliyopo kwenye *Blueprint on Policy and Regulatory Reforms*.

(iii) Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya watu. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni elimu na ujuzi hususan kusomesha kwa wingi wataalam kwenye fani na ujuzi adimu, afya na ustawi wa jamii, maji na usafi wa mazingira, vijana, ajira na wenye ulemavu, habari, utamaduni, sanaa na michezo, utawala bora na huduma bora kwa wananchi, hifadhi ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuimarisha utawala bora ili kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, Serikali itaendelea kujenga miundombinu wezeshi hususan ofisi, makazi na huduma ya jamii katika Makao Makuu ya nchi Jijiini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, vilevile, msukumo zaidi utawekwa katika kuongeza na kuboresha huduma ya maji, kuunga mkono juhudzi za wananchi kukamilisha maboma ya afya na elimu na kujenga mazingira ambayo yatawezesha matumizi ya teknolojia ya kisasa kwenye utoaji wa huduma za elimu na afya kama vile upelekaji wa dawa kwa kutumia ndege zisizo na rubani (*drones*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Serikali imeanza kuandaa Muswada wa Sheria ya Maji ambao pamoja na mambo mengine unapendekeza kuanzhishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini ili kuongeza kasi ya kuondoa kero ya maji kwa wananchi;

(iv) Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango. Miiongoni mwa masuala yatakayopewa msukumo ni pamoja na upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na kwa riba nafuu, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na usimamizi

wa matumizi na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Maeneo mengine ni yale ya kujenga mazingira wezeshi hususan, umoja wa kitaifa, ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo na ulinzi wa rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kushirikisha sekta binafsi mwaka ujao wa fedha. Sekta binafsi inatarajia kuongeza uwekezaji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo hususan katika maeneo ya kipaumbele ikiwemo viwanda vya nguo, dawa za binadamu, bidhaa za ngozi, usindikaji wa vyakula, mafuta, ujenzi wa miundombinu wezeshi, huduma kwa jamii, huduma za fedha, huduma za utalii na kuanzisha na kuendeleza maeneo ya viwanda na maeneo ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kuititia utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Maboresho hayo yamepelekea kuundwa kwa miongozo ya kisera, kisheria na kitaasisi ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa Sera ya Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Kwa msingi huo, miradi ya ubia inayopendekezwa kutekelezwa ni pamoja na ifuatayo:-

- (i) Mradi wa Kusambaza Gesi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara;
- (ii) Mradi wa kujenga hosteli ya wanafunzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) – Dar es Salaam;
- (iii) Ujenzi wa vyuo kumi vya Ufundidi Stadi;
- (iv) Ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Saratani;
- (v) Ujenzi wa Reli ya Mtwara – Mbamba Bay kuititia Mchuchuma na Liganga na ile ya Tanga – Arusha – Musoma;

- (vi) Ujenzi wa Bandari ya Mwambani Tanga;
- (vii) Mradi wa kufua umeme – Somanga Fungu;
- (viii) Uendeshaji wa huduma za usafiri katika Jiji la Dar es Salaam awamu ya kwanza; na
- (ix) Ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa dawa muhimu na vifaa tiba katika mikoa ya Pwani, Mbeya na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu Maeneo ya Kipaumbele kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020 yapo katika Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango, Sura ya Nne.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kama nilivyoeleza mwanzoni, maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge juu ya Mwongozo na Mapendekezo ya Mpango niliyoyawasilisha yatawezesha kuandaliwa kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 ili kuongeza kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na kuchochea matokeo yafuatayo:-

Kuongezeka kwa ubora wa huduma za kijamii; kupungua kwa umasikini; kutengamaa kwa viashiria vya kiuchumi na kijamii; na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji na biashara. Hivyo, Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wakati wa kuandaa Mpango wa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia kwa kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020 na kusimamia Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake. Aidha, Kamati za Mipango

na Bajeti za kila fungu zinatakiwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 17(3) ya Kanuni ya Sheria ya Bajeti za mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kuwasisitiza Waheshimiwa Wabunge kwamba katika michango yao wajielekeze zaidi katika kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kwenye miradi na vipaumbele vya Kitaifa badala ya kila mchangiaji kujielekeza zaidi kwenye miradi mahsusili iyopo jimboni kwake.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa kwa kufanya hivyo, maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge utaiwezesha Serikali kuandaa Mpango mzuri wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2019/2020 na Bajeti ya nchi inayojielekeza kutatua kero za wananchi wetu na kuchochea maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Tunakushukuru sana Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kutupitisha katika jambo hili kubwa linalohusiana na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/2020. Tunakushukuru sana.

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA
DKT. PHILIP I. MPANGO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI
MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA
NA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI
YA MWAKA 2019/20 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kutoa maoni na ushauri kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na kuboresha Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2019/20.
2. **Mheshimiwa Spika**, kinachowasilishwa sasa mbele ya Bunge lako Tukufu ni kwa mujibu wa Kifungu cha 94 cha Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016 kinachoelekeza Serikali kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha unaofuata.
3. **Mheshimiwa Spika**, Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kinajumuisha mapitio ya hali ya uchumi; utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/18 na robo ya kwanza ya mwaka 2018/19; maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2019/20; ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/20; mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa; na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango. Aidha tumeambatanisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu ya kwanza ya utawala wa Serikali ya awamu ya tano 2016/17 - 2018/19.
4. **Mheshimiwa Spika**, Kitabu cha Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali 2019/20 - 2021/22 kimeainisha masuala muhimu ambayo yanatakiwa kuzingatiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

na Taasisi na Mashirika ya Umma wakati wa kuandaa bajeti zao za mwaka 2019/20.

5. Mheshimiwa Spika, Mapendekezo haya ninayowasilisha yamezingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Vilevile, maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo yamezingatia sera, mikakati na programu mbalimbali za maendeleo ya kisekta zikiwemo: Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Afya; Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2016; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu 2016/17 – 2020/21; Mkakati Jumuishi wa Kuendeleza Viwanda 2025; na Mpango Kabambe wa Sekta ya Utalii wa Mwaka 2006. Hivyo, ni vema Waheshimiwa Wabunge watakaposoma vitabu vya Mwongozo na Mapendekezo ya Mpango warejee pia mikakati na programu za kisekta.

6. Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa ushauri na maoni yatakingatiwa kikamilifu katika kuandaa rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/20 utakaowasilishwa Bungeni tarehe 11 Machi 2019 kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, ushauri wa Waheshimiwa wabunge utatumika kuboresha Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2019/20. Hivyo, ninawasihi Waheshimiwa Wabunge katika nafasi yenu ya uwakilishi wa wananchi, mtumie weledi na uzoefu wenu katika kutoa maoni, ushauri kuhusu maeneo muhimu na miradi inayopaswa kuzingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20.

MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI

7. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka

2017. Hata hivyo, ukuaji huu unakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa mikopo na gharama zake na mabadiliko ya bei za bidhaa katika soko la dunia. Aidha, kati ya Nchi Wanachama wa Jumuuya ya Afrika Mashariki, Tanzania na Rwanda zinatarajiwa kuwa na viwango vya juu vya ukuaji wa asilimia 7.2 mwaka 2018, zikifualiwa na Kenya (asilimia 5.5); Uganda (asilimia 5.2); na Burundi (asilimia 0.1).

8. Mheshimiwa Spika, mwaka 2018, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ilifanya zoezi la mapitio ya kubadilisha mwaka wa kizio (base year) kwa Pato Ghafi la Taifa kutoka mwaka 2007 na kuwa mwaka 2015. Zoezi hili ni utekelezaji wa mapendekezo ya Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa ambayo inashauri Nchi Wanachama kufanya zoezi hili kila baada ya miaka mitano. Hivyo, takwimu zilizotumika katika kitabu cha Mpango, Mwongozo na taarifa hii zimezingatia mwaka wa kizio wa 2015.

9. Mheshimiwa Spika, kutohakana na zoezi hilo, mabadiliko yaliyojitokeza ni pamoja na: kuongezeka kwa Pato Ghafi la Taifa kwa asilimia 6.3; kubadilika kwa uwiano wa viashiria vinavyopimwa kwa Pato Ghafi la Taifa ikijumuisha Mapato ya kodi, Nakisi ya bajeti na Deni la Serikali; viwango vya ukuaji; na mchango wa sekta katika Pato Ghafi la Taifa. Kwa takwimu hizo za mwaka wa kizio wa 2015, Pato Halisi la Taifa limekua kwa wastani wa asilimia 6.9 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2013 - 2017). Kwa mwaka 2017, Pato la Taifa limeendelea kukua kwa kiwango kikubwa cha asilimia 7.1 ikilinganishwa na asilimia 7.0 kwa mwaka 2016. Kwa ukuaji huo Tanzania imeendelea kuongoza katika Jumuuya ya Afrika Mashariki ikifualiwa na nchi za Rwanda (asilimia 6.1); Kenya (asilimia 4.8); Uganda (asilimia 4.5); na Burundi (asilimia 0.0).

10. Mheshimiwa Spika, katika robo ya kwanza ya mwaka 2018, Pato Halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 5.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Shughuli za kiuchumi ambazo zilikuwa kwa kiwango kikubwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2018 ni pamoja na: ujenzi (asilimia 20); habari na mawasiliano (asilimia 18.3); usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 9.2); na kilimo (asilimia 7.1).

- 11.** **Mheshimiwa Spika**, ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa umechangia kupungua kwa umaskini. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia wa mwaka 2015/16 ulionesha kuwa idadi ya watanzania wanaoishi chini ya mstari wa umaskini ilipungua kufikia asilimia 26.3 ikilinganishwa na asilimia 28.2 mwaka 2012. Utafiti mpya wa Matumizi ya Kaya Binafsi unaendelea hivi sasa na utafiti huo unatarajiwa kukamilika Machi 2019 na kutupatia hali halisi ya viwango vya umaskini. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa Tanzania Bara umeongekeza kutoka wastani wa miaka 64.3 mwaka 2017 na unatarajiwa kuongezeka hadi wastani wa miaka 64.9 mwaka 2018.
- 12.** **Mheshimiwa Spika**, Mfumuko wa bei uliendelea kushuka na kuwa chini ya asilimia 5 kwa takribani kipindi chote cha mwaka 2017/18. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,483.9 mwishoni mwa mwezi Juni 2018, iliyokuwa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 5.6. Katika kipindi hicho, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kuwa tulivu. Wastani wa mwenendo wa ubadilishaji Shilingi dhidi ya dola ya Marekani ulikuwa kati ya Shilingi 2,231.17 na Shilingi 2,264.97 kwa dola moja ya Marekani, ikilinganishwa na kati ya Shilingi 2,171.0 na Shilingi 2,230.1 kwa dola moja ya Marekani katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2016/17.
- 13.** **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Juni 2018 Deni la Taifa ilifikia dola za Marekani milioni 27,774.86 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 25,350.76 kwa kipindi kama hicho mwaka 2017, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Matokeo ya hivi karibuni ya uchambuzi wa Deni la Taifa, yameonesha kuwa deni la Taifa lipo chini ya ukomo wa hatari na ni himiliyu. Viashiria vyote vya athari za madeni vimeendelea kuwa katika wigo unaokubalika kimataifa. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalikuwa dola za Marekani milioni 8,949.40 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 8,701.7 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Hii ilitokana na ongezeko la thamani ya mauzo ya mazao ya korosho,

karafuu, tumbaku, chai na m Konge; pamoja na kuimarika kwa bei za dhahabu katika soko la Dunia.

14. Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula nchini umeendelea kuimarika. Katika msimu wa 2017/18, uzalishaji ulifikia tani milioni 15.9 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.3 ya chakula kwa kipindi hicho. Kutokana na uzalishaji huo, nchi ilikuwa na ziada ya tani milioni 2.6 za mazao yote ya chakula na hivyo, kujitosheleza kwa asilimia 120.

15. Mheshimiwa Spika, baadhi ya viashiria vya sekta ya kibenki vilivyokuwa vimetetereka mwaka 2017 kwa sababu mbalimbali vimeanza kuimarika baada ya Serikali kuchukua hatua za kuongeza ukwasi ikiwa ni pamoja na Benki Kuu kushusha riba yake (discount rate). Kufuatia hatua hizo, mikopo kwa Sekta Binafsi imeanza kuonesha mwenendo unaordhisha ambapo hadi kufikia Juni 2018 ilikua kwa asilimia 4.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.3 Juni 2017. Riba za amana za kipindi cha mwaka mmoja zilipungua hadi wastani wa asilimia 10.52 ikilinganishwa na asilimia 11.66 mwaka 2016/17. Hata hivyo, viwango vya riba ya mikopo ya mwaka mmoja ilifikia asilimia 18.48, ikilinganishwa na asilimia 15.49 mwaka 2016/17, hivyo kusababisha tofauti kati ya riba ya amana na mikopo ya mwaka mmoja kuongezeka hadi asilimia 7.98 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 3.83 mwaka 2016/17. Kuongezeka kwa riba ya mikopo kulitokana na tahadhari zillizochukuliwa na benki za biashara ili kudhibiti mikopo chechefu na hivyo kuongeza gharama kwa wakopaji, hali ambayo inaweza kuathiri uwekezaji katika shughuli zinazochochea ukuaji wa uchumi. Maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika **Sura ya Pili, Sehemu ya Kwanza ya kitabu cha Mwongozo na Sura ya Pili ya kitabu cha Mapendekezo ya Mpango**.

Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2017/18

16. Mheshimiwa Spika, Mapato ya ndani katika mwaka 2017/18 yalifikia Shilingi bilioni 17,944.9 sawa na asilimia 90 ya lengo la Shilingi bilioni 19,977.0. Kati ya fedha hizo, Shilingi

bilioni 15,191.0 zilitokana na Mapato ya Kodi, sawa na asilimia 89 ya lengo; Shilingi bilioni 2,212.4 zilitokana na Mapato yasiyo ya Kodi, sawa na asilimia 101 ya lengo; na Shilingi bilioni 541.5 zilitokana na mapato ya ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, sawa na asilimia 79 ya lengo.

17. Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo nafuu iliyotolewa ilikuwa Shilingi bilioni 2,466.0 sawa na asilimia 62 ya makadirio ya Shilingi bilioni 3,971.1. Mikopo iliyopatikana kutoka ndani na nje ni Shilingi bilioni 7,055.8, sawa na asilimia 90.9 ya lengo la Shilingi bilioni 7,763.9. Kati ya mikopo hiyo, Shilingi bilioni 1,351.5 ni kutoka vyanzo vya nje na Shilingi bilioni 5,704.4 ni kutoka vyanzo vya masoko ya ndani. Kati ya mikopo ya ndani, Shilingi bilioni 4,835.2 zilitumika kulipia Mtaji wa Deni la Ndani (Rollover) na Shilingi bilioni 869.2 ni Mikopo mipyta kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Maendeleo.

18. Mheshimiwa Spika, matumizi halisi ya Serikali yalifika Shilingi bilioni 25,321.7 sawa na asilimia 80 ya bajeti iliyoidhinishwa ya Shilingi bilioni 31,711.9. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 18,778.5 zilikuwa ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia 93 ya lengo la Shilingi bilioni 20,279.3 na Shilingi bilioni 6,543.2 zilikuwa ni matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 57 ya bajeti ya Shilingi bilioni 11,432.7. Matumizi ya fedha za maendeleo hayajumuishi baadhi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja (D-funds) kwenye utekelezaji wa miradi ambazo hazikupita kwenye Mfumo wa Malipo wa Serikali. Fedha hizi zitajumuishwa pindi taratibu za kiuhasibu zitakapokamilika.

Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi ya Maendeleo Mwaka 2017/18 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2018/19

19. Mheshimiwa Spika, hatua iliyofiga katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo mwaka 2017/18 na robo ya kwanza ya mwaka 2018/19 ni pamoja na:

- (i) **Mradi wa kufua Umeme Unaotokana na Nguvu ya Maji katika Mto Rufiji MW 2,100:** kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi ya kuwezesha Mkandarasi

kuanza kazi kwa wakati. Kazi zilizotekelawa ni: ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 33 kutoka Msamvu hadi eneo la mradi ambapo sehemu za Msamvu – Pangawe (km 14) na Dakawa – Mpakanini mwa Pori la Akiba Selous (km 8.5) zimekamilika kwa asimilia 100 na kukamilika kwa asimilia 100 ya ujenzi wa Kituo cha Kupozea Umeme Pangawe; kukamilika kwa asilimia 100 kwa kazi ya kufikisha maji kwenye kambi za ujenzi, na kuendelea na kazi ya kufikisha maji Stesheni ya Reli ya TAZARA ya Fuga; kukamilika kwa asilimia 55 kwa kazi ya ukarabati na ujenzi wa nyumba zilizokwaua kambi ya RUBADA na kuendelea na uthamini wa mali zisizohamishika; kukamilika kwa asilimia 60 ya ujenzi wa barabara ya Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemere Junction (km 178.39) na kukamilika kwa asilimia 60 ya ujenzi wa barabara ya Kibiti - Mloka – Mtemere – Matambwe Junction – Mto Rufiji (km 210); na kukamilika kwa mifumo ya mawasiliano mbadala kwenye eneo la mradi. Aidha, upembuzi yakinifu wa awali wa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme (Rufiji hadi Chalinze) umekamilika.

- (ii) **Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Standard Gauge:** kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) ujenzi wa reli umeanza na umefikia asilimia 24. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na ujenzi wa njia, madaraja, utengenezaji wa mataruma na ujenzi wa miundombinu ya umeme. Aidha, kazi ya kutandika kilometra 60 za reli imeanza.

Kuhusu kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa kazi ya kutafuta mwelekeo wa njia; na kuendelea kufanya uthamini wa ardhi pamoja na mali. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu zilizosalia za Makutupora – Tabora (km 295), Tabora – Isaka (km 133), Isaka – Mwanza (km 250), Tabora – Uvinza – Kigoma, na Kaliua – Mpanda – Karema na Isaka – Rusumo (km 371).

- (iii) **Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania:** kununuliwa kwa ndege moja aina ya Bombadier Q 400 na moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner; kukamilika kwa sehemu ya malipo ya ununuvi wa ndege 2 aina ya A220-300 ambazo zinatarajiwa kuwasili Novemba, 2018 na Boeing 787-8 Dreamliner moja inayotarajiwa kuwasili mwaka 2020. Aidha, shughuli zinazoendelea ni pamoja na: ukarabati wa jengo la ofisi za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); utafutaji wa masoko ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa ofisi katika maeneo ya kimataifa ikujumuisha Bombay, Bujumbura, Guangzhou na Entebbe; na kuboresha miundombinu ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na mtandao wa mawasiliano ya simu. Aidha, ATCL imeanza kutoa huduma za usafiri kwa miji ya Bujumbura - Burundi na Entebbe - Uganda kuanzia Agosti 2018.
- (iv) **Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga:** kukamilika kwa upembusi yakinifu na usanifu wa mradi; kukamilika kwa tathmini za kijiolojia katika eneo la Chongoleani yatakapo jengwa matenki na gati la kupakia mafuta; kuridhiwa kwa mkataba wa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda; na kuendelea na majadiliano ya mkataba wa ubia.
- (v) **Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia – Lindi:** kuendelea na majadiliano ya mikataba kati ya Serikali na Wawekezaji wa Mradi wakiongozwa na Kampuni ya Shell - Tanzania na Statoil; kuendelea kuandaa mpango wa kuendeleza vitalu vya baharini; kuandaa mpango wa kushirikiana na wadau (stakeholders engagement plan) wa eneo la mradi; na kuendelea na mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi (Transaction Advisor).
- (vi) **Makaa ya Mawe (Mchuchuma) na Chuma (Liganga):** kukamilika kwa taarifa ya awali ya Timu ya Majadiliano iliopewa jukumu la kuchambua vivutio vilivyoombwa na Mwekezaji pamoja na kuainisha maeneo ya mikataba ya mradi yanayokinanza na

sheria na kutoa mapendelekezo ya hatua za kuchukuliwa na Serikali. Aidha, Timu ya Majadiliano ya Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa kina kuhakikisha kuwa uwekezaji huo unakuwa na maslahi kwa Taifa.

- (vii) **Uendelezaji wa Kanda Maalum ya Uwekezaji Bagamoyo:** kufuatia kukamilika kwa makubaliano ya awali ya utekelezaji wa mradi, Timu ya Serikali ya Majadiliano inaendelea na majadiliano ya kina ya mikataba kuhusu uendelezaji wa eneo hilo na wawekezaji. Aidha, majadiliano hayo yamechukua muda mrefu kutokana na kuwepo kwa vipengele vyenye masharti magumu yasiyo na maslahi kwa Taifa.
- (viii) **Miradi ya Umeme:** utekelezaji wa miradi ya kufua umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati vikiwemo maji na gesi unaendelea. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kufua umeme unaotokana na nguvu ya maji **Ruhudji MW 358** (Serikali inaendelea na majadiliano na wafadhili ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za kutekeleza Mradi), Mradi wa kufua Umeme unaotokana na nguvu ya maji **Malagarasi MW 45** (kuendelea na kudurusu upembizi yakinifu wa mradi) na Mradi wa kufua Umeme unaotokana na nguvu ya maji **Rusumo MW 80** (ujenzi umeanza); miradi ya kufua umeme wa gesi **Mtwara MW 300** (upembizi yakinifu unaendelea) na mradi wa **Somanga Fungu MW 330** (upo hatua ya ukamilishaji wa upembizi yakinifu). Aidha, kuhusu usambazaji wa umeme vijijini, vijiji 557 vimeunganishiwa umeme kupitia Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiini Awamu ya Tatu (REA Phase III). Vile vile, mradi umewezesha taasisi 903, shule 1,983 maeneo ya biashara 1,743 na maabara za tiba 19 kuunganishwa umeme.
- (ix) **Miradi ya Viwanda:** (a) **kuimarisha Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)** kwa kutengeneza mashine 64 zikiwemo za kupandia

mbegu za pamba, kusaga karanga, kukausha mbogamboga na kukata majani; ujenzi wa mitambo 55 ya *biogas*; kubuni teknolojia mpya kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa na kukamilika kwa tafiti tatu zinazohusiana na matumizi ya nishati mbadala ya *biogas*; (b) **kuendeleza mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka - Arusha** kwa kukamilisha upimaji wa ardhi na uthamini wa mali za wananchi ili kujua kiasi cha fidia kitakachohitajika; (c) **kuimarisha mradi wa Kuunganisha Matreka TAMCO - Kibaha** ikijumuisha kuagizwa kwa vipande (Semi Knocked Down - SKD) kwa ajili ya kuunganishwa ili kupata matreka 727; na kuunganisha matreka 420, majembe 95 na haro (harrow) 195; na (d) **kuimarisha Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO)** kwa kubuni mashine ya kutengeneza tofali zinazozuia upotevu wa joto, mtambo wa kusindika na kusafisha mafuta ya kula, mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji na usimikaji wa mitambo wa kuzalisha umeme (kW 20) kutokana na nguvu za upepo na juu katika Kituo cha Olduvai Gorge – Ngorongoro.

- (x) **Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) jijini Dar es Salaam:** ujenzi wa Mfugale Flyover (TAZARA) umekamilika na kuanza kutumika. Vile vile, ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo unaendelea.
- (xi) **Ujenzi wa Meli katika Maziwa Makuu:** (a) kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili; na kufikia hatua za mwisho za ujenzi wa meli moja yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 katika ziwa Nyasa unaotarajiwa kukamilika Desemba 2018 (b) kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa meli mpya katika ziwa Victoria yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ambapo mkandarasi yupo katika hatua za awali za kuanza ujenzi; na mkataba wa ujenzi wa chelezo kwa ajili ya kujengea meli umesainiwa; na (c) kufikia hatua za mwisho za kusaini mkataba wa ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika ziwa Tanganyika.

- (xii) **Viwanja vya Ndege:** ujenzi wa jengo la tatu la abiria (Terminal III) la Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere (Dar es Salaam) umefikia asilimia 78. Aidha, ujenzi na ukarabati wa Kiwanja cha Kilimanjaro umekamilika na Kiwanja cha Mwanza umefikia asilimia 70.
- (xiii) **Ujenzi wa Barabara na Madaraja Makubwa:** Hadi Juni 2018, mtandao wa barabara za lami nchini uliflikia kilomita 8,298.12 kwa barabara kuu na kilomita 1,687 kwa barabara za mikoa. Aidha, madaraja makubwa yanayoendelea kujengwa ni pamoja na daraja la Mara (Mara) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 81.3, Sibiti (Singida) asilimia 79.8, Lukuledi (Lindi) asilimia 70, Ruhuhu (Ruvuma) asilimia 65, Mlalakuwa (Dar es Salaam) asilimia 64, Magara (Manyara) asilimia 9 na Momba (Songwe) asilimia 7.5. Aidha, kwa daraja la Selander (Dar es Salaam) na Wami (Pwani), mikataba ya ujenzi imesainiwa.
- (xiv) **Uendelezaji wa Bandari:** katika bandari ya Dar es Salaam utekelezaji umefikia asilimia 35 ambapo, uwekaji nguzo za msingi katika gati Na. 1 umekamilika; na ujenzi wa sakafu ngumu chini ya maji katika gati la kupakua na kupakia magari (Roll on Roll off - Ro-Ro) unaendelea. Aidha, katika bandari ya Tanga, ukarabati wa maegesho, sehemu ya kupakulia shehena na barabara kuelekea lango Na. 2 umefikia asilimia 76 na ujenzi wa gati la mita 300 katika bandari ya Mtwara umefikia asilimia 30.

20. Mheshimiwa Spika, Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo mwaka 2017/18 na robo ya kwanza ya mwaka 2018/19 yameainishwa katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango (**Sura ya Tatu**).

MAFANIKIO KWA KIPINDI CHA 2016/17 – 2018/19

21. Mheshimiwa Spika, yapo mafanikio mengi yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya kwanza

ya utawala wa Serikali ya awamu ya tano (2016/17 – 2018/19). Mafanikio hayo yanajumuisha yafuatayo:

- (i) **Ukuaji wa Uchumi:** kuendelea kuimarika kwa uchumi wa Taifa, ambapo uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2017 kutoka ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2016 na mfumuko wa bei kuendelea kupungua na kuwa katika wastani wa kiwango cha tarakimu moja, chini ya asilimia 5.0.
- (ii) **Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi:** mapato ya kodi yaliongezeka kutoka Shilingi bilioni 12,434 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 15,191 mwaka 2017/18 na mapato yasiyo ya kodi yaliongezeka pia kutoka Shilingi bilioni 1,188 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 2,212.4 mwaka 2017/18. Aidha, ongezeko la mapato yasiyo ya kodi lilitokana na kuimarika kwa ufuatilaji na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato hususan Wizara ya Madini (kutoka Shilingi bilioni 207.9 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 301.2 mwaka 2017/18), Ofisi ya Msajili wa Hazina (kutoka Shilingi bilioni 243.4 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 803.5 mwaka 2017/18), Wizara ya Ardh, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (kutoka Shilingi bilioni 73.3 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 92.2 mwaka 2017/18) na Idara ya Uhamiaji (kutoka Shilingi bilioni 115.3 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 159.3 mwaka 2017/18).
- (iii) **Ulipaji wa Madai:** Serikali ililipa jumla ya Shilingi bilioni 2,288.9 za madai yaliyohakikiwa ya wakandarasi, watoa huduma, wazabuni, watumishi wa umma na madai mengineyo. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 1,611.0 zililipwa kwa wakandarasi, shilingi bilioni 144.6 kwa watoa huduma, shilingi bilioni 218.3 kwa wazabuni, Shilingi bilioni 285.9 kwa watumishi wa umma na Shilingi bilioni 29.1 kwa madai mengineyo.
- (iv) **Barabara:** mtandao wa barabara kuu za lami uliongezeka kutoka kilomita 7,646 Juni 2016 hadi

kilomita 8,298.12 Juni 2018 na mtandao wa barabara za mikoa nao uliongezeka kutoka kilomita 1,398 hadi kilomita 1,687 kwa kipindi hicho. Aidha, ujenzi wa Barabara ya juu ya *Mfugale Flyover* (TAZARA) ulikamilika na kuanza kutumika na ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo unaendelea.

- (v) **Reli:** ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* umeanza, ambapo kwa awamu ya kwanzia ya Dar es Salaam – Morogoro (km 300) ujenzi umefikia asilimia 24. Maandalizi ya ujenzi kwa sehemu ya Morogoro – Makutupora (km 422) nayo yameanza. Faida zitakazotokana na kukamilika kwa reli hii ni pamoja na: kupungua kwa muda wa kusafirisha abiria na mizigo; kuongezeka kwa kiwango cha usafirishaji wa abiria na mizigo; kuongezeka kwa mapato ya Serikali; kuongezeka kwa fursa za ajira; na kupanuka kwa biashara katika vijiji na miji inayopitiwa na reli hiyo. Vile vile, Serikali imeendelea kuboresha reli ya kati inayotumika sasa ambapo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuwezesha usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Mwanza (Mwanza South Port) kwenda Bandari ya Port Bell – Uganda ambapo katika mwaka 2017/18 wastani wa shehena ya mizigo ya tani 200,000 ilisafirishwa.
- (vi) **Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania:** ndege mpya tatu (3) aina ya Bombadier Q 400 na moja (1) aina ya Boeing 787-8 *Dreamliner* zilinunuliwa na kuanza kufanya kazi. Vile vile, sehemu ya malipo ya ndege mbili (2) aina ya A220 – 300 zinazotarajiwa kuwasili Novemba 2018 na moja (1) aina ya Boeing 787-8 *Dreamliner* inayotarajiwa kuwasili mwaka 2020 yamefanyika. Kutoptaka na kuboreshwa kwa ATCL, idadi ya mikoa inayohudumiwa na ndege za ATCL imeongezeka na kufikia 10. Mikoa hiyo ni: Dar es Salaam, Kagera, Mbeya, Kigoma, Ruvuma, Mtwara, Dodoma, Tabora, Kilimanjaro na Mwanza. Aidha, Shirika pia linatoa huduma Zanzibar. Vile vile, Shirika

limeanzisha ofisi katika miji ya Mumbai, Bujumbura, Guangzhou na Entebbe.

- (vii) **Viwanja vya Ndege:** ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria na miundombini yake katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere umefikia asilimia 78. Aidha, upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza umefikia asilimia 70 na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro umekamilika. Upanuzi huu umewezesha kuongezeka kwa: abiria na mizigo; mapato ya Serikali; ajira; biashara za hoteli na maduka; na idadi ya watalii.
- (viii) **Bandari:** ujenzi wa gati la kupakua na kupakia magari (Roll on Roll off - Ro-Ro) na upanuzi wa gati Na. 1 katika bandari ya Dar es Salaam umefikia asilimia 35, na upanuzi wa bandari za Tanga na Mtwara umefikia asilimia 76 na 30 kwa mtiririko huo. Kukamilika kwa ujenzi huo kutawezesha kuongezeka kwa uwezo wa bandari kuhudumia magari kati ya 300,000 hadi 500,000 kwa mwaka; kupungua kwa muda wa kupakua magari na hivyo kuongeza ufanisi wa bandari; kuongezeka kwa mapato ya Serikali; na kuhimili ushindani kutoka bandari za nchi jirani.
- (ix) **Kilimo:** kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo kiliongezeka kufikia asilimia 7.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2016. Ukuaji huu umewezesha kuongezeka kwa usalama wa chakula, kupungua kwa mfumuko wa bei ya chakula kufikia asilimia 3.8 Juni 2018 ikilinganishwa na asilimia 9.8 Juni 2017 na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi kutoka dola za Marekani milioni 866.4 mwaka 2016/17 kufikia dola milioni 1,152.4 mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 33. Vile vile, upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka na kufikia tani 51,700.5 mwaka 2017/18 kutoka tani 36,482 mwaka 2015/16, na tani 435,178 za mbolea zilinunuliwa na kusambazwa katika mwaka 2017/18 ikilinganishwa na tani 302,450 zilizonunuliwa katika

mwaka 2015/16. Aidha, katika kuimarisha Ushirika na Masoko ya Mazao, Vyama vya Ushirika viliongezeka kutoka 7,888 mwaka 2015 hadi 10,990 mwaka 2017.

(x) Huduma za Afya: kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa Hospitali 10 za Wilaya, Vituo vya Afya 295 na nyumba za watumishi wa afya 306. Aidha, bajeti ya ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 31 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 269 mwaka 2017/18. Kuanza kutoa huduma ya kupandikiza figo kwa wagonjwa 28 na hivyo kupunguza gharama kwa wastani kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 20 kwa mgonjwa mmoja endapo angepelekwa nje ya nchi. Vile vile, Serikali imeanzisha huduma ya kupandikiza vifaa vya kusikia (*Cochlear Implant*) kwa watoto ambapo jumla ya watoto 11 wamepatiwa huduma hiyo na hivyo kuokoa shilingi milioni 64 kwa mtoto mmoja endapo angepata huduma hii nje ya nchi.

(xi) Nishati: uzalishaji wa umeme umeongezeka kutoka MWh 6,950,280 mwaka 2016/17 hadi MWh 7,010,590 mwaka 2017/18 ambao umewezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuongezeka kwa idadi ya wananchi waliounganishiwa umeme ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba 2018 jumla ya vijiji 5,181 tayari vimeunganishiwa umeme. Aidha, shughuli za kiuchumi pia zimeongezeka; vilevile, ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji mto Rufiji - MW 2,100 umeanza; Pia, maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kusafirishia Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga yamekamilika.

(xii) Huduma za Maji: miradi 1,595 ya maji vijijini imekamilika, ikiwa na jumla ya vituo vya kuchotea maji 126,610 na uwezo wa kuhudumia wananchi 31,652,500.

(xiii) Viwanda: Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa azma yake ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo viwanda vipyta zaidi ya 3,306 vilijengwa katika mikoa mbalimbali ikijumuisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za ujenzi (sarufi, marumaru, nondo) na kilimo, hususan, kusindika matunda, mafuta na ngozi. Ujenzi wa viwanda vipyta umechangia kupatikana kwa ajira mpya 482,601 mwaka 2017/18.

(xiv) Kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma: Serikali ya awamu ya tano imefanikiwa kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka katika jiji la Dar-es-Salaam kuja hapa katika jiji la Dodoma ambapo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Watumishi wa Umma 6,531 kutoka Wizara zote wamehamia Dodoma. Aidha, inatarajiwa kuwa Mheshimiwa Rais atahamia rasmi Dodoma kabla ya tarehe 31 Desemba 2018.

(xv) Madini: Sheria za Madini zilifanyiwa mapitio ili kuiwezesha Serikali kunufaika zaidi na rasilimali za madini. Aidha, Serikali ilikamilisha ujenzi wa ukuta wenye mzingo wa km 24.5 kuzunguka migodi ya Tanzanite Mirerani ambao umewezesha kupunguza utoroshwaji wa madini. Juhudi hizi na nyinginezo ziliwezesha kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli yanayotokana na madini kufikia Shilingi billioni 301.2 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na lengo la Shilingi billioni 194.4.

(xvi) Elimu: Serikali ya awamu ya tano ilianzisha na imeendelea kutekeleza utaratibu wa kutoa elimumsingi nchini bila ada ambapo Serikali imekuwa ikitoa Shilingi **bilionti 20.9** kila mwezi. Juhudi hizi zimechangia ongezeko la wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza kutoka 1,568,378 mwaka 2015 hadi 2,078,379 mwaka 2018, na kidato cha kwanza kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 562,695 mwaka 2017.

(xvii) **Usafiri wa Majini:** Serikali iliendelea kujenga na kukarabati meli na vivuko katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa Kazi hizi zitarahisisha na kuongeza uwezo wa usafirishaji wa abiria na mizigo. Aidha, uwezo wa meli hizo ni kama ifuatavyo: meli mpya katika ziwa Victoria itabeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo; ziwa Nyasa abiria 200 na mizigo tani 200; na ziwa Tanganyika abiria 600 na tani 400 za mizigo.

Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti na Hatua za Kukabiliana Nazo

22. **Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/18, ni pamoja na zifuatazo:

- (i) Ugumu wa kukusanya kodi kutoka kwa wafanyabiashara waliopo katika sekta isiyo rasmi kwa kuwa hawana sehemu rasmi na za kudumu za kufanya biashara na hawatunzi kumbukumbu;
- (ii) Kutofikiwa kwa lengo la kodi zinazotokana na ajira (PAYE) kulikosababishwa na kutofikiwa kwa malengo ya ajira mpya na kutoongezeka kwa mishahara kwa wafanyakazi kama ilivyokuwa imetarajiwa. Vile vile, kodi hizi zimeathirika kutokana na kupunguzwa kazi kwa wafanyakazi kwenye migodi ya madini kufuatia kupungua kwa shughuli za uchimbaji madini kwa baadhi ya migodi;
- (iii) kushuka kwa biashara za kimataifa kulikopelekea kutofikia malengo ya uingizwaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kama ilivyokuwa imetarajiwa;
- (iv) Upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, hivyo kupunguza ufanisi wa utendaji kazi wa Mamlaka;

- (v) Kupungua kwa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo wakati wa utekelezaji wa bajeti;
- (vi) Changamoto ya masoko na bei ndogo za mazao kwa wakulima; na
- (vii) Kuendelea kuwepo kwa madai mbalimbali yakiwemo ya wakandarasi, watoa huduma, wazabuni na watumishi wa umma.

23. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza mapato, Serikali imechukua hatua mbalimbali, ikiwa pamoja na: kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi na utoaji wa elimu kwa walipakodi ili kuongeza mwamko wa kulipa kodi; kuimarisha mifumo na taasisi zinazokusanya mapato ili kudhibiti ukwepajji kodi na uvujaji wa mapato ya Serikali; kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara na uwekezaji wa Sekta Binafsi; na kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kuititia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Corporation Framework - DCF).

MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2019/20

24. Mheshimiwa Spika, misingi iliyozingatiwa katika kuweka malengo ya uchumi jumla ni pamoja na: uwepo wa amani, usalama, utulivu na umoja hapa nchini na katika nchi jirani; kuimarika kwa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya kiuchumi na kijamii; kutengamaa kwa uchumi wa dunia; utulivu wa bei za mafuta katika soko la dunia; na hali nzuri ya hewa.

25. Mheshimiwa Spika, Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla: Shabaha na malengo ya uchumi jumla ambayo yanatokana na takwimu mpya za mwaka wa kizio wa 2015 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa kufikia asilimia 7.3 mwaka 2019 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 7.2 mwaka 2018, na kuongezeka kwa wastani wa asilimia 7.6 katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22);
- (ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 5.0 katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22);
- (iii) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.7 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 kutoka matarajio ya asilimia 12.5 mwaka 2018/19 na wastani wa asilimia 12.9 katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22);
- (iv) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 21.1 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 na kufikia wastani wa asilimia 20.2 katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22);
- (v) Kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kutoka matarajio ya asilimia 2.9 mwaka 2018/19 hadi wastani wa asilimia 1.1 katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22); na
- (vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.5 katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22).

Mfumo wa Awali wa Mapato na Matumizi ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22)

26. Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadiriwa kuongezeka hadi Shilingi bilioni 23,206.8 mwaka 2019/20 kutoka Shilingi bilioni 20,894.6 mwaka 2018/19 na kukadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 10.1 katika kipindi cha muda wa kati (2019/20 – 2021/22) hadi Shilingi bilioni 28,113.9 mwaka 2021/

22. Mapato ya ndani katika Pato la Taifa yanakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 14.6 mwaka 2019/20 hadi asilimia 14.9 mwaka 2021/22. Mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 11.8 hadi Shilingi bilioni 20,124.1 mwaka 2019/20 kutoka Shilingi bilioni 18,000.2 mwaka 2018/19 na kukua kwa wastani wa asilimia 10.1 katika kipindi cha muda wa kati (2019/20 – 2021/22) hadi Shilingi bilioni 24,385.4 mwaka 2021/22. Uwiano wa Mapato ya kodi na Pato la Taifa unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 12.7 mwaka 2019/20 hadi asilimia 12.9 mwaka 2021/22. Mapato yasiyo ya Kodi (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadariwa kuongezeka hadi Shilingi bilioni 3,082.7 mwaka 2019/20 kutoka Shilingi bilioni 2,894.4 mwaka 2018/19. Aidha, mapato yasiyo ya kodi (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 10.0 na kufikia Shilingi bilioni 3,728.5 mwaka 2021/22.

27. **Mheshimiwa Spika**, misaada na mikopo nafuu inatarajiwa kupungua kutoka Shilingi bilioni 3,380.2 mwaka 2019/20 hadi Shilingi bilioni 3,289.9 mwaka 2021/22. Mikopo kutoka nje na ndani (ikijumuisha Rollover) inatarajiwa kuwa Shilingi bilioni 6,913.2 mwaka 2019/20 na Shilingi bilioni 6,768.6 mwaka 2021/22.

28. **Mheshimiwa Spika**, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kukua hadi Shilingi bilioni 33,500.2 (asilimia 21.1 ya Pato la Taifa) mwaka 2019/20 kutoka Shilingi bilioni 32,476.0 (asilimia 22.5 ya Pato la Taifa) mwaka 2018/19 na kukadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.7 hadi Shilingi bilioni 38,172.5 mwaka 2021/22. Katika mwaka 2019/20, Mishahara (ikijumuisha mishahara ya Taasisi) inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 7,559.0 na kukadiriwa kuongezeka hadi Shilingi bilioni 8,422.7 mwaka 2021/22. Malipo ya riba na mtaji kwa deni la ndani na nje yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 8,625.6 mwaka 2019/20 na kuongezeka hadi Shilingi bilioni 11,023.8 mwaka 2021/22. Kiasi cha kulipia bidhaa, huduma na ruzuku kinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 4,931.2 mwaka 2019/20 na kuongezeka hadi Shilingi bilioni 5,166.1 mwaka 2021/22. Matumizi ya Maendeleo yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 12,384.4 (asilimia 7.8 ya Pato

la Taifa) mwaka 2019/20 na kuongezeka hadi Shilingi bilioni 13,559.8 mwaka 2021/22.

Maelekezo Mahsusni ya Mwongozo

29. Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo na kusimamia Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Kanuni zake. Aidha, Kamati za Mipango na Bajeti za kila Fungu zinatakiwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 17(3) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za mwaka 2015. Mwongozo umebainisha masuala muhimu ambayo hayana budi kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji wa mipango, bajeti na utekelezaji kama ifuatavyo:

A. Mahitaji ya Rasilimali Fedha

- (i) Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yanawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;
- (ii) Kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Mapato;
- (iii) Kubuni vyanzo vipyta vya mapato ikiwa ni pamoja na vile vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21;
- (iv) Kutoingia mikataba yenye vifungu vinavyotoa misamaha ya kodi bila kupata ridhaa ya Waziri wa Fedha na Mipango; na
- (v) Kuhakikisha kuwa kampuni zote ambazo Serikali ina hisa zinaendeshwa kwa ufanisi na hivyo kutoa gawio stahiki kwa Serikali.

B. Udhibiti Katika Matumizi ya Fedha za Umma

- (i) Kuhakikisha thamani halisi ya fedha inazingatiwa katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi kwa kuzingatia misingi ya Kanuni za Ununuzi wa Umma kama *Force Account*, ununuzi wa pamoja na ushindanishwaji wa wazabuni;
- (ii) Kutumia TEHAMA katika mawasiliano Serikalini, kama vile majalada ya kielektroniki kwa lengo la kupunguza gharama na kuongeza ufanisi;
- (iii) Kuhakikisha hati za madai na mikataba ya watoa huduma wa ndani inakuwa katika Shilingi ya Tanzania ili kupunguza athari za mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha;
- (iv) Kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi hasa kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani;
- (v) Kutenga fedha za kulipa madeni yaliyohakikiwa kwa kutumia Ukomo wa Bajeti uliotolewa; na
- (vi) Taasisi na Mashirika ya Umma yenyе uhitaji wa mikopo kuhakikisha zinapata kibali kutoka kwa Waziri wa Fedha na Mipango kama ilivyoinishwa katika Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134 pamoja na Kifungu cha 60(4) na 62(b) cha Sheria ya Bajeti, SURA 439. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufuatilia kwa ukaribu mikataba yenyе dhamana ili kuepuka madeni sanjari.

C. Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma

- (i) Kuhakikisha kuwa Taasisi na Mashirika ya Umma yanachangia asilimia 15 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), (Sura 370), ikijumuisha ziada na itolewe kwa wakati;

- (ii) Kuimarisha ufuatiliaji wa Hisa za Serikali katika kampuni ambazo Serikali ina hisa chache;
- (iii) Kuhakikisha Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara yanaandaa Mwongozo wa Gawio utakaotoa utaratibu wa malipo ya gawio kwa Serikali;
- (iv) Kuchambua taarifa za fedha na mwenendo wa Taasisi na Mashirika ya Umma na kupendekeza hatua stahiki za kuboresha, kuunganisha au kuyafuta kwenye Daftari la Msajili wa Hazina; na
- (v) Kufuatilia viwanda na mashamba yaliyobinafsishwa ili kubaini kama yanaendeshwa kuendana na mikataba ya mauzo na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kurejesha Serikalini mashamba na viwanda ambavyo wamiliki watabainika kukiuka mikataba ya mauzo.

30. Mheshimiwa Spika, maelekezo mahsusni ya Mwongozo yameainishwa kwa kina katika **Sura ya Kwanza, Sehemu ya Pili ya Kitabu cha Mwongozo**.

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2019/20

31. Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 yameainisha maeneo ya kipaumbele yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2019/20. Maeneo hayo yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 na Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango huo. Maeneo hayo ni:

- (i) **Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda:** Ujenzi wa viwanda ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi (Ruvuma, Mtwara, Kigoma na Bagamoyo); Kukuza kilimo cha mazao, Mifugo na Uvuvi; Maliasili

za madini, misitu na wanyamapori; Utalii, Biashara na Masoko; Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa kipekee wa sekta ya kilimo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na ustawi wa wananchi, Serikali itaweka msukumo zaidi katika uendelezaji wa sekta hii kwa kutekeleza mikakati na programu mbalimbali hususan ASDP II, uboreshaji wa masoko ya bidhaa za kilimo na uimarishaji wa bei za mazao ya kilimo;

- (ii) **Ujenzi wa Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji:** Kipaumbele kitatolewa kwa miradi ifuatayo: Nishati, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mtambo wa kufua umeme katika mto Rufiji; Maendeleo ya reli ikijumuisha ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge; na Usafiri wa anga ikiwemo kuboresha Shirika la Ndege Tanzania. Aldha, maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na barabara; madaraja; bandari; usafiri wa majini; teknolojia ya habari na mawasiliano; ardhi na maeneo ya uwekezaji na biashara; huduma za fedha; na ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Vile vile, Serikali itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo yaliyotolewa katika Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara Nchini wa Mwaka 2010 ikiwa ni pamoja na kusimamia mapendekezo yaliyopo kwenye *Blueprint on Policy and Regulatory Reforms*;

- (iii) **Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu:** Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni elimu na ujuzi hususan kusomesha kwa wingi wataalam kwenye fani na ujuzi adimu; afya na ustawi wa jamii; maji na usafi wa mazingira; vijana, ajira na wenye ulemavu; habari, utamaduni, sanaa na michezo; utawala bora na huduma bora kwa wananchi; hifadhi ya mazingira; na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, katika kuimarisha utawala bora ili kuchochaea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, Serikali itaendelea kujenga miundombinu wezeshi hususan ofisi, makazi na huduma za jamii

katika Makao Makuu ya nchi Jijini Dodoma. Vile vile, msukumo zaidi utawekwa katika kuongeza na kuboresha huduma ya maji; kuunga mkono juhudzi za wananchi kukamilisha maboma ya afya na elimu; na kujenga mazingira ambayo yatawezesha matumizi ya teknolojia ya kisasa kwenye utoaji wa huduma za elimu na afya kama vile upelekaji wa dawa kwa kutumia ndege zisizo na rubani (drones). Pamoja na hayo, Serikali imeanza kuandaa Muswada wa Sheria ya Maji ambaa pamoja na mambo mengine unapendekeza kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijiji ili kuongeza kasi ya kuondoa kero ya maji kwa wananchi;

- (iv) **Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango:** Mionganoni mwa masuala yatakayopewa msukumo ni pamoja na upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na kwa riba nafuu, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa matumizi, na kuimarisha mfumo wa ufuatilajji na tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Maeneo mengine ni yale ya kujenga mazingira wezeshi hususan, kulinda umoja wa kitaifa, ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo na ulinzi wa rasilimali za Taifa.

Mikakati ya Kushirikisha Sekta Binafsi kwa Mwaka 2019/20

32. **Mheshimiwa Spika**, sekta binafsi inatarajia kuongeza uwekezaji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo hususan katika maeneo ya kipaumbele ikiwemo: viwanda nya nguo, dawa za binadamu, bidhaa za ngozi, usindikaji wa vyakula, mafuta, ujenzi wa miundombinu wezeshi, huduma za jamii, huduma za fedha, huduma za utalii; na kuanzisha na kuendeleza maeneo ya viwanda na maeneo ya teknolojia.

Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

33. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kuititia utaratibu wa ubia kati ya Sekta

ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Maboresho hayo yamepelekea kuundwa kwa miongozo ya kisera, kisheria na kitaasisi ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa Sera ya Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Kwa msingi huo, miradi ya ubia inayopendekezwa kutekelezwa ni pamoja na: Mradi wa Kusambaza Gesi katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara; mradi wa kujenga hosteli za wanafunzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) – Dar es Salaam; ujenzi wa vyuo kumi vya Ufundji Stadi; ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Saratani; ujenzi wa Reli ya Mtwara – Mbamba Bay kupitia Mchuchuma na Liganga, na Tanga – Arusha – Musoma; na ujenzi wa bandari ya Mwambani Tanga; mradi wa kufua umeme – Somanga Fungu; uendeshaji wa huduma ya usafiri jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza; na ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa dawa muhimu na vifaa tiba katika mikoa ya Pwani, Mbeya na Mwanza.

34. **Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu Maeneo ya Kipaumbele kwa mwaka 2019/20 yapo katika **Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango (Sura ya Nne)**.

HITIMISHO

35. **Mheshimiwa Spika**, Kama nilivyoeleza mwanzoni, Maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge juu ya Mwongozo na Mapendekezo ya Mpango niliyowasilisha yatawezesha kuandaliwa kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 ili kuongeza kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na kuchochea matokeo yafuatayo: kuongezeka kwa ubora wa huduma za kijamii; kupungua kwa umasikini; kutengamaa kwa viashiria vya kiuchumi na kijamii; na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji na biashara. Hivyo, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wakati wa kuandaa Mpango wa Mwaka 2019/20. Vile vile, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2019/20 na kusimamia Sheria

ya Bajeti, SURA 439 na Kanuni zake. Aidha, Kamati za Mipango na Bajeti za kila Fungu zinatakiwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 17(3) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za mwaka 2015.

36. Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kuwasisitizia Waheshimiwa Wabunge kwamba katika michango yao wajielekeze zaidi katika kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kwenye miradi na vipaumbele vyta Kitaifa badala ya kila mchangiaji kujiielekeza zaidi kwenye miradi mahsusili iyopo jimboni kwake. Ninaamini kuwa kwa kufanya hivyo maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge utaiwezesha Serikali kuandaa Mpango mzuri wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20 na Bajeti ya nchi inayojielekeza kutatua kero za wananchi wetu na kuchochea maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania.

37. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2019/20.

38. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Natumaini kila Mheshimiwa Mbunge ana kijitabu hiki.

Tunaendelea Katibu.

NDG. RAMADHAN ABDALLAH- KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutakumbuka kwamba shughuli zetu za kujadili mpango huwa tunazifanya katika utaratibu wa Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, kuanzia leo mpaka Jumatatu ijayo tutakuwa tukifanya hivyo.

Namwomba kila mmoja wetu aende akaisome kwa makini hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na kama alivyoshauri na mimi nishauri pia huu ni mpango wa Taifa siyo mpango wa Jimbo lako. Kwa hiyo, ni vizuri tukajikita hivyo kwenye kuliangalia Taifa letu tunapotoka, tulipo na tunapoenda ili tuweze kuisaidia Serikali kuweka mambo vizuri tunapoelekea kwenye bajeti inayokuja.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Mwenyekiti karibu sana, una nusu saa. (*Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya kutayarisha Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge la Bajeti kuhusu Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa pamoja na Mwongozo wa Kutayarisha Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kujadiliana kwa kina na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendeleko ya Mpango huu. Aidha, katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilipitia na kujadili Mpango wa Miaka Mitano (2016/2017 hadi 2020/2021); Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa miaka Mitatu (2016/2017 hadi 2018/2019) pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2025. Lengo la kupitia taarifa hizo ilikuwa ni kupata mwelekeo wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano kupitia mipango ya Taifa inayotekelzwa kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya hali ya uchumi jumla kwa kipindi cha mwaka 2017. Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua hali ya uchumi inayotokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2017/2018. Maeneo yaliyofanyiwa uchambuzi ni pato la Taifa, mfumuko wa bei, mwenendo wa thamani shilingi, deni la Serikali, urari wa biashara na mikopo kwa sekta binafsi kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.1 hapo chini, naomba nisilisome kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa pato la Taifa ni mojawapo ya vigezo vya kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umaskini. Takwimu zinaonesha kuwa pato la Taifa limekuwa kwa kiasi cha asilimia 7.2 kwa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na asilimia 7.1 kwa mwaka 2016/2017. Mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi ni wa kuridhisha na malengo ya Serikali ni kufikia kiwango cha asilimia 10 ifikapo mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukuaji huu mzuri wa uchumi lazima Serikali ifungamanishe ukuaji huu wa uchumi na ukuaji wa kipato cha mwananchi wa kawaida. Hatua hii itaweza kufikiwa kama Serikali itaongeza bajeti ya kuwekeza kwenye sekta zinazoajiri wananchi walio wengi kama kilimo, mifugo na uvuvi ili zilete ufanisi katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei umeendelea kuwa kwenye kiwango cha chini na kubaki katika wigo wa tarakimu moja kutoka asilimia 5.3 kwa mwaka 2016/2017 hadi asilimia 4.3 kwa mwaka 2017/2018. Serikali inategemea kuwa mfumuko wa bei utaendelea kuwa chini kwa kiwango cha tarakimu moja ili uweze kufikia lengo la asilimia 5 ifikapo mwaka 2020/2021. Kamati inashauri kuwa hatua hii inaweza kufikiwa iwapo Serikali itaendelea na jitihada za kuhakikisha kunakuwepo na udhibiti wa bei ya mafuta kulingana na bei ya soko la dunia, uwepo wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani pamoja na udhibiti wa Sera za Fedha zinazolenga kutunza thamani ya fedha kwa kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili kuchochaea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa thamani ya shilingi. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali, mwenendo wa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Marekani umekuwa tulivu kutokana na usimamizi na utekelezaji madhubuti wa Sera ya Fedha na Bajeti. Hata hivyo, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa kwa mwaka 2016 na 2017, Dola moja ya Marekani ilibadilishwa katika kiwango cha Sh.2,199.3 na Sh.2,242.9. Viwango hivi ni zaidi ya lengo la Sh.2,185.22 iliyojivekea Serikali katika malengo yake ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri ili kuwa na suluhisho la kudumu la kutengemaa kwa thamani ya shilingi, Serikali iongezee mauzo ya bidhaa na huduma nje ili kupunguza nakisi ya urari wa biashara. Aidha, msisitizo uwekwe katika uuzaji nje wa mazao ya kahawa, korosho, karafuu, tumbaku, chai, mkonge pamoja na madini ili kusaidia kupunguza nakisi ya urari wa biashara. Ni muhilmu Serikali ikaanzisha Mfuko wa Kulinda Bei ya Mazao kwenye Soko (*Price Stabilization Fund*) ili kuongeza bei ya mazao yetu katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Serikali. Deni la Serikali limeendelea kukua kutoka Dola za Kimarekani milioni 21,623.26 Juni 2017 hadi Dola za Kimarekani milioni 23,234.26 Juni 2018. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 39.4 ya Pato la Taifa limetokana na Serikali kuendelea kukopa kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali, deni letu linaonekana ni himilivu. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa Serikali iijipime na kuweka ukomo kwenye uwiano wa ulipaji wa deni na mapato ya ndani ili kuona athari yake kiuchumi na kibajeti.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya kibiashara. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inapunguza kukopa kwenye mikopo ya masharti ya kibiashara (*non-concessional borrowing*) kwani ina riba kubwa na kwenye vyanzo vya ndani. Hatua hii itasaidia kupunguza mzigo mkubwa wa ugharamiaji wa mikopo hiyo kuitia ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kudumaza ushindani na ukopeshaji kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa mikopo kwa sekta binafsi imeimarika. Hata hivyo, benki zetu nyingi zipo katika mifumo ya kibiashara na zinajielekeza kukopesha zaidi kwenye shughuli binafsi, biashara na kiasi viwanda. Bado kuna changamoto kwa benki hizi kukopesha wakulima mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu. Serikali inatakiwa kuhakikisha inatatua changamoto hii ili kusaidia ukuaji wa shughuli za kilimo ambazo zina mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019. Kamati pia ilipata fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu (2016/2017 - 2018/2019) na Mpango wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021). Tathmini hiyo ilifanywa kwa kuchambua taarifa illyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango ikiainisha miradi mbalimbali iliyopangwa kutekelezwa, fedha zilizotumika na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika kipindi hicho. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuwasilisha taarifa hiyo kwa kuwa ni mara ya kwanza Serikali inawasilisha Bungeni taarifa ya aina hiyo katika kipindi kama hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa hiyo uliofanywa na Kamati umebaini kuwa Serikali imeweza kusimamia na kutekeleza miradi ya kielelezo (*flagship projects*) ambayo ina lengo la kuchochea uchumi jumla, maendeleo ya viwanda na kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudhi hizo za Serikali, bado kuna changamoto ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi nazo ni zifuatazo:-

(i) Serikali kuchukua muda mrefu kufanya maamuzi kwenye baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo ina manufaa makubwa kwa Taifa. Mfano, Mradi wa Chuma na Makaa ya Mawe ya Liganga na Mchuchuma hadi hivi sasa Serikali bado haijafanya uamuzi. Mfano mwingine ni Serikali

haijawekeza vya kutosha katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu, mathalani ujenzi wa Bandari ya Uvuvi. (*Makofi*)

(ii) Kubadilika badilika kwa vipaumbele na maamuzi kwenye utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo, mathalani mradi wa *Chalinze Express Way*, uendelezaji wa mradi wa *Kurasini Logistics Centre* na Bandari ya Bagamoyo ambapo hatma yake bado haijulikani;

(iii) Kuongeza kasi ya uendelezwaji na uboreshwaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege itakayoendana na kasi ya ununuzi wa ndege;

(iv) Kusuasua kwa ulipaji wa fidia na uendelezaji wa miundombinu katika maeneo maalum ya uwekezaji (*SEZ*) na maeneo ya uzalishaji bidhaa za kuuza nje (*EPZ*);

(v) Upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ilioainishwa katika mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2019/2020. Kamati imepitia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa 2019/2020. Mwongozo umeelekeza Maafisa Masuuli kuzingatia masuala ya msingi ya kisheria, kisera na kikanuni katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/2020. Aidha, mwongozo umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ikiwemo kuandaa mipango inayozingatia mahitaji halisi ya rasilimali fedha, udhibiti wa matumizi yasiyo ya lazima, matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato na malipo ya mtandao, uingizaji wa takwimu za bajeti ya Serikali kwenye mifumo na *PlanRep* na miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya Halmashauri pamoja na ulipaji na udhibiti wa ulimbikizaji wa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makisio ya awali ya bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020 yanaonesha kuwa jumla

ya shilingi triliuni 33.5 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.2 ukillinganisha na shilingi triliuni 32.47 kwa mwaka 2018/2019. Kati ya fedha hizo shilingi triliuni 23.20 sawa na asilimia 69.25 ya bajeti yote zinatokana na mapato ya ndani ambapo mapato ya halmashauri yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 795.68. Mapato ya kodi shilingi triliuni 20.12 na mapato yasiyo ya kodi shilingi triliuni 2.28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inategemea kupata kiasi cha shilingi triliuni 3.38 ikiwa ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 26.3 ikillinganishwa na shilingi triliuni 2.67 kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mwongozo kuainisha maeneo ambayo yatasaidia upatikanaji wa fedha za kugharamia mpango na Bajeti ya Serikali, ni mategemeo ya Kamati kuwa Serikali itajielekeza pia katika kuangalia vyanzo vingine vyataga mapato yanayoweza kusaidia kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kuhakikisha inatekeleza mpango kazi wa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo yaani *DCF* ambapo kwa hatua hiyo inatarajia kuwa misaada na mikopo hii itapatikana kwa wakati na hivyo kufikia malengo.

Mheshimiwa Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo umeainisha mapitio ya utekelezaji wa Bajeti kwa baadhi ya sekta na miradi ya kimkakati yenye lengo la kuchochea uchumi jumla. Maendeleo ya viwanda na kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Hata hivyo, bado Serikali haijaweza kufanya vizuri katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kamati inaendelea kushauri kuwa mwongozo unaokuja unahitajika kujielekeza zaidi katika kufungamanisha programu za maendeleo kwenye sekta hizi na nyingine ili ziweze kuleta tija kwenye ukuaji wa uchumi. Aidha, sekta hizi zipewe kipaumbele zaidi katika mpango wa bajeti ili michango yake isaidie katika kuendeleza na kukuza uchumi wa Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini bado kuna tatizo la upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miradi ya *PPP*. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Maafisa Masuuli wanazingatia maelekezo ya mwongozo yaliyotolewa kwenye utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya Umma na sekta binafsi hasa kwa upande wa kuchambua na kuainisha miradi yenye sifa ya utekelezaji kwa utaratibu wa ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya maboresho ya utendaji na usimamizi wa Mashirika ya Umma. Hatua hii itasaidia Taasisi na Mashirika ya Umma kuongeza ufanisi na tija na kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hiyo, pamoja na pongezi hizi Serikali ihakikishe inatimiza mahitaji ya kibajeti kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma kama yanavyoomba na kuidhinishwa katika bajeti zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2019/2020; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/2020 yanatoa taswira ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/2020 utakavyokuwa. Aidha, mapendekezo ya Mpango huu yanatoa maelezo kuhusu utekelezaji, ugharamiaji, ufuataliaji, tathmini na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yaliyowasilishwa na kufanya majadiliano ya kina na Serikali. Katika majadiliano hayo Kamati ilitoa maoni na ushauri. Hivyo ni matumani ya Kamati kuwa Serikali itazingatia wakati wa maboresho ya Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majadiliano yaliyofanyika kati ya Kamati na Serikali, Kamati ingependa kutoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

- (i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujumuishwaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Mwaka

uliopita; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020 hayana budi kuoanisha/kuendeleza vipaumbele ambavyo havikutekelezwa kwa asilimia 100 katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/2018 na Miradi ambayo Serikali imekwisha wekeza fedha au imeanza kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwepo kwa baadhi ya Miradi ya Maendeleo ambayo ilainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019 lakini haionekani katika Mapendekezo ya Mpango wa Mwaka 2019/2020. Miradi hiyo ni pamoja na:-

- (i) Mradi wa Magadi Soda–Bonde la Engaruka;
- (ii) Kuanzisha Maeneo Maalum ya Uwekezaji Tanga, Bunda na Manyara;
- (iii) Uanzishwaji wa Mashamba ya Miwa na Viwanda vya Sukari;
- (iv) Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo; na
- (v) Mradi wa Chalinze *Express way*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona ni vyema Miradi hii ikajumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Misingi na Shabaha ya Mapendekezo ya Mpango; mapendekezo ya Mpango huu yamejikita katika kufanikisha na kutekeleza malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano hususan kwa miradi ambayo utekelezaji wake unaendelea. Kamati inaona kuwa mapendekezo ya Mpango huu yawe ni dira ya kuagiza na kujenga nidhamu kwa vyombo vikuu vya kupanga, kufuatilia, kutathmini na kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi na shabaha ya mpango huu ijielekeze pia katika kujibu changamoto na vikwazo vyta kimfumo vilivyojitokeza katika kuendesha na kusimamia uchumi katika Mpango unaoendelea kutekelezwa, muda wa utekelezaji wa mradi, kujenga nidhamu ya kazi, uimarishaji wa umakini katika kubuni, kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kufungamanisha Sera na Mikakati ya Serikali kwenye mapendekezo ya Mpango ya Maendeleo; Mapendekezo ya Mpango hayaoneshi moja kwa moja muunganiko uliopo wa Sera na mikakati ya Serikali kwenye Mipango ya Maendeleo iliyoinishwa na miradi mingine imetekelezwa chini ya kiwango kilichotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani Mradi muhimu kama ule wa *SAGCOT* umetekelezwa kwa kiwango cha asilimia nane tu licha ya umuhimu wake kiuchumi. Kamati inashauri, Mapendekezo ya Mpango huu yaoneshe moja kwa moja muunganiko wake na sera na mikakati ya Serikali na mpango husika. Mfano ni mradi wa *ASDP II (Agricultural Strategic Development Plan)*, Mpango Kabambe wa Kuinua Utalii (*Tourism Master Plan*) Mpango wa Kuboresha Mfumo na Uhibiti wa Mazingira ya Biashara na mkakati wa kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza miradi yenye kuchochera upatikanaji wa mapato pamoja na Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa Sekta ya Viwanda (*Integrated Industrial Development Strategy and Master Plan*) ambao unainua mwambao wa Pwani kuwa kitovu cha kuendeleza viwanda na kukuza mauzo ya nje ikiwa ni pamoja na kulenga kufanya usindikaji wa mwanzo kwenye maeneo ya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugharamiaji wa miradi ya vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mapendekezo ya mpango wa maendeleo; Mapendekezo ya Mpango huu yameainisha vyanzo mbalimbali vyta mapato ya kugharamia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2019/2020, ambavyo

kwa ujumla vinatarajiwa kutoa takribani shilingi trillioni 12.384 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo sawa na asilimia 37 ya bajeti yote ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa bado kuna mwenendo usioridhisha wa utoaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Mathalani kwa mwaka wa fedha 2016/2017, bajeti ya maendeleo ilikuwa jumla ya shilingi trillioni 11.82 na fedha iliyotolewa ilikuwa jumla ya shilingi trillioni 6.489 sawa na asilimia 55 ya lengo. Mwaka 2017/2018 fedha iliyoidhinishwa ilikuwa jumla ya shilingi trillioni 11.432 kiasi kilichotolewa ni shilingi trillioni 6.54 sawa na asilimia 57 tu. Kutokufikiwa kwa lengo kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kutopatikana kwa mikopo na misaada ya kibajeti kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuziba nakisi ya bajeti ya maendeleo. Aidha, Serikali iendelee kukopa mikopo yenye masharti nafuu kutoka ndani na nje ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kufungamanisha Sekta ya Kilimo, Uvuvi, Mifugo na maendeleo ya Viwanda; Mpango ya Maendeleo wa Miaka Mitano umejielekeza katika kuhakikisha tunafikia uchumi wa viwanda. Kufungamanishwa kwa sekta zinazotegemeana kuna nafasi kubwa ya kuwezesha nchi kufikia lengo hili mathalani ukuaji wa sekta ya viwanda unategemea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa sekta kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia inaonesha kuwa mapinduzi katika sekta ya kilimo yamechangia sana katika mapinduzi ya viwanda kwa nchi nyngi Duniani zikiwemo Uingereza, Marekani, China, Brazil, India na Ujeruman. Hata hivyo, hapa nchini sekta ya kilimo bado ina changamoto kubwa katika kuhakikisha inazalisha malighafi za kutosha kwa ajili ya mapinduzi ya viwanda. Ili kuhakikisha hatua hii inafikiwa Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

- (i) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi;
- (ii) Upatikanaji wa pembejeo za kilimo za kutosha kwa wakati na kwa bei nafuu;
- (iii) Kuendeleza vituo vya utafiti ili viweze kuzalisha mbegu bora, za kutosha, zinazopatikana kwa bei nafuu na kwa wakati;
- (iv) Kuhakikisha upatikanaji wa nyenzo muhimu za uvuvi na kwa bei rahisi;
- (v) Kuhamasisha na kukuza kilimo cha umwagiliaji;
- (vi) Kuboresha masoko ya mazao ya kilimo na mifugo;
- (vii) Kuweka mazingira wezeshi ya kilimo cha mkataba ili kiwe na manufaa na faida kwa wahusika wote' na
- (viii) Kujenga mazingira wezeshi ya ufugaji wenyewe tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba endapo changamoto hizo zitatatuliwa na Serikali ni wazi kwamba kilimo kitakuwa na mchango mkubwa katika mageuzi ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga mazingira wezeshi ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya maendeleo ya viwanda; moja ya changamoto inayowakabili wawekezaji ni kutopatikana kwa wakati kwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Asilimia kubwa ya ardhi nchini haina mpango wa matumizi bora ya ardhi, hivyo kusababisha wawekezaji kuchukua muda mrefu kupata maeneo ya uwekezaji na wakati mwagine kukata tamaa na kulazimika kuwekeza nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na changamoto hizi, Kamati inaishauri Serikali iharakishe mkakati wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo ya vijiji, wilaya na mikoa ili kurahisisha uwekezaji na maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji wa Sekta ya Viwanda vidogo; Kamati inatambua hatua mbalimbali ambazo Serikali imeendelea kuzichukua katika kuweka mazingira wezesi ya uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Uanzishwaji wa viwanda vidogo ambavyo kimsingi havigitaji mtaji mkubwa ni rahisi kwa Mtanzania wa hali ya kawaida kuvimiliki na kuviendesha. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Mpango huu ukajielekeza katika kuweka mazingira wezesi ya uanzishaji wa viwanda vidogo ambavyo vitatumia malighafi za hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivyo vilenge kuzalisha bidhaa zitakazokidhi viwango vya kimataifa na kuweza kuwa na ushindani katika soko la Afrika Mashariki na nchi nyingine za jirani. Aidha, Kamati inaona kuwa moja ya kichocheo kikubwa cha kuleta mapinduzi ya haraka katika ukuaji wa viwanda vidogo ni uwepo wa *SIDO* imara. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwezo wa utendaji wa *SIDO* kwa kutenga rasilimali fedha na watu ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango; mwongozo umeainisha maeneo ambayo yatagharamia nakisi ya bajeti hasa kwa upande wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali ipunguze kukopa zaidi kwenye soko la ndani la fedha na ijielekeze kukopa nje ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani na wajasiriamali kukopa kwenye soko la ndani la fedha na hivyo kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo (*Flagship Projects*); Kamati inapongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza miradi ya Kielelezo kama vile mradi wa kuzalisha umeme wa Rufiji, mradi wa ujenzi wa reli ya kati

kwa kiwango cha *standard gauge* na mradi wa kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania. Miradi hii itakapokamiliika itakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo katika sekta za viwanda, nishati, biashara, utalii, usafirishaji na kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kumekuwa na utekelezaji usioridhisha wa baadhi ya miradi mikubwa ambayo ingeleta manufaa makubwa kwa Taifa. Miradi hiyo ni ujenzi wa kiwanda cha chuma Liganga, kama nilivyoeleza; na ujenzi wa Reli ya Mtwara - Mbamba Bay na matawi yake ya kwenda Liganga na Mchuchuma; Ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Gesi ya Asili (*LNG*) – Lindi; Uanzishwaji wa maeneo maalumu ya kuchakata gesi pamoja na bidhaa zake yaani Mtwara *Petrochemical Special Economic Zone*; Mradi wa Magadi Soda Engaruka katika Ziwa Manyara; Uanzishwaji wa maeneo maalum ya uwekezaji Bagamoyo unaojumuisha ujenzi wa bandari; na Uanzishwaji wa kituo cha biashara na huduma cha Kurasini (*Kurasini Logistics Centre*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvuvi katika Bahari Kuu na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi; Bunge limekuwa likiishauri Serikali kwa muda mrefu kuhusu rasilimali na mapato yatokanayo na uvuvi katika bahari kuu ndani ya mipaka ya nchi yetu. Kamati inatambua na kuunga mkono mpango wa Serikali wa kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania pamoja na nia ya kujenga bandari ya uvuvi. Hata hivyo, utekelezaji wake umechukua muda mrefu, hadi sasa eneo la ujenzi wa Bandari hiyo halijabainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuleta mafanikio ya haraka katika eneo hili, Kamati inashauri Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

(i) Ibainishe eneo ambalo bandari ya uvuvi itajengwa ili iweze mikakati ya kuanza kujenga haraka iwezekanavyo;

(ii) Iweke mikakati ya kujenga bandari za uvuvi nyingine zisizopungua mbili katika ukanda wa Bahari ya Hindi; na

(iii) Ifanye tathmini ya vifaa na miundombinu ya uvuvi ambayo ilibinafsishwa na haitumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uimarishaji wa Benki ya Rasilimali na Benki ya Kilimo; Uwekezaji katika Sekta ya Viwanda na Kilimo hasa kilimo cha mazao ya biashara unahitaji mtaji mkubwa na huchukua muda mrefu kuzalisha faida pamoja na kuwa na vihatarishi vingi. Mazingira hayo yamesababisha benki nyingi za kibiashara kutovutiwa kutoa mikopo kwa sekta hizo. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Benki ya Rasilimali (*TIB*) na Benki ya Kilimo (*TADB*) kwa kuziongezea mitaji ili ziweze kutoa mikopo kwa sekta hizo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo na Ushiriki wa Sekta Binafsi; moja ya changamoto kubwa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ni kutopatikana kwa rasilimali fedha. Kutopatikana kwa rasilimali fedha kumechangiwa na Serikali kutegemea vyanzo vilivyozoeleka na kutoshirikisha ipasavyo sekta binafsi katika kugharamia miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia ipasavyo mikakati ya kuvutia na kuwezesha Sekta Binafsi kushiriki katika utekelezaji wa Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsus, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati na shule; endapo hili halitafanyika Serikali itakuwa inawavunja moyo wananchi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo; (*Makof*)

(ii) Serikali ihakikishe inalipa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji ambao wamekwisha wasilisha hati ya malipo (*Performance Certificate*) na bado hawajalipwa hivyo kusababisha miradi kutoamili. Aidha, Serikali itekelze kikamilifu miradi maji ambayo bado haijakamilishwa;

- (iii) Serikali ianze kutenga kiwango cha asilimia moja (1%) ya Pato la Taifa kwa ajili ya shughuli za Utafiti na maendeleo;
- (iv) Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha na kuratibu ipasavyo tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili iweze kuleta manufaa yaliyotarajiwaa;
- (v) Serikali ihakikishe inatekeleza mikakati iliyojiwekea kwa vitendo ili kukabiliana na vihatarishi kama ilivyoainishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango. Hatua hii itasaidia kuwa na Mpango unaotekelezeaka na kufika malengo yaliyokusudiwa pamoja na kutekeleza kifungu cha 35(1) hadi (4) nya Sheria ya Bajeti kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na majanga;
- (vi) Serikali ihakikishe inatoa mafunzo ya kutosha kwa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uandaaji wa maandiko ya miradi itakayotekelawa kwa njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
- (vii) Serikali iweke mkakati wa kuvilinda viwanda vya ndani ambavyo vinazalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje pamoja na kuchocheara uzalishaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuzalishwa nchini;
- (viii) Kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika Sekta ya Mafuta na Gesi, Serikali iongeze juhudii za kuiendeleza sekta hii ili iweze kuchangia katika ukuaji wa uchumi;
- (ix) Serikali ihakikishe inatekeleza kikamilifu Mkakati wa Urasimishaji wa Mali na Biashara Tanzania (MKURABITA) ili kupunguza sekta isiyo rasmi na kuongeza ukusanyaji wa mapato;
- (x) Serikali iziwezeshe kifedha Taasisi zake hasa majeshi yake ili yaweze kutengeneza bidhaa zinazotumika katika

majeshi hayo pamoja na mashulenii kama vile sare za watoto wa shule na viatu;

(xi) Serikali ihakikishe inatenga mapato yatokanayo na gesi kama inavyotaka Sheria ya *Oil and Gas* yaani (*Revenue Management*) Act...

MWENYEKITI: Bado dakika moja Mwenyekiti.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE – (MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI): Yaani *Oil and Gas (Revenue Management) Act, 2015* ili zitumike kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kumshukuru, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, kwa ushirikiano walio tupata katika Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali na naomba kuwatambua wajumbe hao lakini sitotaja, lakini naomba waingie kwenye *Hansard* kwa idadi ya Wajumbe wanao julikana katika Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, natambua mchango mkubwa wa Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na ndugu Lina Kitosi na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kuwasilisha na kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa George Simbachawene kwa kuipitia taarifa ya Kamati yako vizuri kabisa na kwa ufasaha, tunakushukuru sana. (*Makofî*)

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU
MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA
TAIFA PAMOJA NA MWONGOZO WA MAANDALIZI
YA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA
2019/2020 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kujadiliana kwa kina na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendeleko ya Mpango huu. Aidha, katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilipitia na kujadili Mpango wa miaka Tano (2016/2017 – 2020/2021), Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa miaka Mitatu (2016/2017 – 2018/2019) pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025. Lengo la kupitia Taarifa hizo lilikuwa ni kupata mwelekeo wa utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano kupitia mipango ya Taifa inayotekelizwa kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja.

**2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI JUMLA KWA KIPINDI
CHA MWAKA 2017**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua hali ya uchumi inayotokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2016/2017-2017/2018. Maeneo yaliyofanyiwa uchambuzi ni Pato la Taifa, Mfumuko wa Bei, Mwenendo wa Thamani shilingi, Deni la Serikali, urari wa biashara na mikopo kwa sekta binafsi kama ilivyoainishwa katika jedwali Na. 1 hapo chini.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na. 1: VIASHIRIA VYA HALI YA UCHUMI KATIKA MWAKA 2016/2017 – 2017/2018

Na.	Kiashiria	Malengo ya Mpango wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021)	Hali ya Utekelezaji	
			2016/2017	2017/2018
1.	Ukuaji wa Uchumi	10.0	7.1	7.2
2.	Mfumuko wa bei	5	5.3	4.3
3.	Deni la Serikali	-	21,623.26	23,234.26
4.	Mwenendo wa Thamani ya shilingi	2,185.62	2,199.3	2,242.9
5.	Vivango vya riba kwa sekta binafsi	-	16.61	17.83
6.	Urari wa biashara (usd bilioni)	-	(1,437.8)	(1,778.0)
7.	Ukuaji wa sekta ya kilimo	7.6	6.4	6.7

Chanzo Wizara ya Fedha na Mpango.

2.1 Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Ukuaji wa Pato la Taifa ni mojawapo ya vigezo vya kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umaskini. Takwimu zinaonesha kuwa Pato la Taifa limekuwa kwa kiasi cha asilimia 7.2 kwa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na asilimia 7.1 kwa mwaka 2016/2017. Mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi ni wa kuridhisha na malengo ya Serikali ni kufikia kiwango cha asilimia 10 ifikapo mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukuaji huu mzuri wa uchumi lazima Serikali ifungamanishe ukuaji huu wa uchumi na ukuaji wa kipato cha mwananchi wa kawaida. Hatua hii itaweza kufanikiwa kama Serikali itaongeza bajeti na kuwekeza kwenye sekta zinazo ajiri wananchi walio wengi kama Kilimo, mifugo na uvuvi ili zilete ufanisi katika uchumi.

2.2 Mfumuko wa bei

Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa bei umeendelea kuwa kwenye kiwango cha chini na kubaki katika wigo wa tarakimu moja kutoka asilimia 5.3 kwa mwaka 2016/2017 hadi asilimia 4.3 kwa mwaka 2017/18. Serikali inategemea kuwa mfumuko wa bei utaendelea kuwa chini kwa kiwango cha tarakimu moja ili uweze kufikia lengo la asilimia 5 ifikapo mwaka 2020/2021. Kamati inashauri kuwa hatua hii inaweza kufikiwa iwapo Serikali itaendelea na jitihada za kuhakikisha kunakuwepo na udhibiti wa bei ya mafuta kulingana na bei ya soko la dunia, uwepo wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani pamoja na udhibiti wa sera ya fedha zinazolenga kutunza thamani ya fedha kwa kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili kuchochaea ukuaji wa uchumi.

2.3 Mwenendo wa thamani ya shilingi

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Maelezo ya Serikali, mwenendo wa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Marekani umekuwa tulivu kutohana na usimamizi na utekelezaji madhubuti wa Sera za Fedha na Bajeti. Hata hivyo, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa kwa mwaka 2016 na 2017 Dola moja ya Marekani ilibadilishwa katika kiwango cha shilingi 2,199.3 na 2,242.9. Viwango hivi ni zaidi ya lengo la shilingi 2,185.22 iliyojiwekea Serikali katika malengo yake ya miaka mitano. Kamati inashauri Serikali ili kuwa na suluhisho la kudumu la kutengemaa kwa thamani ya shilingi, Serikali iongezee mauzo ya bidhaa na huduma nje ili kupunguza nakisi ya urari wa biashara. Aidha, msisitizo uwekwe katika uuzaaji nje wa mazao ya kahawa, korosho, karafuu, tumbaku, chai, mkonge pamoja na madini ili kusaidia kupunguza nakisi ya urari wa biashara. Ni muhimu Serikali ikaanzisha Mfuko wa kulinda bei ya mazao kwenye soko *"Price Stabilization Fund"* ili kuongeza bei ya mazao yetu katika soko la Dunia.

2.4 Deni la Serikali

Mheshimiwa Spika, Deni la Serikali limeendelea kukua kutoka Dola za Kimarekani milioni 21,623.26 (Juni 2017) hadi Dola za Kimarekani milioni 23,234.26 (Juni 2018) Ongezeko hili (sawa na asilimia 39.4 ya Pato la Taifa) limetokana na Serikali kuendelea kukopa kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali Deni letu linaonekana ni himilivu (*Debt Sustainability Analysis - DSA*). Hata hivyo Kamati inashauri kuwa Serikali ijpime na kuweka ukomo kwenye uwiano wa ulipaji wa deni na Mapato ya ndani ili kuona athari yake kiuchumi na kibajeti.

2.5 Mikopo ya kibiashara

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri serikali kuhakikisha inapunguza kukopa kwenye mikopo ya masharti ya kibiashara (*non-concessional borrowing*) ambayo ina riba kubwa na kwenye vyanzo vya ndani. Hatua hii itasaidia kupunguza mzigo mkubwa wa ugharamiaji wa mikopo hiyo kuititia ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kudumaza ushindani na ukopeshaji kwa sekta binafsi (*cloud-out effects*).

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa mikopo kwa sekta binafsi imeimarika. Hata hivyo, Benki zetu nyingi zipo katika mifumo ya kibiashara na zinajielekeza kukopesha zaidi kwenye shughuli binafsi, biashara na kiasi viwanda. Bado kuna changamoto kwa benki hizi kukopesha wakulima mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu. Serikali inatakiwa kuhakikisha inatatura changamoto hii ili kusaidia ukujaji wa shughuli za kilimo ambazo zina mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

3.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu (2016/17 - 2018/19) ya Mpango wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Tathmini hiyo ilifanywa kwa kuchambua Taarifa iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango ikiainisha miradi mbalimbali iliyopangwa kutekelezwa, fedha zilizotumika na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika kipindi hicho. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuwasilisha Taarifa hiyo kwa kuwa ni mara ya kwanza Serikali inawasilisha Bungeni Taarifa ya aina hiyo katika kipindi kama hiki.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa hiyo uliofanywa na Kamati umebaini kuwa Serikali imeweza kusimamia na kutekeleza miradi ya kielelezo ya maendeleo (flagship projects) ambayo ina lengo la kuchochea uchumi jumla, maendeleo ya viwanda na kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo za Serikali bado kuna changamoto ambazo zinakatikiwa kufanyiwa kazi nazo ni: -

- i) Serikali kuchukua muda mrefu kufanya maamuzi kwenye baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo ina manufaa makubwa kwa Taifa. Mfano:
 - Mradi wa chuma na Makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma hadi hivi sasa Serikali bado haijafanya uamuzi.
 - Serikali haijawekeza vya kutosha katika Sekta ya uvuvi wa bahari kuu, mathalani ujenzi wa Bandari ya Uvuvi.

- ii) Kubadilika badilika kwa vipaumbele na maamuzi kwenye utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo, mathalani; mradi wa *Chalinze Express way*, uendelezaji wa mradi wa *Kurasini Logistics Centre* na bandari ya Bagamoyo ambapo hatma yake bado hajajulikana;
- iii) Kuongeza kasi ya uendelezwaji na uboreshwaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege itakayoendana na kasi ya ununuzi wa ndege;
- iv) Kusuasua kwa ulipaji wa fidia na uendelezaji wa miundombinu katika maeneo maalum ya uwekezaji (SEZ) na maeneo ya uzalishaji bidhaa za kuuza nje (EPZ); na
- v) Upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ilioainishwa katika mpango.

4.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa 2019/2020. Mwongozo umeelekeza Maafisa Masuuli kuzingatia masuala ya msingi ya kisheria, kisera na kikanuni katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/2020. Aidha, Mwongozo umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ikiwemo kuandaa mipango inayozingatia mahitaji halisi ya rasilimali fedha, udhibiti wa matumizi yasiyo ya lazima, matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato na malipo ya mtandao (GePG), uingizaji wa takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep, mradi

ya kimkakati ya kuongeza mapato ya Halmashauri (SGRP) pamoja na ulipaji na udhibiti wa ulimbikizaji wa madeni.

Mheshimiwa Spika, makisio ya awali ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2019/20 yanaonesha kuwa jumla ya **shilingi trilioni 33.5** zinatarajiwa kukusanywa na kutumika kwa kipindi cha mwaka 2019/20 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 3.2** ukilinganisha na **shilingi trilioni 32.47** kwa mwaka 2018/19. Kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 23.20** sawa na **asilimia 69.25** ya Bajeti yote zitatokana na mapato ya ndani ambapo mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa **shilingi bilioni 795.68**, mapato ya kodi **shilingi trilioni 20.12** na mapato yasiyo ya kodi **shilingi trilioni 2.28**. Serikali inategemea kupata kiasi cha **shilingi trilioni 3.38** ikiwa ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **asilimia 26.3** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 2.67** kwa mwaka 2018/19.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mwongozo kuainisha maeneo ambayo yatasaidia upatikanaji wa fedha za kugharamia mpango na Bajeti ya Serikali, ni mategemeo ya Kamati kuwa Serikali itajielekeza pia katika kuangalia vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kuhakikisha inatekeleza Mpango kazi wa Kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) ambapo kwa hatua hiyo inatarajia kuwa misaada na mikopo hii itapatikana kwa wakati na hivyo kufikia malengo.

Mheshimiwa Spika, mwongozo umeainisha mapitio ya utekelezaji wa Bajeti kwa baadhi ya sekta na miradi ya kimkakati yenye lengo la kuchochea uchumi jumla, maendeleo ya viwanda na kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Hata hivyo, bado Serikali hajjaweza kufanya vizuri katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kamati inaendelea kushauri kuwa

mwongozo unaokuja unahitajika kujielekeza zaidi katika kufungamanisha programu za maendeleo kwenye sekta hizi na nyingine ili ziweze kuleta tija kwenye ukuaji wa uchumi. Aidha sekta hizi zipewe kipaumbele zaidi katika mpango wa bajeti ili michango yake isaidie katika kuendeleza na kukuza uchumi wa Viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini bado kuna tatizo la upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya Maendeleo na miradi ya PPP. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha maafisa masuuli wanazingatia maelekezo ya mwongozo yaliyotolewa kwenye utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya Umma na sekta binafsi hasa kwa upande wa kuchambua na kuainisha miradi yenye sifa za kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya maboresho ya utendaji na usimamizi wa mashirika ya Umma. Hatua hii itasaidia taasisi na mashirika ya umma kuongeza ufanisi na tija na kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizi Serikali ihakikishe inatimiza mahitaji ya kibajeti kwenye taasisi na mashirika ya Umma kama yanavyoomba na kuidhinishwa katika bajeti zao.

5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/2020 yanatoa taswira ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2019/2020 utakavyokuwa. Aidha, mapendekezo ya Mpango huu yanatoa maelezo kuhusu utekelezaji, ugharamiaji, ufuatiliaji, tathmini na vihatarishi vyaa utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yaliyowasilishwa na kufanya majadiliano ya kina na Serikali. Katika majadiliano hayo Kamati ilitoa maoni na ushauri. Hivyo ni matumani ya Kamati kuwa Serikali itazingatia wakati wa maboresho ya Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa spika, pamoja na majadiliano yaliyofanyika kati ya Kamati na Serikali, Kamati ingependa kutoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

5.1. Ujumuishwaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Mwaka uliopita

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020 hayana budi kuoanisha/kuendeleza vipaumbele ambavyo havikutekelezwa kwa asilimia mia moja katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/2018 na Miradi ambayo Serikali imekwisha wekeza fedha au imeanza kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Miradi husika.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwepo kwa baadhi ya Miradi ya Maendeleo ambayo iliainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019 lakini halonekani katika Mapendekezo ya Mpango wa Mwaka 2019/2020. Miradi hiyo ni pamoja na;

i.Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka;

ii.Kuanzisha Maeneo Maalum ya Uwekezaji Tanga, Bunda na Manyara;

iii.Uanzishwaji wa Mashamba ya Miwa na Viwanda vyta Sukari;

iv.Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo; na

v.Mradi wa Chalinze Express way.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ni vyema Miradi hii ikajumuishwa katika Mpango wa maendeleo wa Mwaka 2019/2020.

5.2. Usimamizi wa Misingi na Shabaha ya Mapendekezo ya Mpango

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango huu yamejikita katika kufanikisha na kutekeleza malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano hususan kwa miradi ambayo utekelezaji wake unaendelea. Kamati inaona kuwa mapendekezo ya Mpango huu yawe ni dira ya kuagiza na kujenga nidhamu kwa vyombo vikuu vya kupanga, kufuatilia, kutathmini na kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, Misingi na shabaha ya mpango huu ijielekeze pia katika kujibu changamoto na vikwazo vya kimfumo vilivyojitokeza katika kuendesha na kusimamia uchumi katika Mpango unaoendelea kutekelezwa, muda wa utekelezaji wa miradi, kujenga nidhamu ya kazi, uimarishaji wa umakini katika kubuni, kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo.

5.3. Kufungamanisha Sera na Mikakati ya Serikali kwenye mapendekezo ya Mpango ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango hayaoneshi moja kwa moja muunganiko uliopo wa Sera na mikakati ya Serikali kwenye Mipango ya Maendeleo ilivoainishwa na miradi mingine imeteklezwa chini ya kiwango kilichotakiwa. Mathalani Mradi muhimu kama ule wa SAGCOT umeteklezwa kwa kiwango cha asilimia Nane (8) licha ya umuhimu wake kiuchumi. Kamati inashauri, Mapendekezo ya Mpango huu yaoneshe moja kwa moja muunganiko wake na sera na mikakati ya Serikali na mpango husika. Mfano ni mradi wa ASDP //

(Agriculture Strategic Development Plan), Mpango kabambe wa kuinua utalii (Tourism Master Plan), Mpango wa Uboresha Mfumo na Udhibiti wa Mazingira ya Biashara (Blueprint for Regulatory Reform to Improve Business Environment), Mkakati wa kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza miradi yenye kuchochaea upatikanaji wa mapato pamoja na Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa Sekta ya Viwanda (Integrated Industrial Development Strategy and Master Plan) ambao unaibua mwambao wa Pwani kuwa kitovu cha kuendeleza Viwanda na kukuza mauzo nje (Water Front Industrial and Export Frontiers) ikiwa ni pamoja na kulenga kufanya usindikaji wa mwanzo (*primary processing*) kwenye maeneo ya mbalimbali.

5.4. Ugharamiaji wa miradi ya vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mapendekezo ya mpango wa maendeleo

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango huu yameainisha vyanzo mbalimbali vya mapato ya kugharamia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2019/20 ambavyo kwa ujumla vinatarajiwu kutoa takribani shilingi trillioni 12.384 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo sawa na asilimia 37 ya bajeti yote ya Serikali. Takwimu zinaonyesha kuwa bado kuna mwenendo usioridhisha wa utoaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, mathalani kwa mwaka wa fedha 2016/17 bajeti ya maendeleo ilikuwa jumla ya **shilingi trillioni 11.82** na fedha iliyotolewa ilikuwa jumla ya **shilingi trillioni 6.489** sawa na **asilimia 55** ya lengo; Mwaka 2017/18 fedha iliyoidhinishwa ilikuwa jumla ya **shilingi trillioni 11.432** kiasi kilichotolewa ni **shilingi trillioni 6.54** sawa na **asilimia 57** tu. Kutokufikiwa kwa lengo kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kutopatikana kwa mikopo na misaada ya kibajeti kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya

ndani ili kuziba nakisi ya bajeti ya maendeleo. Aidha, Serikali iendelee kukopa mikopo yenyenye masharti nafuu kutoka ndani na nje ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

5.5. Kufungamanisha Sekta Kilimo, Uvuvi, Mifugo na maendeleo ya Viwanda

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano umejielekeza katika kuhakikisha tunafikia uchumi wa viwanda. Kufungamanishwa kwa sekta zinazotegemeana kuna nafasi kubwa ya kuwezesha nchi kufikia lengo hili mathalani ukuaji wa sekta ya viwanda unategemea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa sekta kilimo. Historia inaonesha kuwa mapinduzi katika sekta ya kilimo yamechangia sana katika mapinduzi ya viwanda kwa nchi nydingi Duniani zikiwemo Uingereza, Marekani, China, Brazil, India na Ujeruman. Hata hivyo hapa nchini sekta ya kilimo bado ina changamoto kubwa katika kuhakikisha inazalisha malighafi za kutosha kwa ajili ya mapinduzi ya viwanda. Ili kuhakikisha hatua hii inafikiwa Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

- i. Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa Sekta ya Kilimo, mifugo na uvuvi nchini;
- ii. Upatikanaji wa pembejeo za kilimo za kutosha kwa wakati na kwa bei nafuu;
- iii. Kuendeleza vituo vya utafiti ili viweze kuzalisha mbegu bora, za kutosha, zinazopatikana kwa bei nafuu na kwa wakati;
- iv. Kuhakikisha upatikanaji wa nyenzo muhimu za uvuvi na kwa bei rahisi;
- v. Kuhamasisha na kukuza kilimo cha umwagiliaji;

- vi. Kuboresha masoko ya mazao ya kilimo na mifugo;
- vii. Kuweka mazingira wezeshi ya kilimo cha mkataba ili kiwe na manufaa na faida kwa wahusika wote; na
- viii. Kujenga mazingira wezeshi ya ufugaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba endapo changamoto hizo zitatatuliwa na Serikali ni wazi kwamba kilimo kitakuwa na mchango mkubwa katika mageuzi ya uchumi wa viwanda.

5.6. Kujenga mazingira wezeshi ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto inayowakabili wawekezaji ni kutopatikana kwa wakati kwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Asilimia kubwa ya ardhi nchini haina mpango wa matumizi bora ya ardhi hivyo kusababisha wawekezaji kuchukua muda mrefu kupata maeneo ya uwekezaji na wakati mwingine kukata tamaa na kulazimika kuwekeza nchi nyingine. Kutokana na changamoto hizi, Kamati inaishauri Serikali iharakishe mkakati wa Mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo ya vijiji, wilaya na mikoa ili kurahisisha uwekezaji na maendeleo ya viwanda.

5.7. Uendelezaji wa Sekta ya Viwanda vidogo

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua hatua mbalimbali ambazo Serikali imeendelea kuzichukua katika kuweka mazingira wezeshi ya uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Uanzishwaji wa viwanda vidogo ambavyo kimsingi havihitaji mitaji mikubwa ni rahisi kwa mtanzania wa hali ya kawaida kuvimili na kuvyendesha. Hivyo, Kamati inaona ni

muhimu Mpango huu ukajielekeza katika kuweka mazingira wezeshi ya uanzishaji wa viwanda vidogo ambavyo vitatumia malighafi za hapa nchini. Viwanda hivyo vilenge kuzalisha bidhaa zitakazokidhi viwango nya kimataifa na kuweza kuwa na ushindani katika soko la Afrika Mashariki na nchi nyngine za jirani. Aidha, Kamati inaona kuwa moja ya kichocheo kikubwa cha kuleta mapinduzi ya haraka katika ukuaji wa viwanda vidogo ni uwepo wa **SIDO** imara. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwezo wa utendaji wa **SIDO** kwa kutenga rasilimali fedha na watu ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

5.8. Upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango

Mheshimiwa Spika, mwongozo umeainisha maeneo ambayo yatagharamia nakisi ya bajeti hasa kwa upande wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali ipunguze kukopa zaidi kwenye soko la ndani la fedha na ijielekeze kukopa nje ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani na wajasiliamali kukopa kwenye soko la ndani la fedha na hivyo kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mitaji.

5.9. Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo (Flagship Projects)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza miradi ya Kielelezo kama vile mradi wa kuzalisha umeme wa Rufiji, mradi wa ujenzi wa reli ya kat i kwa kiwango cha *Standard Gauge* na mradi wa kuboresha Shirika la ndege la ATCL. Miradi hii itakapokamiliika itakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo katika sekta za viwanda, nishati, biashara, utalii, usafirishaji na kilimo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kumekuwa na utekelezaji usioridhisha wa baadhi ya miradi mikubwa ambayo ingeleta manufaa makubwa kwa Taifa. Miradi hiyo ni;

- i. Ujenzi wa kiwanda cha chuma Liganga, ujenzi wa mgodi wa uchimbaji makaa ya mawe mchuchuma na ujenzi wa Reli ya Mtwara Mbambabay na matawi yake ya kwenda Liganga na Mchuchuma;
- ii. Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata gesi ya asili (LNG) – Lindi;
- iii. Uanzishwaji wa maeneo maalumu ya kuchakata gesi pamoja na bidhaa zake (Mtwara *Petrochemical Special Economic Zone*);
- iv. Mradi wa Magadi Soda Engaruka katika Ziwa Manyara;
- v. Uanzishwaji wa maeneo maalum ya uwekezaji Bagamoyo unaojumuisha ujenzi wa bandari; na
- vi. Uanzishwaji wa kituo cha biashara na huduma cha Kurasini (*Kurasini Logistics Centre*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali itekeleze kwa wakati miradi yote iliyoianishwa katika Mpango wa Maendeleo kama ilivyopanga katika Mipango yake ya kila mwaka.

- 5.10. Uvubi katika Bahari Kuu na Ujenzi wa Bandari ya Uvubi**
- Mheshimiwa Spika**, Bunge limekuwa likiishauri Serikali kwa muda mrefu kuhusu rasilimali na mapato yatokanayo na uvubi katika bahari kuu ndani ya mipaka ya nchi yetu. Kamati inatambua na kuunga mkono mpango wa Serikali wa kufufua Shirika la Uvubi Tanzania pamoja na nia ya kujenga bandari ya uvubi. Hata hivyo, utekelezaji wake umechukua muda mrefu, hadi sasa eneo la ujenzi wa Bandari hiyo halijabainishwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta mafanikio ya haraka katika eneo hili kamati inashauri Serikali ifanye mambo yafuatayo;

- i. Ibainishe eneo ambalo bandari ya uvuvi itajengwa na iweke mikakati ya kuanza kujenga haraka iwezekanavyo;
- ii. Iweke mikakati ya kujenga bandari za uvuvi nyininge zisizopungua mbili katika ukanda wa Bahari ya Hindi; na
- iii. Ifanye tathmini ya vifaa na miundombinu ya uvuvi ambayo iliyobinafsishwa na haitumiki.

5.11. Uimarishaji wa Benki ya Rasilimali na Benki ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika Sekta ya Viwanda na Kilimo hasa kilimo cha mazao ya biashara unahitaji mtaji mkubwa na huchukua muda mrefu kuzalisha faida pamoja na kuwa na vihatarishi vingi. Mazingira hayo yamesababisha Benki nydingi za biashara kutovutiwa kutoa mikopo kwa sekta hizo. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Benki ya Rasilimali (TIB) na Benki ya Kilimo (TADB) kwa kuziongezea mitaji ili ziweze kutoa mikopo kwa sekta hizo muhimu.

5.12. Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo na Ushiriki wa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ni kutopatikana kwa rasilimali fedha. Kutopatikana kwa rasilimali fedha kumechangiwa na Serikali kutegemea vyanzo vilivyozooleka na kutoshirikisha ipasavyo sekta binafsi katika kugharamia miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia ipasavyo mikakati ya kuvutia na kuweshesha Sekta Binafsi kushiriki katika utekelezaji wa Mpango.

6.0 MAONI YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsus, Kamati inatoa maoni ya ujumla kama ifuatavyo: -

- 6.1 Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati na shule, endapo hili halitafanyika Serikali itakuwa inawavunja moyo wananchi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- 6.2 Serikali ihakikishe inalipa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji ambao wamekwisha wasilisha hati ya malipo "*Performance Certificate*" na bado hawajalipwa hivyo kusababisha miradi kutokamilika. Aidha, Serikali itekeleze kikamilifu miradi maji ambayo bado hajakamilishwa.
- 6.3 Serikali ianze kutenga kiwango cha asilimia Moja (1%) ya Pato la Taifa kwa ajili ya shughuli za Utafiti na maendeleo;
- 6.4 Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha na kuratibu ipasavyo tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili iweze kuleta manufaa yaliyotarajiwa;
- 6.5 Serikali ihakikishe inatekeleza mikakati iliyojiveka kwa vitendo ili kukabiliana na vihatarishi kama ilivyoainishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango. Hatua hii itasaidia kuwa na Mpango unaotekelezeka na kufikia malengo yaliyokusudiwa pamoja na kutekeleza kifungu cha 35 (1) hadi (4) vya Sheria ya Bajeti kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na majanga.

- 6.6 Serikali ihakikishe inatoa mafunzo ya kutosha kwa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uandaaji wa maandiko ya miradi itakayotekelawa kwa njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.
- 6.7 Serikali iweke mkakati wa kuvilinda viwanda vyatiani ambavyo vinazalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje pamoja na kuchochea uzalishaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuzalishwa nchini.
- 6.8 Kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika Sekta ya Mafuta na Gesi Serikali iongeze juhudzi za kuiendeleza sekta hii ili iweze kuchangia katika ukuaji wa uchumi;
- 6.9 Serikali ihakikishe inatekeleza kikamilifu Mkakati wa Urasimishaji wa Mali na Biashara Tanzania (MKURABITA) ili kupunguza sekta isiyo rasmi na kuongeza ukusanyaji wa mapato.
- 6.10 Serikali iziwezeshe kifedha Taasisi zake hasa majeshi yake ili yatengeneze baadhi ya bidhaa zinazotumika katika majeshi hayo pamoja na mashulenii (sare, viatu); na
- 6.11 Serikali ihakikishe inatenga mapato yatokanayo na gesi kama inavyotaka Sheria ya Oil and Gas (Revenue Management) Act 2015 ili zitumike kwa ajili ya vizazi vijavyo.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb. Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Mb. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

- | | |
|--|-------------------|
| 1.Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb | Mwenyekiti |
| 2.Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | Makamu Mwenyekiti |
| 3.Mhe. David Ernest Silinde, Mb | Mjumbe |
| 4.Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb | Mjumbe |
| 5.Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb | Mjumbe |
| 6.Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb | Mjumbe |
| 7.Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb | Mjumbe |
| 8.Mhe. Ali Hassan Omar, Mb | Mjumbe |
| 9.Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb | Mjumbe |
| 10.Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb | Mjumbe |
| 11.Mhe. Makame Kassim Makame, Mb | Mjumbe |
| 12.Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb | Mjumbe |
| 13.Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb | Mjumbe |
| 14.Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 15.Mhe. Riziki Said Lulida, Mb | Mjumbe |
| 16.Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb | Mjumbe |
| 17.Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb | Mjumbe |
| 18.Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb | Mjumbe |
| 19.Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb | Mjumbe |
| 20.Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb | Mjumbe |
| 21.Mhe. Stephen Julius Masele, Mb | Mjumbe |
| 22.Mhe. Andrew John Chenge, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb | Mjumbe |
| 24.Mhe. Shally J. Raymond, Mb | Mjumbe |
| 25. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, natambua mchango mkubwa wa

Sekretariati ya Kamati ikiongozwa na Ndg. Lina Kitosi Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndg. Michael Kadebe Mkurugenzi Msaidizi pamoja na Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala na Maombi Kakozi kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

George B. Simbachawene, Mb
MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI
06 Novemba, 2018

MWENYEKITI: Sasa nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Halima Mdee kabla hujafika mbali natumaini tumelewana tumeangalia kilichoingia Bungeni naelewa unanielewa ninachosema, umeshaiona hii?

MHE. HALIMA J. MDEE: Hapana sijakuelewa

MWENYEKITI: Umeshaiona hii?

MHE. HALIMA J. MDEE: Hapana sijaiona.

MWENYEKITI: *Okay, hapana ni tofauti.*

MHE. HALIMA J. MDEE: Yaani ananimbia nimeiona hiyo? Mimi nina *summary* hapa sasa ukiniambia nimeiona...

MWENYEKITI: Aaah! Ni *summary*?

MHE. HALIMA J. MDEE: Unanichanganya kidogo ila hiyo naijua, hiyo naifahamu.

MWENYEKITI: Kwa sababu hapa mezani nina hizi nina hili book kubwa na hii. Sasa hawa wote Waheshimiwa Wabunge wana...

MHE. HALIMA J. MDEE: Hata mimi nina hizo zote mbili na hiyo na nina *summary*.

MWENYEKITI: Sasa unachotakiwa ukisome ni hii kwa sababu ndiyo kila mtu anayo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nitaisoma hiyo hiyo.

MWENYEKITI: Hata kama ni *summary*, lakini ya hii.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nitaisoma hiyo hiyo haina shida.

MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kabla sijatoa maoni yangu ama maombi ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naitaka Serikali irejee maoni yetu ya Mpango wa Miaka Mitatu iliyopita lakini vilevile irejee hotuba mbadala za Kambi Rasmi ya Upinzani za miaka nane iliyopita, itapata utajirisho mkubwa sana kuliko hivi nitakavyovizungumza hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati dhima ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya miaka mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021 ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochaea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu tunaingia mwaka wa nne wa utekelezaji wa mpango huo hai ya uchumi na maendeleo ya watu katika kaya zao hapa nchini ikiwa mbaya zaidi kuliko Awamu zote Nne za Serikali zilizotangulia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti ulifanywa na William Attwell mwaka 2017 na kuchapishwa katika mtandao wa *frontteers Strategy Group* nimeweka hapo *footnote* ni kwamba pamoja na ukuaji wa uchumi wa Tanzania unaotajwa kukua kwa kasi na licha ya ongezeko la idadi ya watu kuwa kubwa, bado uwezo wa wananchi wa kununua bidhaa (*spending/purchasing power*) umebakii kuwa wa chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaendelea kuonesha kwamba, kutokana na kiwango kikubwa cha umaskini nchini Tanzania ambacho kwa sasa kimefikia asilimia 47 ya idadi ya watu wote kwa mujibu wa utafiti huo ambaou umefanyika mwaka jana. Kwa utafiti huu tafsiri yake ni kwamba kwa idadi ya Watanzania milioni 52.6 kama ilivyoripotiwa na taarifa ya Serikali watu maskini ni milioni 24.7. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti huo unaonesha pia kwamba zaidi ya asilimia 70 ya watu wazima wanaofanya kazi hawana kipato cha uhakika. Aidha, kipato hichohicho kisicho cha uhakika, hukumbwa na dhoruba ya kupanda na kushuka kwa mwenendo wa uchumi mara kwa mara. Matokeo yake ni kwamba, watu walio wengi wana uwezo wa kununua mahitaji ya msingi tu ili kuweza kujikimu maisha. Kwa hiyo, hawa ni sehemu ndogo tu ya watu wenye kipato cha ziada cha kuweza kununua bidhaa kwa ajili ya matumizi mengine ya maendeleo. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi na nyie vilevile wengi tumepigika tu hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huo ni kwamba, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano umeshindwa kutimiza dhima yake ya kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo na watu ikiwa huu ni mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mpango huo ambapo wananchi walio wengi hawana uwezo wa kununua bidhaa kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni muujiza wowote unaoweza kufanyika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja uliobaki wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano ili kuifanya asilimia 70 ya Watanzania wasio na kipato cha uhakika kuwa nacho. Aidha, hakuna uhakika kama kwa kipindi cha mwaka mmoja uliobaki tunaweza kufuta kiwango cha umasikini cha asilimia 47 na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya watu wenye kipato cha katika kama Serikali hii ya Awamu ya Tano inavyojinasibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya mpango kushindwa kuifikia dhima yake ni kitendo cha Serikali kuitenga Sekta Binafsi katika mchakato mzima wa uendeshaji wa uchumi wa nchi. Serikali imekiri hili kwenye ukurasa wake wa 55 wa mapendekezo ya Mpango kwamba moja kati ya vihatarishi vyta ndani ni ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Serikali imekuwa ikiichukulia sekta binafsi kama adui na mshindani badala ya mdau muhimu katika maendeleo ya Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa mpango ulieleza vyema kabisa kwamba miradi yote ambayo ni ya kibashara iache itekelezwe na sekta binafsi isipokuwa kama kuna sababu nzito ya kufanya vinginevyo yani kwa lugha ya kimombo *commercially viable project should left to the private sector unless there is strong justification for doing otherwise*, lakini Serikali imeamua kukiuka muongozo wa mpango ulio idhinishwa na Bunge na kung'ang'ania kutekeleza miradi yote yenewe bila kuishirikisha sekta binafsi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni kama vile miradi ya ujenzi ya reli (*standard gauge*), Liganga-Mchuchuma and austral park, Mtwara Petrochemical Special Economic Zone na Bagamoyo Special Economic Zone. Kutokana na uamuzi huu Serikali imejikuta ikikopa mikopo mikubwa ya kibashara ambayo kuilipa ama kuihudumia ni mzigo mkubwa sana kwa Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba ili uchumi uwe shirikishi na miradi ya maendeleo iweze kutekelezwa kikamilifu na kuwanufaisha wananchi lazima Serikali iachane na ukiritimba na ubinafsi na kuipa sekta binafsi nafasi katika ujenzi wa uchumi. Kitendo cha Serikali kung'ang'ania kufanya kila kitu yenewe ni kurudisha nyuma...

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa Halima samahani kidogo, Waheshimiwa Wabunge ambao mnapenda kupiga makof kwa kutumia vitabu nafikiri mnafanya kosa ambalo si

sahihi yaani si ustaarabu hata kidogo tena kitabu chenyewe cha hotuba yenu wenyewe halafu unakipiga kukichakaza...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu.

MWENYEKITI: Dakika zako zitakaa vizuri lakini lazima tuwekane vizuri kwa sababu hata wananchi wakiona tunafanya vitu vya namna hiyo ni jambo ambalo si zuri. Piga makofi kwa mkono wako lakini usitumie hizi *document* kwa sababu nawaona endelea Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kung'anga'ania kufanya kitu yenyewe ni kuturudisha nyuma kwenye enzi za uchumi wa kijamaa ambao ulishashindwa tangu vita baridi imalizike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba mpya na mustakabali wa Mpango wa Taifa endelevu, Katiba ndio taswira hasa ya Taifa katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na hata katika mambo mbalimbali ya utoaji huduma kwa wananchi. Katiba ndio msingi wa utoaji haki na wajibu kwa kila raia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasimu ya pili ya Katiba iliweka misingi, rasimu ambayo ilikuwa na maoni ya wananchi iliweka misingi yenyeye dhamira ya kulisaidia Taifa ili kujikwamua kutoka lindi la umaskini wakujitakia maradhi na ujinga uliopindukia uliosababishwa na Chama cha Mapinduzi na Serikali zake zote zilizotangulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rasimu hii pia inazungumzia mchakato wa kupata viongozi katika ngazi mbalimbali, muundo wa Tume Huru ya Uchaguzi ambapo inapendekeza Tume hiyo iteuliwe na Tume Maalum kuliko ilivyo sasa ambapo Tume husika ni tawi la CCM ndio maana leo tumeshuhudia Wabunge wamekula kiapo ambao na wao wanajua sio chaguo la wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa matamano ya kuwa na Katiba mpya Serikali ilitumia mabilioni ya fedha ikiwa ni sawa na fedha za maendeleo za Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Maliasili na Utalii, Wizara ya Afya, Wizara ya Katiba ya Sheria kwa mwaka 2016/2017 pekee kama ilivyoainishwa kwenye fedha za maendeleo za Wizara mbalimbali kwenye kitabu cha matumizi ya maendeleo, juzuu ya nne kwa mwaka 2017/2018. Mheshimiwa Dkt. Mpango enzi hizo hukuwepo sasa tunakukumbusha kwamba fedha zilizotumika ni nyingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila raia wa nchi hii alitambua umuhimu wa kuwa na Katiba mpya ambayo ilikuwa tegemeo la matumaini mapya ya kuwepo kwa utawala bora ambaou ungechochea kasi ya ukuaji uchumi na kujenga dhana ya uwajibikaji kwa kila raia na viongozi wao. Kinyume na mategemeo ya wananchi walio wengi mchakato wa upatikaji wa Katiba mpya umekuwa na kiza kinene hasa katika Serikali hii ya Awamu wa Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, naomba tu uniambie ni ukurasa wa ngapi kwenye kitabu hiki haya unayoyasema.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ukurasa wa ngapi?

MWENYEKITI: Ndiyo! Huku ndani.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ukurasa wa sita.

MWENYEKITI: Ukurasa wa sita hauna maneno haya.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ukurasa wa 13, sogea sogea mbele kidogo.

MWENYEKITI: Subiri, subiri *we have to sort out this thing. Ok!* Ukurasa wa sita yes, sawa sawa, mpaka hapo uko sawa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika mbili hizo, sijui tatu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 4 Novemba, 2016 Mheshimiwa Rais alinukuliwa akisema hakuwahi kuzungumzia katiba mpya...

MWENYEKITI: Sasa kuanzia hapo ndipo penye shida.

MHE. HALIMA J. MDEE: Daaa!

MWENYEKITI: Mmmh! Kuanzia hapo ndiyo pana shida hapo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuna shida hapo?

MWENYEKITI: Ndiyo! Ukurasa wa tano wa hotuba yako ya mwanzo, wa saba na wa nane.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nimemnukuu Rais tu.

MWENYEKITI: Yale ya mwanzo ambayo yalikuwa *bold* yale, yale ndiyo tumeyatoa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Hata nukuu ya Rais?

MWENYEKITI: Yale uliyoya-*bold* mwanzoni.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli kama hizi. Nadhani hapo nimetoka si ndiyo?

MWENYEKITI: Hapana, wewe ondoa yale uliyoya-*bold* mwanzoni kwenye hotuba uliyopeleka...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii haiwezi kunyooka kama kiongozi...

MWENYEKITI: Unajua tukiwa tunasoma tuna *version* tofauti tofauti inakuwa shida kweli.

MHE. HALIMA J. MDEE: Naomba univumilie.

MWENYEKITI: Nakuvumilia sana, wala sina nia ya kukuungilia. Ungekuwa unatumia hii wala tusingepata tabu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Hapa nipo sawa sasa, naomba niendelee sasa.

Mheshimiwa Spika, nimetoa zote zile nukuu za Rais nimeshaziruka, sawa?

MWENYEKITI: Haya.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii haiwezi kunyooka kama kiongozi anadharau wananchi anaowaongoza. Unyoofu wa nchi unakua pale ambapo tunafanya kazi pamoja kama Taifa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, unaingia kwenye uwanja ambao unaleta ubishi na unaleta malumbano kwa sababu wenzako nao hawawezi kuvumilia maneno ya uchokozi makubwa kiasi hicho kwamba tuna kiongozi anayedharau wananchi kitu ambacho si kweli hata kidogo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Sijataja jina.

SPIKA: Mimi nikuombe Mheshimiwa Halima, hebu pata hiki kitabu hiki halafu ukisome hiki. Tutakuwa hatuna ugomvi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Taasisi imara zinazozingatia misingi ya utoaji haki, ulinzi wa amani na zinazojali uwajibikaji wa pamoja ili kujenga jamii jumuishi kwa maendeleo endelevu. Tunahitaji jamii ya watu huru wanaoishi bila hofu ya kutekwa, kutengwa na wapendwa wao, kuuawa, au vitisho vyta namna yoyote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima kwa mara ya pili tena yaani unayoyasoma hayako humu ndiyo tatizo!

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

MHE. HALIMA J. MDEE: Naenda ukurasa wa saba.

MWENYEKITI: Kwa nini usichukue kile kitabu ambacho Wabunge wote wanacho ukakitumia hicho.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ukurasa wa saba ipo, hii *summary* iko ukurasa wa saba.

MWENYEKITI: Hakuna hayo maneno unayoyasema.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nimeandaa *summary*, ukilazimisha niseme hiki hapa wakati nimeisaidia Serikali utajirisho wa kurasa nyingi, nimeandaa *summary* lakini kila ninachokisoma hapa kipo huku. Sasa kama mnanipangia basi nitawaachia wenyewe, siwezi kuzungumza mnachonitaka nyie.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

MHE. HALIMA J. MDEE: Wewe si u-relax, Mheshimiwa Jenista wewe kinachokusumbua nini? Wewe hofu yako?

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

MHE. HALIMA J. MDEE: Ukurasa wa 13 si ucheki? Mbona sisi hatuwaingiliagi mambo yenu? Hivi vyote viro huko, wanakuchanganya tu hawa na uoga wao tu! Mnasikia Rais amesemwa, mna...

MWENYEKITI: Sasa naomba tusikilizane, naona kama inaelekea huko ukurasa wa 13 sawa. Kama hivyo basi endelea. Yaani shida ni kwamba kwa kawaida kile ambacho kinawekwa mezani ndicho kinachosomwa. Sasa tunaendaje tena? Tunapoelezana tena inakuwaje? Si tunaenda kwa utaratibu? Hata uki-summarize lazima uende na wenzako,

tuwe tunaelewa ni wapi. Huwezi ku-summarize kwa kutuambia mambo ambayo hayapo halafu tukakubali, sio utaratibu. Kwa hiyo, kwa hapa sasa nimeshakuelewa ulipofika nakuruhusu endelea dakika zako nazilinda. (*Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ubarikiwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji taasisi imara zinazozingatia misingi ya utoaji haki, ulinzi wa amani na zinazojali uwajibikaji wa pamoja ili kujenga jamii jumuishi kwa maendeleo endelevu. Tunahitaji jamii ya watu huru wanaoishi bila hofu ya kutekwa, kutengwa na wapendwa wao, kuuawa, au vitisho vya namna yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na Mahakama zilizo huru, zinazoweza kutoa maamuzi yanayozingatia sheria na haki bila mashinikizo ya mtu yoyote. Tunahitaji kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi inayofanya kazi kwa uhuru bila shinikizo la mtu ama kikundi cha watu; tunahitaji kuwa na Bunge lenye uwezo wa kuikosoa Serikali na kuiwajibisha Serikali; tunahitaji Jeshi la Polisi linalozingatia sheria, usawa na haki za binadamu; tunahitaji Jeshi la Wananchi lisiloegemea upande wowote na linalowajibika kwa wananchi wote wa Tanzania; na tunahitaji taasisi zote na idara za Serikali zifuate sheria na kanuni na sio maelekezo na matakwa ya viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuboresha utendaji kazi wa taasisi zetu haitawezekana kamwe kuwa na maendeleo endelevu ndani ya nchi yetu. Ni jukumu letu sote kulitazama jambo hili kwa kina na kulifanyia kazi haraka iwezekanavyo ili kunusuru nchi yetu kuingia katika mipasuko inayotokana na ubaguzi, chuki na visasi na hata kuingia katika majanga yakiwemo machafuko ambayo kimsingi yanaweza kugharimu maisha ya watu wetu, kuporomosha uchumi wetu na kuharibu jina zuri la taifa letu lililolinda misingi ya amani na utulivu tangu uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa hali ya siasa, ulinzi na usalama na athari zake katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Hali ya siasa nchini Tanzania kwa sasa si ya kuridhisha. Wapo wanaona kwamba wao pekee ndio wana haki ya kufanya siasa na kuharamisha wengine kufanya siasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hali ya usalama ina mashaka. Siku hizi matukio ya utekaji na mauaji yenyе kutatanisha yamekuwa ni kawaida katika nchi yetu. Hali kadhalika hali ya ulinzi imedhoofika. Siku hizi kiongozi kupigwa risasi akiwa maeneo yenyе ulinzi au watu mashuhuri kutekwa katika maeneo yenyе ulinzi yamekuwa ni matukio ya kawaida pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yote hayo hayawezi kamwe kuwavutia wawekezaji wakubwa tunaowahitaji katika kuujenga uchumi wetu. Halikadhalika mazingira hayo hayawezi kuwapa motisha wafadhili wetu kutoa fedha za kutekeleza miradi yetu ya maendeleo. Na tayari baadhi ya wafadhili wetu wameanza kukataa kutoa fedha kutokana na mwenendo wa siasa za nchi yetu usioridhisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Watanzania wote wanaopenda kuona haki ikitamalaki katika Taifa, tunalaani na tunapinga vitendo viovu vya uonevu, ukandamizaji, utekaji na sasa majoribio ya mauaji yanayofanywa dhidi ya wanachama na viongozi wa Vyama vya Upinzani hapa nchini. Ikiwa vitendo hivi vitaachwa viendelee bila kukemewa na kushughulikiwa kwa uzito unaostahili, kuna hatari ya kundi linalohisi kuonewa likakosa uvumilivu na hivyo kuathiri amani ya nchi; na amani ikitetereka, hakuna Mpango wowote wa Maendeleo utakaoweza kutekelezwa na kufikia malengo yaliyokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika rasilimali watu kwa maedeleo endelevu; ni nadharia na uzoefu wa kawaida kwamba, Taifa lolote linalotaka kujitegemea na

kujinasua kwenye dimbwi la utegemezi na umaskini linajitahidi sana kuwajengea watu wake uwezo wa kielimu, kiufundi na maarifa ili kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali na hivyo kuweza kuyamudu mazingira yao. Kwa sababu hiyo; Taifa la namna hiyo, huwekeza sana katika elimu ili kuandaa wataalam (rasilimali watu) wa kutosha wenye weledi na wa kuendesha sekta mbalimbali za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imeeleza katika mpango kuhusu miradi ya kimkakati pamoja na maelezo mengi kuhusu uchumi wa viwanda. Pamoja na miradi hiyo ya kimkakati ambayo imeelezwa na Serikali, hajiaelezwa popote kuhusu namna ya kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya kuendesha na kusimamia miradi hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano iko dhahiri; baada ya kununua ndege kwa mabilioni ya shilingi na nyingine tumemsikia hapa Mheshimiwa Dkt. Mpango anajinasibu zinakuja nyingine saba ndiyo tunawapeleka marubani wetu shule kusoma kuweza kuzirusha ndege husika, halikadhalika kuandaa mpango wa biashara wakati ndege zimeshakuja nchini ama nyingine ziko njiani zinakuja, mambo ambayo yangetakiwa kufanyaika wakati wa maandalizi wa mradi. Kwa hiyo, haya ni madhara ya kukurupuka, kila mtu akija anakurupuka tu! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishasema na tunaendelea kusema kuwa huwezi kusema uchumi wa viwanda bila kuanza kuhuisha mfumo wetu wa elimu ili uendane na uweze kufikia lengo kuelekea uchumi wa viwanda. Vivyo hivyo huwezi kuwa na miradi mingi ya kimkakati bila kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya kuiendesha. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri kulieleza Bunge hili juu ya mkakati wa kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango hasa kwenye miradi ya kimkakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukakasi kuhusu Mradi wa *Standard Gauge Railway*. Nani anagharamia? Tukiwa tunajadili Mpango ni wakati muafaka kwa Serikali kutanzua

kitendawili cha mradi huu unagharamiwa na nani? Kwa Taarifa ambazo Kambi rasmi inazo, mradi huu mpaka ukamilike unatarajiwa kuligharimu Taifa dola bilioni 14 yaani sawa na shilingi triliuni 32 yaani bajeti yetu kwa mwaka na chenji inabaki. Kwa *route* ya Dar es Salaam mpaka Rusumo yaani mpakani mwa Tanzania na Rwanda ambayo kilometra zake ni 2600. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Taarifa zilizopo, pesa ambazo zimetolewa na Serikali kupitia kodi za Watanzania ni shilingi 1.169 triliuni. Benki ya *Exim*, Uturuki imetoa bilioni 1.2 dola ambayo ni sawa na triliuni 2.7 lakini vilevile *Standard Chartered Group* juzi Mheshimiwa Waziri alikuwa anapokea wametoa dola bilioni 1.46 ambayo ni sawa na shilingi triliuni 3.8. Hii ya *Exim* na *Standard Chartered* ni mikopo sio sadaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Bunge hili likajua hizo fedha nyininge zitapatikana wapi kwa utaratibu gani na zitalipwaje na sio kwa mradi huu tu na mradi wa *Stiegler's Gorge* ambao tunaambiwa utagharimu *trillions of shillings*. Hiki ndicho chombo cha wananchi. Sasa kama Wabunge hatujui, sijui nani atakayejua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya mafanikio ya kiuchumi ya *SGR*, Serikali imeeleza kuhusu ujenzi wa kipande cha reli kwa kiwango cha *SGR* kutoka Isaka kwenda Rusumo lakini haijaaeleza ujenzi huo kutoka Makutupora hadi Tabora na Tabora hadi Isaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikalieleza Bunge sababu za kiuchumi za kwa nini wajenge reli hiyo mpaka Mwanza na Rusumo kabla kwanza ya kujenga reli hiyo kutoka Tabora - Kigoma kwa ajili ya kufungua fursa za nchi ya DRC. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inapenda kuona reli hiyo ikifungamanishwa

na uchumi katika maeneo ya kimkakati na sio kuelezwu muda wa kusafiri kwa treni ya reli ya kisasa kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam. Hii ni kwa sababu Kambi Rasmi inaamini kuwa mradi huo hautakuwa na tija kwa kulenga tu kupunguza muda wa abiria kusafiri bali kuufungamanisha na sekta nyingine za uchumi kwa ajili ya kuleta tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji duni wa bajeti ya Serikali unavyokwamisha Mpango wa Maendeleo. Tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani kumekuwa na utamaduni mbovu wa kupanga bajeti na kushindwa kuitekeleza jambo ambalo limekwamisha miradi mingi ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kwa Serikali kutekeleza kikamilifu bajeti yake kunatokana na sababu mbalimbali. Mosi ni kuweka makisio makubwa ya makusanyo ya fedha na kushindwa kukusanya kiasi hicho. Kile kiasi kinachoshindikana kukusanya kinakuwa ni makusanyo hewa na ile miradi ambayo ilitakiwa kutekelezwa na kiasi hicho kilichoshindikana kukusanya huwa haitekelezwi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Serikali ilipanga kukusanya shilingi trillioni 29.5 lakini iliweza kukusanya shilingi trillioni 20 tu sawa na asilimia 70.1. Katika mwaka 2017/2018, Serikali ilipanga kukusanya jumla shilingi trillioni 31, lakini iliweza kukusanya shilingi trillioni 21 tu, sawa na asilimia 69 ya lengo. Hii ina maana kwamba asilimia 31 iliyobaki sawa na shilingi trillioni 9.8 ilikuwa ni hewa na kwa maana hiyo haikutekelezwa. Leo Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake anakiri wameweza kukusanya trillioni 17 tu baada ya kukusanya vyanzo vyote lakini bado kwenye mpango wake anatuambia wana uwezo wa kukusanya trillioni 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni kutokutekeleza kikamilifu bajeti iliyoishishwa na Bunge katika Sekta mbalimbali. Nitatoa mifano katika Wizara tatu zinazogusa maisha ya watu wengi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, 2016/2017 pamoja na mbwembwe zote Serikali imetoa asilimia mbili tu ya maendeleo; mwaka 2017/2018 pamoja na mbwembwe zote, na kuwa na hotuba zenyé kurasa nyingi, mliota asilimia 11 tu ya maendeleo. Wizara ya Mifugo mliota asilimia 0, Wizara ya Maji mliota asilimia 25, hatimaye asilimia 22.

SPIKA: Mheshimiwa Halima, muda wako ume...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, kwa kutumia zile dakika zangu zilizobaki naomba ni-*summarize* tu kwa ufupi mambo ambayo tunashauri Serikali dakika moja tu.

SPIKA: Bahati mbaya sana muda hauko upande wako.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu, vipaumbele vya mwisho, dakika moja zile mbili ulizonibania; kwanza hotuba iingie kwenye *Hansard* lakini naomba kwa heshima yako dakika moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo tunadhani Sekta muhimu Serikali mzizingatie na haya yamekuwa yakizungumzwa na Wabunge wa upande zote wala sio Wabunge wa upande wa Upinzani; la kwanza elimu, la pili kilimo, la tatu viwanda la nne maji, llingine afya. Mengineyo yanaweza yaka-*cover* asilimia 40 ya yale mapato yetu lakini hii asilimia 60 iende kwenye hizi Sekta muhimu zinazogusa Watanzania maskini lakini sio hizi Sekta zinazogusa vitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mwenyezi Mungu akubariki. (*Makofi/Vigelegele*)

HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Inatolewa chini ya Kanuni ya 94(5) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, wakati dhima ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) ni Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu; tunaingia mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mpango huo, hali ya uchumi na maendeleo ya watu katika kaya zao hapa nchini ikiwa mbaya zaidi kuliko awamu zote nne za Serikali zilizotangulia.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na William Attwell mwaka 2017 na kuchapishwa katika mtandao wa ‘Fronteers Strategy Group’¹, ni kwamba; pamoja na ukuaji wa uchumi wa Tanzania unaotajwa kukua kwa kasi, na licha ya ongezeko la idadi ya watu kuwa kubwa; bado uwezo wa wananchi wa kununua bidhaa (spending/purchasing power) umebaki kuwa wa chini sana. Utafiti unaendelea kuonyesha kwamba, kutokana na kiwango kikubwa cha umasikini nchini Tanzania (ambacho kwa sasa kimefikia asilimia 47 ya idadi ya watu wote), jumla ya idadi ya wananchi(walaji) wenye uwezo wa kununua bidhaa, ni chini ya nusu ya ile ya Kenya licha ya nchi hiyo kuwa na idadi ndogo ya watu kuliko Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo unaonyesha pia kwamba; zaidi ya asilimia 70 ya watu wazima wanaofanya kazi hawana

¹<http://blog.frontierstrategygroup.com/2017/05/tanzanias-consumers-overlooked-overestimated/>

kipato cha uhakika. Aidha, kipato hichohicho kisicho cha uhakika, hukumbwa na dhoruba ya kupanda na kushuka kwa mwenendo wa uchumi mara kwa mara. Matokeo yake ni kwamba, watu walio wengi wana uwezo wa kununua mahitaji ya msingi tu ili kuweza kujikimu kimaisha. Kwa hiyo, ni sehemu ndogo tu ya watu wenye kipato cha ziada cha kuweza kununua bidhaa kwa ajili ya matumizi mengine ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huo ni kwamba; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano umeshindwa kutimiza dhima yake ya kuchochaea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu ikiwa huu ni mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mpango huo ambapo wananchi walio wengi hawana uwezo wa kununua bidhaa kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni muujiza wowote unaoweza kufanyika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja uliobaki wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano ili kuifanya asilimia 70 ya watanzania wasio na kipato cha uhakika kuwa nacho. Aidha, hakuna uhakika kama kwa kipindi cha mwaka mmoja uliobaki tunaweza kufuta kiwango cha umasikini cha asilimia 47 na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya watu wenye kipato cha katika kama Serikali hii ya awamu ya tano inavyojinasibu.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya Mpango kushindwa kuifikia dhima yake ni kitendo cha Serikali kuitenga Sekta Binafsi katika mchakato mzima wa uendeshaji wa uchumi wa Nchi. Mpango umeeleza vizuri kuwa miradi yote ambayo ni ya kibashara iachwe itekelezwe na Sekta Binafsi isipokuwa kama kuna sababu nzito ya kufanya vinginevyo "*commercially viable projects should be left to the private sector, unless there is strong justification for doing otherwise*"². Lakini Serikali imeamuza kukiuka mwongozo wa Mpango ulioihinishwa na Bunge na kung'ang'ania kutekeleza miradi yote yenye bila kuishirikisha Sekta Binafsi.

² National Five Year Development Plan 2016/17 – 2020/21 p.90

Miradi hiyo ni kama vile Mradi wa ujenzi wa Reli ya Standard Gauge, Liganga Mchuchuma Industrial Park, Mtwara Petrochemical Special Economic Zone na Bagamoyo Special Economic Zone.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba, ili uchumi uwe shirkishi na miradi ya maendeleo iweze kutekelezwa kikamilifu na kuwanufaisha wananchi lazima Serikali iachane na ukiritimba na ubinafsi na kuipa sekta binafsi nafasi katika ujenzi wa uchumi. Kitendo cha Serikali kung'ang'ania kufanya kila kitu yenyewe ni kurutudisha nyuma kwenye enzi za uchumi wa kijamaa ambao ulishashindwa tangu vita baridi imalizike.

2. KATIBA MPYA NA MUSTAKABALI WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa Katiba ndio sheria mama. Katiba ndio taswira hasa ya taifa katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na hata katika mambo mbalimbali ya utoaji wa huduma kwa wananchi. Katiba ndio msingi wa utoaji haki na wajibu wa kila raia. Hivyo basi, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa kuwa na Katiba Mpya inayokidhi matakwa ya wananchi na inayoendana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na hata kutatua kero mbalimbali za kijamii serikali ya awamu ya Nne iliona ni vyema ikatoa fursa kwa wananchi kuleta maoni yao kuhusu aina ya Katiba wanayoitaka ili kuweza kunufaika kwa pamoja kama taifa.

Mheshimiwa Spika, hakuna uchumi bora wa nchi kama hakuna Katiba bora. Katiba ndio chombo pekee cha kulinda uhuru wa kila raia, ni chombo cha kuonyesha dira ya kule tunapotaka kuelekea na miiko yetu kama taifa. (*Constitution is the only safeguard of our liberties; it is a solid expression of our vision and values as a nation*). Kwa mantiki hiyo **hatuwezi kamwe** kuendelea kiuchumi kama hatuna katiba inayotoa taswira ya kule tunapotaka kwenda.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa matamanio ya kuwa na katiba mpya; serikali ilitumia mabilioni ya fedha ikiwa ni sawa na fedha za maendeleo za Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Maliasili na Utalii, Wizara ya Afya, Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2016/2017 pekee kama ilivyoainishwa kwenye fedha za maendeleo za Wizara mbalimbali kwenye kitabu cha Matumizi ya Maendeleo Juzuu ya Nne kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mabilioni hayo yaliyotumika serikali ilitumia muda mrefu wa takribani miezi mitatu ikijumuisha wajumbe zaidi ya 600 ambapo kila mjumbe alilipwa posho isiyopungua shilingi 300,000 kwa siku huku watendaji mbalimbali nao wakilipwa posho. Hii ikiwa na maana kwamba fedha za walipa kodi wa nchi hii ndizo zilizotumiwa na serikali ya CCM katika kutafuta Katiba mpya. Kwa umuhimu huo miradi ya huduma za kijamii kama maji, hospitali, madawa, nishati ya umeme ambapo huduma hizi muhimu kwa kila mwananchi hazikupewa kipambele kwa wakati huo kama mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, kila raia wa nchi hii alitambua umuhimu wa kuwa na katiba mpya ambayo ilikuwa tegemeo la matumaini mapya ya kuwepo kwa utawala bora ambao ungechochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kujenga dhana ya uwajibikaji kwa kila raia na viongozi wao. Kinyume na mategemeo ya wananchi walio wengi mchakato wa upatikaji wa Katiba Mpya umekuwa na kiza kinene hasa katika serikali hii ya awamu wa Tano chini ya John Pombe Magufuli.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

Mheshimiwa Spika, Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeweka misingi ya uwajibikaji katika usimamizi wa maliasili ya Taifa kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 27 (1) na (2) na Ibara ya 28 (1) ya Katiba.

(1) Kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Jamhuri ya Muungano,mali ya Mmlaka ya Nchi na mali yote inayomililiwa kwa pamoja na wananchi ,na pia kuiheshimu mali ya mtu mwininge

(2) Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya Mamlaka ya Nchi nay a pamoja ,kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhiflu, na kuendesha uchumi wa taifa kwa makini kama watu ambaao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya taifa lao.28 (1) Kila raia ana wajibu wa kulinda,kuhifadhi na kudumisha uhuru,mamlaka,**ardhi** na umoja wa taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa vifungu hivi katika Katiba ya Mwaka 1977 bado maliasili za nchi hii kama wanyamapori, misitu, madini, gesi, hewa, mafuta, maji na uvuvi, na hata mgawanyo wa ardhi umegubikwa na rushwa. Rasilmali zetu hususani madini na wanyapori yamekosa usimamizi mzuri kiasi kwamba wachache ndio wanaonufaika na wananchi wetu hususani wale wanaozunguka maeneo hayo wamebaki kuwa maskini wa kutupwa. Vijiji vinavyozunguka misitu ya hifadhi na migodi imekuwa ikikumbwa na mapigano ya mara kwa mara,manyanyaso makubwa kutoka kwa baadhi ya wawekezaji na hata vifo kwa raia wema wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika,mfano dhahiri nimauaji yaliyowahi kutokea katika mgodi wa Geita ambayo yamekuwa yakiripotiwa ikiwa ni pamoja na mauaji ya mwanafunzi wa darasa la tano katika shule ya Kivukoni marehemu Hoja Juma, vitendo vya mauaji, utesaji na kuwabambikizia kesi wanavijiji katika vijiji vinavyozunguka mgodi wa North Mara (NMGM), madhara ya kiafya pamoja na ucheleweshaji wa fidia katika maeneo mbalimbali ambayo serikali imewakaribisha wawekezaji bila kujali mustakabali wa wananchi katika maeneo hayo. Katika bonde la Loliondo wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakiishi kama wakimbizi kutokana na manyanyaso makubwa wanayopata kutoka kwa baadhi ya wawekezaji wa kigeni huku serikali ikiyafumbia macho kutokana na rushwa kubwa kubwa zinazowanufaisha vigogo wa juu serikalini. Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiipigia kelele kampuni ya Ortello

Business Corporation (OBC) kutoka falme za kiarabu ambae amekuwa mwiba mkubwa kwa wananchi wa Loliondo na kuona kama wametengwa katika taifa lao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi kuhusu ushirikishwaji katika maamuzi yanayohusu utumiaji wa maliasili katika maeneo yao. Wananchi katika maeneo mbalimbali yenyе rasilimali wamekuwa wakiyatunza vizuri na bila uharibifu wowote lakini pale wanapoanza kuletwa wawekezaji **bila kuwashirikisha na kinyume na matarajio yao** basi wananchi hao wamekuwa wakileta vurugu jambo ambalo sio afya kwa wawekezaji na haileti taswira nzuri katika sekta ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje. Mfano, vurugu zilizowahi kutokea Mwezi Januari na Februari 2013 mkoani Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani illeleza kwa kina sana katika hotuba ya nishati na madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kuhusu katiba na mustakabali wa madini, mafuta na gesi asilia ikitoa mifano hai ya uzoefu wa nchi mbalimbali zilizofanikiwa baada ya kutatua changamoto mbalimbali za kikatiba, kisheria na kisera ili kulinda rasilimali za nchi. Mfano, nchi ya Norway imeweka mwongozo wa uwajibikaji katika matumizi ya maliasili kwenye Katiba yao Ibara ya 110 (b) ambapo ibara hiyo inasema "*every person has a right to an environment that is conducive to health and to natural surroundings whose productivity and diversity are preserved. Natural resources should be made use of on the basis of comprehensive long-term considerations whereby this right will be safeguarded for future generations as well*". Mwaka 2009 nchi ya Bolivia ilianza mchakato wa kupata katika mpya ambao pamoja na mambo mengine katiba hiyo ililenga kuhakikisha kuwa mafuta na gesi asilia yanawanufaisha wananchi wa Bolivia.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ni dhahiri katiba ya sasa ya mwaka 1977 haitaweza kutuhakikisha kuwa rasilimali zetu zinatukomboa katika lindi la umaskini ambao umetukabili kwa takribani miaka 56 sasa hata baada ya uhuru. Msimamo wa katiba pekee ndio utakaoweza kufafanuliwa vizuri katika

sheria zetu zinazolinda rasilimali zetu. Mfano, katika Katiba ya Bolivia imeeleza bayana kuwa serikali ya nchi hiyo itakapoingia ubia na makampuni binafsi katika utafutaji na uvunaji wa mafuta na gesi asilia itakuwa na hisa zisizopungua asilimia hamsini na moja (51%) ya hisa zote. Jambo hili limewekwa bayana ndani ya katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa mifano hii iliyo wazi ni kuwa Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa katika usimamizi wa rasilimali zetu na ili kujikwamua katika hili tunahitaji maoni ya rasimu ya pili ya katiba ambayo ilipendekeza namna bora ya kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali zetu ili ziweze kumnuifaisha kila mwananchi.

Mheshimiwa Spika, tulipofika sasa kama taifa hatuhitaji kuwa na katiba yenye viraka viraka. Tunahitaji kuwa na katiba mpya inayoendana na kasi ya ukuaji wa uchumi na ushindani wa kibiashara, mabadiliko ya kimfumo katika teknolojia, mashirikiano ya nchi mbalimbali na misimamo ya taifa na utaifa wetu, utawala bora, inayozingatia demokrasia , haki za binadamu na utawala wa sheria. Hivyo, rasimu ya pili ya katiba imetoa maoni ya wananchi ambayo kimsingi yanashabihiana na uhitaji huo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanataka kuona katika ikiwashirikisha katika kumiliki faida zitokanazo na rasilimali zao ,ikiwa ni pamoja na michakato ya wazi ya utoaji wa leseni,katiba inayotoa mamlaka kwa Bunge kupitia na kuridhia mikataba mbalimbali inayohusu uvunaji wa maliasili ya Taifa ili kuongeza uwazi. Lakini pia, katiba itoe fursa kwa wananchi kuwa na sauti dhidi ya bunge lao, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanapata taarifa ya kila kinachoendelea ndani ya Bunge kwa kuwa Bunge ndio mkuu wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kurejesha mara moja mchakato wa rasimu ya pili ya katiba kwani katiba pendekenzwa haikuzingatia maoni ya wananchi . Vilevile, Kambi Rasmi ya

Upinzani inaitaka serikali kutatua mkwamo wa mchakato wa katiba uliojitokeza katika serikali hii ya awamu ya tano bila sababu mahususi. Kuendelea kwa mkwamo huu kunatoa taswira hasi kwa serikali ya awamu ya tano sio tu ndani ya nchi bali pia katika medani za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kwa umuhimu huu wa katiba mpya Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli kurejea katika Ibara ya kwanza ya Katiba ya Japan inayosema *"The Emperor shall be the symbol of the State and of the unity of the People, deriving his position from the will of the people with whom resides sovereign power"*. Ikiwa na maana kwamba Mheshimiwa Rais azingatia matakwa ya wananchi katika kuwalettea kile walichokionomba kwa muda mrefu ambacho ni rasimu ya pili ya Katiba.

2.1. Katiba Mpya ni Msingi wa Kujenga Taasisi Imara kwa Maendeleo Endelevu

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani imezuka desturi kuwatukuza viongozi wa umma na kufuata maelekezo yao katika utendaji wa Serikali na kuweka kando mifumo ya kitaasisi iliyopo kwa mujibu wa sheria jambo ambalo limekuwa kikwazo kikubwa katika kuifikia azma ya Taifa ya kuwa na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na desturi hiyo mbaya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa Serikali kukemea kasumba hiyo na badala yake kuwekeza katika *"Kujenga Taasisi Imara kwa Maendeleo Endelevu (Building Strong Institutions for Sustainable Development)"* Sababu kubwa ya kuweka msisitizo huo ni kutokana na ukweli kwamba; ili kuwa na uendelevu (sustainability) katika jambo lolote ni lazima kuwe na mifumo imara ya kitaasisi, kanuni, taratibu na sheria zitakazofuatwa juu ya namna ya kutekeleza jambo hilo; na sio kufuata matakwa ya mtu au kikundi cha watu katika kufanya hivyo kwa kuwa watu ni wa kupita lakini taasisi na mifumo itabaki.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji taasisi imara zinazozingatia misingi ya utoaji haki, ulinzi wa amani na zinazojali uwajibikaji wa pamoja ili kujenga jamii jumuishi kwa maendeleo endelevu. Tunahitaji jamii ya watu huru wanaoishi bila hofu ya kutekwa, kutengwa na wapendwa wao, kuuawa, au vitisho vya namna yoyote. Tunahitaji kuwa na mahakama zilizo huru, zinazoweza kutoa maamuzi yanayozingatia sheria na haki bila mashinkizo ya mtu yoyote. Tunahitaji kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi inayofanya kazi kwa uhuru bila shinikizo la mtu au kikundi cha watu, tunahitaji kuwa na Bunge lenye uwezo wa kuikosoa serikali na kuiwajibisha serikali, tunahitaji jeshi la polisi linalozingatia sheria, usawa na haki za binadamu. Tunahitaji Jeshi la Wananchi lisiloegemea upande wowote, na linalowajibika kwa wananchi wote wa Tanzania na tunahitaji taasisi zote na idara za Serikali zifuate sheria na kanuni na sio maelekezo au matakwa ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, ili taasisi nilizotaja ziweze kuwa imara ni lazima tuwe na Katiba Bora itakayoweka utaratibu wa jinsi taasisi hizo zinapaswa kuendeshwa. Aidha, katika kujenga taasisi imara tunahitaji kuwa na viongozi wanaoheshimu katiba na sheria za nchi. Katika ulimwengu wa sasa, hatuhitaji kumjenga mtu mmoja au kikundi kidogo cha watu kwa kuwa hao watapita ila taasisi zatabaki. Katika historia; mifumo ya nchi iliyomjenga mtu mmoja au kikundi kidogo cha watu imesambaratika, na kuziacha nchi hizo katika migogoro mikubwa na udikteta wa kutisha.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana kwamba taasisi tulizo nazo zimekuwa dhaifu sana na udhaifu huo umesababishwa na vingozi wanaopenda kutawala kwa kutumia njia za mkato – wasiopenda kufuata taratibu za kisheria za kitaasisi. Tumeshuhudia sheria zikivunjwa na viongozi kwa kutoa kauli au matamko ambayo ni kinyume na sheria; watu wananyimwa haki zao za kikatiba na kisheria lakini taasisi husika zinazotakiwa kukemea mambo hayo zimekaa kimya.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano mdogo tu wa uchaguzi wa marudio wa kata 43 za udiwani na ubunge. Ule haukuwa

uchaguzi bali ni unyanganyi wa kimabavu kwani kulikuwa na uporaji wa wazi wa karatasi za matokeo ambapo vyombo nya dola vilitumika vibaya kuingilia uchaguzi huo. Lakini Tume ya uchaguzi ambayo ndiyo taasisi yenye dhamana ya kusimamia uchaguzi huo haikutimiza wajibu wa kusimamia chaguzi hizi ipasavyo na hili linatia shaka na kujenga hisia kwamba chombo hiki pengine kinafuata maelekezo kutoka kwa mtu au chombo fulani. Udhaiyu kama huo, upo katika taasisi nydingi ikiwemo Ofisi ya Msajili wa Vyama nya siasa anayeshabikia migogoro ya vyama nya siasa badala ya kuwa msuluhishi.

Mheshimiwa Spika, Ni muda mwafaka sasa kama taifa kuunda taasisi imara zenye uwezo wa kujisimamia na kufanya kazi kwa ufanisi. Mfano; Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) ni lazima iweze kujitathimini katika utendaji wake ili kuzuia taasisi hiyo kufanya kazi kwa visasi, uwepo wa taasisi inayotathimini utendaji wa Jeshi la Polisi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ofisi ya msajili wa vyama nya siasa nk.

Mheshimiwa Spika, Kutohana na udhaifu wa taasisi zetu, tumeshuhudia vyombo nya dola kama polisi vikivunja sheria kwa makusudi na watendaji wake wakuu wakijinasibu hadharani kwamba wanafuata maelekezo. Utendaji wa namna hii unajulikana kabisa ni kinyume cha sheria. Lakini hoja ya msingi ni kuwepo na chombo huru inachotathimini utendaji kazi na uwajibishaji wa taasisi hizi ili kupunguza utovu mkubwa wa nidhamu unaofanywa na baadhi ya watendaji wakuu kwa kivuli cha maelekezo kutoka juu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na taasisi ya kuangalia maadili ya watumishi wa umma, lakini kwa bahati mbaya sana taasisi hii inakosa nguvu ya kufanya kazi kutohana na mashinikizo kwani watendaji wake wakuu ni wateule wa lkulu. Jambo hili liko wazi kwa kuwa taasisi imeshindwa kuwachukulia hatua wateuliwa wa lkulu kwenye sakata zima la kuhusu vyeti feki. Pia, tumeshuhudia watendaji wa Serikali ambaao ni wateuliwa wa lkulu wakifanya kazi za uenezi wa

Chama cha Mapinduzi. Masuala kama haya yanapelekea wananchi kukosa imani na taasisi hii ya kushughulikia maadili ya viongozi wa umma.

Mheshimiwa Spika, bila kuboresha utendaji kazi wa taasisi zetu haitawezekana kamwe kuwa na maendeleo endelevu ndani ya nchi yetu. Ni jukumu letu sote kulitazama jambo hili kwa kina na kulifanya kazi haraka iwezekanavyo ili kunusuru nchi yetu kuingia katika mipasuko inayotokana na ubaguzi, chuki na visasi na hata kuingia katika majanga yakiwemo machafuko ambayo kimsingi yanawenza kugharimu maisha ya watu wetu, kuporomosha uchumi wetu na kuharibu jina zuri la taifa letu lilitolinda misingi ya amani na utulivu tangu uhuru.

3. MWENENDO WA HALI YA SIASA, ULINZI NA USALAMA NA ATHARI ZAKE KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, upo uhusiano wa karibu sana kati ya hali ya siasa, ulinzi na usalama na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Ni ukweli usiobishaniwa kwamba; kama hali ya siasa, ulinzi na usalama katika taifa haipo vizuri; ni dhahiri kwamba kunakuwa na mvurugano wa mambo jambo ambalo ni kikwazo kwa utekelezaji bora wa Mpango wowote wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hali ya siasa nchini Tanzania kwa sasa si ya kuridhisha. Wapo wanaoona kwamba wao pekee ndio wenye haki ya kufanya siasa na kuharamisha wengine kufanya siasa. Aidha, hali ya usalama ina mashaka. Siku hizi matukio ya utekaji na mauaji yenye kutatanisha yamekuwa ni kawaida katika nchi yetu. Hali kadhalika hali ya ulinzi imedhoofu. Siku hizi kiongozi kupigwa risasa akiwa maeneo yenye ulinzi, au watu mashuhuri kutekwa katika maeneo yenye ulinzi yamekuwa ni matukio ya kawaida pia. Mazingira yote hayo hayawezi kamwe kuwavutia wawekezaji wakubwa tunaowahitaji katika kuujenga uchumi wetu. Halikadhalika mazingira hayo hayawezi kuwapa motisha wafadhili wetu kutoa fedha za kutekeleza miradi yetu ya maendeleo. Na

tayari baadhi ya wafadhili wetu wameanza kukataa kutoa fedha kutokana na mwenendo wa siasa za nchi yetu usioridhisha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na watanzania wote wanaopenda kuona haki ikitamalaki katika taifa, tunalaani na tunapิงا vitendo viovu vya uonevu, ukandamizaji, utekaji na sasa majaribio ya mauaji yanayofanywa dhidi ya wanachama na viongozi wa vyama vya Upinzani hapa nchini. Ikiwa vitendo hivi vitaachwa viendelee bila kukemewa na kushughulikiwa kwa uzito unaostahili, kuna hatari ya kundi linalohisi kuonewa likakosa uvumilivu na hivyo kuathiri amani ya nchi; na amani ikitetereka, hakuna Mpango wowote wa maendeleo utakaoweza kutekelezwa na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ni mwaka mmoja na mlezi miwili sasa imepita tangu Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Tundu Lissu anusrike kifo baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi wakati Mkutano wa Nane wa Bunge ukiwa unaendelea na vikao vyake hapa Dodoma na mpaka sasa hakuna taarifa rasmi iliyotolewa na Serikali juu ya kukamatwa kwa watu waliohusika na tukio hilo. Ikiwa polisi wameshindwa kufanya uchunguzi na kuwakamata wahalifu hao ndani ya mwaka mmoja na miezi miwili, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni muujiza wowote unaoweza kutendeka ili watu hao wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria hata kama polisi wataongezewa miaka mingine miwili. Tafsiri ya ukimya huo wa Serikali ni rahisi; kwamba hakuna dhamira ya dhati wala utayari wa kushughulikia jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, si nia yangu kuorodhesha matukio mabaya wanayofanyiwa viongozi wa upinzani hapa nchini kwa kuwa ni mengi na pia tumeyasema sana humu bungeni; na wakati mwingine kuamriwa kuyafuta katika hotuba zetu, lakini hili la kutuwinda kwa lengo la kutuuwa, hatuwezi kamwe kulinyamazia. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa wananchi wote kupaza sauti zao kupinga uonevu na ukandamizaji wa haki, kupinga matukio ya utekaji, utesaji na

umwagaji damu katika nchi. Aidha, tunatoa wito kwa waumini wa dini na madhehebu mbalimbali kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu awaponye wale wote walioathirika na matukio hayo lakini zaidi sana kuliepusha taifa na laana kwa damu ya watu wasio na hatia iliyomwagika katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ili Mpango huu wa Maendeleo tunaoujadili leo uweze kufikia malengo yaliyokusudiwa, ni lazima tuutekeleze tukiwa na umaja na mshikamano kama taifa. Kamwe haitawezekana kuyafikia hayo maendeleo tunayotaka kwa kubaguana kwa itikadi za kisiasa, au kwa kubezana, kunyanyasana, kuoneana, kuumizana na kuuwana. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa viongozi wote katika ngazi mbalimbali kuitunza na kuilinda amani ya nchi yetu kwa kutenda haki, na kuacha mara moja tabla za ubaguzi, uonevu, ukandamizaji na unyanyasajili dhidi ya watu wanaowaongoza.

4. UWEKEZAJI KATIKA RASILIMALI WATU KWA MAEDELEO ENDELEVUU (INVESTING ON HUMAN CAPITAL FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT)

Mheshimiwa Spika, ni nadharia na uzoefu wa kawaida kwamba; taifa lolote linalotaka kujitegemea na kujinasua kwenye dimbwi la utegemezi na umasikini linajitahidi sana kuwajengea watu wake uwezo wa ki-elimu, ki-ufundi na maarifa ili kuweza kukabiliana changamoto mabalimbali na hivyo kuweza kuyamudu mazingira yao. Kwa sababu hiyo; taifa la namna hiyo, huwekeza sana katika elimu ili kuandaa wataalamu (rasilimali watu) wa kutosha wenye weledi wa kuendesha sekta mbalimbali za uchumi.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu hiii, Serikali ya awamu ya kwanza ilikuja na sera ya Elimu ya Msingi kwa Wote - Universal Primary Education na kujikita sana kwenye elimu ya kujitegemea ambayo iliwapatia wengi maarifa ya kujajiri na kuendesha maisha yao. Hata elimu ya juu iligharamiwa kwa asilimia 100 na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Licha ya nchi yetu kuwa bado kwenye dimbwi la umasikini; na licha ya kuwa bado nchi inakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa rasilimali watu, Serikali hii ya awamu ya tano imechagua kuwekeza katika vitu badala ya watu. Ni kweli tunahitaji maendeleo ya vitu kama tunavyoona Serikali ikijenga reli ya kisasa, viwanja vyta ndege, kununua ndege mpya ujenzi wa mabarabara nk. lakini nachelea kusema kwamba vitu hivyo vinaweza kudumu kwa muda mfupi mno kama hatutawajengea watu wetu uwezo wa kuvifanya wenyewe na kuviendesha. Kambi Rasmi ya Upinzani ingefurahi kuona makandarasi wa kujenga reli ya kisasa; na hata mabarabara yetu wakiwa ni watanzania wenzetu. Lakini tathmini fupi inaonyesha kuwa miradi mikubwa ya maendeleo hapa nchini iko mikononi mwa makandarasi wageni. Watu wetu wanaambulia kazi za kuchimba mitaro, kubebea mizigo na kufanya kazi zile ambazo hazihitaji ujuzi na matokeo yake hata ujira wao ni ule wa mboga tu.

Mheshimiwa Spika, Katika ulimwengu wa utandawazi, ufunguo wa mafanikio ya kiuchumi unategemea sana uwezo wa nchi kupata na kutumia ujuzi/maarifa kwa ufanisi na kwa faida katika sekta za kipaumbele na ambazo zinaweza kukua.Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya uwekezaji mkubwa katika rasilimali watu, kwa kuwa watu wenye ujuzi ndio msingi mkuu wa kuwepo kwa mfumo wa viwanda unaochochaea ukuaji wa uchumi. Uwekezaji katika vitu na katika taasisi ni vikamilisho muhimu vyta rasilimali watu; kwani rasilimali (vitu) haitatumiwa vizuri, iwapo itakosa ujuzi wa kiufundi na kiuongozi.

4.1. Miradi ya Kimkakati na Maandalizi ya Rasilimali Watu kwa ajili ya Kutekeleza na Kuendesha Miradi Hiyo

Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya tano imeeleza katika mpango kuhusu miradi ya kimkakati pamoja na maelezo mengi kuhusu uchumi wa viwanda. Pamoja na miradi hiyo ya kimkakati ambayo imeelezwa na serikali, haijaaelezwa popote kuhusu namna ya kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya kuendesha na kusimamia miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani kutokukubaliana na namna miradi hiyo inavyogharamiwa lakini ni lazima kwa vyovytote huwezi kuendesha miradi kama ya ununuzi wa ndege, reli kwa kiwango cha standard gauge au mradi wa stiglers gorge bila kuandaa wataalam na rasilimali watu ambaa wataendesha na kusimamia miradi hiyo ili iweze kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, haitashangaza kusikia kwamba kwa sasa Shirika la Ndege ndio linapeleka wataalam nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza kuendesha na kusimamia shirika hilo jambo ambalo lingetakiwa kufanyika wakati wa maandalizi ya mradi ili kuwe na mwendelezo wa kuendesha shirika hata baada ya kupata ndege ambazo zinahitaji wataalam.

Mheshimiwa Spika, tulishasema na tunaendelea kusema kuwa huwezi kusema uchumi wa viwanda bila kuanza kuhuisha mfumo wetu wa elimu ili uendane na uweze kufikia lengo kuelekea uchumi wa viwanda. Vivyo hivyo huwezi kuwa na miradi mingi ya kimkakati bila kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya kuiendesha. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri kulieleza Bunge juu ya mkakati wa kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango hasa kwenye miradi ya kimkakati.

5. UDHAIFU WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO KATIKA KUKABILIANA NA MAJANGA NCHINI

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa katika nchi yetu tumekumbwa na majanga mbalimbali ya asili ambapo mengine yanatokana na uzembe ikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya usafiri na mengine yanayotokana na Serikali kushindwa kuchukua hatua za awali na za dharura kabla ya majanga hayo kutokea.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha sasa tutegemee athari nygingi za kimazingira na majanga ya asili yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi. Mabadiliko ya tabia nchi huathiri sekta karibu zote kama Taifa lisipojiandaa kukabiliana nayo mapema.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hajasahau majanga kama ya tetemeko lilitokea Kanda ya Ziwa Victoria tarehe 10 Septemba, 2016 ambapo Mkoa wa Kagera uliathiriwa zaidi ambapo wananchi wengi walikufa, wengine kukosa makazi, chakula na maji safi na salama. Aidha miundombunu ya elimu pamoja na afya iliathiriwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Serikali vifo vilivyoripotiwa kutokana na tetemeko hilo ni 17, Majeruhi 440, nyumba zilizobomoka 2,063, nyumba zilizopo katika hatari ni 14,081, nyumba zilizopata uharibifu mdogo 9,471 na jumla ya watu ambaao walihitaji msaada walikuwa 126,315.

Mheshimiwa Spika, pamoja na athari hizo, majibu ya Serikali kwa wananchi kupitia Rais wa nchi ilikuwa "Serikali hajasababisha tetemeko" na kama hilo halitoshi Serikali iliwataka wananchi kujenga nyumba zao wenye kwa kuwa Serikali haiwezi kufanya kazi hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inachukulia kauli hizo kama kejeli kwa wananchi ambaao hutoa ridhaa kwa Serikali iliyopo madarakani kuongoza nchi. Badala Kiongozi Mkuu wan chi kuwa mfariji anageuka na kuwa mtu wa kuongeza machungu kwa wananchi walioathiriwa na janga hilo.

Mheshimiwa Spika, Kabla vidonda vyaya tetemeko havijapona vizuri, hivi karibuni Taifa llikumbwa na janga lingine kubwa ambapo tarehe 20 Septemba, 2018 Meli ya MV Nyerere ilizamana na kusababisha vifo zaidi ya 200 ambapo ilikuwa ikifanya safari ya Kisiwa cha Bugorora kuelekea Kisiwa cha Ukara.

Mheshimiwa Spika, kilichoshangaza katika janga hili ni kuwa shughuli za uokoaji zilisitishwa kwa sababu ya giza huku kukiwa hakuna hatua za dharura kuwaokoa wahanga wa ajali hiyo. Aidha, wahanga wengi waliokolewa na miili mingi kuopolewa kwa kushirikiana na wavuvi wanaofanya shughuli katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, majanga haya mawili nimeyaeleza kwa sababu ni ishara kwamba Serikali hii ya CCM haina mkakati wala nia ya kuhakikisha kuwa inakuwa na bajeti, vifaa na kutumia teknolojia kukabiliana na majanga nchini.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu, licha ya mabadiliko ya tabia nchi kuathiri kila sekta kama nilivyooleza awali; bado hakuna kipaumbele chochote kinachopewa eneo hili. Ukrejea Randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu (fungu 37) kwa mwaka wa fedha 2017/18, kifungu 2001 mradi namba 6575 "*Kujenga Uwezo wa Kujianadaa na Kukabili Maafa*" hakuna fedha yoyote ya ndani iliyokuwa imetengwa kwa ajili shughuli hiyo. Fedha za nje zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo zilikuwa ni shilingi 440,000,000/-; lakini hadi mwezi kufikia mwezi Februari 2018 hakuna fedha yoyote iliyopokelewa.

Mheshimiwa Spika, Aidha, katika kifungu hicho cha 2001 mradi namba 5306 "*Kuimarisha Taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi na Mifumo ya Tahadhari*" haukuwa umetengewa fedha yoyote ya ndani. Fedha ya nje ilikuwa ni shilingi 1,021,618,000/- na hadi mwezi februari 2018 zilikuwa zimetolewa shilingi 283,986,200 sawa na asilimia 28.7 pekee.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu 2018/2019 kifungu hicho 2001 chenye miradi hiyo hiyo hakikutengewa fedha yoyote ya ndani. Fedha za nje zilizotengwa ni shilingi 176,530,200/- kwa maradi namba 6575 na shilingi 286,923,269/- kwa mradi namba 5306. Hata hivyo fedha hizo zimepungua ukilinganisha na mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, wakati nchi yetu imeridhia mikataba ya kimataifa kuhusu namna ya kukabiliana na athari za kimazingira na mabadiliko ya tabia nchi; lakini kinachofanyika ndani hasa suala la kutenga na kutekeleza bajeti kuhusu masuala hayo ni kinyume na jinsi ilivyokuwa imekubaliwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba Tanzania imekuwa inachukua hatua mbalimbali katika kuelezea mabadiliko ya tabianchi kwa muktadha wa nchi yetu na hivyo kutayarisha

nyaraka muhimu za mkakati kama vile "The National Climate Change Strategy (2012) and the Zanzibar Climate Change Strategy (2014)" ambazo zinazeleza kwa kina hatua za kuchuka katika kukabiliana na Mabadiliko ya Tabinanchi. Kambi Rasmi inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini kila mara inashindwa kutenga na kutoa fedha za ndani ikiwa kulikuwa na Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Mabadiliko ya Tabia Nchi?

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utelezaji wa Mpango Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Mwaka 2016/2017-2018/2019 cha Oktoba, 2018 ambacho amewasilisha Waziri katika Bunge lako tukufu ukurasa wa 14 miradi namba 48 na 49 yaani kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa na kuimarisha taarifa za mabadiliko ya tabianchi na uboreshaji wa mifumo ya tahadhari za awali serikali haikutenga hata senti kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa Serikali imewaacha wahisani kushughulikia dhamana ya watu wetu kwa sababu katika taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo wahisani walitoa fedha walizoahidi kwa zaidi ya 95% huku serikali ikitenga na kutoa sifuri katika miradi hiyo hiyo. Katika hali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani haikushangaa kuona Mkuu wa Mkoa wa Mwanza akisitisha shughuli za uokoaji kwa sababu ya kuingia kwa giza.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi kama vile ukame wa muda mrefu, mvua kubwa zinazosababisha mafuriko na ambapo athari hizo huathiri shughuli za kiuchumi na maisha ya wananchi kwa ujumla, kwa sababu hiyo tunaitaka Serikali kuanzisha mfuko wa fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na sio kutenga sifuri katika bajeti kwa miaka miili mfululizo huku nchi ikiendelea kukumbwa na majanga mbalimbali ambayo athari ni kubwa na kuangamiza maisha ya watu. **Aidha, ni wakati muafaka sasa Serikali ikaishirikisha Sekta Binafsi katika kukabiliana na majanga.** Sekta Binafsi ingekuwa imepewa nafasi katika masuala ya kukabiliana na majanga na uokozi, yamkini vifo

viliyotokea wakati wa kuzama kwa kivuko cha MV Nyerere vingeweza kupekwa.

6. UHUSIANO WA KIMATAIFA NA ATHARI ZAKE KATIKA MIPANGO YA SERIKALI

6.1. Ukakasi Kuhusu Mradi wa Reli ya Standard Gauge railway na Uhusiano wa Kimataifa

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani katika uchambuzi wake imerejea kitabu cha Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya mwaka wa fedha 2018/19 katika ukurasa wa 18, Serikali imeeleza kuwa Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki nchini China tarehe 17 hadi 20 Desemba, 2017 ambapo serikali inaeleza pia kuwa katika ziara hiyo Waziri aliwasilisha kwa serikali ya China miradi ya kimkakati ambayo Serikali inategemea kuitekeleza ikiwemo mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR), kusafirisha umeme kutoka Rufiji hadi Chalinze na Chalinze hadi Dodoma, mradi wa kufua umeme wa Stiglers Gorge, ujenzi wa Bwawa la Maji la Kidunda na ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya serikali hakuna sehemu ambayo wameonyesha wala kueleza idadi ya miradi ambayo serikali imeshaingia makubaliano ya awali na serikali ya China kwa ajili ya utekelezaji. Aidha, sote tunatambua kuwa taarifa zilizokuwa kwa umma ilikuwa makubaliano ya awali kati serikali ya Tanzania yalishafikiwa kuhusu China kushiriki katika ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR). Ni jambo gani ambalo lilipelekea China kujitoa katika mradi huo?

Mheshimiwa Spika, sote tunambua kuwa kwa sasa SGR inajengwa na Kampuni kutoka Uturuki, lakini kama tulivyoeleza kuwa wakati wa serikali ya awamu ya nne taarifa zilitolewa kuwa China ndiyo itakayojenga SGR kwa mkopo kutoka Bank ya Exim ya China. Kama Waziri na serikali kwa ujumla walilitambua hili, ni sababu gani ilimfanya Waziri wa

Mambo ya Nje kwenda tena China kufanya majadiliano kuhusu mradi huo ambao wamebadili mkandarasi? Kuna tofauti gani kwa maslahi ya Taifa ambayo tumeipata kuwaacha Wachina na kwenda kwa Waturuki?

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo ya Serikali bado kuna mkanganyiko kuhusu namna ugharamiaji wa mradi wa SGR kwa kuwa mara kadhaa Rais Magufuli amenukuliwa akisema kuwa SGR inagharamiwa na fedha za ndani kwa asilimia 100, wakati huo huo Waziri wake wa Mambo ya Nje anazunguka kwenye mataifa ya nje kutafuta ufadhili. Ukweli ni upi?

Mheshimiwa Spika, aidha hivi karibuni Waziri wa Fedha na Mipango alinukuliwa na vyombo vyaa habari akiomba Benki ya Barclays kuona namna ya kutoa mkopo kwa serikali kugharamia ujenzi wa SGR. Je serikali inafaidika na nini kwa kutoa kauli tofauti tofauti kuhusu ugharamiaji wa mradi huu?

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Jarida la The Economist Intelligence inaonesha kuwa kuna ugumu kupata mikopo ya ujenzi wa miradi nchini Tanzania na pia hakuna uwazi kuhusu ghamama na lini miradi hiyo itakamilika jambo ambalo linatoa taswira hasi kwa wawekezaji na taasisi za fedha za kimataifa. Aidha, kitendo cha kukosekana kwa uwazi kama ni fedha za nje au ni za ndani zinatumika kujenga SGR kunatoa ishara ya mazingira ya ujisadi.

6.2. Tathmini ya Mafanikio ya Kiuchumi ya SGR

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza kwamba ujenzi wa Reli kwa kiwango cha Standard gauge (SGR) utatoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Katika hali ya kushangaza tarehe 20 Septemba, 2018 jarida la Expogroup liliripoti kuwa Tanzania imepata mkopo wa dola bilioni 1.4 ambazo ni zaidi ya trillioni 3 kutoka Benki ya Standard Chartered kwa ajili ya kugharamia kipande cha Morogoro hadi Makutupora Dodoma³.

³ https://www.expogr.com/tanzania/build-expo/detail_news.php?newsid=5472&pageid=2

Mheshimiwa Spika, habari hiyo ni tofauti na maelezo ambayo yamekuwa yakitolewa na Rais Magufuli kuwa tunajenga Reli ya kati kwa fedha zetu wenyewe. Kwa sababu jarida hilo limemnukuu Waziri wa Fedha, ni vema akalieleza Bunge lako tukufu kuhusu utaratibu wa ugharamiaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imemeleza kuhusu ujenzi wa kipande cha reli kwa kiwango cha SGR kutoka Isaka kwend Rusumo lakini haijaleza ujenzi huo kutoka Makutupora hadi Tabora na Tabora hadi Isaka.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikalieleza Bunge sababu za kiuchumi za kwa nini wajenge reli hiyo mpaka mwanza na rusumo kabla kwanza ya kujenga reli hiyo kutoka Tabora hadi Kigoma kwa ajili ya kufungua fursa za nchini ya DRC.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inapenda kuona reli hiyo ikifungamanishwa na uchumi katika maeneo ya kimkakati na sio kuelezwu muda wa kusafiri kwa treni ya reli ya kisasa kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam. Hii ni kwa sababu Kambi Rasmi inaanini kuwa mradi huo hautakuwa na tija kwa kulenga tu kupunguza muda wa abiria kusafiri bali kuufungamanisha na sekta nyingine za uchumi kwa ajili ya kuleta tija.

6.3. Ushiriki Hafifu wa Nchi yetu katika Mikutano ya Kimataifa ya Kimkakati Unavyoweza Kuathiri Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni mwaka 2017/2018 tulieleza kwa kirefu kuhusu umuhimu wa Rais kufanya ziara za kimkakati nje ya nchi ikiwemo kushiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Kongamano la Kiuchumi Duniani na mikutano mingine ambayo kiongozi wa nchi anabeba taswira ya Taifa letu kimataifa.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Rais kwa sasa ni kutosafiri kwenda nje ya nchi, jambo ambalo kama Kambi tunaona nchi inashindwa kupata fursa ambazo tungezipata kwa

kushiriki mikutano na makongamano ya kimataifa ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, imefikia hatua Makamu wa Rais anazidiwa kuiwakilisha nchi katika mikutano ya kimataifa wakati Rais wa nchi yupo. Mfano mdogo ni kongamano la hivi karibu la nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola ambapo viongozi wengine wa Afrika Mashariki walifanya vikao vingi vya kimkakati na wadau wengine wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ukitazama picha ambazo zilisambaa mtandaoni kuhusu vikao vya kimkakati alivyofanya Rais wa Jamhuri ya Kenya Uhuru Kenyatta; na alivyofanya Makamu wetu wa Rais na wadau wa maendeleo wakati walipohudhuria Kongamano la nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola utaona tofauti kubwa sana. Vikao vya Rais Kenyatta vilikuwa vingi na alikutana na wadau mbalimbali wa maendeleo tofauti na vikao alivyofanya Makamu wetu wa Rais vilikuwa vichache na pia wadau wachache. Hii inatoa taswira jinsi ambayo kama nchi hatupo makini kwenye masuala ya kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, ghamama za safari za nje zisitumiwe kama kisingizio cha Rais kutohudhuria mikutano ya kimataifa bali utazamwe umuhimu wa ziara hizo kwa nchi kwa ajili ya kujenga diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni umezuka utamaduni wa kuwahuisha viongozi wastaa fu kwenye mikutano ya kimataifa. Mara kadhaa ameonekana Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete katika mikutano kadhaa ya kimataifa bila kuelezwu wazi kama analiwakilisha Taifa au ameenda kwa mwaliko binafsi katika mikutano hiyo.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwenye kitabu chake cha randama uk. 25 serikali inaeleza yafuatayo;

" Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na

*Mheshimiwa Abdulrahman Kinana kwa ajili ya kumwakilisha
Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
kwenye sherehe za uapisho wa Mheshimiwa Paul Kagame,
Rais wa Rwanda tarehe 18 Agosti, 2017"*

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo ya Wizara ni ukweli kuwa kwa sasa viongozi wastaifu wanaiwakilisha serikali kwenye masuala ya kimataifa. Hoja ya msingi hapa ni je wastaifu ambao hawana mamlaka ya kiserikali tena, kwa sasa wanayo mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya serikali?

Mheshimiwa Spika, serikali imekiri na kuthibitisha kuwa imefikia hatua hata Katibu Mkuu wa CCM anagharamiwa na fedha za walipakodi kuiwakilisha serikali kwenye masuala ya uhusiano wa kimataifa. Tabia kama hii ni ishara kuwa serikali inayo nia ya kuigeuza nchi hili kuwa ya Chama kimoja kwa sababu serikali imeanza kukifanya chama kushiriki kwenye hafla za kimataifa kwa ghamra za fedha za walipa kodi ambao sio wote wanakiunga mkono Chama cha Mapinduzi.

6.4. Ukiukwaji wa Haki za Binadamu na Taswira ya Taifa letu Kimataifa

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili mwaka huu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilizindua taarifa yake ya mwaka 2017 ambapo jambo kubwa ambalo lilionekana kwa mwaka huo ni Watu Wasiojulikana walivyo Tishio la Haki za Binadamu nchini. Pamoja na taarifa hiyo, taarifa ya Mambo ya Ndani ya Marekani kuhusu Tanzania imeeleza na kuonesha matukio kadhaa ya ukiukwaji wa haki za binadamu nchini.

Mheshimiwa Spika, Aidha tarehe 10 Mei, 2018 asasi za kiraia 65 duniani zilimwandikia barua Rais Magufuli kuitaka serikali yake kuangalia namna ya kushughulikia tishio la mazingira mabaya kwa waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu na vyama via upinzani.

Mheshimiwa Spika, Asasi hizo za kiraia zimeeleza wasiwasi wao kuhusu hali ya watu kupotea, matukio ya watu

wasiojulikana kama vile kupigwa risasi kwa Mheshimiwa Tundu Lissu, kutekwa kwa Azory Gwanda na hivi karibuni kutekwa kwa Mfanyabiashara mkubwa nchini Mohamed Dewji, kuzuiwa kwa shughuli za kisiasa, kuminywa kwa uhuru wa kutoa maoni na kujumuika, kutumia sheria kandamizi kudhibiti vyombo vyaa habari na uhuru wa kutoa maoni.

Mheshimiwa Spika, Asasi hizo za kiraia zimeionya serikali kuwa ule msemo na sifa ya Tanzania kama kisiwa cha amani itapotea kama serikali isipochukua hatua za dharura kudhibiti hali mbaya ya kumomonyoka kwa misingi ya haki za binadamu nchini.

Mheshimiwa Spika, Wameshauri kuwa vifungu vyote vyaa Sheria ya Makosa ya Mtandao na Kanuni mpya za matumizi ya mitandao zilizotangazwa na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo zifutwe, kuvifutia adhabu vyombo vyote vyaa habari ambavyo vimeadhidiwa, uchunguzi huru ufanyike dhidi ya matukio ya utesaji, utesaji, kupotea kwa watu na wengine kushambuliwa kwa risasi pamoja na kuhakikisha kuwa uhuru wa watu wa kujumuika kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa unazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, imefikia hatua hata vyombo vyaa dola ambavyo kimsingi vilitakiwa kulinda wananchi na mali zao sasa vimekuwa sehemu ya mauaji na utesaji wa wananchi. Hili ni tatizo na janga kwa taifa kwa sababu Tanzania sio kisiwa ni sehemu ya Jumuiya za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na kigugumizi kuridhia Mkataba wa Kimataifa dhidi ya utesaji na kutwezwa (**International Convention Against Torture and Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment**) jambo ambalo linatoa taswira mbaya kwamba haina mpango wa kulinda haki za binadamu hapa nchini. Kutokana na mlolongo wa matukio haya ya utesaji, utesaji, kupigwa risasi kwa wananchi na mauaji katika vituo vyaa Polisi, Kambi Raski ya Upinzani inaitaka sasa Serikali kuuleta mkataba huo bungeni ili uridhiwe na Bunge ili matukio hayo ya ukiukwaji wa haki za binadamu yaweze kukomeshwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa matukio ambayo yanatokea nchini kwa sasa yanayofanywa na watu wasiojulikana ni wazi kuwa taswira ya Tanzania katika sura ya kimataifa imechafuka na ni lazima serikali ichukue hatua. Kama serikali inaziba masikio kwenye mambo kama haya taifa letu litatengwa na Jumuiya ya Kimataifa. Matokeo ya kutengwa au kunyooshewa kidole na Jumuiya ya Kimataifa kuna athari kubwa sana katika uchumi kwa kuwa bado Serikali inategemea misaada mingi ya kibajeti kutoka katika Jumuiya ya Kimataifa lakini pia pia watalii na wawekezaji ambao ni sehemu muhimu ya ujenzi wa uchumi wetu wataacha kuja kutokana na hofu ya usalama wao na hivyo kuathiri ukuaji wa uchimi wetu.

6.5. Serikali Kushindwa Kuitumia Diaspora Kiuchumi

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu imeshazungumza vya kutosha kuhusu umuhimu na namna serikali inavyoweza kuwatumia Watanzania wanaoishi na kufanya kazi katika mataifa mbalimbali duniani (**Diaspora**) kwa ajili kushiriki katika kujenga uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tulishawahi pia kushauri kuwa ili kuwe na uhusiano wa moja kwa moja kati ya nchi na Diaspora ni vema serikali ikaona haja ya kuwa na utaratibu wa uraia wa nchi mbili/ uraia pacha kama baadhi ya mataifa mengine yalivyofanya na kuendelea kunufaika na watu hawa ambao kimsingi ni Watanzania wenzetu. Zipo hoja kinzani zilizowahi kujengwa kuhusu pendekezo hili na mojawapo ni uwezekano wa kukosekana kwa uzalendo ikiwa Mtanzania atakuwa raia wa nyininge bila kuathiri uraia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Tumeshawahi pia kueleza namna nchi za Kenya, Ghana, Nigeria, Misri, Ethiopia na Afrika ya Kusini zinavyonufaika na kuwatumia vizuri Diaspora ambapo mapato yanayotokana na Diaspora (Remittance) yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2010 pekee taarifa ya Benki ya Dunia inaonyesha kuwa zaidi ya dola za kimarekani bilioni 40 ulikuwa mchango wa Diaspora kwa bara zima la Afrika.

Taarifa hiyo inaonyesha pia kuwa akiba ya Diaspora kwa mwaka ilikadiriwa kuwa zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 53⁴.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imetajwa kuwa moja ya nchi 12 zenyne Diaspora wengi katika nchi ya Canada. Je serikali imeweka mkakati gani kuwatumia watu hawa kunufaika na masuala ya biashara, uwekezaji, teknolojia na fursa za mikopo ya masharti nafuu?

Mheshimiwa Spika, ni vema serikali ikafahamu kuwa kwa kushirikiana na Diaspora tunaweza kunufaika na utaratibu wa PPP kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo kuliko sasa ambapo fedha za ndani nyngi zinatumika kwenye miradi mingi ambayo faida yake haitapatikana hivi karibuni na mikopo yenyne masharti magumu.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kushangaza umeibuka utaratibu wa serikali ya awamu ya tano ya kuwakamata Watanzania ambao wanafanya kazi na kuishi nje ya nchi wakiwa kwenye Viwanja vyatundege wakiwa na fedha zao na kuwapa tuhuma za uhujumu uchumi au utakatishaji fedha. Utaratibu huu unaanza kuwarudisha nyuma Diaspora kuingiza fedha nchini kwa ajili ya shughuli zao binafsi na shughuli za kibiashara. Kambi Rasmi ya Upinzani inalaani utaratibu huu ambao unazuia nchi yetu kunufaika na Diaspora. Serikali isijifiche kwenye makosa ya uhujumu uchumi au utakatishaji fedha kwa sababu makosa hayo yalikuwepo na utaratibu wa kuingiza fedha za kigeni unajulikana.

7. NAFASI YA SEKTA BINAFSI KATIKA UKUAJI WA UCHUMI

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Shirika la Fedha Duniani ya Januari 2018 kuhusu mapitio ya saba ya Mwongozo wa Sera ya Tanzania⁵ imeeleza pamoja na mambo mengine kuwa

⁴http://siteresources.worldbank.org/EXTDECPROSPECTS/Resources/476882-1157133580628/DfD_FullReport.pdf

⁵ IMF Country Report No. 18/11

The Seventh Review Under The Policy Support Instrument.

pamoja na pato la taifa kuonekana kukua mazingira ya biashara nchini sio rafiki kwa uwekezajina maendeleo ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo ya sasa, inaonekana dhahiri kuwa shughuli za kiuchumi ni dhaifu na hivyo kupelekea kushindwa kuzalisha ajira na kupunguza umasikini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kueleza kuwa pamoja na taarifa ya biashara nyingi kufungwa ambayo tulieleza kwa kirefu katika hotuba yetu ya mpango kwa mwaka uliopita, Waziri wa Fedha alijibu kwa idadi ya biashara mpya zilizofunguliwa na kueleza kwa propaganda kuwa biashara zilizofungwa zilikuwa zinahusishwa na ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Spika, kufungwa kwa biashara nchini sio jambo la kushangilia kwa sababu ni dhahiri kuwa wafanyabiashara hao walikuwa wanalipa kodi, na hivyo kuongezeka kwa makusanyo. IMF wanaeleza kuwa makusanyo ya kodi yameshuka tofauti najinsi ilivyokuwa inategemewa na hivyo kupelekea utekelezaji wa bajeti ya serikali kuwa dhaifu.

Mheshimiwa Spika, aidha bado mikopo isiyolipika katika mabenki ni tatizo kubwa pamoja na takwimu za Serikali kuonyesha kuwa Benki Kuu imetoa maelekezo kwa Mabenki kupunguza mikopo chechefu, jambo hilo ambalo linaathiri pia mazingira ya ufanyaji biashara kwa sababu kutokana na madhaifu yaliyopo katika mfumo wa sasa kodi na maelekezo ya kiutawala yasioangalia maslahi ya wafanyabiashara hupelekea wafanyabiashara kushindwa kulipa mikopo kwenye mabenki ya ndani⁶.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mara nyingine tena inakiri katika taarifa zake kuwa ukuaji wa mzunguko wa fedha nchini bado ni chini ya 12% ikilinganishwa na ukuaji wa 16.4% kwa mwaka ulioishia Julai 2015⁷. Tafsiri ya hali hii ni kuwa tusitarajie

⁶ Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti, Oktoba 2018 ukurasa wa 13

⁷ Ibid, ukurasa wa 12

wananchi kuwa na ahueni kama mzunguko wa fedha bado uko chini kiasi hiki na pia tusitarajie sekta binafsi kuendelea kukua katika awamu hii ya tano.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Rais inajinasibu kuwa mfumuko wa bei umepungua nchini, huku wakishindwa kuelewa kuwa kama mzunguko wa fedha ni mdogo kama ambavyo wanakiri katika vitabu nya mpango, hali ya sekta binafsi nchini iko taabani, mikopo katika mabenki hailipiki, watumishi wa serikali hawaongezewi mishahara wala posho, kupunguzwa kwa wafanyakazi katika mashirika ya umma na binafsi, hakuna kipyka kwenye hili kwa sababu ni ishara na ni wazi kuwa uwezo wa wananchi kununua umepungua na hivyo ni lazima mfumuko wa bei utakuwa chini.

Mheshimiwa Spika, sio chini ya miezi sita illyopita Rais alipokea kinachoitwa gawio kutoka katika Shirika la Simu la TTCL huku Rais akipongeza ‘management’ ya shirika na kuwataka waongeze mishahara kwa watumishi. Kabla Watanzania hawajasahau, Mkurugenzi Mtendaji amenukuliwa na Vyombo nya Habari akieleza kuwa Shirika linatarajia kupunguza Wafanyakazi 555. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuihoji Serikali juu ya uhalisia wa gawio hilo na kile ambacho kimetangazwa hivi karibuni cha kupunguza wafanyakazi. Ni vema pia Serikali ikafahamu athari za kucheza na mahesabu ya uchumi kisiasa na kipropaganda kwa sababu mara zote hesabu hazidanganyi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya IMF pia inaeleza kuwa hadi kufikia mwezi Septemba mwaka 2017 mikopo isiyolipika katika mabenki ya biashara iliongezeka kutoka asilimia 9.1 hadi 12.5.Hali hii ilipelekeea mabenki nchini kupata hasara kubwa jambo ambalo halijawahi kuwepo toka mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hatua za Benki Kuu kupunguza kima cha chini cha fedha zinazohitajika kuhifadhiwa na Benki za Biashara nchini ikiwa ni pamoja na kushusha kiwango cha riba bado sekta hiyo ilifanya vibaya na hivyo kuathiri mazingira ya biashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mauzo ya bidhaa kwenda nje ya nchi (export) yalionekana kushuka na pia makusanyo ya ushuru wa bidhaa nayo yalishuka kutokana na wananchi kupunguza matumizi ya bidhaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuangalia kwa umakini hali ya uchumi wa nchi kuliko kuendelea kutoa kauli za kuwashawishi wananchi kuwa hali ni nzuri wakati katika takwimu hali inaonekana tofauti.

Mheshimiwa Spika, serikali haiwezi kukusanya kodi ya kutosha kama mazingira biashara na sera za kodi ziko hovyo. Aidha serikali haitapiga hatua kama maamuzi ya namna ya kuboresha biashara yanafanywa na serikali kuu bila hata kuzingatia uhalisia wa mazingira ya biashara. Ikumbukwe kuwa serikali imejinasibu kupunguza matumizi ya kawaida kwa ajili ya kubana matumizi, jambo hili ni jema hasa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Kupunguza matumizi kwa sekta muhimu ambazo wafanya biashara walikuwa wanaingia mikataba ya kibashara pamoja na zabuni za serikali usitegemee kukua kwa biashara nchini kwa sababu serikali ndiyo inayohitaji huduma na kupata huduma na bidhaa ni lazima ishirikishe sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, yapo pia malalamiko ya wazabuni ambao walikuwa na madeni na serikali kwa sababu ya huduma au bidhaa ambazo walihudumia katika taasisi mbalimbali za serikali ambao hawajalipwa na serikali inasema bado inahakiki madeni hayo kama ni halisi. Wahanga wa uhakiki huu ni wafanya biashara ambapo pamoja na kushindwa kuendelea kufanya biashara kwa sababu ya madeni, hata madeni hayo yakilipwa bado hayalipwi kulingana na bei ya soko au kuangalia na thamani ya shilingi yetu ambayo bado inasuasua.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Bunge kupitia Kamati zake za kisekta zinazohusika na masuala ya uwekezaji na biashara nchini kuangalia hali hii ambayo si njema katika mustakabali wa Taifa letu na kuchukua hatua za dharura kuisimamia serikali ili kuepuka anguko la uchumi ambalo linakuja mbeleni.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo wa taifa 2018/2019 inazungumzia mazingira mazuri ya uwekezaji nchini. Ifahamike kuwa katika taarifa iliyotolewa na Bank ya Dunia ya ‘Doing Business 2019: Economy Profile Tanzania’ inaonyesha bado Tanzania ni moja ya nchi yenye mazingira magumu katika uwekezaji wa kibashara. Ni nchi ya 163 duniani katika unafuu wa uanzishaji wa biashara (starting a business). Pamoja na hayo Tanzania ni nchi ya 150 katika utika ukiritimba wa vibali vya ujenzi, ni nchi ya 146 duniani katika uvezeshaji wa usajili wa biashara, ni nchi ya 167 katika malipo ya kodi ikiwa na maana kuwa ina kodi nyingi katika mazingira ya kuanzisha biashara, na ni nchi ya 131 katika kuwalinda wawekezaji (Protecting minority Investors).⁸

Mheshimiwa Spika, Hii ikiwa na maana kwamba bado serikali yetu haijaweza kuthamini mchango wa sekta binafsi nchini na kuipa kipaumbele kinachostahili. Nchi kama Kenya ambayo ni nchi majirani wamejitatihidi katika kuhakikisha uanzishaji wa biashara na kuwalinda wawekezaji ni moja ya kipaumbele muhimu ambacho kinachochaea kukua kwa sekta binafsi nchini humo.

Mpaka sasa Kenya ni nchi ya 61 duniani katika kuhamasisha mazingira mazuri ya uwekezaji huku nchi kama Botswana ikishika nafasi ya 86. Hivyo ni wakati muhimu sasa kwa wataalamu wetu kujifunza kutoka kwa wenzetu ili kujua ni mbinu gani za kimsingi ambazo wametumia ili kuweza kuwavutia wawekezaji, kupanua sekta binafsi na kuishirikisha sekta binafsi katika maedeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani katika sera yake ya kushirikisha sekta binafsi katika maendeleo ya nchi inalenga kuhakikisha inaweka mazingira mazuri ya uwekezaji, uanzishaji wa biashara nchini, mifumo mizuri ya kikodi na kuwa na sheria na kodi zinazotabirika ili serikali na sekta binafsi ziweze kushirikiana kwa ufanisi katika kukuza uchumi wa nchi

⁸<http://www.doingbusiness.org/content/dam/doingBusiness/country/t/ tanzania/TZA.pdf>

7.1. Ushirikishwaji Hafifu wa Sekta Binafsi katika Uwekezaji kwenye Sekta ya Miundombinu

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya uwekezaji kwenye reli ya *standard gauge* (SGR), Mradi wa umeme wa Stiegler'sGorge, bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda mpaka Tanga na mradi wa Bandari ya Bagamoyo ambao kwa sasa hauzungumziwi sana lakini hakuna mkakati wa wazi wa namna miradi hiyo inagharamiwa.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa Rais John Magufuli anasikika akisema kuwa miradi hiyo inagharamiwa na fedha za ndani za walipa kodi, na wakati mwingine Waziri wa Fedha ananukuliwa akisema kuwa miradi hiyo inagharamiwa na fedha za mikopo mbalimbali. Hata hivyo kutokuwa wazi kuhusu gharama za miradi mikubwa na muda wa kuimaliza kunazua sintofahamu kuhusu uwezekano wa kumaliza miradi hiyo mikubwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kuwa kama serikali haitashirkisha sekta binafsi kuititia ubia (PPP) wachambuzi wa uchumi wameshauri kuwa deni la taifa litaendelea kukua na kuwa mzigo kwa walipa kodi. Aidha ikumbukwe kuwa serikali imekua ikikopa sana ndani na hivyo kutengeneza ushindani na wawekezaji wa ndani ambao pia wanatumia mikopo kuendeleza biashara zao.

Mheshimiwa Spika, Ushirikishwaji wa sekta binafsi sio utachochea tu mazingira ya biashara na mzunguko wa fedha nchini bali pia itaipunguzia serikali mzigo wa kuwekeza kwenye kila mradi mkubwa jambo ambalo linasababisha ugumu katika kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje na kuepuka serikali kukopa sana ndani kugharamia miradi hiyo.

8. UTEKELEZAJI DUNI WA BAJETI YA SERIKALI UNAVYOKWAMISHA MIPANGO YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani, kumekuwa na utamaduni mbovu wa kupanga

bajeti na kushindwa kuitekeleza jambo ambalo limekwamisha miradi mingi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kushindwa kwa Serikali kutekeleza kikamilifu bajeti yake kunatokana na sababu mbalimbali. Mosi, ni kuweka makisio makubwa ya makusanyo ya fedha; na kushindwa kukusanya kiasi hicho. Kile kiasi kilichoshindikana kukusanya kinakuwa ni makusanyo hewa; na ile miradi ambayo ilitakiwa kutekelezwa na kiasi hicho kilichoshindikana kukusanya huwa haitekelezwi kabisa. Kwa mfano:-

§ Katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi triliioni 29.54 lakini iliweza kukusanya mapato kutoka vyanzo vyote yaliyofikia shilingi triliioni 20.7 sawa na asilimia 70.1 ya lengo. Hii ina maana kwamba, asilimia takriban 30 iliyobaki (sawa na shilingi triliioni 8.83) ilikuwa ni makusanyo hewa, na miradi iliyotakiwa kutekelezwa na kiasi hicho haikutekelezwa.

§ Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi triliioni 31.71 lakini iliweza kukusanya kiasi cha shilingi triliioni 21.89 sawa na asilimia 69 ya lengo. Hii ina maana kwamba asilimia 31 iliyobaki (sawa na shilingi triliioni 9.82) ilikuwa ni hewa na kwa maana hiyo haikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Sababu ya pili, ni kutotekeleza kikamilifu bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika sekta mbalimbali. Nitatoa mifano katika wizara tatu zinazogusa maisha ya watu wengi moja kwa moja kwa miaka miwili (2016/17 na 2017/18):-

i. Wizara ya Kilimo:-

§ Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Kilimo iliyodhinishwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 100.527 lakini hadi Machi, 2017 zilitolewa shilingi bilioni 2.252 sawa na asilimia 2.22 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hii ina maana kwamba takribani asilimia 98 ya bajeti hiyo haikutekelezwa.

§ Katika mwaka wa fedha 2017/18; wizara hii iliidhinishiwa na Bunge fedha za maendeleo jumla ya shilingi bilioni 150.253 (150,253,000,000/-) lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2018; ni shilingi bilioni 16.5 tu (16,520,540,444/-) zilikuwa zimetolewa ikiwa ni sawa na asilimia 11 tu ya fedha za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa. Hii ina maana kwamba asilimia 89 ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya kilimo haikutekelezwa.

ii. Wizara ya Mifugo na Uvuvi:

§ Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliidhinishiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 4 lakini zilizotolewa ni shilingi milioni 130 tu sawa na asilimia 3.25 ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Hii ina maana kwamba,takribani asilimia 97 ya bajeti hiyo, haikutekelezwa.

§ kwa mwaka wa fedha 2017/18 Wizara hii iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 4 (**4,000,000,000/=**) kama fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya mifugo na uvuvi; lakini hadi kufikia mwezi machi, 2018 hakuna hata shilingi moja ambayo ilikuwa imepokelewa kutoka hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika sekta hizo. Hii ina maana pia kwamba asilimia 100 ya bajeti ya maendeleo katika sekta za mifugo na uvuvi haikutekelezwa kwa kipindi hicho.

iii. Wizara ya Maji

§ Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliidhinishiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 913.836 lakini zilizotolewa zilikuwa ni bilioni shilingi 230.997 sawa na asilimia 25 ya fedha iliyoidhinishwa. Hii ina maana kwamba, asilimia 75 ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya maji kwa mwaka huo haikutekelezwa.

§ Kwa mwaka wa fedha 2017/18, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 623.606 lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2018, fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 135.191 sawa na asilimia 22 ya fedha zilizoidhinishwa. Hii ina maana pia kwamba asilimia 78 ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya maji haikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Sababu ya tatu inayoifanya Bajeti ya Serikali ishindwe kutekelezwa ipasavyo ni Utovu wa Nidhamu ya Matumizi ya Fedha kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Sheria ya Fedha.Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kifungu cha 41(1) ni kwamba; Ikiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazikutosha kutekeleza majukumu ya Serikali “*Serikali itatakiwa kuwasilisha Bungeni kwa idhini, bajeti ya nyongeza ya fedha zillzotumika ambazo zimezidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge au kwa madhumuni ya kugharamia mahitaji ambayo hayakupangwa*”. Aidha, utaratibu huu unatiliwa nguvu na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001(Public Finacne Act, 2001)ambapo kifungu cha 18 (3) na (4) kinaitaka Serikali kuleta Bungeni bajeti ya nyongeza (mini-budget) kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha zilizoidhinishwa awali hazikutosha.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo wa kisheria umekuwa ukivunjwa na Serikali kwa kufanya matumizi ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge jambo ambalo linaua dhana ya madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali; lakini pia kunatoa mwanya wa wizi na ubadhirifu wa fedha za umma. Ikiwa matumizi yanafanyika nje ya bajeti; bajeti ya namna hiyo haina uhalali kuwa haina baraka za Bunge.

Mheshimiwa Spika, upotevu wa fedha wa shilingi triliuni 1.5 uliobainika na CAG yamkini unatokana na matumizi ya fedha kiholela yanayofanywa na Serikali bila kuidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi ya mtumizi ya Serikali yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyodhinishwa na Bunge. Mifano hiyo ni pamoja na:-

§ Ujenzi wa Ukuta kwenye machimbo ya Tanzanite – Mirerani

§ Ujenzi wa Hosteli za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

§ Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege – Chato

§ Kuhamishia Makao Makuu Dodoma bila bajeti ya kufanya hivyo zoezi hilo kutumia fedha nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, utovu wa nidhamu ya matumizi yay a fedha zilizoidhinishwa na Bunge umekwenda mbali zaidi kwa kuzipatia baadhi ya wizara nyongeza ya fedha katika bajeti zake tofauti na zile zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Taarifa ya Serikali kwenye Kamati ya Bajeti ya Bunge kuhusu matumizi ya serikali kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 na mwelekeo hadi Juni 2018 inaonyesha kwamba baadhi ya wizara zilipatiwa fedha zaidi ya bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

- i. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambapo bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, ilikuwa ni shilingi 4,616,070,000; lakini kiasi kilicholipwa hadi kufikia Machi 2018 ni shilingi 8,880,870,019 sawa na **(257%)**
- ii. Tume ya Uchaguzi:- bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 2,470,031,000. Kiasi kilicholipwa mpaka mwezi Machi 2018 kilikuwa ni shilingi 6,031,856,200 sawa na **(326%)**
- iii. Ofisi ya Rais (TAMISEMI), bajeti iliyidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 8,212,296,000. Kiasi kilicholipwa mpaka mwezi Machi 2018, kilikuwa shilingi 17,122,775.005 sawa na **(278%)**
- iv. Wizara ya Mambo ya ndani: - Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 4,405,897,000; lakini kiasi kilicholipwa mpaka mwezi Machi 2018 kilikuwa ni shilingi 11,318,896,430 sawa na **(343%)**
- v. Ofisi ya Makamu wa Rais:-Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi 2,879,167,000; lakini kiasi kilicholipwa mpaka mwezi Machi 2018 ni shilingi 5,811,478,145 sawa na **(269%)**

Mheshimiwa Spika, Matumizi yote haya ambayo hayakujumuishwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa na Bunge yanaifanya Bajeti ya Serikali kutotekelezeka ipasavyo kwa kuwa fedha hizo za nyongeza kwa baadhi wizara nilizotaja yamkini zimetolewa kwenye miradi mingine na kwa maana hiyo miradi hiyo haikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nimetoa mifano hiyo michache lakini ukifanya uchambuzi wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kutekeleza miradi mbalimbali utakuta kwamba zaidi ya asilimia 60 ya fedha hizo hazikutolewa; na kwa maana hiyo miradi iliyokusudiwa kutekelezwa na fedha hizo haikutekelezwa. Kwa mantiki hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili; ni kwa nini inawahadaa wananchi kwa kutoa makisio makubwa ya bajeti ambayo kwa miaka mitatu mfululizo imekuwa ikishindwa kuyafikia? Aidha, ni kwani nini inashindwa kutekeleza bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na wakati huo huo inafanya matumizi ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge kutekeleza shughuli ambazo hazipo katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo?

9. MWENENDO WA HALI YA UCHUMI WA TAIFA

9.1. Deni la Taifa

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishaeleza kuwa mionganini mwa majukumu msingi ya Wizara ya fedha ni pamoja na jukumu la kusimamia deni la Taifa. Hata hivyo, deni hili limeendelea kuwa kubwa kila mwaka jambo ambalo limekuwa na athari kubwa katika bajeti ya Serikali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hivyo kuathiri uchumi wetu na maisha ya wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania kuhusu tathmini ya nusu mwaka ya mwenendo wa uchumi (Mid-Year Review) katika mwaka wa fedha 2017/18 iliyotolewa mwezi Februari, 2018 ni kwamba; deni la taifa liliongezeka kwa dola za kimarekani milioni 1,054.6 (sawa na shilingi triliioni 2, bilioni 320 na milioni 120)⁹ kutoka dola za kimarekani milioni 19,957.6 (sawa na shilingi **triliioni 43 , bilioni 906 na milioni 720**) mwezi **Juni 2016**; hadi kufikia dola za

⁹ Fedha ya kitanzania imekokotolewa kwa kutumia viwango vya kubadilisha fedha (exchange rate) ya dola ya kimarekani kwa shilingi ya tanzania ambayo kwa sasa ni shilingi 2,200 kwa dola moja ya Marekani.

kimarekani milioni 21,012.2 (sawa na shilingi **triliuni 46 , bilioni 226 na milioni 840**) **mwisho wa mwezi Desemba, 2017.** Deni hilo linajumuisha deni Serikali la nje na deni la sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo; Deni la ndani liliongezeka kwa asilimia 8.6 na kufikia shilingi 12,810,300,000,000/= (**triliuni 12, bilioni 810, na milioni 300**). Kwa hiyo, ukijumlisha deni la nje na la ndani utapata jumla ya deni la taifa kuwa ni **shilingi 59,037,140,000,000/= (triliuni 59, bilioni 37, na milioni 140)**

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayoelezwa ya kuongezeka kwa deni ni mikopo mipya pamoja na mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha (exchange rate fluctuations). Katika nusu ya kwanza ya mzunguko wa bajeti ya 2017/18, Serikali ilikopa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 556.0 (sawa na shilingi triliuni 1, bilioni 223, na milioni 200) ambapo kati ya fedha hizo dola za kimarekani milioni 471.1 (sawa na shilingi triliuni 1, bilioni 36 na milioni 420) zilipokelewa kama fedha taslimu na kiasi kilichobakia cha dola za kimarekani milioni 84.9 (sawa na shilingi bilioni 186 na milioni 780) zilingia kwa mfumo wa ugharamiaji wa moja kwa moja wa miradi ya maendeleo (direct project financing)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho hicho cha nusu ya kwanza ya mzunguko wa bajeti ya 2017/18; Serikali ililipa kiasi cha dola za kimarekani milioni 453.7 (sawa na shilingi bilioni 998 na milioni 140) kama marejesho ya mkopo wa nje. Kati ya fedha hizo, dola za kimarekani milioni 315.2 (sawa na shilingi bilioni 693 na milioni 440) zilikuwa ni marejesho ya deni msingi (principal repayments) na kiasi kilichobakia cha dola za kimarekani milioni 138.5 (sawa na shilingi bilioni 304 na milioni 700) kilikuwa ni malipo ya riba (interest payments).

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kulazimika kulipa riba ya shilingi bilioni 304 na milioni 700 ni matokeo ya kiburi cha Serikali hii ya CCM cha kutotaka kupokea na kuufanya kazi ushauri wa muda mrefu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa kutochukua mikopo yenye masharti ya kibiashara. Fedha

hii tunayolipa kamariba ni fedha ambayo ingetumika kugharamia huduma za jamii kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maangalizo yote ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiipatia Serikali hii kuhusu kupunguza kwa kadri iwezekanavyo au kuacha kabisa kuchukua mikopo yenye masharti ya kibiashara; safari hii Serikali imepanga kukopa jumla ya shilingi triliioni 8 bilioni 904, na milioni 727¹⁰ katika mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, ukiangalia sura ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19 utaona kwamba Serikali imetenga shilingi **triliioni 10, bilioni 4, na milioni 840** kwa ajili ya kulipa deni la taifa.

Mheshimiwa Spika, hatua tuliyofikia ya kukopa shilingi triliioni 8 yenye masharti ya kibiashara na kulipa madeni kwa shilinigi triliioni 10 ni mbaya sana. Hii haina tofauti na kuwa kwenye mzunguko wa madeni yasiyoisha (vicious cycle of debts). Tukishakubali kuwa katika mzunguko wa madeni maana yake tuko katika mzunguko wa umasikini pia (viscious cycle of poverty).

Mheshimiwa Spika, mikopo ya masharti nafuu ambayo Serikali inatarajia kukopa kwa mawaka wa fedha 2018/19 ni jumla ya shilingi triliioni 2.676. Hiki ni kiasi kidogo na kimeendelea kushuka mwaka hadi mwaka. Tafsiri ya kushuka kwa mikopo yenye masharti nafuu ni kwamba nchi yetu haikidhi vigezo vyta kupatiwa mikopo ya masharti nafuu. Na hii ni kwa sababu deni la taifa halijafanyiwa uhakiki (credit rating) ili kujiridhisha Serikali inakopesheka kwa kiwango gani. Kwa sababu hiyo; mashirika mengi ya fedha duniani yamejitoa kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa nchi yetu kwa kuwa hakuna uhakika kama mikopo hiyo itaweza kurejeshwa. Matokeo ya jambo hilo, Serikali imekosa namna nytingine ya kumudu gharama za kuendesha nchi, badala yake imekimbilia kwenye mikopo ya masharti ya kibiashara jambo ambalo linaendelea kudidimiza uchumi wan chi.

¹⁰ Tazama Jedwali la Sura ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kwamba kukua kwa deni la Taifa kunaisababishia serikali kuendelea kuwa tegemezi na hivyo kushindwa kutatua kero za klichumi za wananchi. Jambo la kusikitisha ni kwamba pamoja na ukweli huo, serikali imeendelea kukopa mikopo mikubwa yenyé masharti ya kibashara hali ambayo inazidi kufanya hali ya maisha kwa wananchi yaendelee kuwa ngumu kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi kulipa madeni hayo badala ya kuzitumia fedha hizo kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishatoa rai kwa Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum (Special Audit) katika kitengo cha deni la Taifa (Fungu 22) ili tuweze kujua mikopo tunayoichukua kila mwaka inatumika kufanya nini, atoe taarifa ya miradi iliyotekelizwa kutokana na mikopo hiyo kama ni ya miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa mpango wa Taifa wa Maendeleo. Halikadhalika ukaguzi huu maalum utatuwezesha kama Taifa kujua kiwango halisi cha deni la Taifa ambalo tunadaiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilishatoa ushauri kwa Serikali hii kutenganisha deni halisi la Taifa na matumizi mengineyo yanayohusu Mfuko Mkuu wa Hazina ili kuziba mianya ya ubadhirifu au matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kisingizio cha Deni la Taifa. Katika muktadha huo huo, ili kudhibiti Serikali kukopa mikopo mikubwa yenyé masharti ya kibashara, ambayo hatimaye yanaliingiza taifa kwenye mzigo wa madeni; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza pia kwamba; Kabla Serikali hajia kopa; ilete pendekezo la mkopo huo Bungeni pamoja na orodha ya miradi itakayotekelizwa kwa kutumia mkopo huo ili Bunge liidhinishe. Pendekezo hili lilizingatia msingi kwamba Bunge ndicho chombo cha uwakilishi wa wananchi, na kwa kuwa mikopo hii inakuja kulipwa na wananchi kupitia kodi zao, ni vema wananchi wakashirikishwa kupitia wawakilishi wao juu ya mikopo ambayo Serikali inachukua kwa niaba ya wananchi.

§ **Takwimu Kengeufu za Deni la Taifa**

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017, inaonyesha kwamba kiwango cha deni la taifa kimeshushwa kwa kiasi cha **shilingi 4, 588,390,000,000/= (trilioni 4, bilioni 588, na milioni 390)**

Mheshimiwa Spika, CAG anasema kwamba, mapitio yake ya deni la taifa yalibaini kwamba kiwango cha deni la taifa kilifiki **shilingi 46,081,430,000,000/= (trilioni 46, bilioni 81 na milioni 430)** kufikia Juni, 2017; lakini kiwango hicho hakikujumuisha madeni ya **shilingi bilioni 4,588,390,000,000/=**, ikiwa ni madeni ya mifuko ya pensheni kiasi cha **shilingi 4,421,750,000,000¹¹ na shilingi 166,640,000,000/=** ikiwa ni dhamana zilizokiukwa masharti chini ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, ukichukua kiwango cha deni la taifa kilichoshushwa **chashilingi 4, 588,390,000,000/=**; ukajumlisha na kiwango cha jumla ya deni la taifa cha **shilingi 59,037,140,000,000/=** kilichotolewa na BOT, utakuta kwamba jumla ya deni la Taifa ni **shilingi 63,625,530,000,000/= (trilioni 63, bilioni 625, na milioni 530)**.

Mheshimiwa Spika, ukirejea hotuba ya Waziri Mkuu aliyoitoa hapa Bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi katika Ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2018/19; tarehe 4 Aprili, 2018; alisema kuwa deni la Taifa hadi kufikia

¹¹ Kwa mujibu wa Taarifa ya CAG kuhusu Ukaguzi wa Fedha za Serikali Kuu ya Machi, 2018; Shilingi 4,421,750,000,000/= ni sawa na asilimia 4.14 ya Pato la Taifa ambalo kwa sasa ni shilingi 106,867,000,000,000/= (trilioni 106 na bilioni 867).

Desemba, 2017 ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 25,419.6¹². Ukibadili dola hizi kuwa shilingi za Tanzania kwa 'exchange rate' ya shilingi 2,200/= kwa dola moja ya Marekani utapata jumla ya **shilingi 55,923, 120,000,000/= (trilioni 55, bilioni 923, na milioni 120).**

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki cha deni la taifa cha takriban shilingi trilioni 63 ni sawa na asilimia 59.43 ya Pato la Taifa ambalo kwa sasa ni shilingi trilioni 106.867 kwa mujibu wa taarifa ya CAG.

Mheshimiwa Spika, kuna mkanganyiko kuhusu uhimilivu wa deni la taifa dhidi ya pato la taifa. Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Fedha ni kwamba pato la taifa kwa sasa ni shilingi trilioni 50.5 Na kwa mujibu wa hotuba hiyo; uhimilivu wa deni kwa sasa ni asilimia 34 ya pato la taifa wakati ukomo wa uhimilivu ni asilimia 56 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia takwimu za uchambuzi wa deni la taifa uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni – ambapo deni la taifa limefikia shilingi trilioni 63; ni kwamba deni la taifa si himillivu tena. Takwimu zinazotolewa na Serikali haziwezi kuaminika tena kwa kuwa Serikali hiyo hiyo ina takwimu tofauti kuhusu deni la taifa; na pia kuhusu pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa fedha, anasema kuwa pato la taifa ni shilingi trilioni 50.5; taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge inaonyesha kuwa pato la taifa ni shilingi trilioni 86. Wakati huo huo, CAG anasema kuwa pato la taifa kwa sasa ni shilingi trilioni 106. Katika Mazingira hayo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapata mashaka juu usahihi wa deni la taifa na pia pato la Taifa.

¹² Tazama Hotuba ya Waziri Mkuu akiwasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi katika Ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2018/19 uk.9 aya ya 16.

Mheshimiwa Spika; pamoja na ukengeufu huo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashukuru kwa Serikali kujumbua yenyewe kwamba deni la taifa si himilivu tena kwa kutumia kigezo cha deni dhidi ya pato la taifa. Hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusu hali ya uchumi ukurasa wa 9 aya ya 16 inasema kwamba; "Pato halisi la taifa kwa mwaka 2017, liliifikia shilingi milioni 50,525,087 (trilioni 50.5). Kwa hiyo, ukilinganisha na deni la taifa ambalo kwa sasa ni shilingi trillioni 63 ni wazi kwamba nchi iko rehani.

Mheshimiwa Spika, kuwa deni la taifa limefikia zaidi ya nusu ya pato la taifa; na ukomo wa kukopa ni asilimia 50 ya pato la Taifa ambayo tumeshaivuka kwa mujibu wa takwimu alizotoa Waziri Mkuu. Hivyo kuendelea kusema kuwa deni ni himilivu ni kujivika kilemba cha ukoka, na kujitoa ufahamu, mambo ambayo hayakubaliki katika kanuni za uchumi. Kwa sababu hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalisihi Bunge kuazimia kuunda Kamati Teule kuchunguza uhalisia wa deni la Taifa na Pato la Taifa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kushikilia msimamo wake wa kuitaka Serikali kupitia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya uchunguzi maalumu (Special Audit) ya mwenendo wa deni la taifa na kushauri hatua za kuchukua ili taifa liepukane na athari za deni hilo katika uchumi wan chi.

Mheshimiwa Spika, Ujasiri wa kusema deni letu ni himilivu, lazima uendane sambamba na uwezo wetu wa kiuchumi wa kukusanya KODI. Deni linaweza kuwa himilivu kama uwezo wa nchi kukusanya kodi unafikia japo 36% ya Pato la Taifa. Kwa mantiki hiyo,kwa pato letu la Taifa la shilingi Trillion 125, tulitakiwa kwa mwaka tuwe tunakusanya kodi isiyopungua shilingi Trillion 45 kwa mwaka. Kwa makusanyo haya tutakuwa na uwezo wa kulipa deni ,mishahara kwa watumishi wetu na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa hali ilivyo sasa uwezo wetu wa kukusanya ni 14% tu ya pato la Taifa. Taarifa ya Wizara ya Fedha kwa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti inaonyesha kwamba Kati ya shilingi Trillion 17.3 zilizopangwa kukusanya na TRA katika mwaka wa fedha 2017/18. Mpaka Mwezi Machi 2018 kiasi kilichokusanya ni shilingi trillion 10.7 tu. Kwa "makusanyo ya Trillion 1.3 kwa

mwezi kama tunavyoambiwa na TRA" inatarajiwa mpaka mwaka wa fedha unaisha makusanyo ya Kodi yatafikia shilingi Trillion 14tu!

Mheshimiwa Spika, Kutohana nauwezo mdogo wa kukusanya mapato unaokwenda sambamba na **mzigo mkubwa** wa deni la Taifa. Utekelezaji wa Bajeti unadhihirisha hilo kwani $\frac{3}{4}$ ya fedha inayokusanywa inakwenda kwenye kulipa deni la Taifa na Mishahara kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, Kwa uchambuzi huu utaona kwamba kuna tofauti ya takwimu za deni la taifa zilizotolewa na Benki Kuu; zilizokaguliwa na CAG na zilizotolewa na Waziri Mkuu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni takwimu zipi sahihi kati ya hizo?

Mheshimiwa Spika, ukengeufu huu wa takwimu unatokana na udhaifu uliopo katika mfumo mzima wa usimamizi wa deni la taifa. Mfumo huo, umepitwa na wakati. Mkakati wa Taifa wa Madeni (NDS) wa mwaka 2002 uliandaliwa kwa mazingira ya sheria ya Mikopo ya serikali , Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 (Miaka 43 iliyopita). Hali ya uchumi na mazingira ya kuanzishwa kwa sheria na mkakati wa NDS yamebadilika mno kutohana na mabadiliko ya kiuchumi ambayo yametokea.

Mheshimiwa Spika, Kutohana na kupanuka kwa wigo wa deni la Taifa katika suala la vipengele na mikopo mikubwa ambayo imefanyika, sheria na miongozo inayosimamia deni la Taifa haiko sambamba na maendeleo hayo na vyombo vinavyotumika vimepitwa na wakati na kwa sababu hiyo kufanya usimamizi wa deni la taifa kuwa changamoto.

Mheshimiwa Spika, Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali anabainisha ¹³ katika ripoti yake ya Machi, 2017 kwamba: **mfumo uliopo sasa unaongeza uzembe katika uendeshaji**,

¹³Ripoti kuu ya mwaka ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali, kuhusu taarifa za fedha za Taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka unaoishia Tarehe 30 Juni ,2016. Machi 2017, uk.76

uratibu duni na kutokuwa na taarifa za kutosha katika vitengo na taarifa sahihi kupitia taasisi na kusababisha kuwa na rekodi zisizosahihi na zisizojitosheleza kuhusiana na deni. Alishauri mfumo mzima wa usimamizi wa deni la taifa ufanyiwe maboresho (reform); ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi yaliyopo sasa; na hivyo kuweza kuwa na usimamizi mzuri (management) ya deni la taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza; maboresho hayo yaliyopendekezwa na CAG yalishafanyika?

9.2. Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwamba Pato la Taifa kwa kutumia kizio cha 2015 kwa mwaka 2017 lilikuwa ni shilingi milioni 125,624,406 na pato la taifa kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2018 lilikuwa kwa asilimia 8.4 sawa na shilingi milioni 136,176,856.1. Shughuli za kiuchumi zilizochangia ukuaji huo ni; Ujenzi 28.2%; Kilimo(mazao,mifugo,uvuvi na misitu) 23.1%; utawala na ulinzi 7.4% na usafirishaji na uhifadhi mizigo 7.3%. Lakini katika kipindi hicho shughulizi za kiuchumi zilizokua kwa kasi kubwa ni ujenzi 20% habari na mawasiliano 18.3%, utawala na ulinzi 15.5%, Kilimo 7.1%. Wakati huo huo shughuli za kiuchumi zenye mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika ni Kilimo 31.4% na Ujenzi 13.9%

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa uwekezaji kwenye sekta husika una uhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa sekta husika, lakini mchango wa sekta kwenye pato la Taifa una uhusiano wa moja kwa moja na idadi ya watu wanaojihusisha na sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi inaonesha kuwa sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli binafsi 22.8%; shughuli za biashara 20.5%; shughuli za **uzalishaji viwandani 11.1% na kilimo 6.9%**. Hii maana yake ni kuwa Tanzania haiwezi kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati kutoptera na ukweli kuwa uwekezaji unaofanyika kwenye maeneo muhimu ya kutupeleka kwenye uchumi huo hawapewi kipaumbele cha

uwekezaji. Rejea Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 Uki.8

9.3. Mwenendo wa Bei Nchini

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mpango aya ya 2.2.3.3 unaonesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2018 mwenendo wa mfumuko wa bei umebakia katika wigo wa tarakimu moja. Katika mwezi Januari ulikuwa silimia 4.0, Juni 3.4% na Agosti 3.3%. Wakati huo bei za vyakula mfumuko ulipungua kutoka 6.7% hadi 3.2%. Aidha kwa upande wa bei za nishati uliongezeka kutoka 10.4% hadi 18.7% kutoptana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ufanuzi ni kwa vipi bei za mafuta zinapanda wakati huo huo bei za vyakula zinashuka. Kwa kawaida vyakula vingi vinazalishwa maeneo ya vijijini, na inalazimu kuingia ghamama za usafirishaji hadi sokoni. Kwa kutumia "Marketing equation" za kupanga bei kwenye soko, jambo hili la mafuta yako juu sana na bei za bidhaa zinazoletwa sokoni ziko chini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa kuwa Serikali inaficha ukweli kwamba uwezo wa wananchi kufanya manunuzi umepungua sana (Purchasing power) kutoptana na ukweli kuwa Serikali iliondoa fedha kwenye mzunguko, na pia fedha nyingi zinatolewa kwa makampuni ya nje yanayojenga, na pia athari za vyeti feki kwa wananchi pamoja na makampuni kupunguza wafanyakazi na hivyo kupelekea mzunguko wa fedha kuwa haba. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kutoa tamko kuhusu mzunguko mdogo wa fedha ambao umewafanya wananchi kushindwa kununua bidhaa na inachukua hatua gani kurudisha mzunguko wa fedha katika viwango vinavyokubalika.

9.4. Sekta ya Fedha

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa uchumi hauwezi kuimarika kama sekta ya fedha inashuka kiutendaji, Takwimu za mwenendo wa sekta ya benki kwenye Kitabu cha

Mapendekezo ya Mpango aya ya 2.2.3.6 (a) inaonesha ujazi wa fedha kwenye Mabenki umeongezeka kwa wastani wa asilimia 7.0 na kufikia shilingi bilioni 25.2945 mwaka 2017/18 kutokana na kuimarika kwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kuimarika kwa sekta binafsi na rasilimali za kigeni katika benki za Biashara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili halina uhalisia kwani katika kipindi husika imeshuhudiwa mabenki mengi yanafungwa na kupelekea wananchi kupoteza akiba zao, Mfano ni kufungwa kwa Benki ya Wanawake, Benki ya Twiga, na mabenki ya wananchi (Community banks) katika maeneo mbalimbali hapa nchi. Aidha, uimara wa sekta ya benki kwa kuwa na ukwasi wa kutosha ni kutokana na ukweli kwamba zinashindwa kutoa mikopo kwa kuogopa kutokea kwa mikopo isiyolipika na hivyo kupelekea kuweka masharti magumu sana kwa wakopajî.

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonesha kuwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umefikia asilimia 4 mwezi Juni 2018 ukilinganishwa na asilimia 1.3 mwezi Juni 2017. Sehemu kubwa ya mikopo ikiwa ni ya shughuli binafsi 22.8% (Shughuli zisizoza uzalishaji), na shughuli za uzalishaji viwandani na kilimo mikopo ilikuwa ni kwa 11.1% na 6.9% kwa mfuatano. Shughuli za biashara zilikuwa ni 20.5%, uhalisia hapa ndipo kwenye watu wengi sana lakini asilimia hiyo halendani na uhalisia wa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni kwamba bado sekta ya benki haijakuwa imara kuendesha uchumi wetu au hali halisi ya biashara ni ngumu kiasi kwamba benki zinashindwa kutoa mikopo kutokana na uwezekano wa kuongezeka kwa mikopo chechefu (NON PERFORMING LOANS) na hivyo kulazimika kuweka vigezo/masharti ya mikopo kuwa magumu kiasi kwamba wafanyabiashara kushindwa kuyatimiza, Katika Ukurasa wa 9 wa Kitabu cha Mwongozo wa Mpango, aya ya 2.2.3.6 (d) imeelezwa kuwa riba za mikopo zilongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 17.83 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilikia 16.61 mwaka 2016/17. Kwa mujibu

wa mwongozo ni kwamba ongezeko hilo lilitokana na tahadhari zilizochukuliwa na benki za biashara kudhibiti mikopo chechefu.

Mheshimiwa Spika, maneno tahadhari zilizochukuliwa na mabenki ya biashara katika kudhibiti mikopo chechefu hayamaanishi kitu kingine isipokuwa kuzidisha ukali wa masharti jambo ambalo linapunguza idadi ya wakopaji hasa wakopaji wapya wasiokuwa na dhamana za kuweza kuaminiwa na benki. (NEGATIVE IMPACT ON BORROWING)

9.5. Biashara ya Kimataifa

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2017/18 mauzo nje ya nchi yalikuwa dola za Kimarekani milioni 8,949.4 na mwaka 2016/17 ilikuwa dola za Kimarekani 8,701.7 wakati manunuzi yalikuwa dola za kimarekani milioni 10,157.6 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na dola za marekani milioni 9,701.1 mwaka 2016/17.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu zote zilizotolewa katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango aya ya 2.2.3.5(a) zinaonesha kuwa kuna uwiano hasi (NEGATIVE BALANCE OF PAYMENT) katika biashara ya kimataifa. Uchumi wetu umakua kwa mtindo gani kama hatuna fedha nyingi za kigeni katika biashara zetu za kimataifa? Tunajengaje uchumi unaokua kama tunaagiza sana bidhaa kutoka nje kuliko mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi?Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini ili kuwa imara katika kuwa na fedha za kigeni za ziada inatakiwa manunuzi ya bidhaa na teknolojia toka nje iwe kidogo kulinganisha na mauzo ya bidhaa na ujuzi nje ya nchi, jambo hili ni kinyume na takwimu za Serikali.

Mheshimiwa Spika,Kambi Rasmi ya Upinzani inawasiwasi na takwimu zilizotolewa za kuwa tuna akiba ya fedha za kigeni zipatazo dola za kimarekani milioni 5,483.9 hadi Juni 2018 kama zilivytotolewa na Serikali, na kipindi kama hicho mwaka 2017 zilikuwa ni dola milioni 5,000.4

9.6. Uchumi wa gesi – Tanzania

Mheshimiwa Spika, kugunduliwa kwa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara kilitajwa kwamba ni ukombozi wa uchumi kwa watanzania lakini zaidi sana kwa wakazi wa Lindi na Mtwara. Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali ya tarehe 16 Mei, 2013 kwa Umma kuhusu Faida ya Gesi Asilia kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara imeainisha faida nyingi sana kwa wakazi wa mikoa hiyo ikiwemo ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea na Kiwanda cha Kuchakata gesi(LNG) katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa mkoa wa Lindi kuna Kampuni za Maurel and Prom na Kampuni ya Statoil, aidha kwa mkoa wa Mtwara kulikuwa na Kampuni za Wentworth Resources, Dominion na Kampuni ya Orphir East Africa Ventures Ltd. Hizo zilikuwa ni Kampuni zinazohusika na Gesi Asilia, pia uwekezaji wa Karakana ya Kiufundi wa Kampuni ya Schlumberger ambayo hutoa huduma kwa Kampuni za utafutaji mafuta na gesi kwa nchi za Msumbiji, Kenya, Uganda na Afrika ya Kusini.Ujenzi wa mitambo ya kusafishia gesi yenye uwezo wa kusafisha gesi futi za ujazo milioni 210 kwa siku katika kijiji cha Madimba Mtwara Vijijini na futi za ujazo milioni 140 kwa siku Kijiji cha Songo songo Mkao wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa Status Report ya Kampuni ni Kampuni ngapi za uchimbaji na uchakataji wa gesi ambazo bado zipo na zinaendelea na uwekekazaji katika Sekta ya gesi, na miradi ambayo imeshatekelezwa kutokana na upatikanaji wa gesi ikiwa ni pamoa na viwanda vya mbolea nk.

9.7. Benki ya Uwekezaji Tanzania -(TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viwanda kwa kiwango kikubwa kinategemea kwa kiwango kikubwa utendaji wa benki yetu ya uwekezaji katika kutoa mikopo ya muda mrefu tofauti na mikopo ya kibashara ambayo inatolewa na mabenki ya b Bashara ambayo muda wake wa kuanza kurejesha mkopo ni muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu za benki hiyo zinaonesha kuwa Benki inadai (mikopo chechefu) kiasi cha shilingi 230,669,526,932.24 yenye dhamana zenyе thamani ya shilingi 550,832,170,833 na hivyo kuifanya benki hiyo kuwa na mikopo chechefu ya 35% kwa Decemba 2016 (2015: 14%) ikiwa ni ongezekola kama 150%. Kiwango hiki ni kikubwa sana kulinganisha na kiwango kilichotolewa na BOT kuwa mikopo chechefu cha 24% kwa Benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Benki ilikuwa iliua "bonds" za chini ya mwezi mmoja ni shilingi bilioni 199 ambazo zilitakiwa zilipwe ndani ya mwezi mmoja hadi mitatu za thamani ya shilingi bilioni 124.6; miezi 4-6 shilingi 27.6 bilioni; na miezi 6-12 shilingi 49.2 na zaidi ya mwaka mmoja shilingi 41.9 bilioni; lakini Benki ilishindwa kutimiza matwaka au makubaliano na wakopeshaji. Na hivyo benki inadaiwa na wateja wake hao. (*Rejea Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge tarehe 19/10/2017- Ofisi ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali*)

Mheshimiwa Spika, Benki hii ya uwekezaji ni muhimu ifanyiwe mkakati wa kuona ni namna gani taweza kulipa madeni hayo ambayo yanaikabili. Kwa kuangalia mikopo chechefu na mikopo ambayo benki imeshindwa kuwalipa wateja wake ni dhahiri kwamba Benki ya uwekezaji iko mbioni kufilisika kama ambavyo mabenki mengine yamefilisika.

Mheshimiwa Spika, kuyumba kwa benki ya uwekezaji ni dalili kuwa Tanzania kufikia kwenye azma ya kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati kwa mwaka 2025 ni ndoto za mchana ambazo mara zote hazina uhalisia.

9.8. Ajira Kutokana na Viwanda Vitumiavyo Gesi Asilia

Mheshimiwa Spika, Serikali iliwaahidi wananchi ajira nyingi kutokana na matokeo ya upatikanaji wa Gesi Asilia. Ajira hizo zimeainishwa katika jedwali hapo chini. Pamoja na ahadi hiyo nzuri kwa wananchi, uwekezaji katika sekta ya gesi una mwelekeo wa kususua jambo ambalo limefanya ajira zilizoahidiwa kuwa hewa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka

Serikali kulieleza Bunge hili, ni miradi mingapi imejengwa kutokana na upatikanaji wa Gesi Asilia, na miradi hiyo imetoa ajira kiasi gani kwa wananchi?

Na	Kiwanda	Ajira halisi	Ajira zinazohusiana	Jumla ya Ajira
1.	Dangote (Cement)	500	800	1,300
2.	Ammonia Processing Plant	400	1500	1,900
3.	Fertilizer Plant(Urea)	400	1600	2,000
4.	Methanol Processing Plant	500	1500	2,000
	Jumla	1,800	5,400	7,200

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini, 2013

10. MCHANGO WA SEKTA YA MAJI KATIKA UCHUMI

10.1. Uhakika wa Maji na Raslimali za Maji.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji iliyowasilisha Bungeni Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2018/2019, imeelezwa kuwa Tanzania bado ipo katika nafasi ya kwanza katika nchi za Afrika ya Mashariki kwa kuwa na kiwango cha mita za ujazo zipatato 1,800 kwa kila mtu kwa mwaka. Hata hivyo kiwango hiki ni pungufu ya kiwango cha mwaka 2012 kama ilivyoelezewa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na shughuli mbali mbali za kibinaadamu, ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya raslimali za maji, kiwango cha maji kinatarajawa kupungua kwa asilimia 30 ifikapo mwaka wa kilele cha Dira ya Taifa (Tanzania Development Vision) yaani mwaka 2025; na kufanya upatikanaji wa maji kwa wakazi wa nchi hii kushuka hadi kufikia kiwango cha mita za ujazo 1,400 kwa mtu kwa mwaka. Hali hii itaiweka Tanzania katika hali ya wasiwasi (Water Stress) kwani kiwango hicho kinaendelea kupungua siku hadi siku na kuwa chini ya upeo wa hali ya usalama wa maji (Water Security). Kulingana na vigezo vyta kimataifa, nchi

hufikia sifa ya kuitwa "a water stressed country", pale ambapo maji kwa ajili ya matumizi ya wakazi wake ni chini ya mita za ujazo 1,700.

Mheshimiwa Spika, iwapo, hatua za haraka na za kimkakati hazitachukuliwa, nchi yetu itapoteza sifa ya kuwa na maji ya uhakika na usalama wa maji utapotea. Hivyo basi, Tanzania inaweza kuingia katika kundi la nchi zenyе sifa ya 'uhaba wa maji' yaani "a water scarce country". Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua hatari ya kupungua kwa raslimali za maji na kukosekana kwa bayoanuai endelevu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inatoa tahadhari kwa Serikali, na Watanzania kwa ujumla juu ya uwezekano wa kutokuwa na raslimali za maji na kwa mantiki hiyo maji ya kutosha kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, kijamii na mazingira.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa raslimali za maji na maji yenye ni tishio kwa usalama na amani, kwani ni chanzo cha migogoro mionganoni mwa watumiaji wa maji. Vile vile bila ya kuwa uhakika wa maji, shughuli za kiuchumi kama vile viwanda, kilimo, mifugo, madini, utalii, usafirisaji wa majini; na, uzalishaji wa nishati zitadorora. Pamoja na hayo, uhaba wa raslimali wa maji unathiri upatikanaji wa maji ya kunywa na maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Ikumbukwe pia raslimali za maji ni muhimu kwa ajli mazingira na bayoanuai endelevu.

Mheshimiwa Spika, Uhaba wa maji unatishia uwepo wa wanyamapori, misitu, nyuki na hata viumbe hai vinavyoishi kwenye maji. Maeneo eovu ambayo ni muhimu kwa ajili ya mazalia ya viumbe hai na hifadhi ya raslimali za maji ikiwa pia ni maeneo ya hifadhi ya mafuriko yanaendelea kuharibika kwa sababu ya matumizi mabaya ya raslimali za maji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na Sera ya Maji ya Taifa (National Water Policy- Nawapo) 2002; sheria za maji na miongozo mbali mbali ya matumizi bora yaraslimali za maji, bado raslimali za zinaendelewa kuharibika kwa sababu ya matumizi holela ya raslimali hizo.

Mheshimiwa Spika, Matumizi yasiyostahili ya raslimali za maji ni pamoa na kuharibiwa ka vyanzo vya maji; miundo mbinu hafifu ya kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, hali inayosababisha upotevu mkubwa wa maji; uchafuzi wa vyanzo vya maji ikiwa ni pamoa na maziwa, mito na vyanzo vingine vya raslimaji za maji na maji; mifumo hafifu ya majitaka mijini hali inayopelekea kuwa na uchafuzi mkubwa wa vyanzo vya maji; ukataji wa miti na uharibifu wa uoto wa asili; ongezeko la watu kwa ujumla na kwa namna ya pekee ongezeko la watu na makazi mijini isiyolingana na upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu; na pia ongezeko la viwanda hususan vile visivyokidhi vigezo vya teknolojia salama (safer technology) vinavyosababisha si tu utumiaji wa maji usio wa tija; bali pia usiotumia teknolojia salama kwa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania bado hajajipanga vyema kupambana na upungufu wa raslimali za maji na maji; Kambi ya Upinzania Bungeni inakuja na sera mbadala ili kuokoa Taifa hili katika balaa la uhaba wa raslimali za maji na maji kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii na watu wake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali kuwa Tanzania imeridhia mikataba mbali mbali ya kimataifa kuhusu maendeleo endelevu hususan maendeleo ya raslimali za maji, kuanzia Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mar del Plata (Argentina, 1977); Mkutano wa Dublin 1992 ambapo Tanzania ilikubaliana na Makubaliano ya kimataifa juu ya misingi ya Maji na Maendeleo Endelevu na Ajenda 21 ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa uliofanyika Rio de Janeiro juu ya Mazingira na Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka kumbukumbu vizuri, Kambi ya Upinzania Bungeni inarejea misingi ya maendeleo ya raslimali za maji (principles of Integrated Water Resources Management) kama ifuatavyo:

- i. Maji ni raslimali yenye ukomo (finite), inayoweza kuathirika kiraishi. Maji ni muhimu kwa maendeleo ya jamii, uchumi na mazingira.

- ii. Uendelezaji na usimamizi wa raslimali za maji ufanyike kwa njia shirikishi kwa kushirikisha kikamilifu makundi mbali mbali katika jamii, hususan watumiaji wa maji; waandaaji wa mipango na wenyewe kutoa maamuzi.
- iii. Kwa kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia na nafasi ya kipekee ya wanawake katika utunzaji, usimamizii na matumizi ya maji; wanawake wanapaswa kushiriki kikamilifu katika maamuzi ya matumizi ya maji.
- iv. Ni lazima kutambua kuwa maji yana thamani kifedha na kiuchumi, hivyo maji yathaminishwe katika matumizi yake yote ikiwa ni pamoja na matumizi ya maji katika maendeleo endelevu ya bayoanuai na mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi hili ya kimataifa ya maendeleo endelevu ya raslimali za maji, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeweka kipaumbele na msisitzo mkubwa katika Kutunza na Kulinda raslimali za maji kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, walinzi na watunzaji wakuu wa raslimali za maji ni watumiaji wa maji wenyewe. Hivyo basi ni muhimu kuimarisha ugatuaji wa majukumu ya ulinzi na utunzaji wa maji kwa watumiaji wenyewe, na kuimarisha stadi ya ushirikishaji wa wadau na jamii katika Ofisi za Mabonde ya Maji; Taasisi za Kijamii katika vidakio vya Maji (Water Resources Sub-Catchment Forums), na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na ugatuaji huo wa majukumu, taasisi zote zenye mamlaka ya usimamizi wa raslimali za maji ni lazima ziwe na mfumo rasmi wa uwajibikaji, ili kuwezesha si tu ufuatiliaji na tathmini wenyewe vigezo bayana vya utekelezaji; bali pia kutoa motisha na pongezi kwa utekelezaji mzuri wa majukumu; na kuchukua hatua stahiki kwa watendaji na wadau wasiotekeliza majukumu waliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na wadau mbali mbali wanaofuatilia maendeleo ya raslimali za maji, usalama na uhakika wa maji, kupaaza sautijuu ya uhaba wa mifumo ya kuhifadhi maji. Changamoto hii inapunguza uwezo wa taifa wa kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya misimu na viwango vya mvua yanahitaji maandalizi imara ya mifumo ya kuitisha maji ya mafuriko, na pia mifumo ya kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi wakati wa vipindi virefu vya ukame.

Mheshimiwa Spika, Utunzaji, uendelezaji na usimamizi wa raslimali za maji ni jukumu la sekta zote kwani wote ni wahusika katika kazi za kuthibiti, kutumia, na kusimamia raslimali hizo. Kambi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuhimiza umuhimu wa uratibu wa wadau na shughuli zao zinazogusa matumizi ya raslimali za maji. Majukwaa ya uratibu na ushiriki wa wadau na jamii kwa ujumla yanahitaji fikra mpya na mbinu mbadala za utendaji wa kazi zao. Kwa msisitizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaweka mkazo kwa Serikali kuweka mfumo bora zaidi wa uratibu wa wadau, kwani ni moja ya takwa la kimfumo kama ilivyooneshwa hapo juu katika msingi wa pili wa Misingi ya Maendeleo ya Raslimali za Maji.

10.2. Maji na Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeazimia kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Lengo hili litafikiwa iwapo uzalishaji katika sekta za kiuchumi; na utoaji wa huduma utakidhi vigezo stahiki vya nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sekta zote za uazalishaji zinahitaji maji ya kutosha na yenye ubora. Tukianza na kilimo, inafahamika kuwa ndio sekta kuu ya uzalishaji nchini. Kilimo kinatoa mahitaji (livelihood) ya wananchi kwa zaidi ya asilimia 80% na kuchangia takriban robo (24%) ya pato la taifa. Mazao ya kilimo huiletea Tanzania angalau asilimia 30% ya mapato ya biashara ya nje; na kilimo kinatoa ajira kwa asilimia 75% ya nguvu kazi ya nchi; na kati yake asilimia 90 ya wanawake hujishughulisha na kilimo. Ikumbukwe kuwa sekta ya kilimo ni muhimu kwa usalama wa chakula ambapo kulingana na

takwimu rasmi za sekta ya kilimo za mwaka 2013; ilithibitishwa kuwa asilimia 75 ya mahitaji ya chakula yanatokana na shughuli za kilimo zinazofanyika nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo imeandaa mkakati kabambe miaka kumi, wa Kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi yaani " Strategic Climate Smart Agriculture Programme 2015-2025". Inatarajiwa kuwa kupitia mkakati na programu hii, kilimo cha umwagiliaji kitafanyika katika hekta zipatazo millioni 1.5 na kunufaisha kaya milioni 2.3 na kuongeza uzalishaji kwa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, azma hii ni njema sana kinadharia. Kambi ya Upinzani Bungeni inastaajabishwa na malengo haya na ingependa kujua je Wizara imetambua uwepo wa maji ya kutosha kwa mtiririko wa uhakika kwa ajili ya umwagiliaji zisizokatika ili shughuli za programmu hii zifanyike kwa ufanisi katika kipindi cha miaka saba ijayo na kufikia lengo linalotarajiwa?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inafuatilia kwa karibu mijadala mbali mbali kuhusu matumizi ya raslimali za maji kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na umeme/nishati, yaani " Water- Energy-Food neux". Kambi ya Upinzani Bungeni inauliza ni kwa kiwango gani sekta husika zimeoanisha vipaumbele vyao ili kuhakikisha raslimali za maji zinatumika kwa ufanisi ili kufikia malengo yao ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni imemptia taarifa mbali mbali zinazohuzu kilimo cha umwagiliaji nchini. Taarifa nydingi zinaonesha kuwepo kwa migogoro ya matumizi ya maji baina ya watumiaji waliopo katika nyanda za juu za vidakio vya maji na wale waliopo chini; vile vile upotevu mkubwa wa maji kutokana na miundombinu hafifu.

Mheshimiwa Spika, kupitia hotuba hii, Kambi ya Upinzani Bungeni inarejea mfano wa migogoro kati ya watumiaji wa raslimali za maji katika kidako cha Ruaha Mkuu ambapo matumizi ya maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika

msimu wa kiangazi huathiri si mazingira na wanyapori katika mbuga ya Ruaha, bali pia utalii na uzalishaji wa umeme kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Tungependa kujua Wizara ya Maji na zile nyingine zinazotumia raslimali za maji, zimejipanga vipi ili kuratibu si tu mipango yao, bali pia fedha kwa ajili ya uwekezaji wa pamoja ili kujenga na kuendeleza miundombinu na utunzaji wa vyanzo vya maji ili kujihakikishia usalama na uhakika wa maji katika vipindi na misimu yote ya uzalishaji?

Mheshimiwa Spika, Ni kwa namna gani vipaumbele vya upanuzi wa kilimo cha umwagiliaji katika sekta ya kilimo vinaoana na vipaumbele vya hifadhi na matumizi endelevu ya raslimali za maji kwa ajili ya kizazi kilichopo na vizazi vijavyo?

11. SERIKALI YA AWAMU YA TANO IMEUA MFUMO WA UGATUAJI WA MADARAKA KWA SERIKALI ZA MITAA

Mheshimiwa Spika, Ugatuvi wa madara ni sera ambayo ni upelekaji wa huduma na maamuzi kwa wananchi. Na Serikali imekuwa ikitekeleza mpango huo kwa miaka kadhaa iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli kwamba tafiti nyingi sana zimefanyika kuhusiana na faida za ugatuvi wa madaraka kutoka serikali kuu kwenda serikali za mitaa. Mbali ya tafiti zilizofanywa na taasisi zisizo za Kiserikali pia Serikali kwa kutumia washauri waelekezi wa ndani na nje wamefanyia kazi suala hili la ugatuvi wa madaraka kwa kiwango kikubwa sana na kuja na sera ya D by D, sambamba na program ya maboresho ya Serikali za mitaa ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, Moja ya lengo kuu la maboresho ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1998 kuhusiana na ugatuvi wa madaraka ilikuwa ni kuwa na mfumo huru wa kiutawala katika ngazi ya Serikali ya mitaa ambapo baraza la madiwani lilikasimiwa madaraka ya kusimamia sera na utoaji wa huduma, kusimamia watendaji katika ngazi zao.

Mheshimiwa Spika, Kwa mtazamo huo wa ugatuzi wa madaraka ilikuwa ni kujenga mfumo imara wa kiutawala ambao ungekuwa ni nguzo kuu ya kuimalisha utoaji wa huduma na utoaji wa maamuzi katika ngazi za Serikali za mitaa. Ukiwa na uwezo wa kutoa maamuzi maana yake una uhakika wa uendeshaji wa eneo husika bila ya kutegemea msaada wa aina yoyote kutoka ngazi yoyote ya utawala.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa **“Policy Paper on Local Government Reform 1998”** iliandaliwa na kuweka bayana umuhimu wa KUGATUA madaraka ya Serikali Kuu kwenda SERIKALI ZA MITAA (decentralization by devolution au kwa jina lake maarufu D by D).

Mheshimiwa Spika, Chini ya Sera hii, Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa (Local Government Reform Programme-LGRP) ilianzishwa kwa dhamira ya kuziimarisha Serikali za Mitaa ili kusukuma mbele utekelezaji wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini yaani Poverty Reduction Strategy na baadaye MKUKUTA, na vile vile kuhakikisha kuwa Halmshauri za Miji na Wilaya zinatoa huduma bora kwa wananchi wake hususan huduma za Afya, Maji, Elimu, na huduma za ughani n.k. (angalia mpango wa “LGRP Medium Term Plan and Budget July 2005 – June 2008” OR – TAMISEMI: Juni 2005)

Mheshimiwa Spika, Malengo maalum ya Programu hiyo yalikuwa ni:

- i. Kugatua madaraka ya Serikali kuu na kuyapeleka kwenye Serikali za Mitaa (LGAs) ili ziwe na madaraka kamili (to create more autonomous Local Government Authorities), kupitia “political decentralization
- ii. kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kupitia watumishi wa umma wanaowajibika kwa Serikali za Mitaa zenyewe (*“de-linking of local authority staff from the respective line-ministries, making them accountable to the LGA who will be their employer, fully responsible for all*

human resource management"- Administrative Decentralization)

iii. Kuziwezesha Halmashauri kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake na kuwa na mfumo wa mgawanyo wa mapato kati ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa (financial decentralization)

iv. Kwa umuhimu wa kipekee maboresha pia yalikuwa na dhamira kuu ya kubadilisha mfumo wa mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kutoka mfumo wa Serikali Kuu wa kuwa na "**control role**" na hivyo kuwa na wajibu wa kutunga sera na kuweka vigezo vya ubora wa huduma; na kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza sera kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia raslimali fedha na utaalamu ili ziweze kutoa huduma inayolingana na ubora uliowekwa na kukubalika.

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kuwa, Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ilitekelezwa sambamba na programmu nyingine za uboreshaji wa Sekta za Umma na Sekta Binafsi. Moja kati ya nyanja muhimu za uboreshaji wa Sekta ya Umma ni uboreshaji wa Utumishi wa Umma yaani Civil Service Reform Programme (CSRP 1998), ambayo baadaye iliboreshwa na kutengeneza programu maalum ya miaka kumi na mitano Public Service Reform Programme (2000 -2015) yenye malengo makuu yafuatayo:

i. Kuboresha utendaji

ii. Kuweka tabia ya kufuatilia, kupima na kutathmini utendaji katika utumishi wa umma na utoaji wa huduma za umma

iii. Kuweka mifumo ya kuinua kiwango cha ubora wa huduma (quality improvement cycles).

Mheshimiwa Spika, Maboresho hayo yalidhamiria kuimarisha utawala na utoaji huduma. mambo ambayo ni muhimu sana katika kuiondoa nchi yetu kwenye umasikini na pia kufikia vigezo vya mpango wa Maendeleo ya Millenia wa

kupunguza umasikini wa kipato na nchi yetu kuwa na uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, katika program ya maboresho ya Serikali za mitaa iliyochukua takriban miaka kumi kuanzia mwaka 1998 hadi 2008 ilikuwa inaenda sambamba na kuboresha sheria zinazohusika kuongeza vyanzo vya mapato kwa Serikali za mitaa kama ambavyo zilivyotungwa na Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kwa masikitiko makubwa ni kwamba uwekezaji wote huo uliofanywa na Serikali za awamu ya tatu na awamu ya nne umekuwa ni kazi bure, kwa vile katika uhalisia madaraka yamerudishwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya tano ambayo wananchi walikuwa na matumaini makubwa kwayo katika kugatua madaraka kwa lengo kukuza Demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi katika mipango yao ya maendeleo na utawala bora inafanya kinyume kabisa na matarajio ya wananchi.

12. UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO YA TAIFA

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 yamelenga kuzingatia vigezo vya mwenendo wa viashiria vya uchumi, ukusanyaji wa mapato ya serikali, upatikanaji wa michango ya washirika wa maendeleo na uwekezaji wa sekta binafsi.

12.1. Mwenendo wa viashiria vya uchumi

(a) Kasi ya ongezeko la ukuaji wa watu

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha mapendekezo ya mpango 2019/20 kimebainisha mambo kadhaa katika kuangalia viashiria vya uchumi ikiwemo ongezeko la idadi ya watu, umiliki wa mali za kudumu, upatikanaji wa chakula n.k

Mheshimiwa Spika, ifahamike kuwa ongezeko la watu sio kiashiria kibaya katika uchumi, ila kutokana na kwamba serikali imeshindwa kuendana na kasi ya ukuaji wa watu basi kiashiria hiki cha uchumi ni changamoto kubwa kwa serikali hii.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2012 baada ya sensa iliyofanyika nchini ambapo idadi ya watu nchini ilikadiriwa kuwa takribani milioni 44; idadi ya watu imekuwa ikikua kwa kasi ambapo mpaka sasa kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa katika mapendekezo ya mpango zinaonyesha kuwa mpaka mwezi Februari 2018, Tanzania Bara pekee ilikadiriwa kuwa na watu milioni 52.6.

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hii, ni ajabu sana kusikia viongozi wakubwa wa serikali wakitoa kauli za kebehi, mizaha na ambazo zina athari kubwa katika ukuaji wa uchumi kutokana na viongozi hao kuhamasisha watu kuzaliana huku wakijua wazi serikali haina uwezo wa kutoa huduma bora za afya, elimu na maji.¹⁴ Bado nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira kwa vijana ambao ndio wenyewe jukumu la kuongeza familia, bado wananchi wengi wanaishi katika lindi la umaskini na ujinga, elimu duni ya afya ya uzazi na ongezeko kubwa la watoto wenyewe utapiamlo na wale wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hii, tafsiri yake ni kuwa; serikali imeshindwa kuwa jawabu kwa wakulima, wafanyakazi na , wafanyabiashara. Kambi Rasmi ya upinzani inaitaka serikali kuhakikisha kasi ya ukuaji wa ongezeko la watu unaakisi kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuhakikisha huduma bora na za msingi zinawafikia wananchi ili ukuaji huo uwezo kuwa na tija kwa kuongeza nguvu kazi. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka viongozi wakuu wa nchi na wale waliopewa dhamana kupima kauli zao,na kuacha kutoa kauli ambazo kimsingi zinaweza kuleta athari kubwa katika uchumi wa nchi na kuongeza majanga kwenye jamii.

¹⁴<https://theworldnews.net/tz-news/rais-magufuli-awataka-watanzania-wasiogope-kuzaliana-nchi-yetu-imeanza-kuwa-ya-mfano>

(b) Viashiria vya Umaskini

Mheshimiwa Spika, Serikali imeorodhesha katika Mapendekezo ya Mpango mwenendo wa viashiria vya umaskini katika kaya. Katika Mapendekezo hayo, Serikali imebainisha kuwa umaskini unaonyesha kupungua ikiwa kaya inamili simu ya mkononi,friji,pikipiki,magari,redio, baiskeli na ardhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na serikali kuainisha viashiria hivi, inaonyesha wazi kama nchi bado hatujawa makini (serious) katika masuala ya misingi ya uchumi. Tukumbuke kwamba umiliki wa samani au mali kama simu, friji, baiskeli,redio *sio mali za kudumu* kama ilivyoadikwa kwenye mapendekezo ya mpango ukurusa wa 11. Ifahamike kuwa mara nyingi katika jamii zetu mali kama hizi huweza kutolewa na ndugu, rafiki au jirani kama zawadi, msaada na ni wachache sana wenye uwezo wa kununua mali hizi wenyewe hususani maeneo ya vijiji. Wakati mwingine hata utunzaji (maintenance) hutegemea misaada ya ndugu, jamaa au marafiki.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi zilizoendelea au zilizo serious na masuala ya kiuchumi zimejikita kupima viashiria vya umaskini kwa kuangalia masuala ya kupungua kwa vifo hususani vifo vya watoto (child mortality), upatikanaji wa chakula na lishe bora(nutrition), muda wa kuwepo masomoni na kuanza shule kuanzia elimu ya awali mpaka elimu ya juu (years of schooling and enrollment), pamoja na ubora wa maisha ikiwepo upatikanaji wa maji safi na salama, uhakikika wa nishati ya umeme,nishati ya kupikia, ardhi ,aina ya nyumba,na samani nydingine ndogondogo huja kama viashiria vya ziada15.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba ni aibu kubwa kwa nchi yetu kujikita katika kupima viashiria vya umaskini kwa vigezo ilivyovianisha lakini pia Kambi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mpango huu wa maendeleo na unawezaje kufanikiwa ikiwa hali ya kiuchumi ya wananchi inazidi kuwa duni katika uhalisia ikiwa bado idadi ya watoto wenye utapiamlo nchini ni kubwa, kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijiji, kuongezeka

kwa matukio ya mauaji ndani ya familia na huku idadi ya wanaume wanaotelekeza wake na watoto ikizidi kuongeza kwenye jamii na hii ikiwa ni moja ya ishara mbaya ya kiuchumi?

12.2. Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18 serikali ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi triliioni 31.6. Katika fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 11,432.7 zilitengwa kama fedha za maendeleo , ambapo mpaka mwezi June 2018 kiasi cha shilingi bilioni 6,543.2 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni asilimia 57 tu ya lengo.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi serikali imekuwa ikitoa fedha za maendeleo chini ya makadirio kama inavyoonekana kwa mwaka 2017/18. Hii imekuwa kama desturi ya serikali kushindwa kutoa fedha za maendeleo kwa ukamilifu. Mathalani kwa mwaka 2016/17 katika kitabu cha mpango wa maendeleo ya taifa uk 14, kinaonyesha kuwa serikali ilitenga bilioni 11,820.503 kwa ajili ya shughuli za maendeleo lakini kufikia februari 2017, ilitoa shilingi bilioni 3,975.4 tu ambapo kati ya hizo fedha za ndani zilikuwa ni 26.2 % na fedha za nje zilikuwa 7.37% tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo mapato ya halmashauri yameshuka kutoka shilingi bilioni 665.4 mwaka 2016/17 mpaka shilingi bilioni 345.7 Agosti, 2018. Kitendo cha serikali kujipambanua kuwa kina kasimu mamlaka ya ukusanyaji kodi kwa Mamlaka ya Mapato (TRA) ili kuongeza mapato huku ikijua kabisa TRA haina rasilimali watu wa kutosha katika kazi ya ukusanyaji mapato hususani maeneo ya vijijini na miji midogo .Vilevile, kumekuwepo na matamko mbalimbali ya wanasiasa ambayo kimsingi yameathiri ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri nyingi nchini hususani zile zinazotegemea tozo za mazao na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha serikali kupoka vyanzo vya mapato (own source) kutoka serikali za mitaa kwenda serikali kama ilivyo kwenye Sheria ya Fedha 2016/2017/, kodi ya

majengo n.k kimeathiri halmashauri nyingi nchini na hivyo zimeshindwa kuijendesha huku miradi mingi ya maendeleo ikikwama. Pamoja na hilo kuanzishwa kwa TARURA ambayo nayo imepoka tozo za vituo vya mabasi na maegesho ya magari binafsi imeathiri mapato mengi ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na serikali hii imezidi kujigamba kuwa imeongeza ukusanyaji wa mapato basi watuambie fedha hizo zimetokana na nini wakati hakuna vyanzo vypya vilivyobuniwa na serikali mpaka sasa? Kambi Rasmi inatambua kuwa, serikali imekuwa na tabia ya kupanga mipango mikubwa ya ukusanyaji fedha huku ikijua haina uwezo wa kuitekeleza mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kila mwaka bajeti ya serikali inaonyesha kupanda lakini upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa bajeti ya maendeleo umekuwa sio wa kuridhisha. Pamoja na sababu zilizoanishwa katika kitabu cha mpango wa maendeleo ya taifa 2017/18 ukurasa wa 14, Kambi ya Upinzani imeweza kubaini sababu zifuatazo ambazo zinaikwamisha serikali hii kushindwa kutekeleza bajeti ipasavyo:

1. Sheria na mifumo ya kodi sio rafiki kwa walipa kodi na hivyo hamshawishi mwananchi kulipa kodi kwa hiari au kuona ni jukumu na haki yake kimsingi kuchangia maendeleo ya taifa (willingness)
2. Serikali imeshindwa kupanua wigo wa walipa kodi. Mara nyingi imekuwa ikitusanya kodi kutoka kwa watu wale wale kwa kuweka viwango vikubwa vya kodi na hivyo kukatisha tamaa walipa kodi na kutengeneza mianya ya ukwepaji kodi
3. Mazingira ya biashara na uwekezaji nchini hayatabiriki na hivyo kusababisha wafanyabiashara wengi hasa wakubwa kuogopa kuleta mitaji au kuwekeza mitaji yao nchini.Hii ni pamoja na matamko ya viongozi wakubwa wa serikali yanayowakatisha tamaa wawekezaji na kurudisha nyuma jitihada za sekta binafsi katika kuchangia maendeleo ya nchi.

4. Ucheleweshaji wa utoaji fedha hasa za misaada , kutoaminika kupata mikopo kutoka mataifa ya nje na kukatisha misaada ya kifedha katika miradi ya maendeleo kunaweza sana kukachangiwa na mahusiano mabovu na mataifa ya nje, kutoheshimu mikataba ya kimataifa ikiwa ni pamoja na kutoheshimu baadhi ya haki za binadamu, kuminya uhuru wa wa habari n.k

5. Kupoka mamlaka ya ukusaji mapato kutoka serikali za mitaa (local government) kwenda serikali kuu imekuwa ni moja ya sababu kubwa kwa kuwa kwenye serikali za mitaa ndipo hasa miradi inapoibuliwa na vyanzo vya mapato huibuliwa huko.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua uhalisia wa makusanyo ya serikali badala ya kuweka makadirio makubwa ya mpango huku ikijua kabisa haina uwezo wa kutekeleza. Fedha za maendelo zinazotolewa zimekuwa chini ya kiwango kwa muda mrefu. Sera mbadala ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalenga katika kuhakikisha ugatuaji wa madaraka unalenga kupunguza mamlaka na majukumu ya serikali kuu na badala yake mamlaka yanapelekwa karibu na wananchi ili waweweze kujiletea maendeleo kwa ukaribu zaidi.

13. MPANGO WA MAENDELEO NA UKUAJI WA ELIMU YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo wa taifa mwaka 2017/18 serikali ilitenga takribani bilioni 1 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa vyuo vya ufundi katika mikoa mbalimbali. Jambo hili si geni kwa serikali kutenga fedha za ujenzi wa vyuo vya ufundi nchini. Hii ikiwa na maana kwamba dhamira ya serikali ni kuhakikisha kuwa tuna nguvu kazi kubwa ya vijana ambao wamepata ujuzi katika fani za ufundi.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya taifa 2019/20 uk 37 serikali imebainisha ina lengo la kusomesha kwa wingi wataalam katika fani na ujuzi adimu ikiwa ni kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la aibu sana kwa nchi yetu ambayo kila mwaka inazalisha wasomi na wajuzi katika fani mbalimbali lakini wajuzi hawa hawajaweza kukwamua nchi yetu katika hali duni ya kiuchumi, teknolojia na ubinifu. Pamoja na kuwa serikali yetu inazalisha wahandisi na wataalamu wengine wengi bado nchi yetu haijaweza kuwatumia ipasavyo katika kuvumbua na ugundua teknolojia yetu ambayo tunaweza kujivunia.

Mheshimiwa Spika, mathalani katika ujenzi wa barabara, madaraja, na hata majengo makubwa utawakuta raia wengi wa kigeni wakipewa kazi hizo huku wataalam wetu wengi wenye ujuzi hawana kazi. Katika ujenzi wa madaraja utawakuta wataalam wetu wengi wakiishia kufanya kazi za upimaji na kusuka nondo, wengi hawana ubunifu wa ziada na hawajatengenezewa mazingira mazuri ya kuwa wabunifu. Hata pale ambapo anatokea raia mwenye vipaji vyta ugunduzi wengi hawapewi ushirikiano ili kuwasaidia kufikia malengo yao. Hali kadhalika katika fani nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, moja ya tamko la kisera la serikali hii ni "ujenzi wa uchumi wa viwanda". Azma hii inashindwa kufanikiwa kwa kuwa tu nchi yetu bado haijawekeza vyta kutosha katika kuwatumia watalaamu wetu, sayansi, teknolojia na ubunifu. Kwa kiasi kikubwa tunategemea teknolojia kutoka nje na hatuonyeshi nia thabiti ya kuhakikisha tunawekeza katika ubunifu na uvumbuzi ili kuweza kupata teknolojia yetu. Nchi kama Singapore, Korea Kusini, Thailand na Malaysia wameweza sana kuwekeza nguvu katika nyanja ya teknolojia na ubunifu na hivyo kufanikiwa sana katika kunyanya maendeleo ya uchumi .

Mheshimiwa Spika, kilimo chetu kinaweza tu kufanikiwa endapo tutawekeza katika teknolojia. Tutaweza kufungamanisha uchumi wa viwanda na kilimo endapo tutapanua wigo wa tafiti, kupunguza urasimu na kuruhusu vijana wetu kuwa wabunifu kuanzia mashulenii, kukuza vipaji vyta wabunifu na kuwatambua katika fani mbalimbali. Katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2019/20-2021/22 umeainisha kuwa shughuli za Uzalishaji

viwandani zinatarajiwa kukua kwa asilimia 8.0 kwa mwaka 2018 lakini Kambi ya Upinzani inataka kujua shughuli hizo za uzalishaji viwandani zinawezaje kukuwa ikiwa serikali inashindwa kuwekeza ipasavyo katika teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, Sera Mbadala ya Kambi Rasmi ya Upinzani inalenga katika kuhakikisha inawekeza katika elimu ya ufundi, kujenga mazingira wezeshi ya ugunduzi na uvumbuzi kuanzia mashulenzi, kuwekeza katika tafiti na teknolojia katika nyanja zote ili kuwa na jamii inayoendana na mabadiliko ya utandawazi.

14. USAWA WA JINSIA KATIKA MPANGO WA BAJETI

Mheshimiwa Spika, JINSIA ni dhana inayoelezea tafsiri ya jamii kuhusu wajibu na haki za KE na ME katika jamii, tofauti na JINSI ambayo ni dhana inayoelezea tofauti za kimaumbile au kibaiolojia – yaani hali ya kuzaliwa mwanamke au mwanaume. Kwa kuwa jinsia inahusika zaidi na wajibu au shughuli wanazofanya wanaume au wanawake, basi kwa vyovypote vile shughuli hizo zitakuwa na uhusiano wa moja kwa moja au vinginevyo katika kujenga na kukuza uchumi wa taifa.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu linatambua umuhimu wa mchango wa jinsia zote mbili katika kulijenga taifa na ndio maana waasisi wa taifa letu walifiki kuweka picha au taswira ya mwanaume na mwanamke katika Nembo ya Taifa wakimaanisha kwamba taifa litajengwa na wanaume na wanawake katika kazi zao na nafasi zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ili wanaume na wanawake waweze kutekeleza jukumu hilo la kujenga taifa, ni lazima wapatiwe fursa sawa ili waweze kutumia maarifa yao na uwezo walio nao kutoa mchango wao katika ujenzi wa taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha hakuna ubaguzi wa kijinsia, ili watu wote waweze kupata fursa sawa za kushiriki katika shughuli za kiuchumi na hivyo kutoa

mchango wao katika ujenzi wa uchumi wa taifa. Miongoni wa hatua hizo ni pamoja na kuridhia mikataba ya kimataifa na kikanda inayohusu kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake ikiwemo:

- i. Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake (CEDAW 1979)
- ii. Maazimio ya Beijing
- iii. Ajenda ya Umoja wa Afrika Kuhusu Usawa wa Jinsia au Katika Mkakati wa AGENDA 2063
- iv. Itifaki ya Usawa wa Jinsia wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) (2007)
- v. Malengo Makuu ya Milenia na Sasa Malengo 17 Endelevu ya Dunia (SDGs) nk

Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira hiyo njema ya Serikali, bado kuna changamoto kubwa katika kuzingatia usawa wa kijinsia katika sekta mbali mbali za kiuchumi. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

- i. Wanawake na wasichana wengi hapa nchini hawana fursa na haki sawa katika takriban maeneo yote ya jamii ikiwemo kufikia, kutumia na kumiliki rasilimali zikiwemo ardhi, fedha, taarifa, teknolojia na kubwa zaidi katika elimu hasa watoto wa kike nk. Kwa mfano utafiti wa TDHS 2010 ulibaini kuwa ni asilimia 8 tu ya wanawake wanamiliki ardhi yao peke yao ikilinganishwa na asilimia 30 ya wale wanaomiliki katika mfumo wa pamoja. Aidha, utafiti uliofanywa na Oxfam, 2012 ulibaini kwamba ni asilimia 5 tu ya wanawake wanaofanya kazi za kilimo wenye kumiliki ardhi yao, na asilimia 44 wanafanya shughuli za kilimo kwenye ardhi inayomilikiwa na waume zao na asilimia 35 wanafanya kilimo katika ardhi inayomilikiwa na ukoo. Katika utafiti huo, ilibainika pia kwamba ni asilimia 13 tu ya kaya zinazoongozwa na KE

wanapata mikopo ikilinganishwa na asilimia 33 ya kaya zinazoongozwa na wanaume. Hali hii inazuia wanawake kupata fursa za kuijendeleza kiuchumi.

ii. Wanawake na wasichana bado hawana fursa sawa na wanaume kufikia huduma bora za kijamii zikiwemo elimu, afya, maji , nishati na huduma za ugani. Kwa mfano Demographic Health Survey 2010 ilibainisha kuwa asilimia 19.1 ya wanawake wenyewe umri katika miaka 20 – 24 hawana elimu kabisa ikilinganishwa na asilimia 10.5 ya wanaume.

iii. Wanawake hawana fursa sawa na wanaume katika maamuzi kuhusu maslahi yao kuanzia ngazi ya familia hadi taifa. Utafiti wa DHS 2010 ulibaini pia kwamba katika uongozi wanawake katika ngazi za wilaya na serikali za mitaa wanawake walikuwa ni asilimia 10tu au pungufu.

Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali ubaguzi huo wa kijinsia katika fursa mbalimbali bado kuna ongezeko kubwa la ukatili dhidi ya wanawake na watoto, vitendo vya ubakaji kwa wanawake, mimba za utotoni kwa wasichana na mila kandamizi dhidi ya wanawake hususan ukeketaji, utakasaji, nyumba ntobhu, nk.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:

- i. Kuweka lengo mahusi la kuzingatia usawa wa kijinsia ili lielekeze jinsi ya kutafsiri jinsia katika malengo/ vipaumbele vingine vyote na pia kuendeleza juhudini zilizokwishakufanyika kaitka kufikia usawa wa kijinsia katika ngazi mbalimbali za jamii.
- ii. Kuweka mazingira ya kuwajengea uwezo wasichana katika kujenga wataalam wenyewe ujuzi maalum.
- iii. Kuweka mfumo wa bajeti unaozingatia usawa wa kijinsia.

15. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kurejea tena wito wangu kwa Serikali na wananchi wote wenye mapenzi mema; kwamba; "hili taifa ni letu sote" Hakuna Mtanzania zaidi ya mwingine – wote ni watanzania. Hizi kauli za kusema kwamba kuna wazalendo na wasio wazalendo au wapinga maendeleo, ni kauli za kichochezi na kibaguzi na hazilijengi taifa bali zinalipasua.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika hakuna yeote mwenye hati miliki ya Taifa hili. Kama kuna kiongozi aliyepewaa dhamana ya kuliongoza taifa hili kwa kipindi fulani cha muda; atambue kwamba hiyo ni dhamana tu – tena ya muda mfupi, lakini hii nchi sio mali yake. Ana wajibu wa kuliunganisha taifa na sio kulisambaratisha au kuligawa kwa misingi ya aina yoyote ile - iwe ya kidini, kitikadi au ukanda.

Mheshimiwa Spika, Utangamano katika taifa ni jambo la msingi sana. Umoja na mshikamano wa kitaifa ndio moyo wa taifa lolote duniani linalohitaji kuwepo na kuendelea kuwepo. Inatakiwa Mtanzania mmoja akiumizwa iwe tumeumizwa wote; mmoja akipotea tuhuzunike wote; - lakini yanayoendelea sasa; ya wengine kupotea huku wengine wanafanya sherehe; wengine kuuwawa huku wengine wakiendelea na shughuli zao kana kwamba hakuna kilichotokea; tunajenga utamaduni na desturi mbaya kuwahi kutokea duniani; na yamkini tukaingia kwenye kitabu cha rekodi za dunia (the guiness book of records) za kuwa taifa la kwanza duniani lisilojali utu wa mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tena; uhalali (legitimacy) hautafutwi kimabavu. Hali kadhalika heshima hailazimishwi bali huja yenyewe kutohana na matendo mema afanyayo mtu na watu wengine kuwiwa kumpa heshima. Ili uheshimike kama kiongozi timiza wajibu wako kwa kutenda haki kwa kila mtu – kwa kufanya hivyo Mungu ataiamuru heshima ikufuate – hata kama uko usingizini. *"But don't kill or plan to kill, demanding for respect and legitimacy by force; it will backfire"*

Mheshimiwa Spika, majibu sahihi ya kuondokana na athari za utukufu binafsi (personal glory) katika kuongoza nchi ni kujenga mifumo na taasisi imara zitakazojisimamia na kujindesha kwa namna ile ile hata kama atakuja kiongozi mwininge ili tuweze kuwa na uendelevu (sustainability) katika utendaji wa Serikali na pia kuondoa manung'uniko dhidi ya viongozi. Dawa pekee ya kuondoa kufanya kazi kwa upendeleo (subjectivity and bias) ni kuongozwa na sheria, taratibu na kanuni na sio utashi wa mtu. Kujenga taasisi imara kwa maendeleo endelevu inawezekana ikiwa tutahuisha mchakato wa Katiba Mpya. Ingawa Mkuu wa Nchi ameshaweka wazi msimamo wake kwamba hana mpango na Katiba Mpya, kwake yeye ni kuchapa kazi tu, bado mchakato wa Katiba Mpya unabaki kuwa changamoto kwa Serikali hii, kwa kuwa huwezi kuchapa kazi tu bila mwongozo au kanuni za kuifanya kazi hiyo ili ifikie malengo yaliyokusudiwa. Kuchapa kazi tu bila kuwa na mipaka na malengo yanayokusudiwa ni sawa na kwenda bila mwelekeo na kwa hiyo, hatari ya kutumbukia shimonii ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Halima James Mdee (Mb)

WAZIRI KIVULI WA FEDHA NA MIPANGO

NA MSEMADI MKUU WAKAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI

KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

6 Novemba, 2018

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Unajua rafizi zetu wa Kambi rasmi walileta kabrasha kubwa kweli sasa hii shughuli pepu hii. Jamani muwe mna-*summarize* mambo. (*Kicheko*)

Sasa hili utalisomaje kwa nusu saa hata uwe profesa wa maprofesa haiwezekani. Kwa hiyo, nawashauri tu twende

kwenye pointi moja kwa moja ili Waziri wa Fedha aweze kuona mnasema nini au aone hasa mnachokieleza.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, tutaanza uchangiaji wetu jioni na kwa mujibu wa Kanuni ile ya tano ya uendeshaji bora wa shughuli za Bunge moja kwa moja nielekeze tu kwamba kwa sababu kwenye mpango huu huwa karibu Wabunge wote tunachangia na tungependa iwe hivyo.

Basi tujitahidi kuandaa hotuba zetu katika dakika 10. Tukifanya dakika 15 ambapo wanachangia watu wanne kwa muda wa saa moja nzima nadhani hatuwezi kufika popote. *At least* tukifaka 10 tunapata watu sita *in one hour*. Itatusaidia kidogo kwenda mbele zaidi.

Nimwombe kila mmoja wetu anayechangia asome vizuro hotuba zote. Soma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, asome Taarifa ya Kamati iliyyosomwa na Mheshimiwa Simbachawene hapa lakini pia hii hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani nayo isomwe, halafu ijibiwe. Kuna mambo hapa ningekuwa Mbunge wa kawaida ningepiga kwelikweli. Basi kwa hatua hiyo Waheshimiwa Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimimiwa Wabunge tukae.

Sasa kama nilivyokwishaeleza nilivyokuwa kwenye Kamati ya Mipango tutaendelea na uchangiaji jioni na orodha tayari tunayo ya vyama vyote, kwa hiyo tuwahi jioni kusudi tuweze kuanza kuichambua hotuba hii au mapendekezo haya yanayohusiana na Mpango wa Maendeleo ya Taifa pamoja na mwongozo wa kuandaa shughuli zinazoendana na mpango huo. Kila aliyeomba awahi kufika tu tutaanza na uchangiaji kama kawaida.

Baada ya hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 kamili jioni ya leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Kamati ya Mipango!

Waheshimiwa Wabunge, tukae. Habari za jioni. Tunaendelea, ratiba yetu ya leo ni Mipango ya Serikali. Tunaanza na Mheshimiwa Hassan Masala, Mheshimiwa George Lubeleje.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuweza kuwa mchangaiji wa kwanza wa Mpango wa Serikali kwa mwaka 2019/2020. Naomba nijielekeze kwenye eneo moja baada ya kuwa nimeupititia mpango wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kabla sijasema nilichokusudia kusema naomba nitumie nafasi hii kwanza kupongeza jitihada kubwa ambazo zimekuwa zinafanywa na Serikali yetu katika kuhakikisha mipango tulioipanga mwaka 2018/2019 inakwenda, lakini wakati huo tuna-focus kuangalia namna ya kutekeleza mipango ya mwaka wa 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukamilisha mipango ambayo tunaipanga kwa sehemu kubwa lazima tuangalie mambo gani ambayo yanatuwezesha kuhakikisha mipango yetu tunayoipanga inakwenda sambamba. Leo naomba nijielekeze kwenye eneo moja tu la kilimo kwa sababu ya kazi kubwa au faida kubwa ambayo tunaipata kuitia kilimo ambacho tunakishiriki au tunakifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuptitia kilimo ndiko ambako tumekuwa tunaboresha huduma nyingine za kijamii. Kuptitia mipango ambayo Mheshimiwa Waziri leo ameiwasilisha hapa kwa sehemu kubwa ndiko ambako tunapata fedha kwa ajili ya kuhakikisha mambo mengine yote yanakwenda ikiwemo maji, afya, barabara, lakini pia tunapozungumzia viwanda lazima tuzungumzie malighafi ambazo zinatokana na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba pia, nitumie nafasi hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wamefanya kazi kubwa, lakini kwetu sisi wakulima ambao tunatokana na zao la korosho ambalo limetoa mchango mkubwa sana kwa mwaka wa fedha uliopita nimeona nilizungumzie hili kwa kina kwa sababu, kama sitafanya hivi hata wakulima ambao nawawakilisha hapa ndani nafikiri hawawezi kunielewa. Kwa hiyo, naomba njielekeze zaidi kuzungumzia zao la korosho na namna ambavyo limeleta fedha nyingi kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu na hivyo kuhakikisha mipango tunayoipanga inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu wamefanya kazi ya kukaa na wanunuzi wa korosho, lakini pia, wamefanya *intervention* kubwa sana kuhakikisha hali inayoendelea sasa hivi katika maeneo yanayolima korosho haiendelei kuwa mbaya. Katika hili naomba nitoe pongezi kwa niaba ya wale ambao tunawawakilisha kwa sababu, walichokifanya viongozi hawa ni sehemu ya kilio ambacho sisi wakulima tayari tulishakuwanacho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambazo zimechukuliwa na viongozi wetu bado yako mambo ambayo niliona nitumie nafasi hii kuishauri Serikali. Vikao walivyovifanya pamoja na wafanyabiashara, pamoja na kwamba, matarajio yetu yalikuwa ni kuona korosho za wakulima zinaondolewa, lakini bado mpaka leo ninapozungumza kwa makadirio ya haraka haraka kuna jumla ya tani 34,000 kuptitia vyama vikubwa vitano mpaka sasa hivi zimekusanywa. Katika hizi

tani ambazo zimekusanywa jumla ya tani 2,500 *plus* kwenda 3,500 ndizo ambazo zimeuzwa mpaka leo ninapozungumza kwa mnada uliofanyika leo kwenye baadhi ya maeneo ya Tandahimba kule kupitia *TANECU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii na muda ambao tunao kwa kweli, kidogo inatupa mashaka sisi wakulima ambao tumewekeza sehemu kubwa ya fedha zetu kwenye eneo hili. Kwa hiyo, nataka tuone kupitia watu wa Wizara ya Fedha, lakini pia kupitia watu wa Wizara ya Kilimo na pia kupitia Mheshimiwa Rais mwenyewe kwa sababu, yeche ndio mtu wa mwisho ametoa kauli na tunaamini kiitifaki yeye ndiye pia, anapaswa kurudi na kwenda kulizungumzia jambo hili, basi apokee mapendekezo ambayo yanatoka kwa wakulima ili tuweze kuwasaidia kuondokana na hasara ambayo inaweza kwenda kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara ambao walikaa kwenye kile kikao ni kama wamesusia, naweza nikasema hivyo. Kwa sababu, ukiangalia *trend* ya tani wanazozichukua na makubaliano yaliyofanyika hayafanani na kiasi cha korosho ambacho wakulima tunategemea tukiuze. Misimu kwa kawaida huwa inaanza mwezi wa 10, leo tunapozungumza ni mwezi wa 11, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anazungumza kwamba, msimu wa korosho ni miezi mitatu, ni kweli, lakini kuna vitu ambavyo nafikiri bado hajajua korosho na hajaishi korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimueleze kwa sisi tunaotoka kwenye maeneo ya korosho, ikishaanza kunyesha mvua hiyo miezi mitatu ambayo anaihesabia ambayo mpaka sasa hivi hatujafanya biashara itakuwa tena hakuna biashara ambayo inaenda kufanyika kule mara mvua itakapokuwa imeanza kunyesha kutokana na *Jiografia* ya maeneo yetu, lakini pia kutokana na hali ya hewa ambayo inaathiri kwa kiasi kikubwa sana korosho za wakulima ambao wametumia gharama kubwa kuzihudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya juu katika minada hii ni Sh.3,016/= na bei ya chini imebaki Sh.3,000/= ileile, jambo

ambalo sisi tunashukuru kwa sababu, Mheshimiwa Rais alizingatia gharama za uzalishaji ambazo wakulima wamezifanya katika kipindi chote cha kuandaa mashamba, kuvuna, kuokota pamoja na kupeleka kwenye maghala. Ushauri ambao nataka niutoe ni huu ufuatao; kwa sababu wanunuzi wameshindwa kununua hizi korosho kwa kadri ya makubaliano yalivyokuwa yamewekwa, pendekezo la kwanza ambalo nataka nitoe ni kwa Serikali kwa kadri ilivyokuwa imezungumzwa siku ile ya kikao ambacho Mheshimiwa Rais alifanya, Serikali ione uwezekano wa kuzinunua hizi korosho kama hiyo njia tumejipanga nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ambayo nimeshaitaja kwamba, tuliotegemea wanunuzi wazinunue wameshindwa kununua na sasa hivi muda unakwenda na tunategemea watarudi kwenye duru ya pili ambayo pia, haloneshi matumaini ya kwamba, bei itaenda kupanda zaidi ya bei ambayo Mheshimiwa Rais ameipendekeza. Kwa hiyo, Serikali yetu kama imejipanga na fedha ipo, basi tunaomba ichukue hatua za makusudi za haraka kunusuru hali inayoendelea kule sasa hivi, ili korosho za wakulima ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pendekezo la pili, hebu twende tuangalie kwenye Bodi ya Korosho yenyewe. Bodi ya Korosho kuna tozo na kuna fedha ambazo kama Serikali itaenda kuzikata nina hakika zitaenda kumpunguzia mnunuzi mzigo na hivyo azma ya kununua korosho kwa Sh.3,000/= itabaki palepale na haitaathiri pendekezo ambalo Mheshimiwa Rais amelitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo ya kwanza ambayo napendekeza ikatwe ni tozo ya *service charge*. Hawa wanakata Sh.10/=, badala ya Sh.10/=, nashauri Serikali ingewaagiza watu wa bodi wakate Sh.5/= ibaki kwa wanunuzi Sh.5/=, ibaki kwa watu wa bodi kwa ajili ya ku-service hizo huduma ambazo wanaendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili naomba nipendekeze kukata fedha ya kugunia; fedha ya gunia

inakatwa Sh.52.5/= napendekeza ingekatwa Sh.42/= ili 10/= itakayokatwa iingie katika kuhakikisha mnunuzi habebi mzigoto kwa sababu wanazozitoa za kushuka kwa soko la dunia. Basi naamini kwa kufanya hivyo itaenda kupunguza uzito ule wanaoupata sasa hivi kwenda kununua korosho zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pendekezo la tatu tuiangalie pia, *export levy* ambayo kimsingi kuna 15% ambayo tayari hata Mheshimiwa Rais alishaizungumzia. Naomba nishauri hapa, badala ya 15%, Serikali ingebakiwa na 9% ili tuache 6% kwa wanunuzi, nayo pia itaenda kutusaidia. Ikiwezekana hii tutakwenda kusaidia kununua korosho kwa bei ambayo Mheshimiwa Rais ameipanga na hii nafikiri itaenda kutunufaisha sisi wakulima ambao tumeingia gharama kubwa kwa ajili ya kuhakikisha kilimo kinakwenda kutunufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la mwisho katika eneo hili ni kupitia makato yale yote yaliyoko kwenye fedha ya mjengeko wa bei. Kuna makato ambayo kwa hali ilivyo na kwa sababu, hatukujipanga na hiki ambacho kinajitokeza, basi tungeangalia kwenye ile fedha ya mjengeko wa bei Sh.240/= kuna fedha kule za vyama, kuna fedha kule kwa ajili ya kuhudumia vyama vya ushirika, hizi zote tungeziangalia vizuri, lakini pia tungetoa maelekezo kwenye halmashauri zetu ziondoe zile fedha ambazo hazina ulazima kukaa kwenye fedha hii, ili mkulima aweze kunufaika, lakini pia, wafanyabiashara wasipate hasara ambayo wanafikiri wataipata kama watachukua korosho zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendezo lingine ambalo naomba nitoe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje, wajiandae Mheshimiwa Allan Kiula na Mheshimiwa Lulida.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuchangia hoja hii ya mipango. Kwanza kabisa nianze na sekta ya umeme; niishukuru sana Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba vijiji vingi vinakuwa na huduma ya umeme. Kwa Jimbo la Mpwapwa ni vijiji sita tu ambavyo bado havijapata huduma ya umeme kwa hiyo, nishukuru na niipongeze sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya umeme ni maendeleo ya nchi na uchumi wa nchi kwa sababu, kijiji kikipata umeme wataanzisha viwanda vidogovidogo vya kukamua mbegu za mafuta kwa mfano alizeti, ufuta, karanga na Serikali itapata mapato pale. Kwa hiyo, naionomba Serikali, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na ameshafika Mpwapwa kutembelea kuona hii hali ya huduma za umeme, vile vijiji ambavyo bado havijapata umeme Kazania, Kiogegeya, Chimaligo, Mkanana, Kibolian, Nana, Namba 30 Mafuto pamoja na Majami, naombwa sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi nao wapate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni sekta ya ujenzi. Mawasiliano ni muhimu sana katika nchi yoyote duniani, bila mawasiliano nchi hiyo itakuwa haina maendeleo. Barabara za lami zinatengenezwa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais amesimamia hiyo kazi hasa Dar-es-Salaam ambako kuna msongamano mkubwa sana wa wananchi, lakini haya mabasi yanayokwenda kasi yamepunguza msongamano, lakini hata *fly overs* ambazo zinajengwa zimesaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombwa nikumbushe suala la ujenzi wa barabara. Pamoja na kwamba, Serikali inajitahidi kujenga barabara za Kitaifa na mko, lakini hata hizi za wilaya kwa mfano, barabara ya kutoka Mbende – Kongwa – Mpwapwa, hili suala nimeshalizungumza muda mrefu sana hata Mheshimiwa Waziri Mkuu wiki mbili zilizopita alikuwa Mpwapwa tumeshamwambia ni ahadi ya Marais karibu wanne wote wanaahidi kwamba, tutatengeneza hii barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Wilaya ya Mpwapwa na uchumi wa Mpwapwa, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kwa mwaka huu wameitengea fedha ni kidogo sana, milioni 500 ni sawasawa na kilometra moja tu. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Waziri wa Mipango wakati anasoma alikuja Wilaya ya Mpwapwa kufanya mazoezi na barabara ile alipita, anaifahamu vizuri sana, hebu wanisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za vijijini ni muhimu. Tusiseme kwamba barabara za lami tu, ndio barabara za lami ni muhimu, lakini vijijini ndiko wanakoishi wakulima na watu wa mijini wengi hawana mashamba, hawalimi, wanategemea chakula kutoka vijijini, sasa magari yasipopata barabara nzuri za kupita watasafirishaje haya mazao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* ni kweli imeundwa naishukuru Serikali, lakini iongezewe bajeti. Naomba lile fungu lile la mafuta, Mfuko wa *Road Fund*, basi angalau tugawane *TANROADS* wapate 60% na *TARURA* wapate 40% waweze kufanya matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu ni mbaya sana. Waziri wa *TAMISEMI* ameshafika maeneo ya Mima, Barabara ya Mima ni mbaya haipitiki, sasa na mvua zinaanza, Barabara za Mkanana. Naishukuru sana Serikali imetenga milioni 48 na kwa upande wa barabara ya Mima imetengewa zaidi ya milioni 60 na tayari Wakandarasi wameshasaini mikataba kwa hiyo, hivi karibuni wataanza kutengeneza. Kwa hiyo, pamoja na barabara za Kitaifa, barabara za Mikoa, lakini vilevile Serikali izingatie barabara za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni sekta ya maji, sekta ya maji ni muhimu sana, maji ni uhai, maji ndio uchumi wetu, maji ndio maendeleo na maji ndio kila kitu. Kwa hiyo, naiomba Serikali pamoja na juhudini kwamba, visima vya maji vimechimbwa karibu viji vingi sana; kwa mfano mimi katika jimbo langu visima vimechimbwa vingi, lakini bado wananchi wana tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwasaidie akinamama kusafiri mwenda mrefu, ukiwa na ndoo, ukiwa na sijui kitu gani unakwenda kutafuta maji kilometra 10 mpaka 15. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali suala la huduma ya maji ni muhimu sana. Naishauri Serikali kila kijiji kiwe na kisima cha maji ili kuwapunguzia hawa akinamama matatizo ya kusafiri mwendo mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta nyengine ni sekta ya afya, ni kweli Serikali imejitahidi sana maana afya, ukisema Wizara ya Afya ni hospitali, vituo vya afya na zahanati na zahanati, hospitali, vituo vya afya si majengo tu isipokuwa ni dawa, lazima majengo hayo yawe na dawa za kutosha na yawe na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudzi za Serikali kutenga fedha za kutosha karibu billioni 269 kwa ajili ya kununua dawa, lakini bado tatizo hili ni kubwa katika hospitali zetu, watumishi ni wachache; utakuta zahanati wanaohudumia zaidi ni wale *medical attendant*, hatusemi kwamba, hawafanyi kazi nzuri, *medical attendant* ndio wanafanya kazi nzuri, ndio wanatoa dawa, wanachoma sindano na hata kuzalisha akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ilikuwa na mpango wa kuanzisha vyuo vingi kwa ajili ya ku-*train* au kufundisha hawa *Clinical Officers* au *Clinical Assistants*, lakini mpaka sasa bado watumishi hao ni wachache sana. Naomba vyuo vile ambavyo Serikali, Wizara ya Afya iliahidi basi vifunguliwe kwa ajili ya kufundisha *Clinical Officers* pamoja na *Clinical Assistants* ili waweze kupelekwa kwenye zahanati zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na haya machache, lakini nakushukuru sana. Naiomba Serikali ikumbuke barabara za Mpwapwa, Kongwa, pamoja na Mbande pamoja na Daraja la Godegode ambacho ni kiungo kikubwa cha Jimbo la Mpwapwa na Jimbo la Kibakwe. Hivi sasa wananchi wanazunguka kutoka Kata za Mbuga kuja Kata ya Lumuma, Kata ya Kitatu Pwaga

wanazungukia Kibakwe ambayo ni zaidi ya kilometra 100 na nauli ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono kwa asilimia mia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Allan Kiula, jiandae Mheshimiwa Riziki Lulida.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kuweza kupata nafasi ya tatu ili kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Muongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2019/2020. Kwanza kabisa niipongeze Wizara na wataalam kwa kazi kubwa wanayofanya na kwa kutuletea hizi nyaraka. Nyaraka hizi zimekuja zioko vizuri tu, zisingekuja hizi nafikiri watu wasingekuwa na maneno mengi ya kusema, lakini nyaraka hizi zimeandikwa kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda nianze kwanza kuhusu mwenendo na viashiria vya uchumi. Napenda niseme jambo kidogo hapo, ndugu zangu nafikiri wapo Waheshimiwa Wabunge huwa hawarejei tulipotoka, lakini Mheshimiwa Waziri katika Bunge lililopita alikwishaweka vigezo, unaposema uchumi unakua na *projection* ni 7.2 maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimshauri tena Waziri hilo darasa atakapokuwa anahitimisha aweze kulifungua tena kwa sababu wapo watu wana ubishani ambaao hauna takwimu. Hata hivyo, pia wanachanganya sana kukua kwa uchumi na suala la umaskini, upimaji wa umaskini una vigezo vyake na kukua kwa uchumi kuna vigezo vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ukurasa wa nane kwenye hotuba ya Waziri napenda nizungumzie suala la uhimilivu wa deni la Taifa. Jambo hilo pia katika kikao

kilichopita lilishafunguliwa darasa humu tunapimaje uhimilivu wa deni la Taifa. Niipongeze Serikali kwa kuwa wazi kwa sababu Serikali imesema deni la Taifa limekua kutoka dola za Marekani milioni 25 mpaka 27, kwa hiyo, Serikali haina jambo la kuficha hapa imeeleza wazi na vigezo vya upimaji viko wazi. Kwa hiyo, hao wanaotaka kubishana na takwimu inabidi wajipange ili waweze kueleza hili jambo kwa ukamillifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze tena Wizara, Wizara imetuletea *documents* tatu, nafikiri wengine hawana au hawajazisoma. Moja ya *document* inasema taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 mpaka 2018/2019, ukifuatilia hapo utaona mambo makubwa ambayo yameshafanyika ndani ya miaka mitatu. Sasa watu wanaposema mpango unafeli sasa inakuwa ni changamoto kubwa sana. Nawashauri waende wakasome tena na hilo Waziri hana sababu ya kuwajibu kwa sababu wanazo hizo nyaraka za rejea ambazo wanaweza wakasoma wakiwa mahotelini kwao au kwenye nyumba walizopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la makusanyo ya mapato. Napenda nijikite kwenye suala la ukusanyaji wa mapato yanayokusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Tumeona wamekusanya asilimia 89, kwanza niwapongeze asilimia 89 kwa watu ambao wanajua ukusanyaji wa mapato hiyo ni A na wamefanya kazi kubwa sana ukizingatia wapo watu wengine wanataka kukwepa mapato kwa hiyo kunakuwa na ushindani. Kwa hiyo, *TRA* wamefanya kazi kubwa sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona changamoto za ukusanyaji wa mapato, lakini moja ya eneo ambalo lilizungumzwa na ambalo tumekuwa tukizungumza ni suala la sekta isiyo rasmi. Ni muhimu *TRA* wakaa chini wakaangalia namna ya *ku-formalize* hiyo sekta isiyo rasmi. Jambo kubwa ambalo limekuwa linaleta changamoto ni viwango vikubwa vya kodi au viwango visivyo rafiki. Kwa hiyo, hawa watu tunaotaka kuwa *formalize* lazima tufanye utafiti tuone tunawaingizaje kwenye wigo wa kodi, kwa hiyo wanaweza

wakaanza kidogo tukawatambua; tukiwatambua, tukawalea watakuwa wanakua kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nalisema kwa dhati kabisa kwa sababu natoka vijiji; kumekuwa na malalamiko makubwa sana na mengi kuhusu viwango vya kodi na utaratibu mzima wa ukadiriaji. Kwa hiyo, niwashauri wenzetu wa Mamlaka ya Mapato wakae watoe mapendekezo ambayo mapendekezo hayo yataweza kuwashawishi watu kuweza kulipa kodi badala ya kukwepa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la ugharamiaji wa miradi ya kielelezo. Kabla sijafika kwenye ugharamiaji wa miradi ya kielelezo niseme kwenye ukusanyaji wa Mamlaka ya Mapato lazima tuangalie zile nguzo kuu za uchumi, tukiimarisha nguzo kuu za uchumi, tukiimarisha nguzo kuu za uchumi tutegeme makusanyo mengi kutoka kwenye kodi za ndani. Hii biashara ya bidhaa kutoka nje kuingia huku ndani ikikata tunakuwa hatupati mapato ya kutosha. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba uchumi wetu unaweza kuongeza ukusanyaji wa mapato katika ile idara ya kodi za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugharamiaji wa miradi ya kielelezo. Ugharamiaji wa miradi ya kielelezo ni jambo muhimu sana, miradi imeanishwa na ilianishwa tangu tulivyowasilisha mpango wa miaka mitano na mara nyingine wenzetu hawa wanakuja kusema hiki kimetoka wapi, lakini wakichukua kile kitabu cha mwanzo kabisa wataweza kuona miradi hii yote imetoka sehemu gani. Kwa hiyo, ni muhimu fedha zikatolewa na fedha hizo zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la mikopo na misaada kutoka nje. Takwimu zinaonesha kwamba hatukuweza kufanikiwa sana na sisi tulitegemea sana huko, sasa lazima tuweke mpango mkakati imara wa kuona kwamba hilo jambo haliwezi kururudisha nyuma, tuhakikishe kwanza vyanzo vyetu vya mapato tunavifanyia utafiti wa kutoka na tunaangalia *associated risk* kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sekta ya kilimo; sekta ya kilimo na yenye ipo kwenye suala zima kuna miradi ya kielelezo kule kuna mashamba ya sukari na vitu vya namna hiyo. Nipendekeze kabisa kwamba mpango huu lazima uangalie namna ya kumsaidia mkulima wa kawaida (mkulima mdogo). Wakulima wadogo hawana *access* na mikopo, kwa hiyo wakulima wadogo wakiweza kupata mikopo wataweza kuchangia kwenye kilimo ambayo ni malighafi, malighafi hiyo itakwenda kwenye viwanda. Hilo ni jambo muhimu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kwenye vyombo vya habari juzi tu mbegu ya alizeti kilo moja Sh.35,000; sasa nani anayeweza kumudu Sh.35,000 na akalima na huo uzalishaji wake umepimwa wapi. Ni muhimu jambo hilo likaangaliwa na yale mazao ya kimkakati yakafuatiliwa kwa karibu kama ambavyo Waziri Mkuu amekuwa akifuatilia suala zima la zao la pamba na korosho. Sasa na zao la alizeti lifuatiliwe. Kama tuliongeza kodi kwa mafuta yanayotoka nje ni muhimu mazao kama alizeti yakapewa kipaumbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo ukipita ukitoka Shelui ukaja Singida, Dodoma mpaka Gairo yapo mafuta mengi sana barabarani wananchi wanashika yapo mkononi. Je, kuna mkakati gani wa kuweza kuyaingiza hayo mafuta kwenye mzunguko wa kawaida (ulio rasmi) na wale wananchi wakaweza kunufaika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala zima katika sekta ya afya, tulizungumza mwanzo, suala la ugharamiaji wa maboma ambayo nguvu za wananchi zilitumika. Jambo hilo bado halijapata jawabu lake. Tumejikita kuweza kutoa fedha kujenga vitu vya afya na Hospitali za Wilaya tunashukuru, lakini yapo maboma mengi sana ambayo wananchi walijajenga na walitarajia Serikali iwasaidie kufunika. Tunaomba jambo hili na lenyewe liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo marefu, nishukuru Serikali kwenye mipango mikakati yake kwa

kuweza kuboresha miundombinu kwa sababu miundombinu ni mhimili mkubwa wa uchumi ikiwemo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Riziki Lulida, jiandae Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema ambaye amenijaalia kuweza kuwa hapa na kuweza kuchangia katika hoja iliyopo hapo mezani. Vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu aliteremsha vitabu vinne na aliwateremshia Manabii mbalimbali ikiwemo Injili alimteremshia Nabii Issa (*Alayh-Salaam*); Taurati kwa Nabii Mussa; Zaburi kwa Nabii Daud na Quran kwa Nabii Muhammad (*Swalla-Allah Alayh Wasalaam*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na madhumuni ya kuteremsha vitabu hivi ni kuwaweka binadamu katika mfumo wa kujua kuna Mwenyezi Mungu na kumwabudu Mwenyezi Mungu katika matendo yaliyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitabu hivyo vyote hakuna mahali palipozungumzia suala la ushoga. Ushoga ni dhambi ambayo haitakiwi na inatakiwa ikemewe, sio mfumo wa kiafrika ni mifumo ya watu wa nje, wao waendelee na mifumo wao na watuachie na utamaduni wetu wa kiafrika wa kumuabudu Mungu aliye sahihi katika vitabu vyake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo ninakwenda katika hoja iliyopo mezani. Mipango iendane na maeneo ambayo sasa hivi yalikuwa nyuma kwa muda

mrefu. Mkoa wa Lindi, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Kigoma na Singida hii ni mikoa ilikuwa nyuma na Serikali inahitajika isimame kutoa kipaumbele na kuwahurumia wananchi wa maeneo hayo ni na wao waendane na wenzao. Nitazungumzia Mtwara *Corridor* na baadhi ya maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usinione pengine napenda sana kuangalia Mikoa ya Lindi na Mtwara, ndiyo mikoa ambayo iko nyuma, hakuna cha kubishana katika hilo. Tulliteewa Mradi wa *LNG* (*Liquefied Natural Gas*), ule mradi umenyamaza, upo kimya, hatujui kinachoendelea ni kizunguzungu. Wananchi wa eneo la Likong'o wamechukuliwa maeneo yao huu ni mwaka karibu wa nne au wa tano hawaruhusiwi kulima wala kufanya maendeleo ya namna yoyote, hawajalipwa fidia zao na hali ngumu ya uchumi kama hivi tunategemea watu kama wale wanafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri mwenye dhamana atuambie mradi mkubwa kama ule umefikia wapi hata kwa kutoa semina kwa Wabunge, Wabunge wawe na uelewa, lakini wale wananchi ambao wananyanyasika na ardhi zao, hawajui wanalima nini, wanakula nini, Serikali imetumia kitu gani cha kuwasaidia wale watu. Wamejipanga vipi kuwainua watu wale amba ni maskini wanategemea mikorosho na kilimo chao wapate chakula, sasa hivi hawana chakula. Naomba Serikali yenye dhamana ikawahurumie wale watu na iwatengenezee mazingira bora kwa kila Mtanzania inawezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja katika suala la mazao mchanganyiko kuna korosho, pamba, alizeti, katani, dengu, maharage na kadhalika. Wananchi wamekwama na mazao yao, hawajui wafanye nini. MBAazi za mwaka jana hazikuuzwa zimekaa majumbani na nyingine zimeachwa shambani mpaka zimeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe angalau ushauri; Rwanda wenzetu wamejiingiza katika mfumo wa

kibiashara unaitwa *African Improvement Food*. Hiyo maana yake wamejiunga na taasisi mbalimbali za nje wanatengeneza mifumo ya mazao yao kupeleka *direct* nje bila kupitia kwa wababaishaji wa katikati ambao wametunzungusha kwa muda mrefu. Leo karanga za Dodoma, Singida na Shinyanga zinapelekwa Rwanda na kahawa ya Bukoba inapelekwa Uganda. Sasa tujiulize kwa nini wenzetu wameweza sisi tumeshindwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na taasisi moja *Board of External Trade* sielewi imefia wapi, ina maana wale wange-link na mashirika mbalimbali ya nje ya kibiashara kama soko la *European Union* tungekuwa sasa hivi tusingekaa tunababaishana na watu ambao wameshakuwa wababaishaji tumewatajirisha sasa hivi wamekuwa wanatudhalilisha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ubabaishaji wamezoea kutuona wananchi wa Tanzania tukiendelea kuwa maskini wao waendelee kuwa matajiri na hawapo tayari kushirikiana na sisi angalau kututoa katika umaskini. Tanzania ya kuweza kusaidia viwanda na maendeleo ya kilimo inawezekana, tujipange tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni *champion* na hoja mara nyingi itakuwa haieleweki lakini kutakuwa na siku watu wataielewa. Nina hoja kubwa ya Selous, nina hoja kubwa ya mjusi tunakimbizana na mama ntilie. Pato la mjusi nani analisimamia? Nataka nitoe onyo au niisaidie Serikali kwanza Lindi Vijiji iitwe Tendeguru *District*, maana yake ukisoma suala la Tendeguru wanasema *it's a loss science, it's not a loss science, it's a life science.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanavyosema Tendeguru haijulikani duniani wakati mimi Riziki nilikuwa Tendeguru juzi na watakapokuja wao wakienda kuvumbua pale wataonekana sisi tumeiacha Tendeguru haionekani. Naomba kila Mtanzania ajifunze kukimbia na maendeleo ya Tanzania. Mapato yale kuyaachia vijiji vile wakiwa hawana

shule, maji na barabara; *revenue* ambayo inapatikana kule tuje na sisi tupate mrabaha, tatizo lipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku nalizungumza tatizo lipo wapi? Mjusi yule toka mwaka 1903 yuko Tristan Ujerumani wanafanya *exhibition*, wanapata mapato, hivi jamani Serikali hii mnashindwa hata kujua Lindi inapata nini au tozo yake ni nini? Mimi nakuwa hapa kila siku nayumba napiga kelele hamnielewi ninalolizungumza, lakini nina imani kutatokea watu wachache watakaoniunga mkono na kulielewa hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Selous; Selous ni ya pili katika dunia kwa ukubwa wake. Selous ni eneo ambalo ni shamba la bibi linachezewa, watu wanachimba madini, wanamaliza wanyama na matokeo yake pato la utalii wa Tanzania litapatikana wapi. Kuna *corridorya* Tembo kutoka Selous kwenda Niyasa na Niyasa – Selous. Kuna *corridor* ya Tembo kutoka Rukwa Rukwati kwenda mpaka Katavi – Zambia, hizi *corridor* zote hazijakuwa *promoted*. Tunahitaji kufanya *promotion* ya kutosha na tutoe hela ya kutosha utalii wa Tanzania badala ya kutegemea asilimia 17.2 naomba sasa hivi kwa pamoja tujipange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu ambao tupo katika Kamati moja ya Kupambana na Ujangili na Kuendeleza *Conservation* twende kwa pamoja tupambane kwa hili mpaka tujue Selous inapata patola aina gani na matumizi yake yanakwendaje ili nchi nayo ipate uchumi bora badala ya kukimbizana na mama ntilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa barabara. Ili tuendeleee tunahitaji uchumi bora ambao utapatikana katika mawasiliano na ikiwemo barabara. Nahuzunika sana, juzi wamekwenda kupiga kelele Liwale wamepata kiti Liwale lakini Liwale iko kisiwani. Ina maana wanawapenda watu wa Liwale wawapigie kura lakini Liwale iendeleee kuwa kisiwa, zikianza mvua za mwezi wa 11 hakuna

hata Mbunge wa Liwale kwenda Liwale, mimi sielewi. Kwa nini wanawafanya watu wa Liwale wawe kisiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Dar es Salaam ukifika Nangurukuru kwenda Liwale unazunguka mpaka Nachingwea, ni miezi mitatu tu ndipo unakwenda Liwale. Wanalima korosho, ufuta na mbaazi hali yao ni duni kwa vile hawana barabara. Naomba Mwenyezi Mungu alijaalie Bunge hili na wanaonisikia hao wenye kuweka hizo hela na mafungu waisaidie Liwale, Nachingwea na maeneo mengine ili uchumi wa Tanzania uweze kukua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina mengine, nawashukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jitu, wajlandae Mheshimiwa Kiruswa na Mheshimiwa Msigwa.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa ya kuchangia leo na pia nishukuru kwa taarifa zote zilizoletwa mbele yetu na ninaishukuru Wizara kwa kuweka mpango mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika baadhi ya maeneo tuendelee kushauri. Moja, ili Serikali iweze kuendelea kupata mapato makubwa na tuweze kukusanya mapato mengi, suala zima la kuhakikisha *blueprint* yetu ya kuhakikisha kwamba *business environment* iwe nzuri ni muhimu lianz kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile rasimu imeletwa na imeanza kufanyiwa kazi lakini bado; haya mengine yote tunayosema Serikali isipopata uwezo wa kukusanya fedha za kutosha uzalishaji wetu uwe bidhaa zinazalishwa kwa bei ya ushindani ili tuweze kushindana na bidhaa zinazotoka nje bado itakuwa hatujawasaidia Watanzania na ndoto yetu ya kufika kwenye uchumi wa viwanda haitafikika, kwa sababu

bidhaa zetu siku zote zitakuwa ni za gharama ya juu kuliko bidhaa zinazotoka nje ya nchi na sehemu kubwa tunakwamba ni kutokana na hizi *Regulatory Bodies*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kushauri kila wakati tukija kwenye bajeti tunatoa mbili, tatu basi, lakini bado changamoto ya wafanyabiashara wote na hivi viwanda ni hizi *regulatory bodies* zetu ambazo ada na tozo ni kubwa mno na tusipozirekebisha mapema bado ndoto yetu haitafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu kuliko yote kwenye jambo hilo pia ni suala la Wabunge kuja huku kujitahidi kupitia kamati zao na Wabunge binafsi kuondoa baadhi ya kodi na Serikali kwa nia njema inaondoa kodi kwa mfano kwenye chakula cha mifugo tukaondoa kodi zote za *VAT* na pia kwenye *ingredient* zake, zile *raw materials* za kutengenezea zile chakula cha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya muda tu kupitia Wizara ya Mifugo wakaleta kanuni zikarudishwa sasa kwa kupitia kanuni tozo mbalimbali ambazo tumerudi pale pale bado hatupo *competitive*. Kwa hiyo, suala la kutumia kanuni vibaya huku tunaondoa halafu unarudisha kwa njia ya kanuni bado hatutakuwa tunawatendea haki Watanzania na tutakuwa tunajidanganya sisi wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuendelee kuhakikisha kwamba *bring business*, hizo Wizara zote zikae pamoja na bila Serikali kuwa na uratibu, pawe na chombo cha uratibu kwamba kila wizara sasa wote mkubaliane kwamba nini kitoke na nini kibaki ili viwanda vyetu vifanye kazi vizuri na uzalishaji uwe na bei nafuu ili tuweze kushindana kwenye soko la ndani na bidhaa nyingine tuweze kupeleka kwenye masoko ya nje, hayo hayawezekani zaidi ya kufanyika ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha, nashukuru hapa mmesema tuendelee kuboresha *SIDO* na vyuo vingine vya ufundi. Bila kurudisha ile asilimia 2 ya *SDL VETA* ili tuweze kuwaandaa vijana wengi ambao watakuwa *technicians* kwenye viwanda vyetu, hatutapata msaada wowote kwa sababu kuwa na watu wengi wenyе *degree* ambao hawajui kushika vyuma na kuendesha mitambo, haisaidii, inatakiwa hawa wa huku chini kwenye *VETA* ndio wawe wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo inakwenda na masuala ya *IT*, kwa hiyo, *VETA* zetu pia mifumo yao lazima ibadiliike tuendane na mifumo ya teknolojia ya kisasa ya kutumia *IT*. Kwa hiyo, nashauri kwamba ile asilimia 2 ambayo tunapeleka kwenye *Loans' Board* ingerudi *VETA* ili tuboreshe *VETA* na *SIDO* na vyuo vingine ili tuwe na wataalam wa kutosha kwenda kwenye viwanda vya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Tanzania hatutakuwa tunajaribu kutengeneza au ku-*invent* gurudumu kwa sababu tayari limeshavumbuliwa. Cha kufanya ni kuangalia vitu mbalimbali na kuchukua mifano mizuri kama walivyofanya nchi za Bara la Asia, *Tiger Economy*, nasi *copy and paste* ili tuweze kuwa na viwanda vidogo vitakavyosindika mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuwekeza zaidi kwenye kilimo, mifugo na uvuvi ambapo asilimia 75 ya Watanzania wako huko. Tukiwekeza huko zaidi na tutukifungamanisha sekta hizo pamoja na viwanda, tayari tutakuwa tumepata ajira lakini pia Serikali itakuwa inapata mapato yake kutohana na shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujikite kwenye maeneo makuu matano. Moja, tujikite kwenye kilimo cha kuzalisha sukari ambayo tunaagiza kwa wingi. Pili, tujikite kwenye kuzalisha mafuta ya kupikia ambayo ndiyo *second largest import* yakifuatiwa na mafuta ya magari. Tatu, tuwekeze kwenye mbegu kwani asilimia 75 ya mbegu tunaagiza kutoka nje ya nchi. Nne, tuwekeze kwenye suala

la mboga mboga, matunda na nyama maana vingine vinatoka nje, vyote hivi tuna uwezo wa kuzalisha ndani ya nchi. Tuweke mazingira wezeshi kwa sababu hizo bidhaa zikizalishwa ndani ya nchi kwa ubora wake nina uhakika tutaongeza ajira na mapato ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu, hakuna *fair competition* na *fair play* kwenye *business*. Leo kuna watu ambao wanatozwa kodi kuliko watu wengine ndiyo maana watu wengi wanatoka kwenye *formal sector* kwenda kwenye *informal sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja tu, ukiwa na kampuni ambayo ni *limited* au kampuni iliyosajiliwa, gharama zenu za uzalishaji ni sawa na yule ambaye hajasajili kampuni yake, anayejientesha kama Jitu Soni, lakini huyu mmoja mwenye *limited company* atatozwa kodi zaidi ya 26 au 27, anashindwa sasa kumudu. Kwa hiyo, naye pia ataamua kuondoka kwenye *formal sector* arudi kwenye *informal sector*. Ndiyo maana *informal sector* miaka yote inaendelea kukua na hakuna *incentive* ya kurudi kwenye *formal sector* kwa sababu hizi *regulatory boardies* ndiyo zinawamaliza kwa kuwatoza kodi kubwa na huko kwenye *informal sector* hawana mamlaka kwenda kutoza. Kwa hiyo, hakuna *fair competition* kwenye *business environment* na katika mazingira ya kufanya kazi.

Mhehimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo tukija kwenye ukusanyaji wa mapato, hapo pia hakuna *fair play*. Kwa sababu unakuta duka moja mtu amesajiliwa kwenye VAT ambayo mapato yake ni madogo lakini wenzake kumi ambao wako jirani naye hawajasajiliwa huko kwenye VAT, unakuta huyu mtu anashindwa kufanya biashara. Kwa hiyo, katika eneo moja kama ni *EFD machine* wote wawe nazo, kama kuna mtu ambaye ana *VAT machine* wote waliofanana naye wawe nazo. Tukiwa kwenye *fair play* kila mmoja akiwa anafanya biashara kwa usawa, nina uhakika manung'uniko yatakuwa hayapo lakini kila mmoja atalipa stahiki yake na Serikali itapata mapato yake na tupunguze kiasi cha kodi na tozo ili watu wengi waweze kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wasipokuwa na *economic spending power*, kukua kwa uchumi kama hau-relate na uchumi wa mtu mmoja mmoja bado itakuwa hatujawasaidia watu. Mtu akiwa na uwezo wa ku-spend zaidi, Serikali itakusanya *indirect taxes* kwa wingi zaidi na hizi *flagship projects* na hii mengine yote tunayoitarajia tutaweza kuitekeleza kwa kodi zetu wenyewe bila kutegemea au kuomba msaada kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu ni kwamba pawe na *fair competition* na hii *formal sector* na *informal sector* tuiangalie. Leo hii kuna wanafanya biashara wanalipa kodi, ada, leseni na kila kitu lakini kuna mtu anafanya biashara hiyo hiyo kwenye baraza yake halipi hata senti tano. Hivi huyo mtu baada ya muda naye si ataamua kuwa machinga kama huyo ambaye yuko hapo nje? Kwa hiyo, lazima Serikali iwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba kila mmoja analipa kodi anayostahili kulipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tukiwa na miradi, kwa mfano *AMSDP II*, naishukuru Serikali kwani huu ni mpango na mkakati mzuri sana lakini hauna *time frame*; hatujui tunaanza lini na tunamaliza lini. Kitu chochote ambacho hakina *time frame* kwamba *it starts 1st of January and ends 30th of December* tayari hapo umeshapoteza mwelekeo. Ni vizuri tuhakikishe kwamba mradi huo tunaupa *time frame* na fedha zote ambazo tunatakiwa kuwekeza huko tupeleke kwa wakati ili waweze kutekeleza ule mradi kwa wakati maana utasaidia nchi nzima. Kama ilivyokuwa *SAGCOT (Southern Agricultural Growth Corridor)*, naendelea kuiomba Serikali ianzishe na maeneo mengine kama *Lake Zone* na Kanda ya Kusini ili wote tuendelee kunufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ajiandae.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia katika mpango huu. Nianze kwa kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuendelea kupeleka mbele maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuelekeza pongezi zangu za dhati katika maeneo kadhaa ambayo ni dhihirisho la uhakika kinyume na hoja walizotoa wenzetu wa Kambi ya Upinzani kwamba maendeleo ya nchi yetu yanarudi nyuma. Napingana nao kwa sababu hata ukiangalia katika upande wa ukuaji wa uchumi nchi yetu iko katika mstari wa mbele inaongoza katika Ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuwa na ukuaji wa asilimia 7.1 mwaka 2017 na mwaka huu asilimia 7.2. Inaonekana kwamba uchumi wetu unakua na hakuna sababu ya kutilia mashaka hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Serikali yetu kwa sababu nimeangalia katika baadhi ya mambo yanayotekelawa nikaona kwamba kuna mapinduzi makubwa katika sekta ya madini. Mabadiliko makubwa yamefanyika katika sera na sheria na mapato yameongezeka, sawasawa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, Wizara ya Ardhi na hata Uhamiaji. Nimesoma katika mpango, nami napenda kupongeza hilo na kuishauri Serikali kwamba tuendelee katika kutumia hii teknolojia ya kielektroniki kwani ndiyo imekuwa chanzo cha makusanyo ya Serikali kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani kuona hili likichukuliwa kama kipaumbele cha kwanza na Wizara yetu ya Maliasili na Utalii kwa sababu kuna tozo nyingi ambazo zimetawanyika na zinawakera wateja wetu ambaao ni watalii. Natamani kuona kitu ambacho napendekeza kiitwe *One Stop Payment Centre* ambapo mtalii kwa kutumia mifumo ya mitandao ambayo itaanzzishwa anaweza aka-book parks anazotaka kwenda akiwa kwao, akalipia kwa credit card yake fees zinazohusika, akalipia hata visa, akifika airport anaonesha tu kwamba ameshalipia na anaongozwa mpaka kwenye parks zetu akatalii kwa raha zake na

kuondoka bila kubugudhiwa. Tukifanya hivyo, naamini sekta ya utalii itaongeza mapato kwa kiwango kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Serikali katika sekta ya elimu. Ukiangalia sekta hii sasa hivi kuna sera ya elimu msingi bila malipo ambayo imeongeza idadi ya watoto wanaosoma. Pia napenda kuipongeza Wizara kwa sababu wameonesha jitihada katika kuchapisha vitabu vya kiada na rejea hata katika ngazi ya chini kuanzia elimu ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kwamba kwa sababu tuna azma kubwa ya kufundisha wataalam wa fani mbalimbali katika nchi yetu, hatutaweza kuwa na wataalam wabobevu na wenye msingi imara tusipowekeza katika elimu ya awali kwa kuhakikisha kwamba hizi shule zinazoitwa shule shikizi ambazo jamii ndiyo inawatafuta walimu, tena ambao hawajasomea, naiomba Serikali iweke katika huu mpango wa mwaka huu unaokuja mkakati kabambe wa kuhakikisha kwamba shule shikizi zinasimamiwa na Serikali ama kwa kuwapelekea walimu au kwa kuhamasisha jamii waaajiri walimu ambao wamesomea jinsi ya kutoa elimu ya awali. Ni katika kutoa elimu bora katika ngazi ya awali ndiyo tunapata watoto ambao wameiva kwenda elimu ya msingi, sekondari, vyuo na kuwapata wataalam katika fani mbalimbali zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilipokuwa napitia hii taarifa ya Kamati...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati wameelezea baadhi ya miradi mikubwa ambayo ingeiletea faida Serikali yetu lakini inaonekana haijawekwa katika mpango wa mwaka 2019/2020. Wametaja mradi mmoja unaoitwa Mradi wa Magadisoda wa Bonde la Engaruka, nafikiri wamekosea na wakasema upo katika Ziwa

Manyara, ni ukurasa wa 22 lakini Bonde la Engaruka haliko katika Ziwa Manyara liko katika Wilaya ya Monduli na Bonde hilo lina ziwa kwa lugha yetu ya Kimasai linaitwa Orboloti Langaruka, ni eneo la mpakani mwa Longido na Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika kuangalia kwa kina manufaa ya mradi huu kwa jamii zinazozunguka eneo hilo, watakapokuwa wanafanya usanifu na naamini umeshafanyika, ili kuepusha migogoro wabainishe uhalisia wa maeneo yaliyopo katika Wilaya ya Monduli maana asilimia kubwa ya ziwa liko katika Wilaya ya Monduli lakini kuna maeneo pia ya bonde hilo ambayo yanaangukia katika Wilaya ya Longido. Napenda kutoa ushauri huo ili kuepusha migogoro ambayo inaweza ikazuka baadaye wananchi watakapokuwa wanadai manufaa yatakayotokana na mradi huo wa magadisoda katika Bonde la Engaruka kwenye hilo Ziwa la Orboloti na haliko katika Ziwa Manyara na naomba hilo liangaliwe na kusahihishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala ambalo Kamati imeleta kuhusu ukamilishaji wa miradi ambayo inaonekana inakwenda kuwapatia wananchi nguvu za kiuchumi na maendeleo. Kwa mfano, wananchi siku hizi wanahamasishwa waanzishe miradi mbalimbali, waanzishe majengo ya zahanati yajengwe mpaka lenta; waanzishe majengo ya shule, madarasa na nyumba za walimu wajenge mpaka lenta na nyumba za madaktari. Inapofikia mahali ambapo wananchi wamekamilisha ile miradi na Serikali ikaendelea kuchelewesha kuja kuwaunga mkono na kumalizia inawavunja wananchi moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Kamati kwa sababu ni maoni yao na kuisihi Serikali iwekeze katika kuweka bajeti ya kutosha kumalizia miradi ambayo imeanzishwa kwa nguvu za wananchi. Tuna miradi mingi ya mfano ambayo ningeweza kutoa katika Jimbo langu, lakini kwa sababu tunachangia mpango kwa ujumla wake katika kuielekeza na kuishauri Serikali, naomba nisiende huko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika zilizobakia naomba nielekeze maoni yangu katika kuchangia hili suala la Wakala wa Maji Vijijini. Kwa kweli kama tulivyoanzisha TARURA, naishauri Serikali ifanye haraka kuanzisha wakala huu. Ningefurahi kujua ni lini Wakala wa Maji Vijijini utaanzishwa kwa sababu moja ya vyanzo vya migogoro katika Taifa letu na hata dunia kwa sasa hivi vinatokana na masuala ya ardhi na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya maji ndiyo yamesababisha kuwa na mgongano mkubwa kati ya jamii zinazoishi katika maeneo yaliyohifadhiwa ambayo ndiyo yenye maji nyakati za kiangazi na maeneo mbalimbali kama Hifadhi za Taifa au Ranchi za Kitaifa. Tukipata wakala huu ukaharakisha kasi ya kupeleka maji katika maeneo mahsusini ya wafugaji, tutaepusha migogoro mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika hili suala la ardhi, naomba pia nidokeze kwa kusema kwamba hii Sera ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo inasema kwamba kuna sera ya kupanga, kupima na kusajili ardhi ipewe kipaumbele katika huu mpango wa mwaka wa fedha unaokuja ili kila kipande cha ardhi basi kiweze kupimwa; maeneo ya uwekezaji yaweze kubainishwa na maeneo ya wafugaji na wakulima yaweze kutenganishwa ili kupunguza migogoro ambayo inaendelea kutukabili kila wakati na huenda ikawa ni changamoto moja ya kutopeleka mbele maendeleo ya Taifa letu. Sasa hivi kuna migogoro mingi kati ya vijiji na vijiji, wilaya na wilaya na hata mkoa na mkoa na nafikiri hii sera ya kupima, kupanga na kurasimisha usajili wa ardhi, ingepewa kipaumbele katika mpango wa 2019/2020 tutaweza kupiga hatua kubwa katika kuharakisha kasi ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa muda ulionipa, basi naishia hapo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima tena tumerudi mahali hapa kama kawaida. Bila kusahau, nampongeze Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Halima Mdee kwa hotuba iliyosheheni mawazo pevu ambayo naamini Mheshimiwa Dkt. Mpango atayafanya kazi. Sisi kama Wapinzani tumekuwa tukitoa ushauri mwangi, kwa manufaa ya Taifa hili na Serikali hii namshauri Waziri apitie kitabu cha Sera Mbadala za CHADEMA zitamsaidia katika kuandaa mpango kwa sababu tunapenda kulisaidia Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, tumekuwa tukitoa mpango wa mwaka mmoja mmoja kutoka kwenye mpango wa miaka mitano. Kwa *experience* ambayo imeonekana sasa hivi, hasa hii miaka miwili ya karibuni, kuna miradi mingi imeingizwa ambayo haikuwepo kwenye mpango wa miaka mitano, jambo ambalo linatufanya tuonekane kama Taifa hatujui tunakotaka kwenda lakini ni wakati muafaka wa kujitafakari kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mdee katika hotuba amezungumzia sana kuhusiana na suala la Katiba, kwamba ni kipaumbele na kilio cha wananchi na amesema kwamba mipango yote mizuri hii kama hatutaangalia kilio cha wananchi itakuwa haina maana. Kwa kuongeza hapo, Mheshimiwa Dkt. Mpango nataka tujiulize maswali kama manne kama Taifa tunapoendelea na mipango hii, vinginevyo tutakuwa tunapoteza muda na tunapoteza kodi za wananchi. Hebu tujiulize kama Taifa, tunapopanga mpango huu nchi yetu kidiplomasia ikoje *as we speak?* Mahusiano yetu na mataifa mengine yakoje? Wanatuonaje kama Taifa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkapa aliwahi kusema, Tanzania inauhitaji ulimwengu kuliko ulimwengu unavyoitaji Tanzania. Ni maneno ya hekima ambayo tunatakiwa tuyatafakari, watu wanatuonaje kwa sasa? Katika historia hajawahi kutokea, tunamkuta hata Balozi wa EU anaitwa kujadili mahusiano na Taifa letu, kuna nini?

Tunatakiwa tujiulize, tunazungumza masuala ya kujipanga, lazima tujue Taifa letu limekaaje Kimataifa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tujiulize *foreign investors* wanaionaje nchi yetu, *are they comfortable* kufanya biashara katika nchi yetu? Hatuwezi kukaa kimya tukajipongeza hapa tukawa na sifa nyingi na pambio lakini hatujilizi haya maswali. Wawekezaji wanajionaje kuwepo katika nchi hii? Wako salama, wanaweza wakafanya biashara zao? Takwimu zinaonesha kwamba *foreign investors* wanafunga virago wanaondoka katika nchi yetu kwa sababu wanaona hawako salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, wawekezaji wa ndani wako salama? Hiyo *purchasing power* kwa watu wetu ipo? Haiingii akilini matajiri wa nchi hii wote hawana raha. Kama tajiri mkubwa, billionea, anaweza akakamatwa katika nchi hii, akatekwa, akafichwa, akarudishwa, mambo yakaendelea kama yalivyo, nani atakuwa na raha ya kutaka kuleta hela katika nchi hii akafanya biashara? Serikali haisemi chochote, hatujui nani amemkamata, amerudishwa, alivyokamatwa hajapewa hata nafasi ya kusema alikuwa wapi, nani atakuwa kuweka biashara hapa ndani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo hatuwezi kufumba macho kwamba hayapo katika nchi. Bado mnataka tukuze uchumi, haya ni masuala ambayo kama Wabunge lazima tujadili. Serikali lazima iwe *accountable*, usalama wa wafanyabiashara wetu ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza mambo ya kidiplomasia. Kuna *clip* moja ilikuwa inatembea, kuna Wanaigeria wawili walikuja hapa nchini wameitangaza dunia nzima jinsi ambavyo hatuko *friendly* kwa wageni. Kuna *clip* moja inamwonesha mtu wa Denmark/Danish alikuja kuwekeza, anamwomba Rais aingilie kat, hatuko *friendly* kwa hawa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Mheshimiwa Dkt. Mpango Serikali haieleweki inaendesha uchumi wa aina

gani? Ni uchumi wa ujamaa na kujitegemea *hundred percent* ambao Mwalimu Nyerere alishindwa wakati ule au ni uchumi wa aina gani, tufafanuliwe. Kama ni uchumi tufafanuliwe watu wanakuja kuwekeza katika uchumi wa aina gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, tuijulize, mazingira ya *civil servants*, katika Awamu ya Tano kila mtu amekuwa *intimidated*, kila mtu ametishwa. Tumezungumzia masuala ya Katiba, Taifa letu kwa sasa haliko *united*. Tunatakiwa tuwe na kitabu kimoja, tuwe na Katiba ambayo inatu-unite Watanzania wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapigana Vita ya Uganda, Mwalimu Nyerere alituunganisha wote, tuliona umuhimu wa kupigana Vita ya Uganda, lakini leo vita ya uchumi ni kubwa ambapo wote kwa pamoja tunatakiwa tushikane na kitu kinachoweza kutushikanisha ni Katiba. Hivi tunapozungumza maofisini watu wako *timid*, wana hofu, *culture of impunity* imekuwa ya hali ya juu sana, kila mtu anafanya anavyotaka halafu watu hawachukuliwi hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, hasa wateule wa Rais, wanaonekana wanamtii Rais peke yake, hakuna *chain of command*, kila mtu ni kambale. Utakuta Ma-DC hawaheshimu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa hawaheshimu Mawaziri, kila mtu anafanya anachokitaka. Hii imesababisha kusiwe na *discipline* katika utendaji kazi katika ofisi za umma. Ni wakati muafaka kama Taifa *kuji-unite* pamoja, tuwe pamoja; upinzani ndani ya Serikali, watendaji wa umma na watu wote tushikamane pamoja ili tulijenge Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *culture of impunity*, mfano mzuri ni bwana mkubwa mmoja hapa kila siku anatoa mambo ya ajabu. Ametoa matamko ambayo tumesikia hata watalii hawataki kuja nchi hii. Utakuzaje utalii kwa namna hii? Halafu Serikali mnasimama mnasema aliyojasema ni ya kwake yeye, siyo msimamo wa Serikali. Sasa

anawezaje mtu kusema mambo yake kwa kutumia *instruments* za Serikali? Amekaa kwenye ofisi na bendera ya Serikali na Polisi wa Serikali wanamlinda halafu mnasimama mnasema aliyoyasema ni ya kwake mwenyewe. Kama yake mwenyewe mbona hamjamchukulia hatua? Unatumiaje ofisi ya Serikali halafu mnasema ni ya kwake mwenyewe? Hatuwezi kujenga uchumi katika Taifa ambalo liko *scattered*, Taifa ambalo limetawanyika na halina umoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Utalii naye anasimama bila kuangalia madhara ya vile anavyo-*twit*; ana-*twit*, saa hiyo hiyo London nao wanarudi na majibu kwamba tuna-*cancel trip* na mnajua utalii unachangia fedha ya kigeni asilimia 17. Sasa tutajengaje uchumi wa namna hii Mheshimiwa Mpango na unapimaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapaswa tuweke mambo ya msingi. Tukianza na mambo ya msingi mambo ya juu yatajijenga yenyele lakini kuna matatizo, wafanyakazi hawako *comfortable*...

TAARIFA

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana mchangiaji anayechangia ambaye ana jina la Mchungaji. Ni Mchungaji gani anashabikia usenge na ndoa za jinsia moja?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy, hiyo lugha siyo ya Kibunge. Mheshimiwa Msigwa, endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *we are in a serious business*, tunazungumzia masuala ya uchumi na masuala ya uchumi yakiyumba tutayumba wote hapa. Hizi mbinu ambazo Serikali ya Awamu ya Tano

inazitumia ni mbinu ambazo zilitumika karne ya 17 hazifanyi kazi leo. Katika jamii hii watu wanatishwa, hakuna usalama ndani, utajengaje uchumi ambapo hakuna demokrasia, hakuna uhuru wa mawazo na watu hawawezi kujieleza? Humu humu ndani watu tunashindwa kujieleza, tunajengaje uchumi wa hivyo? (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nijue kwamba chama chake juzi walikuwako kwenye Taifa fulani, chama cha Msigwa, wakakutana na mashoga 40 na kufanya kikao, hiyo inaboreshaje demokrasia yetu na inasaidiaje katika...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msigwa endelea.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Na walizungumza nao nini?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge waliongea bila mpangilio)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Serikali ya Awamu ya Tano imeleta kongamano kujipima namna ya utendaji kazi. Waliokwenda kwenye kongamano ni hao hao watendaji akina Mheshimiwa Kabudi. Ni hao hao wanaofanya kazi, ni hao hao wanaojipima, ni hao hao wanaojisifu. Hamtaki hata kusikia sisi tunawaonaje? Humu ndani *we are not intruders*, sisi ni *part and parcel* ya *development* ya nchi hii. *You don't want to hear* sisi tunawaonaje. Mnafanya kazi wenyewe, mnajipima wenyewe, mnajipongeza wenyewe, halafu mnajitekenya wenyewe. Hiki ni kipimo gani mnachofanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo niliyoyasema lazima tujitafakari, mahusiano yetu na Kimataifa yako wapi? Tunahusiana vipi kwa sababu sisi siyo kisiwa. Rais wetu mpendwa mnampa kazi kubwa sana, lakini hamumshauri, ameshindwa kwenda... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwilima ajiandae Mheshimiwa Ntimizi.

MBUNGE FULANI: Hayupo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwilima hayupo, Mheshimiwa Ntimizi ajiandae Mheshimiwa Rehani.

MHE. MUSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika mpango. Kwanza kabisa nianze kwa pongezi. Naipongeza Serikali kwa kutekeleza mpango ambao tuliuipitisha hapa mwaka 2017, leo tunaona uanzishwaji wa ujenzi wa *Standard Gauge* unaendelea, napongeza sana, pamoja na kwamba kuna baadhi ya watu wanasema *Standard Gauge* tunazungumzia kwenye muda wa kusafiri tu. Sisi watu wa Tabora na mikoa mingine tunarajia *Standard Gauge* itakuja kutusaidia katika usafirishaji wa haraka na bei nafuu wa mazao yetu, mfano tumbaku na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia ununuaji wa ndege unaofanyika. Tulikuwa tunasema ni tatizo kubwa sana, lakini sasa Shirika letu la Ndege linaleelekea kuja kuchangia katika uchumi wa nchi yetu, lazima nipongeze hili. Tuna ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya nchi nzima. Limekuwa ni kelele sana na tumekuwa tunalizungumzia sana hili, lakini Serikali yetu sikiu imeanza kukarabati vituo vya afya takriban 200 sasa katika maeneo yetu. Vilevile kuna ujenzi wa Hospitali za Wilaya, zimetoka takribani shilingi bilioni moja na nusu katika Wilaya zetu na ujenzi wa Hospitali za Wilaya

unaendelea. Ni utekelezaji wa mipango mizuri ambayo tulipanga mwaka uliopita na sasa inaonekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miundombimu tumeshuhudia ujenzi wa barabara kubwa nchi nzima. Pia *flyover* za Dar es Salaam, zinasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamo. Kuna ujenzi unafanyika Mkoa wa Tabora, tulikuwa tunasema sana barabara kubwa ya Chaya - Nyahua ambayo inaunganisha karibu mikoa mitano ya Kanda yetu huku, ujenzi wake umefikia asilimia 30. Mipango yote hii ilikuwa mizuri na sasa inatekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na machache ya kushauri. Nikanza na eneo la utangulizi la Mheshimiwa Waziri, nina maeneo matatu ya kuzungumzia. La kwanza ni vipaumbele ambavyo vimewekwa katika hii miaka mitatu ya mpango wetu. Moja la vipaumbele ni suala la viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda vyetu. Hapa nilitaka nizungumzie maeneo mawili tu kwa kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni *SIDO*. Unapozungumzia *SIDO* ni eneo ambalo linasaidia uchumi mdogo wa maeneo yetu ya vijijini. Katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, amezungumzia kilimo kilivyokua kwa 7% na kusaidia usalama wa chakula, kupunguza mfumuko wa bei, ku-stabilize uchumi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kilimo kiende vizuri pamoja na upelekaji wa mbolea na upatikanaji wa masoko na kadhalika, lakini kilimo chenyewe kinahitaji zana za kilimo. *SIDO* wanatengeneza majembe ya ng'ombe ambayo tunayatumia sana vijijini, wanatengeneza mashine za bei rahisi za kusagia na kukamulia mafuta na kadhalika. Nina hakika *SIDO* ikiwezesha, wananchi wetu watanufaika sana na uchumi utazidi kukua katika maeneo yetu ya vijijini ambao unakuja kuchangia katika uchumi mkubwa wa nchi hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka Serikali iliangularie sana ni *CAMARTEC*. *CAMARTEC* ni Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini ambacho kipo Arusha. Watu wengi hawaifahamu *CAMARTEC* lakini wanatengeneza zana za kilimo na teknolojia za vijijini, ni sawasawa na *SIDO*. Hawa wanatengeneza mashine za kupandia mbegu za mazao mbalimbali ikiwemo tumbaku, korosho na kadhalika. Pia wanatengeneza kwa bei nafuu mashine za kusagia karanga na nafaka nyingine. Nasisitiza kwamba mpango huu uangalie sana haya maeneo mawili kwa maana ya *SIDO* na *CAMARTEC* ili kusaidia wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo limepeewa kipaumbele katika mpango ni kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Hapa naomba nongoosee upatikanaji wa huduma bora za afya vijijini kwetu. Kama nilivyosema ili wananchi waone ukuaji wa uchumi wao, zile huduma mbalimbali lazima zionekane zinapatikana katika maeneo yetu. Siyo tu kupata fedha mfukoni, lakini unapozungumzia huduma za afya, leo upatikanaji wa dawa ni asilimia takribani 80 katika maeneo yetu. Tumeongeza bajeti ya dawa na dawa zinapatikana. Mheshimiwa Dkt. Mpango katika hili nakupongeza. Pia naipongeza Serikali kama nilivyosema katika suala la ujenzi wa vituo vyaa afya na hospitali zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia ujenzi wa barabara kuu zinazosaidia usafirishaji na ufanyajji wa biashara kwa gharama nafuu. Nimesema barabara zinatengenezwa, lakini hapa naomba nizungumzie suala la *TARURA*. *TARURA* inatengeneza barabara zetu ndogo kuja katika barabara kuu. Ili mkulima asafirishe mazao yake kwa gharama nafuu ni lazima barabara zetu za vijijini ziwe nzuri. Leo tusipoiweshe *TARURA* hata hizi barabara kubwa tunazozijenga zitakuwa hazina manufaa makubwa sana kwa wananchi wetu. Naomba tuiwezeshe *TARURA* ili barabara zetu zipitike vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo hilo, kuna suala la upatikanaji wa maji safi na salama. Nimeona tunachimba visima katika maeneo mengi, lakini nashauri tuangalie uchimbaji wa mabwawa makubwa yatakayosaidia upatikanaji mkubwa wa maji tukiyawekea miundombinu. Yako maeneo yanayowezekana kuwekewa miundombinu hiyo, tuwekeze katika uchimbaji wa mabwawa makubwa na kuyawekea miundombinu ili kusaidia wananchi wetu katika maeneo mbalimbali. Mpango pia uangalie kwenda kukamilisha miradi ya maji ambayo imeanzishwa vijijini na imekwama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nishauri, kama kweli kilimo kinasaidia katika uchumi wetu, tuwekeze katika mpango wa kilimo cha umwagiliaji. Tukiwekeza katika kilimo cha umwagiliaji tuna uhakika wa kupata mazao mengi zaidi, maana tutapa fedha zaidi kwa wakulima wetu, kodi tutapata nydingi na vilevile usalama wa chakula utaongezeka na uchumi wa nchi yetu utaongezeka. Sijaona mpango uliozungumzia kilimo cha umwagiliaji, mwaka jana nilisema na mwaka huu narudia kusema, tunayo maeneo mazuri ambayo yaktengenezewa miradi ya umwagiliaji itatusaidia sana. Kwa hiyo, nashauri mpango uangalie eneo la umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA* ni sehemu ambayo inahitajika sana kuwekeza. Naomba tuongeze fedha katika miradi ya *REA*, pamoja na juhudzi zinazofanyika za kuongeza upatikanaji wa umeme kwa miradi, mfano *Stiegler's Gauge*. Tukiwekeza katika *REA* maeneo yetu ya vijijini yakapata umeme wa uhakika, tutakuwa na teknolojia ya kisasa ya ghamama nafuu ya kusaidia uzalishaji kwenye maeneo yetu. Kwa kweli miradi ya *REA* bado inasuasua kwa sababu ya kukosekana kwa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la tatu la uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji. Kwanza naipongeza Serikali, tulishauri uboreshaji wa bandari zetu ikiwemo ya Dar es Salam. Sasa hivi Bandari ya Dar es Salaam inaboreshwa,

inaongezwa kina, maana yake ufanyaji wa biashara katika eneo lile unaweza ukasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo moja la *blue print*. Tumeandaa *blue print* ili kusaidia mazingira ya uwekezaji katika nchi yetu ya Tanzania...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Nilimtaja Mheshimiwa Rehani lakini Mheshimiwa Zedi ana dharura. Kwa hiyo, tunampa Mheshimiwa Zedi ajiandae Mheshimiwa Komu.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene niweze kuchangia kwenye taarifa hii muhimu sana inayohusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi kubwa anayofanya. Takwimu rasmi ziko wazi kwamba uchumi wa Tanzania ndiyo uchumi unaokua kwa kasi kuliko chumi zote za nchi za Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeupitia Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa na kwa mujibu wa mpango huu, Serikali imepanga kukusanya na kutumia takribani shilingi triliuni 33 na kat i ya hizi takribani shilingi triliuni 23 ambayo ni sawa na asilimia 69 ni fedha ambazo zinatokana na mapato yetu ya ndani. Naipongeza Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuja na mpango ambao hatimaye tutatengeneza bajeti ambapo asilimia 69 karibu asilimia 70 ya fedha zote zitaghamiwa kutoptaka na fedha zetu wenywewe za ndani. Natoa pongezi sana kwa hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia vipaumbele vilivyoorodheshwa kwenye mpango huu lakini nina ushauri

kwamba kipaumbele namba moja ambacho tunatakiwa kupambana na kuhangaika nacho ni kukuza uwezo wa kukusanya mapato. Katika bajeti siku zote tunazungumza namna tunavyotumia fedha lakini bajeti na mpango siku zote vina pande mbili; kwanza inabidi uwe nazo ndiyo unaweza kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kipaumbele changu cha kwanza nadhani Serikali itumie nguvu, itumie mikakati na ubunifu na wataalam wote ilionao ili kuhakikisha kwamba tunapata mapato kwanza kabla ya kuona kwamba tutayatumiaje. Hii itawezekana tu pale ambako tutaweza kuwa wabunifu na kuja na vyanzo vipyta nya mapato. Tupanue wigo na tuondokane na zile njia za kiasili (*traditional ways*) za kupata fedha ambazo kila mwaka ndiyo tunazo hizo hizo. Kwa hiyo, lazima tuumize vichwa tuje na vyanzo vipyta. Mazingira yetu ya kiuchumi na kijamii yanawezesha jambo hiki kuwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni lazima tuwe na namna ambayo tutaweza kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato. Kwa sababu kuwa na vyanzo nya mapato ni jambo moja lakini kuweza kukusanya na kudhibiti mianya ya upotevu wa hayo makusanyo ni jambo lingine. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba ni lazima Serikali kwa kuititia Wizara ya Fedha iimarishe namna ambavyo mapato yatakusanya lakini yatadhibitiwa ili yasiweze kuponyoka na kwenda kwenye vyanzo vingine ambavyo havitarajwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuwa na mapato unajionyesha kutokana na mwenendo wa namna ambavyo tumekuwa tukipanga bajeti lakini namna ambavyo tumekuwa tukitoa fedha kwenda kutekeleza bajeti hizo. Taarifa ya Kamati ya Bajeti ukurasa wa 16 umebaini kwamba kumekuwa na mwenendo usioridhisha wa utoaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2016/2017 bajeti ya fedha za maendeleo ilikuwa ni shilingi trilioni 11 lakini zilizopelekwa zilikuwa ni shilingi trilioni 6.4 tu ambayo

ni asilimia 55 tu ya fedha zilizopaswa kupelekwa. Mwaka 2017/2018 bajeti iliyotengwa ili kwenda kugharamia miradi ya maendeleo ilikuwa shilingi trillioni 11.4, lakini fedha zilizoweza kupatikana na kwenda ziliwuwa shilingi trillioni 6.5, hii ni sawa na asilimia 57 tu. Ndipo hapo umuhimu wa kuwa na fedha unakuja kabla ya kufikiria kutumia. Kwa sababu kupanga bajeti ni jambo lingine lakini kuzipata fedha ili ziende zikagharamie ni jambo lingine. Ndiyo maana unakuta bajeti ni kubwa lakini fedha zinazokwenda ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nadhani ni kipaumbele, nikubaliane na maoni ya Kamati ya Bajeti ukurasa wa 24 ambapo impendekeza Serikali ione kwamba ni jambo la kipaumbele kutenga na kupeleka fedha kwa ajili ya kuezeka na kukamilisha maboma ya zahanati na shule yaliyopo nchi nzima. Ukipita kwenye Majimbo ya Wabunge wengi utakuta kuna maboma mengi ya zahanati, madarasa ya shule ambayo wananchi walitumia nguvu zao lakini Serikali iliahidi ingekamilisha lakini haikukamilisha. Jambo hili linavunja moyo wananchi. Nakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti yaliyoko ukurasa wa 24 kwamba Serikali itafute fedha, itenye na ipeleke fedha ili maboma ya zahanati na shule yakakamilishwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye maji. Kuna matatizo kwenye sekta ya maji. Wakandarasi wengi wamefanya kazi lakini hawajalipwa mpaka leo. Katika Halmashauri yangu ya Nzega kuna wakandarasi wanadai zaidi ya shilingi milioni 560 tangu mwezi Juni. Wamekamilisha miradi ya maji, wametengeneza *performance certificate* lakini hawajalipwa. Kwa hiyo, jambo hili linadhoofisha ukamilishaji wa miradi ya maji na baadaye linaleta malalamiko kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba miradi hii kama ya maji ambayo ina vyanzo vya fedha mahsus, Serikali ihakikishe kwamba miradi hii inakamilika. Kwa hiyo, hawa wakandarasi wa maji ambao naamini wako nchi nzima, fedha zao zitengwe, zipelekwe

na wakalipwe ili miradi ya maji iweze kukamilishwa na wananchi wetu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni miradi ya umeme, *REA III* kasi ni ndogo. Natambua dhamira ya dhati ya Serikali lakini kuna haja ya kuongeza kasi na hii maana yake ni kuongeza fedha ili wakandarasi hawa waweze kutandaza na kusambaza umeme kwa kasi ambayo inatarajiwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komu ajiandae Mheshimiwa Masele.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Mapendekezo ya Mpango huu wa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyosoma kuanzia tu ule ukurasa wa kwanza nikaanza kupata wasiwasi baada ya kuona kwamba miradi ya kimkakati kwa kweli imekuja mingine mipya lakini ile ambayo ilikuwepo siku zote tunaizungumza haijaaelezwa kwamba ni kwa nini imeondoka na imefikia wapi katika utekelezaji wake? Siku za nyuma tulikuwa na miradi ya kimkakati kama Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga; Mradi wa Magadi Soda ya Engeruka; Mradi wa Kiwanda cha Matairi (*General Tyre*) na *Kurasini Logistic Centre*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha kwamba hatujui ni kwa nini sasa miradi hii haipo tena ukweli na taarifa mbalimbali zinaonyesha kwamba hakuna chochote ambacho kimefanyika katika kuikamilisha hii miradi. Miradi

hii imechukua pesa nyingi za walipa kodi na nyingine ni mikopo. Kwa hiyo, tungependa sana kufahamu ni kwa nini hii miradiimeachwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine cha muhimu sana ni kwamba ukiangalia miradi hii kwa karibu ni miradi ambayo kweli ingetupeleka kwenye maendeleo ya viwanda lakiniimeachwa. Sasa ni mapenzi tu ya watu amba wako kwenye madaraka sasa hivi au ndiyo utaratibu wa kuendesha nchi yetu? Napenda nipaye maelezo kuhusiana na jambo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tumekuwa tukizungumza karibu muda wote wa Serikali ya Awamu ya Nne hasa mwishoni juu ya uchumi wa gesi. Leo ukiangalia katika mapendekezo haya sioni namna ambayo tunakwenda kutumia hiyo fursa ya uchumi wa gesi. Hili na lenyewe napenda nifahamu ni nini hasa kilichopelekea hali hii? Sababu ninazozisikia ni kwamba eti sisi kama Watanzania hatutanufaika sana kutokana na mikataba ambayo imekuwepo. Napenda kujua, hivi kweli ni sahihi kuchimbia hiyo rasilimali ambayo tumepewa na Mungu na kuwaachia hao au tukazungumze nao na kuona ni namna gani tutafanya? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fursa ambazo zingepatikana kutokana na uchumi wa gesi, kuna ajira zaidi ya 7,000 kutokana na vile viwanda ambavyo vingeweza kuanzishwa kule kama vya mbolea, *cement* na vya gesi yenye. Yote hayo tumeyakimbia na kwenda kuingia kwenye mambo mengine ambayo kwa kweli mimi siku zote naita ni kucheza kamari kama ule mradi wa ndege. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii vilevile inaacha maswali mengi juu ya Serikali hizi ya CCM. Hivi hakuna mahusiano kati ya Serikali iliyotangulia na hii ya sasa hivi? Au tuamini kwamba hizo Serikali zote zilizopita zilikuwa ni za wapigaji tu na ndiyo zimeifikisha hii nchi sasa inakuwa kama ndiyo inaanza upya? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na hiyo, ukweli ni kwamba tungefuatilia uchumi wa gesi na ile miradi mingine ya kipaumbele, leo tusingekuwa tunakwenda kuingia kwenye mgogoro wa kwenda kwenye *Stiegler's Gauge* ambapo tunakwenda kugombana na jamii ya Kimataifa. Vilevile *sustainability* ya huo mradi unaacha maswali mengi, kwa sababu kuna mambo ya mabadiliko ya tabia nchi, pia kuna uchumi wa utalii ambaao tunakwenda kuua bila sababu yoyote ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyine kwenye hii ni ushirikishaji wa wadau ambaao imetamkwa huku, lakini ukienda kuangalia hali halisi sasa hivi ya nchi yetu ni tofauti. Unapozungumza ushirikishaji wa wadau ni pamoja na kushirikiana na jamii ya Kimataifa. Nataka ni-echo hoja aliyotoa hapa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba sisi tumeamua kujitenga na dunia. Kama Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ameamea kutokuhudhuria mikutano yote mikubwa hata ya Umoja wa Mataifa, nafikiri ni lazima sisi kama Bunge tuchukue nafasi yetu, tushauri, tuseme siyo sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama suala ni gharama, ukienda pale *UN* unakuwa na fursa ya kukutana na viongozi wengine wa dunia kwa kutumia gharama hizo za kukupeleka wewe *UN*. Sasa kinachotufanya tusiende kwenye Jumuia ya Madola, tusiende kule Davos ni nini? Hivi sisi kweli tunaweza kuwa kisiwa tukaishi wenyewe tu humu humu ndani kama kuku anaatamia halafu tukaweza kuvuka kweli? Kwa hiyo, naomba sana Bunge lako liangalie jambo hili na kuliwekeaa utaratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kushirikisha wadau vilevile ni kuangalia haki kwa wadau, *is not one way traffic*. Siyo suala la kwamba Serikali inaweza ikafanya tu jinsi inavyotaka kwa wadau. Leo wako wafanyabiashara wakubwa kwenye nchi hii ambaao wako ndani kwa visingizio mbalimbali. Siungi mkono ufisadi lakini nafikiri kuna haja ya kuchukua hatua za makusudi wale wote ambaao wamewekwa ndani kwa sababu mbalimbali, kesi zao au

mashauri yao yafanywe kwa haraka ili waweze kurudi kufanya kazi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumweka ndani mtu ambaye ana uchumi mkubwa kwa maana ya uwekezaji katika hii nchi, maana yake ni kufunga vilevile shughuli zake za kiuchumi. Hii vilevile inawatisha wawekezaji wengine kuingia kwenye biashara na Serikali yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye uchumi wa viwanda ambao ni kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano. Taarifa zinaonyesha kwamba sasa hivi tuna viwanda zaidi ya 52,000, maana hivyo viwanda ukivigawa kwa Majimbo tulyonayo hapa kila mtu angepaswa aone kwake kuna viwanda kama 300 hivi, lakini kule Moshi Vijiji hatuna kiwanda hata kimoja. Hata ukimwuliza ndugu yangu Mheshimiwa Japhary hapa au ndugu yangu Mheshimiwa Selasini hapa, hatuna viwanda 10. Sasa hivyo viwanda vinajengwa wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba Serikali haijengi viwanda bali inajenga mazingira wezeshi kwa ajili ya viwanda kuwepo. Serikali hii imekuwa ikituambia kwamba itafidia yale maeneo ya *EPZ* na *SEZ*, itakuwa inatengeneza mazingira mazuri kwa ku-harmonize zile mamlaka za udhibiti, itakuwa inarejesha yale maeneo na viwanda ambavyo vilibinafsishwa lakini havifanyi vizuri lakini kwenye mambo yote hayo ambayo Serikali inapaswa kufanya ni sifuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima amesema hapa na akatoa *datasana* kwenye hiki kitabu cha Hotuba ya Kambi ya Upinzani, ukienda kwenye ule ukurasa wa 70, anasema tulipaswa na Serikali inasema siku zote, tunaweka nguvu kwenye kilimo na mifugo kwa ajili ya kupata malighafi kwa ajili ya viwanda hivi ambavyo tunavipigia debe. Mheshimiwa Halima ametuambia hapa kwamba kwenye kilimo katika mwaka 2016/2017 tumetekeleza bajeti kwa asilimia 2; mwaka 2017/2018 tumetekeleza bajeti kwa asilimia 11. Ukienda kwenye mifugo, tumetekeleza kwa

asilimia sifuri mwaka 2017/2018. Pia hizo bajeti hazitoshi, ni finyu, lakini pamoja na ufinyu wenyewe bado tunakwenda kutoa sifuri halafu tunasema tunajenga uchumi wa viwanda. *We are joking! Tunafanya utani na haya mambo na tunawatania Watanzania, hatuwatendei haki. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ANTONY C. KOMU: Ndiyo nimemaliza? *(Makof)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Vulu halafu Mheshimiwa Rehani.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa na kuipongeza Serikali yangu kwa kutimiza miaka mitatu katika utekelezaji wa shughuli zake. Pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais, pongezi nyingi kwa Baraza la Mawaziri, pongezi nyingi kwa viongozi wote waliokuwa maeneo mbalimbali. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia Mpango wa Maendeleo. Naomba kwanza nianze kupongeza kwa yale ambayo yemetekelawa kwa wakati na yakakamilika. Hapo hapo, naipongeza Serikali kwa kuthubutu kutengeneza reli ya *Standard Gauge* kwa kutumia fedha za ndani kitu ambacho siyo cha kawaida. Kwa kutumia fedha za ndani, Mheshimiwa Rais amethubutu na ameweza kuanza kujenga reli hiyo. Ujenzi wa reli hiyo utatusaidia kukuza uchumi wetu kwa sababu itarahisisha suala la usafiri iwe wa abiria, iwe wa mizigo kwa Tanzania na hata kwa nchi jirani na kwa muda mfupi sana. Ujenzi wa reli unakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ambazo zinaunganisha Mikoa yote nchini Tanzania hata zile za kwenye Halmashauri zetu tunakotoka. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ufufuaji wa reli ya kutoka Ruvu – Tanga – Moshi. Hili ni jambo jema. Reli hii ilisahafulika kwa muda mrefu sana. Ukichukulia hii awamu ya uchumi wa viwanda, reli hii itakuwa kiunganishi cha usafiri hasa kwa wale ambao mikoa yao imepakana na reli hii, wanaofanya biashara ikiwemo Mkao wetu wa Pwani, ambako kuna viwanda vingi, imevunja *record*, viwanda vingi vinazalisha na malighafi zinatoka ndani na nje ya nchi yetu. Kwa hiyo, hili litakuwa litasaidia sana na sisi wote hapa ni mashuhuda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napongeza Serikali kwa juhudzi ambazo zimeanza upya za ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Hii ni bandari ambayo inatakiwa ijengwe kwa wakati kwani itasaidia katika kukuza uchumi wetu na wa nchi nyngine. Kuna kikwazo kidogo, sina mashaka, nina uhakika Serikali italifanyia kazi kwa maana ya kulipa fidia wale wananchi waliokaa katika maeneo yale ili ujenzi uanze na uende kwa wakati na watu wa kujenga hiyo bandari tunawajua ni watu wa kutoka Oman na Wachina wako pale wanasubiri. Kwa hiyo, ulipaji wa fidia ni jambo la msingi na juhudzi tunaziona. Juzi tulikuwa na Makamu wa Rais katika Mkao wetu wa Pwani, aliweka juhudzi ya kwenda kuona jinsi bandari ile ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vibaya kama tutaweka utaratibu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi. Nchi yetu ina eneo kubwa sana la ukanda wa bahari lakini hatuna bandari mahsusizi kwa ajili ya uvuvi. Ni wakati muafaka sasa tukaweka Bandari ya Uvuvi ikaweza kuwasaidia wavuvi wakubwa na hata wadogo wadogo. Bandari zetu za uvuvi ziwepo lakini yale maeneo ya fukwe (*beach*) ambapo wanachi wanaweza kwenda wakapumzika, ijlukane hili ni eneo la kupumzika na hili ni eneo la biashara ya uvuvi kuliko sasa hivi maeneo mengi ya ufukwe yamechanganyika kati ya wavuvi na watu wanaotaka kwenda kupumzika jioni. Mfano mzuri, miaka ya nyuma, pale Posta ya zamani ule ufukwe ultengenezwa vizuri na wananchi wengi jioni walikuwa wanakwenda kupumzika, wanapata upepo wa bahari na kupata afya nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tupo kwenee awamu ya uchumi wa viwanda ambao unakwenda sambamba na nguvu kazi ya wananchi ambayo inatokana na afya bora, naipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na Hospitali za Wilaya. Kwenye maeneo ambayo majengo hayajakamiliika, yalijengwa kwa nguvu za wananchi, ni vyema sasa Serikali ikaongeza juhudzi zake, ikatenga fedha, ikashirikiana na wale wananchi kwenye yale maboma, wakajenga na kuhakikisha majengo yale yanakamiliika ili wananchi wetu waweze kupata huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya ujenzi ndiyo hiyo tunaiona na magari ya wagonjwa tumeona yamepelekwa, tunaomba maeneo mengine ambako hamna magari ya wagonjwa yapelekwe. Kwenye maeneo ambayo majengo yamejengwa na vyumba vya upasuaji vimeshajengwa, nashauri na kuiomba Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka vifaa tiba na miundombinu ya kuweza kufanya kazi vizuri katika hayo maeneo, kwa maana ya Madaktari wa Upasuaji, Madaktari wa Macho na wa magonjwa mbalimbali ili iweze kukidhi *standard* ya kile kituo ambacho kimejengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta maeneo mengi hawana hata vifaa vya kupimia sukari kwa wagonjwa wasukari na vya kupimia *pressure*. Ni vizuri sasa tukapeleka zaidi hivyo vifaa kule chini vitasidia wananchi wasiweze kuhamishwa kutoka hospitali hiyo kwenda kwenye ngazi ya Hospitali ya Wilaya au ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika naipongeza Serikali yangu kuititia Wizara ya Afya kwa hatua ilizofikia kuhakikisha afya ya mama na mtoto inaimarika. Inahakikisha idadi ya vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua inapungua, hali kadhalika na matatizo mengine yanayomkuta mwana mama. Hili ni jambo jema lakini bado kampeni hii naomba iendelee. Pia naomba ikiwezekana vile vifaa vya kujifungulia mama kwa sababu mama naye ana haki ya kuzaa salama na mtoto hana kosa lolote, anahitajika

azaliwe, aishi maisha salama, ni vyema basi vile vifaa tiba ikaangaliwa uwezekano, bei iliyokuwepo siyo kubwa sana, lakini bado siyo vibaya kama itapungua zaidi ya hapo, ikibidi hata wakipewa bure nao ni haki yao ya msingi. Kwa hiyo, ni vizuri tukaliangalia hilo ili kuweza kumlinda mama mjamzito, mama anayejifungua halikadhalika na yule mtoto anayezaliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yangu inavyosaidia watoto wanaozaliwa na vichwa vikubwa. Mungu azidi kuwasaidia hao watoto lakini juhudzi tumeziona. Maagizo na maelekezo kwenye Halmashauri zetu tunayasikia yakitolewa. Haya ni mambo mazuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigosie suala la maji. Maji ni muhimu sana. Tunalenga kumtua mama ndoo kichwani lakini pia tunalenga kumtua na baba ndoo kichwani kwa sababu naye kama hajaoa lazima akajitafutie mwenyewe maji. Juhudi ya Serikali iliyofanyika kusogeza huduma ya maji tunaipongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mikubwa ya maji tulioiono, tumeona Mradi wa Maji wa Kisarawe, nashukuru Serikali na imefanya vizuri lakini naomba *speed* isilegee, iendelee, *speed* iwe nzuri, watu waweze kupata maji, hasa wale ambao hawajapata maji ya bomba kwa muda mrefu hasa Wilaya ya Kisarawe. Vilevile kuna Mradi wa Maji Mkuranga na Chalinze na naipongeza Serikali kwa Mradi wa Maji wa Mafia Jibondo. Hicho kisiwa kilikuwa hakijawahi kusikia hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Rehani ajiandae Mheshimiwa Mlowe.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja. Naomba nichangie na nishauri Serikali katika mpango huu, nikimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha maoni yake. Nami naomba niwasilishe maoni ambayo naona yanaweza kuisaidia Serikali hii kuiondoa hatua moja kwenda hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa la mwanzo ambalo nataka kuanza nalo ni suala zima la uwekezaji katika bahari kuu. Nchi zote za visiwa na nyingine zilizozungukwa na bahari suala hili limekuwa kipaumbele na wenzetu limewatoa na ndiyo nguzo ya uchumi wao. Tanzania hatufaidiki hata asilimia moja katika maeneo ya uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni huu, kama tumeweza kununua ndege, kwa nini tushindwe kununua *long vessels* mbili tu ambazo zitawenza kuongeza mapato zaidi ya shilingi bilioni 7.8 kwa kila bamvua. Wale wenzangu wa Pwani wanaelewa bamvua ni kipindi kile cha uvuvi tu kwa kila *long vessel* moja. Kwa hesabu za haraka nilizozipiga ni kwamba tukiwa na *long vessels* mbili tunahitaji wataalam katika mchakato mzima wa uwekezaji wa viwanda vyta samaki na uvuvi wa bahari kuu karibu 3,640; lakini tunahitaji *hard labor* katika eneo hilo karibu wafanyakazi 48,000 wakati mmoja na hawa watakuwa wanafanya kazi kwa pamoja ambapo meli moja inakwenda Pwani, meli moja inapakua mzigoto kutoka baharini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia sasa hivi ina mahitaji zaidi ya asilimia 67 ya samaki. Tuna *demand* kubwa *in the world* wa samaki aina ya *tuna* katika soko la China, *Nordic countries*, Japan. Sasa hivi samaki aina ya *tuna* wamepanda kutoka dola 8,000 kwa tani mpaka dola 18,000 kwa tani. Hiyo *demand* haijawahi kutokea duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni sehemu ambayo sisi kama nchi tunakiwa tuiangalie. Nami nashangaa *Doctor*, kwa nini hili lisiwemo katika mpango wa sasa hivi? Tumechelewa sana, kwa sababu uwekezaji uliokuwepo hapa, *input* na *output* haziko sambamba, ni *only*

two percent ya input, lakini una output ya 98% kwenye total production ambayo tunaweza tukaifanya katika maeneo hayo. Wewe ni mchumi na unaelewa hapa ni kitu gani tunachokizungumza. Naomba tufanye restructuring tuhakikishe kwamba tunakuwa na uwekezaji katika eneo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika eneo hilo, tutaaanzisha viwanda ambavyo vitaweza kuchakata hawa samaki. Tukiianzisha bandari moja ya uvuvi hapa nchini ambayo mwenzangu ameshaidokeza pale, inaweza kutuingizia mapato mengi sana. Kwa mfano, ukaguzi wa *long vessel*/moja tu ambayo tutajipa leseni sisi kama Tanzania ni dola 40,000. Ndani ya nchi kwa mwaka mmoja tunaweza kusajili zaidi ya meli 40 au 100, ni kiasi gani ambacho nchi itaweza kuingiza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kila meli moja inayokuja kukagua lazima ichukue vyakula ndani ya nchi, inaanzia tani 10 mpaka 17. Hizi ni fursa ya soko la bidhaa ambazo tunazalisha wananchi hapa, wakulima watakuwa wamepata sehemu ya soko na vyakula mbalimbali vitaweza kuuzwa kwenye maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hicho tu, niliwaambia watu, maji haya ya kawaida ambayo yanatiwa katika vile vyombo, kila meli moja tungeizua zaidi ya shilingi milioni mbili au shilingi milioni nne. Mbali na upande wa mafuta, tutaweza kufanya biashara kubwa kabisa ya uwekezaji katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitu ambacho kinaweza kututoa ni hili suala la uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu. Kwa sababu meli, hii *long vessel* ndogo ya kawaida ina uwezo wa kuvua kuanzia tani 42,000 mpaka 105,000 na tunaweza kuinunua meli hii kwa dola za Kimarekani 450,000 na hizi mbili au zile kubwa zaidi tukainunua kwa dola 700,000 kitu ambacho kinawezekana kwa nchi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijielekeze huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda nishauri ni eneo ambalo bado kama nchi uwekezaji wake hatujaufanya. Wenzetu nchi za nje na nchi nyingine ambazo ziko ndani ya eneo la Sahara zinawekeza kwenye *research*. Namwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango aangalie suala hili la *research*. Nchi yoyote duniani haipigi hatua kama haikuwekeza kwenye *research*. *Research* hupotezi, ndiyo mwongozo utakaokupelekea kufikia yale malengo uliyokusudia. Tuna tatizo katika uwekezaji katika eneo hili, tunazungumza sana na kama *Doctor* kazi yako kubwa na wewe ilikuwa ni *research* lakini *priority* za maeneo ya *research* hazijakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Baraza na hayo malalamiko yapo katika kila eneo la *research* unaambiwa kwa kweli fedha katika maeneo hayo zinazokwenda kwa kiwango kidogo sana. Siyo tu kwenye *research* kwenye maeneo ya kilimo na mifugo lakini hata maeneo ya elimu na viwanda, huko kwenye viwanda bado hatujafanya utafiti wa kutosha tukagundua viwanda gani tunahitaji kama nchi? Tuwekeze kitu gani tuweze kutoka hapa? Je, tuwekeze kwenye viwanda vyta chuma ambavyo vinapatikana ndani ya nchi au tuwekeze kwenye viwanda vyta aina gani? Nafikiri hili nalo lioneokane katika huu mpango, kuna vipaumbele katika maeneo hayo na litatutoa katika kipindi kifupi tu kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la utalii. Bado kama nchi sisi tunapata *tip* tu, hatufaidiki na *fee* zinazotokana na utalii. Wanaoshughulika na tasnia ya utalii wanaelewa, nchi yoyote ili ifaidike na utalii unatakiwa uwe na *link* ambayo itakuunganisha kutoka mtalii anapotoka na aweze kulipa ndani ya nchi. Watallii wetu wengi wanalipa kwao, wanalipa kwenye makampuni yao, wanakuja na *travelling card* ndani ya nchi hapa, hatufaidiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili liangaliwe upya. Kwa kweli kiwango tunachokipata hapa nchini ni kidogo sana, tungeweza kupata zaidi ya mara 20 au 50 ya

pato ambalo wanapata wenzetu na tungeweza kwenda kujifunza Mauritius na Seychelles, nchi ndogo watu wachache, lakini kipato chake kinachotokana na utalii ni kikubwa. Leo mtalii nchini kwetu mpaka kufika hapa, mchakato wote ule anatoa dola 15 lakini akiingia Seychelles kufanya utalii, mtalii yejote lazima atoe dola karibu 160 za mwanzo hizo. Ni *entry fee* ambazo wao wamezitengenezea mazingira. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba twende tukafanye utafiti kwa wenzetu, tukae nao, watupe ujanja na mbinu tuweze na sisi kuwekeza katika hayo maeneo. Vivutio tulivyokuwananavyo vinalipa. Leo hii watalii ambaa wanakuja katika maeneo yetu, kwa mfano, Ngorongoro ukiwazuia, kwa kweli yatakuwa maandamano makubwa. Sasa kama vivutio hivi *potential* viko nchini na tunaweza kuvi-control wenyeewe, tuwe na usimamizi mzuri tupandishe kipato ambacho kitawea kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumza kidogo suala la mbegu ambazo tunasema kwamba tunataka tuzizalishe ndani ya nchi, tuna tatizo. (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mlowe ajiandae Mheshimiwa Masele.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja hii ya mpango. Awali ya yote, namshukuru Mungu ambaye ametujalia uhai nami siku hii ya leo kusimama hapa na kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Halima Mdee kwa uwasilishaji mzuri na kwa taarifa nzuri aliyoitao. Naomba Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango ayachukue mawazo ya Upinzani, ni mazuri sana, ayafanyie kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kuchangia hoja hii kwa kuanza na sekta ya kilimo. Katika hotuba hii, ukurasa wa 29, imeeleza kwamba kwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo umeongezeka kwa asilimia 7.1 mwaka 2017 ukilinganisha na ile ya 2016 ya 5.6. Suala la kilimo ni changamoto kwa wananchi wetu. Mwaka huu wakulima wengi wamekata tamaa kulima na hasa wa zao la mahindi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wananchi wetu wamejitalidi wamelima sana na wakapata mazao mengi sana ya mahindi, lakini kohoja kilichopo, sasa hivi wamefungia mahindi yao, yako ndani ya nyumba, panya wanakula, kwa sababu debe moja la mahindi ni Sh.2,500. Huu ni mfano wa eneo moja tu ambako natoka Mkoa wa Njombe. Wananchi wanafika mahali wanashindwa mbolea wanunuaje kwa sababu akiiza mahindi hata debe sita au kumi na kitu bado hawezi kununua hata chakula cha nyumbani. Hata akiiza maroba matano hawezi kununua mbolea au hata sukari kwa hela hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi tutawasaidiaje wananchi hawa. Pendekezo langu, kwa sababu bei ya zao la mahindi na mazao mengine kama mbaazi zimeshuka, basi na bei za pembejeo zishuke kusudi hawa wananchi wapate morali kuweza kulima tena mazao yao na mwakani waweze kuuza kama mtakuwa mmefanya utaratibu wa kuwawezesha kuuza mazao yao kwa bei zinazotakiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye hotuba ya Upinzani, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Kilimo iliidhinishiwa fedha za maendeleo shilingi bilioni 100, lakini hadi Machi 2017 fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 2.2. Halikadhalika mwaka 2017/2018, Wizara iliidhinishiwa fedha za maendeleo shilingi bilioni 150.2 lakini hadi mwezi Machi ziliikuwa zinatolewa tu shilingi bilioni 16.5. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii tunawezaje kuendelea na mpango huu kama kile ambacho tumepanga

mwaka jana na mwaka juzi tumeshindwa kukitekeleza? Naiomba Wizara kufuata haya Waheshimiwa Wabunge tunayoyapendekeza. Tunapoidhinisha bajeti, maana yake ile bajeti itolewe, isiwe tunaidhinisha kwenye makaratasi halafu ukija kwenye hali halisi kiasi kinachotolewa sicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la maji. Suala la maji nalo ni changamoto kubwa sana katika nchi nzima. Hata leo hii ukizunguka mkoa mmoja hadi mwingine, unaona kwa jinsi gani watu wanavyohangaika na suala la maji. Hata maeneo ambayo yana vyanzo vyta maji vyta kutosha kama vile Mkoa wa Njombe, bado pale Njombe Mjini hakuna maji. Hilo ni eneo ambalo lina vyanzo vyta maji, sembuse maeneo ambayo hayana hata vyanzo vyta maji vyta kutosha! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aone ni namna gani zinatengwa fedha za kutosha na kutafuta vyanzo vingine vyta kuweza kukidhi haja na hitaji hili la wananchi. Kwa sababu kwanza fedha zinazotengwa ni kidogo sana hivyo wananchi hawa wanashindwa kupata mahitaji ambayo yanetakiwa wayapate. Naomba Mheshimiwa Mpango atenge pesa iende kwenye Wizara husika ya Maji ili iweze kutekeleza miradi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, kuna suala la wataalam wanaokwenda kwenye utekelezaji wa hiyo miradi. Katika Halmashauri nydingi wanapelekwa wataalam ambao wanaenda kuharibu ile miradi, wakishaharibu wanapelekwa sehemu nydingine, baada ya hapo sasa Halmashauri zinaanza kubanwa kwamba mbona miradi haikutekelezeka vizuri. Mfano mzuri ni Njombe, naweza nikatoa hata mfano wa Mradi wa Utengule Ngaranga. Mradi ule umetekeliza chini ya kiwango. Mabomba hayafai, viungio vinakatika, hadi sasa hivi mradi umekamilika lakini maji hayatoki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye taarifa ya Waziri anasema kwamba miradi ya maji vijijini iliyotekeliza ni 1,595 na imeshakamilika. Naomba kujua,

hii miradi anayosema imetekelizwa, je, imefuatiliwa na kuona inafanya kazi? Nachoomba, tunapoandika taarifa hizi, tuhakikishe tumetembelea na kuona kweli miradi inafanya kazi, ndio tuweze kuiingiza hapa kwenye taarifa yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la viwanda. Kwenye taarifa ya Waziri, ukurasa wa 31 amesema viwanda vipya ni zaidi ya 3,306. Naomba kujua, hivyo viwanda ni vya aina gani? Hivyo ni viwanda ambavyo vilikuwa toka kipindi cha Nyerere au? (*Makofi/Vigelele*)

*(Hapa kengele illia kuashiria
kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Masele ajiandae Mheshimiwa Dau.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hotuba ya Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti kuhusiana na Mapendelekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kwanza kuipongeza Serikali, Mheshimiwa Waziri pamoja na Mawaziri wote na Watanzania wote kwa ujumla, kwa namna ambavyo wanaunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano katika kuhakikisha kwamba Tanzania yetu inakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha Serikali chenye mapendelekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2019/2020, ukurasa wa 34 - 49, vimeelezwa vipaumbele mbalimbali ambavyo Serikali yetu tayari imeshaanza kuvitekeleza na vingine viko katika hatua nzuri na naamini kabisa kwamba vipaumbele hivi vitakapokuwa vimekamilika, vitaifanya Serikali na Taifa letu la Tanzania kuwa mionganoni mwa mataifa ambayo kwa kweli yatakuwa yamepiga hatua kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ujenzi wa mradi wa uzalishaji wa maji wa Rufiji wenye *megawatt* 2,100; ujenzi wa reli ya kati, maendeleo ya ujenzi tumeyaona na juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa amekwenda kukagua utekelezaji na tukapata taarifa pia kwa Mkurugenzi wa Shirika la Reli, Bwana Kadogosa, alieleza mambo mengi. Tunaamini kabisa kama wale wa Shirika la Voda wanavyosema kwamba yajayo yanafurahisha, nami nina imani kabisa kwamba kwa kweli ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano hakika yajayo yanafurahisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ambayo imejaaliwa kwa mambo mengi na naomba Watanzania wote tushikamane kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunaiunga mkono Serikali yetu. Katika mambo yote ambayo Serikali yetu imejipanga kuyatekeleza, tushikamane pamoja na tuone kwamba miundombinu ambayo inajengwa na Serikali ni kwa ajili ya Watanzania wote. Ndege zinazonunuliwa, reli na treni zitakazokuwa zinahudumia Watanzania, zitakuwa ni kwa ajili yetu wote na kwa maslahi ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba tunayo mambo machache ambayo kimsingi tunatakiwa tuyazingatie na kupambana nayo hasa juu ya suala zima la hifadhi ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Bila kumung'unya maneno, nataka niseme tu kwamba uharibifu wa mazingira ni adui mkubwa ambaye anaweza akasababisha harakati zetu za kujikomboa na kutaka kulifanya Taifa letu liende mbele kukwama. Kwa ajili hiyo, napendekeza kwa kweli habari nzima ya utunzaji wa mzingira ipewe kipaumbele katika maeneo yetu ya utawala katika mikoa, vijiji, wilaya na kila sekta ijpambanue katika kuhakikisha kwamba tunahifadhi mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji wa miti ovyo, tumezunga athari zake katika Kanda ya Ziwa na hasa mikoa ya Shinyanga, Tabora hata kwetu Geita, athari zake tunaziona. Kwa maana hiyo, naomba kwa kweli Watanzania

wenzangu ambao bado hawajapata athari ya ukataji wa miti, waje wajifunze Kanda ya Ziwa ili waweze kuona ni namna gani mvua haziwezi kupatikana kwa uhakika na kwa maana hiyo tunapata shida kweli kweli. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu ijipange kuhakikisha kwamba tunakuwa na mkakati wa upandaji miti katika maeneo ambayo yameathirika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni eneo la mazingira wezeshi kwa wawekezaji, yaani yale mazingira ambayo yanaweza kusababisha uvutiaji wa wawekezaji kutoka nchi za nje kuja kuwekeza katika nchi yetu. Katika tafiti mbalimbali zimeonesha wazi kwamba Tanzania haina mazingira rafiki ya wawekezaji katika sekta mbalimbali. Wakati tunapojoandaa kutengeneza Tanzania ya viwanda, basi mazingira ambayo yanatuonesha kwamba sisi tunakuwa *ranked* wa namba za mwisho, tuyarekebishe ili kusudi kusababisha nchi yetu iweze kuwa ni eneo la kupendelewa na wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kweli katika hatua mbalimbali ambazo imezifanya. Katika sekta ya afya ambayo kimsingi Taifa lolote ambalo linataka kuendelea lazima watu wake waweze na afya njema na Serikali yetu imewekeza vya kutosha katika sekta ya afya. Tumeona jinsi ambavyo vituo vya afya vimeboreshwa na hata upatikanaji wa dawa na wenyewe umekuwa wa kuridhisha. Kwa hiyo, naipongeza Serikali na naomba iendelee na moyo huo na ikiwezekana kwa kweli maeneo ambayo bado hayajapata huduma za Hospitali za Wilaya kama huko kwetu Mbogwe, basi Serikali ione uwezekano wa kutuingiza katika utaratibu ikiwezekana miaka ijayo tupatiwe Hospitali ya Wilaya ili kusudi wananchi wa kwetu huko nao waweze kupata huduma za afya katika ukamilifu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la viwanda. Napendelea kabisa Serikali yetu pia ilitupie macho suala zima la utengenezaji wa viwanda vya mbolea. Kama ambavyo tumeweza kufanikiwa katika sekta ya viwanda vya

kutengeneza saruji, basi na utengenezaji wa mbolea Serikali ione uwezekano huo ili kusudi suala zima la sekta ya kilimo iweze kupata msukumo wa peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda pia vyatengenezaji wa madawa ya binadamu na wanyama pamoja na viuadudu ni muhimu. Naomba viwanda hivi na vyenyewe vipewe kipaumbe ili kusudi Tanzania yenyewa watu asilimia zaidi ya 75 wanaotegemea kilimo, basi kilimo hiki kiwe na tija. Watu wetu watakapokuwa wamepata miundombinu ya madawa na viuadudu na vile visumbufu vyatengenezaji wa mazao ya biashara na ya chakula utakuwa uko katika hali nzuri na matokeo yake Tanzania ya viwanda itakuwa imefikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa mara nyingine kwamba naisifu Serikali kwa kazi zake nzuri ambazo imeendelea nazo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Dau, ajiandae Mheshimiwa Frank Mwakajoka na tutamalizia na Mheshimiwa Mabula.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza sana mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutuletea mpango huu mzuri sana ambao kwa kiasi kikubwa sana unahitaji maoni yetu sisi Wabunge kuweza kuuboresha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mezani kwangu hapa nina nyaraka kama tatu hivi zote zinahitaji sisi Waheshimiwa Wabunge tuzipitie ili tutoe maoni ili na Mheshimiwa Dkt. Mpango ayazingatie atakapokuja mwezi Machi hapa kutuletea mpango wenyewe. Nitakuwa na maoni katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni ugharamiaji wa mpango. Nitazungumzia namna gani mpango utagharamiwa kwa kupitia miradi ya *PPP*. Sijaona hasa, bahati nzuri tulirekebisha Sheria ya *PPPBunge* liliopita ili tuone namna gani tunaweza tukavutia miradi mingi ya *PPP* ili kupunguza mzigo wa Serikali katika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa sana, bado sijaona hasa namna gani miradi ya *PPP* inaweza ikatupunguzia mzigo. Kama tatizo ni sheria, basi hiyo sheria ileteni tena tuibadilishe ili tupate kuvutia wawekezaji wengi. Miradi niliyoiona humu ndani, kwa heshima sana, miradi sijui ya kujenga *Hostel* za *CBE*, miradi ya kujenga *VETA* na *MSD*, kwangu ni miradi mizuri, lakini naiona ni miradi midogo. Tunahitaji kuvutia miradi mikubwa zaidi ili miradi hii ya *PPP* ipunguze mzigo kwa Serikali yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, imezungumzwa sana hapa. Nami nilipata bahati wiki mbili zilizopita, tulikuwa na ziara ya Makamu wa Rais, tumeona pale hali inakwenda vizuri lakini tunaihitaji bandari hii sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Bagamoyo pamoja na mradi wa *Standard Gauge* ni miradi miwili pacha. Tunahitaji meli kubwa ziende pale. Bandari ya Dar es Salaam pamoja na kwamba tunaiboresha hivi sasa lakini hizi meli zinakwenda kwa *generations*. Bandari ya Dar es Salaam inaweza ika-host pale meli ambayo ni za *third generation* basi na sasa hivi dunia inakwenda mpaka kwenye *tenth generation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji tupate Bandari ya kisasa ya Bagamoyo ambayo itaweza kubeba mzigo mikubwa, meli kubwa zenyenye kubeba mpaka *container* 10,000 ndiyo *SGR* itakuwa na maana zaidi. Kwa sababu ile *SGR* inahitaji iwe *feeded* na mizigo mizito. Kama meli haziwezi kufunga katika Bandari ya Dar es Salaam kutokana na ufinyu wa magati pale, tutarajie kwamba

Bandari ya Bagamoyo itakapokuwa kubwa ndiyo itaweza kuifanya SGRkuwa na manufaa zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa suala la Bandari ya Uvuuvi. Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami, tulipokuja kwenye Kamati tulizungumza hili suala la Bandari ya Uvuuvi, tunahitaji kuwa na bandari hii pengine sambamba na ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, pale pale tuweke na *section* ya Bandari ya Uvuuvi ili tupate kuua ndege wawili kwa jiwe moja. Kwa sababu tunaona suala la ujenzi wa Bandari ya Uvuuvi limekuwa likisusua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni shahidi, tulitenga pesa mwaka 2013/2014 shillingi milioni 500 kwa ajili ya *feasibility study*. *Feasibility study* imefanyika lakini hakuna kinachoendelea. Bajeti hii tuna shillingi milioni 300 kwa ajili ya *feasibility study* ya hiyo hiyo Bandari ya Uvuuvi na bado hatujaua hata *location* Bandari ya Uvuuvi itakuwa wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba sana Bandari ya Uvuuvi iunganishwe na ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ili tumalize hili tatizo. Hili suala ambalo amelizungumza ndugu yangu Mheshimiwa Rehani vizuri kabisa la kuwa na meli zetu wenyewe kwa ajili ya uvuvi katika Bahari Kuu ni muhimu sana pamoja na kufufua lile Shirika letu la Uvivu la *TAFICO*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu leo yupo hapa. Kwenye masuala haya ya usafiri wa bahari, nilikwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukakaa pale *Speaker's Lounge* na Mheshimiwa Waziri Mbarawa kuhusiana na tatizo la usafiri katika Kisiwa cha Mafia na meli ile ambayo Bakhresa ameipa Serikali bure kabisa ili ije itusaidie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Isack Kamwele hataki

kuipeleka meli ile Mafia. Ameniambia *point-blank* kwamba hatupeleki meli hii Mafia kwa sababu hakuna abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wananchi wa Mafia wako katika kadha kubwa sana ya usafiri hivi sasa. Tunasafiri na magogo ambayo wakati wowote yanaweza yakapata madhila yakazama. Leo Serikali imepewa meli bure na Bakhresa, iko pale *DMI*, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Nditiye amenipa ushirikiano mkubwa sana kwenye hili, lakini Waziri Kamwele amenitamkia. Namwambia mbona kuna maagizo hapa tuliongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu na wakati ule Waziri Mbarawa, tukakaa pale *Speaker's Lounge*, Mheshimiwa Waziri Mkuu akatoa maagizo? Yeye anasema, hayo mambo ya siasa, achana nayo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa, hivi maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mambo ya siasa? Mheshimiwa Waziri Kamwelwe anakataa kutekeleza maagizo ya Waziri Mkuu anayaita maagizo ya kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, nimeongea na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Hawa Mchafu anisaidie kufikisha huu ujumbe. Mheshimiwa Hawa Mchafu anakwenda kuongea na Mheshimiwa Waziri Kamwele anamwambia siwezi kupeleka meli Mafia itabidi nitoze nauli labda Sh.100,000, hailipi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu anieleze, je, ile habari ya kupeleka meli Mafia ni habari ya kisiasa? Labda Waziri atakapokuja kujibu atuambie, kwa sababu meli tumepewa bure, haihitaji usanifu, haihitaji bajeti, haihitaji sijui upembuzi yakinifu, inatakiwa kauli tu kwamba meli peleka Mafia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza pale Nyamisati kuna watu 150 wanalala pale wamekosa boti na wanatasafiria boti za mbaao. Boti ya kisasa ipo lakini wakubwa hawataki kuipeleka Mafia kwa makusudi tu. Sasa mnaipeleka

wapi basi? *At least* mtuambie mnaipeleka wapi kwa sababu kule Zanzibar boti za Bakhresa ziko nyingi tu. Huwezi kupeleka sehemu nyingine yoyote isipokuwa labda ni Mafia. Mheshimiwa Waziri anasema achana nayo hiyo. Kwenye bajeti hii tunashukuru sana...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOHN W. HECHE: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 64, nimemskiliza mchangiaji, hizi taarifa anazotoa ni nzito sana kwamba Watanzania wenzetu wanaoishi Mafia wanaambiwa na Waziri tamko alilotoa Waziri Mkuu ni la kisasa. Sasa naomba tuje nani anayesema uongo kati ya mchangiaji na Waziri Kamwelwe ili Bunge hili lichukue hatua. (*Makof/Kicheko*)

MWENYEKITI: Kaa chini. Mheshimiwa Dau, endelea. (*Makof/Kicheko*)

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingekuwa taarifa, basi nasema nimeipokea na naomba iwe sehemu ya mchango wangu. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasisitiza, sitaki niwe mbashiri mbaya, likitokea tatizo pale kwenye kivuko kile cha kutoka Nyamisati kwenda Mafia, halafu watu wakapoteza maisha, tunachokuomba Mheshimiwa Waziri Kamwelwe usije Mafia kuendesha zoezi la rambirambi pale. Maana yake inaonekana wewe ni fundi sana wa kukusanya rambirambi na masuala ya uokozi, sisi hatuko tayari kwa hilo. Kama unataka kutusaidia, utusaidie sasa hivi, usitusaidie wakati wa majanga kwa sababu meli ya kisasa kabisa ipo. (*Makof/Kicheko*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae Mheshimiwa Mabula.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jambo la kwanza kabisa, napenda niseme tu kwamba naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Taifa haliwezi kujengwa na kundi moja, Taifa hili litajengwa na Watanzania wote. Hotuba ambayo leo tumeisoma hapo, naomba sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango ajaribu kuitumia, italisaidia Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tumekuwa tunatable hotuba zetu lakini kila mwaka tunashauri ni namna gani Serikali yetu ihakikishe kwamba inachukua ushauri na baadaye inatekeleza ushauri huo lakini kila wakati ushauri huu hamuufanyii kazi. Nasi hatuchoki kwa sababu tuko kwenye nchi hii na hatuna nyingine ya kuishi, mngekuwa peke yenu kwenye nchi hii tungewaachia mwendelee na matatizo yenu lakini kwa sababu Taifa hili ni letu wote, tutaendelea kushauri mpaka kipindi ambacho mtakuja kuelewa na mkaamini kwamba tunahitaji kujenga Taifa hili tukiwa wamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia sana kuhusiana na mpango ambao umeletwa siku ya leo. Ukweli tu ni kwamba shughuli ambazo zinafanyika katika nchi hii, tumeona kabisa badala ya kuhakikisha kwamba tunapeleka maendeleo kwa wananchi lakini tunaona maendeleo haya yanakuwa kwenye vitu badala ya wananchi. Hili ni tatizo kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kuhusiana na hali halisi ya uchumi wa nchi hii. Hebu

tuangalie, katika Taifa hili tunasema Serikali inataka kuondoa umasikini. Unaondoaje umaskini wa Watanzania kama hakuna namna yoyote ya kupeleka fedha katika maeneo ambayo wananchi wengi wanapatikana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nichukulie kwenye suala la kilimo, uvuvi na mifugo karibu 65% ya Watanzania wako kule lakini huwezi kuamini fedha za maendeleo hazipelekwi kule. Mpango unaletwa hapa lakini inaonesha siyo kipaumbele cha nchi. Sasa tunataka kujua ni namna gani Serikali hii ambayo mnasema ni ya Awamu ya Tano, maana mimi najua ni Serikali ya CCM ile ile, lakini nyie mnajipambanua kwamba Serikali ya Awamu ya Tano, huu ni uwongo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 tulitenga bajeti kwenye kilimo shillingi billioni 101 lakini fedha ambayo ilikwenda kutekeleza shughuli za kilimo kule ilipelekwa shillingi bilioni 3 peke yake. Hapa tunasema kwamba tunakwenda kupunguza umaskini wa Watanzania, unapunguzaje umasikini wa Watanzania wakati kinachoonekana ni kwamba mnatekeleza uchumi wa vitu na siyo uchumi wa watu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili limekuwa ni sugu. Ukienda kwenye upande wa mifugo, tulitenga shillingi bilioni 4 lakini mpaka sasa hivi fedha ambayo ilipelekwa kwenye mifugo ilikuwa karibu shillingi bilioni 3 peke yake. Tunaona kabisa ni jinsi gani ambavyo Serikali hajajipanga kumaliza umasikini wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika nchi hii tatizo kubwa liliopo ni mazingira mabaya ya biashara. Kwa kweli katika nchi yetu kumekuwa na tatizo kubwa sana la mazingira magumu ya kufanya biashara. Tusipoliangalia jambo hili, tutaendelea kutwanga maji kwenye kinu. Sasa hivi tunasema kwamba wawekezaji waje katika nchi hii itakuwa ni jambo gumu, kwa sababu hata wawekezaji waliopo Tanzania ambao ni wazawa wameshindwa kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona biashara inafungwa...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji hapa amesema...

MWENYEKITI: Kanuni?

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Hii siyo Awamu ya Tano ni uwongo mtupu. Sasa sijui ni awamu ya ngapi, atuthibitishie huyu Mheshimiwa Mwakajoka, hii ni awamu ya ngapi? Kama siyo Awamu ya Tano yeye asingekuwemo Bungeni. Kwa hiyo, naomba atuambie sasa hii ni awamu ya ngapi kama hii siyo Awamu ya Tano ambayo amesema ni uwongo mtupu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakajoka?

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hajui kanuni, ngoja niendelee tu, nitamsamehe hivyo hivyo, kwa sababu ameamua kusimama tu na yeye auze sura kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli tu ni kwamba mazingira ya kufanya biashara ambayo yapo katika nchi hii ni tata sana. Lazima tukubaliane, tusipoweza kuondoa kero ambazo zinawahusu wafanyabiashara katika Taifa hili, tujue kabisa tunakoelekea Taifa hili linakwenda kuzama na tutaeendelea kusema tu kwamba Taifa linaenda vizuri lakini ukweli ni kwamba mazingira ni magumu, hata wafanyabiashara wa ndani wanashindwa kufanya biashara, biashara zinafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliopita tulimwambia Mheshimiwa Dkt. Mpango atupe sababu ni kwa nini biashara katika nchi hii zinafungwa? Alichokisema Mheshimiwa Dkt. Mpango ni kwamba wafanyabiashara wengi wanakwepa kodi. Hiyo siyo kweli. Wafanyabiashara wanalipa kodi lakini mazingira yamekuwa magumu, hata taarifa za Kimataifa zinaonesha kabisa kwamba tuko kwenye nafasi mbaya sana. Nchi hii katika mazingira bora ya biashara tunashika nafasi ya 167 kwamba mazingira ni magumu. Kwa hiyo, tunaomba tunaposhauri jambo hili tuwe tunaeleweka tunashauri kwa sababu ya maslahi ya nchi hii. Hatushauri kwa sababu tu tunataka kuzungumza ndani ya Bunge hili. Naomba hilo jambo lieleweke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na sekta binafsi hazishirikishwi ipasavyo katika Taifa hili. Kumekuwa na tatizo kubwa sana. Serikali hii inaonekana inafanya kazi kama vile ni Serikali ya ujamaa na ukisoma mpango hapa unasema sekta binafsi inashirikishwa lakini ukweli ni kwamba sekta binafsi haishirikishwi kabisa katika kupanga maendeleo ya nchi hii na kuhakikisha kwamba Taifa hili linasonga mbele. Kwa hiyo, naomba sana haya mambo yote yajaribu kutazamwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, leo tumepata taarifa kwamba wale wadau wa korosho ambao walikuwa wanununa korosho wameamua kuachana na korosho zetu na sasa hivi hawatanunua tena korosho. Kwa sababu Mheshimiwa Rais alisema kwamba Serikali itanunua, tunaomba kesho ikiwezekana tupate taarifa kwamba Serikali sasa inapeleka fedha na kuanza kupima hiso korosho za wakulima ili wakulima hawa waendelee kuuza korosho zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia tena yule mtu ambaye alinunua tani 500, anasema alikosea tu sifuri ile, lakini ukweli tu alikuwa ameamua kununua tani 50 ambazo alikuwa ameshalipia kipindi kile. Kwa hiyo, tunaomba Serikali pia ijiandae kununua hizi korosho kama ambavyo imewaaahidi wananchi wa Mtwara na Lindi kuhakikisha

kwamba korosho zao zinanunuliwa na wanapata hizo fedha kwa ajili ya kijiandaa na kilimo katika msimu unaokuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusiana na sekta binafsi ambavyo inashirikishwa katika Taifa hili. Ukiangalia kwenye mikopo ya Serikali, mikopo wa ndani mpaka sasa hivi umefikia karibu shilingi trillioni 5. Hizi fedha ambazo zinaoneshwa kwenye mikopo wa soko la ndani ni kwamba kama Serikali inaendelea kukopa kwenye sekta za fedha za ndani, tafsiri yake ni kwamba inaendelea kuhakikisha kwamba mabenki yanashindwa kukopesha wafanyabiashara wadogo wadogo ambao ni wajasiriamali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo hii ambayo Serikali inakopa kwenye soko la ndani badala yake tena imeshindwa kuziwezesha sekta binafsi ili ziweze kuhakikisha kwamba inatekeleza miradi yote ambayo Serikali inakuwa inakopea hizi fedha. Kinachoendelea ni kwamba tumeona makampuni makubwa ambayo yanatekeleza miradi mbalimbali katika nchi hii ni ya nje siyo makampuni ya ndani. Tunaomba Serikali hii ihakikishe kwamba inayawezesha makampuni ya ndani ili fedha ambazo zinazokopwa katika masoko ya ndani zihakikishe kwamba pia makampuni ya ndani yanatekeleza miradi mbalimbali ambayo inafanyika katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haiwezekani, tunaomba pia Serikali iweke sheria ikiwezekana makampuni ya ndani yashirikiane na makampuni ya nje ili *percent* kidogo ambayo inaweza ikapatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi hii kwa wakandarasi wa nje, basi na wakandarasi wa ndani waweze kupata fedha hizo. Kwa hiyo, tunaomba jambo hilo lifanyike kama ambavyo tunashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni pamoja na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kamwelwe.
(*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Anajibu tuhuma.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumzia jambo ambalo limetokea jioni hii ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa Dau, katika mchango wake amenituhumu kwamba nilitoa maneno ambayo yanaonekana kwamba nimemdhara Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba aliniagiza, nami nikasema kwamba haya maneno ni ya kisiasa. Sijawahi kuongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba Mheshimiwa Mbunge alinipigia simu akiwa anaomba kwamba ile meli ambayo mfanyabiashara Bakhresa ametoa kwa Chuo chetu cha *DMI* kwa ajili ya mafunzo kwamba meli ile ikiwezekana pia iwe inafanya safari kati ya Dar es Salaam – Mafia - Nyamisati. Baada ya kunipa hiyo taarifa nikamwambia nitaiulizia. Nikamwagiza Katibu Mkuu akaandika barua *DMI* kuuliza kama, je, hiyo meli inaweza ikafanya safari kwenda kule? Wakasema wako katika matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa wananchi wa kati ya Nyamisati na Mafia, tarehe 24, Serikali imetoa fedha na tumetangaza tenda kwa ajili ya kutengeneza meli itakayofanya biashara ya kubeba abiria kati ya Nyamisati na Mafia. Kwa hiyo, hilo limeshafanyika tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba maneno aliyoyatumia siyo mazuri sana, kwa sababu Waziri Mkuu mimi ni bosi wangu, lakini yeye mwenyewe sijawahi kuongea naye.

MHE. MBARAKA K. DAU: Taarifa.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Sasa hawezi akapandikiza maneno ambayo nimezungumza mimi na yeze akayapeleka kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge waliongea bila utaratibu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa miaka mitatu. Ni ukweli usiopingika kwamba Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Wasaidizi wake imefanya kazi kubwa sana kwa kipindi hiki tulichonacho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ule ule usiopingika Mheshimiwa Waziri wa Fedha amefanya jitihada kubwa sana, kila ambayo tulidhani tunawenza kuyafanya toka tulipoanza, tumeyafanya kwa sehemu yake kwa kiasi kikubwa sana. Haitakaa itokee na haitawezekana kila linalofanyika na Serikali watu wakalisema vizuri, hasa wanapoitwa Wapinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijikite kwenye mpango niseme maneno machache ya kushauri. La kwanza...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mabula ngoja kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, tutaanza kutajana majina ya watu wanaofanya fujo. Naomba amani kwenye Bunge, Bunge linaendeshwa na Kanuni.

Mheshimiwa Mabula, endelea.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kuishukuru Serikali, moja kati ya mipango ambayo inatazamia kuifanya ni kuhakkisha nchi yetu na miji yetu yote mikubwa inapimwa, inapangwa, inarasimishwa na kuhakkisha Watanzania hawa wanaondokana na wimbi la umasikini ikiwa ni moja ya kipaumbele, lakini ikiwa ni sehemu ya kuongeza thamani ya ardhi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Wizara ya Ardhi imefanya kazi kubwa sana, hasa kuhakkisha ardhi kubwa inapimwa lakini kuendelea kukagua mipaka na kuweka mipaka ili kuonyesha maeneo yanayostahili kutumika na yasiyostahili. Maeneo yote ya miji ambayo yametengenezewa mpango kabambe yanazo changamoto kubwa. Ukichukua kwenye miji mikubwa, kwa mfano, Mwanza ni moja kati ya mji ambao umeetengenezwa kwa ajili ya mpango kabambe lakini huu mpango kabambe unaenda sambamba na urasimishaji wa makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaofanya zoezi la urasimishaji wa makazi ni Halmashauri. Nami naiomba sana Serikali, Halmashauri zetu peke yake haziwezi kufikia kiwango tunachokitegemea kama Wizara. Ni vyema sasa Serikali ikaangalia uwezekano wa kuwekeza fedha. Nami niwapongeze, Serikali imenunua vifaa kupitia Wizara kwa ajili ya upimaji, hii ni hatua kubwa sana. Vifaa hivi vikitumika vizuri, Wizara ikiwezesewa, Halmashauri zikawa zinapewa kazi ya kupima maeneo na tukatengeneza mipaka zitaondoa migogoro ya ardhi ambayo bado ni mikubwa sana kwenye nchi hii. Kwa namna tunayoendanayo, hatuwezi kumaliza kwa wakati na migogoro itaendelea kuwa mikubwa kila leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukizungumza kwenye mpango mkakati wa upangaji miji, chukulia mfano wa Mwanza, ni mji ambao umeinuka, una milima mingi, yako maeneo bado hayatakiwi kupimwa. Unapozungumza kuweka mkakati wa kuboresha maeneo, wanapokuja wadau kushiriki kwenye ule mpango, wanapomkuta

mwananchi hajamilikishwa hili eneo, bado hana haki ya lile eneo na kipande ambacho amekiishi zaidi ya miaka 40. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali, moja ya mkakati ni kuhakikisha maeneo yote yanayotakiwa kurasimishwa kwenye miji yapimwe, yarasimishwe na wananchi hao wakabidhiwe hati. Kwanza, tunaongeza thamani ya eneo lakini pili tunamtambua mmiliki ambaye ametusaidia kutunza eneo hilo zaidi ya miaka 40. Haya yamejitokeza Nyamagana kwenye Kata zaidi ya tatu, Igogo, Nyachana, Mbugani, Isamilo, Mabatini na nyiningine nydingi pamoja na miji mingine yote mikubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine napenda nishauri, tumezungumza habari ya viwanja vya ndege. Ni kweli kabisa tunatamani kila sehemu kuwe na kiwanja cha ndege ikiwezekana. Nami nashukuru sana, nataka niishauri Serikali, viwanja ambavyo viko kimkakati tuvipe kipaumbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unapozungumzia uwanja wa ndege wa Mwanza, uwanja ule uko kimkakati. Haiwezekani leo tuna miaka sita tunauangalia tu hatutaki kuujenga uwanja ule kwa kiwango kinachostahili. Leo tuko 70% upande gani? Ni majengo ya abiria, *running way*, jengo la mizigo au ni *controlling tower*? Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe tunaweka kipaumbele kwenye mambo ambayo tunatazamia yatazalisha matokeo makubwa ili Serikali iweze kupata kipato kikubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda kuchangia ni juu ya sekta binafsi katika utekelezaji wa viwanda vya ndani. Ni kweli naunga mkono, ni vyema kila mkoa ukawa na hivyo viwanda 100, nami napongeza sana na Wakuu wa Mikoa wamefanya kazi kubwa lakini hivi viwanda 100 vina uwezo wa kuajiri mtu 1 mpaka 5. Dhamira

yetu sisi tulioko kwenye miji mikubwa tunavyo viwanda vya kimkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mwanza tuna viwanda vya samaki. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mpango amesitiza kuhakikisha tuna viwanda vinavyotumia malighafi ya ndani. Viwanda vya samaki vya Mwanza malighafi ya ndani ni samaki, operesheni imepita sasa hivi mazao ya samaki ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni lazima tukubaliane kwamba bila kuvipa uwezo viwanda hivi, ambavyo mnyororo wake ni mkubwa, vitaajiri watu wengi lakini vitaongeza ukuaji wa kipato kwa kila mtu mmoja mmoja kuanzia mvuvi, mchuuzi mpaka uuzaji mkubwa. Ndiyo maana tunazungumza habari ya kiwanja cha ndege, tunazungumza habari ya ujenzi wa meli na kuboresha meli nyingine zote zilizopo. Tukifanya hivyo itatusaidia sana. Lengo ni lazima tuwe na kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nawashukuru sana Wizara ya Afya, wamefanya jambo moja zuri sana kuptitia TAMISEMI. Kila Kituo cha Afya kinachotakiwa kujengwa kinapelekewa fedha zake, kama ni shilingi milioni 500 au ni shilingi milioni 400 na wanaamua tunataka kujenga vituo 200, vinajengwa 200 kwa wakati na vinakamilika. Sasa haya ni lazima tuenende nayo katika kuhakikisha tunausaidia umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno kwamba vitu tunavyovifanya haviwasaidii watu siyo kweli. Hivi leo unataka kuniambia zahanati zinazojengwa haziwasaidii wananchi wa kawaida? Zinawasaidia akina nani? Kwa hiyo, ni lazima tukubali, kupanga ni kuchagua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mwakajoka pale amesema, nchi hii tumepewa wote, lakini

aliyepewa nchi hii sasa hivi kuhakikisha anaishughulikia, anaijenga sawasawa ni aliyepewa dhamana, ni Chama cha Mapinduzi. Hiki ndicho kina dhamana ya kuangalia wapi kuna tatizo na wapi hakuna tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumechagua kupeleka maji, kujenga hospitali, kupeleka dawa, kutengeneza barabara, meli na *standard gauge* na haya ndiyo mahitaji ya wananchi. Leo Waheshimiwa Wabunge mniambie nani kwenye mikutano alishawahi kuulizwa suala la Katiba? Binafsi sijawahi kuulizwa swali la Katiba na nimekuwa na mikutano zaidi ya 1,000, wananchi wanaauliza maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunapozungumza Katiba, niulize humu ndani leo mnisaidie, nani anaitaka Katiba? Ni mwananchi, mwanasiasa au nani mwingine? Sote tunajua, sisi wanasiasa ndiyo tunataka Katiba kwa sababu tunataka dola, tunataka madaraka. Utafika wakati tutajua ni wakati gani tubadilishe Katiba kwa manufaa ya Watanzania na wakati gani tuendelee mbele? (*Makof*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge waliongea bila mpangilio)*

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Kwa hiyo, hizi nyiningine ni porojo na kelele nydingi haziwezi kutusaidia. Nachoamini, Watanzania wengi leo kila unayemgusa anataka yatokanayo na maendeleo, mambo yanayotatua changamoto zake za kila kunapokucha. Huo ndiyo msingi. (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 7 Novemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*